# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA

Nguvu ya Kuwa na Riziki

GARY KEESEE

M A P

# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA

## Nguvu ya Kuwa na Riziki

I N D

GARY KEESEE

U Z I

**Your Financial Revolution**
***Power of Provision,*** Kiswahili By Gary Keesee

© Gary Keesee, 2023

Originally published in English
ISBN: 978-1-945930-39-3

Faith Life Now
P.O. Box 779
New Albany, OH 43054, USA

You can reach Faith Life Now Ministries on the Internet at
FaithLifeNow.com

**Mapinduzi yako ya Kifedha**
***Nguvu ya Kuwa na Riziki,*** Kiswahili na Gary Keesee

© Gary Keesee, 2023

Awali kilichapishwa katika lugha ya Kiingereza
ISBN: 978-1-945930-39-3

Faith Life Now
P.O. Box 779
New Albany, OH 43054, USA

Unaweza kufikia Faith Life Now Ministries kwenye mtandao kupitia
FaithLifeNow.com

Isipokuwa imebainishwa vingine, Maandiko yote yametolewa kutoka Tafsiri ya ‘UNION’ ya Biblia Takatifu. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote.

Maandiko yaliyowekwa alama (NASB) yametolewa kutoka New American Standard Bible®, Hakimiliki © 1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972, 1973, 1975, 1977, 1995 na The Lockman Foundation. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote.

Maandiko yaliyowekwa alama (NLT) yametolewa katika Tafsiri ya New Living Bible. Hakimiliki © 1996, 2004, 2015 na Tyndale House Foundation. Imetumiwa kwa ruhusa ya Tyndale House Publishers, Inc., Carol Stream, Illinois 60188. Haki zote zimehifadhiwa.

Maandiko yaliyotiwa alama (GNT) yametolewa kutoka katika Biblia Takatifu (Today’s English Version, Toleo la Pili) la Biblia Takatifu. Hakimiliki © 1992 na Jumuiya ya Biblia ya Marekani. Haki zote zimehifadhiwa.

Kimechapishwa nchini Kenya. Haki zote zimehifadhiwa chini ya Sheria ya Hakimiliki ya Kimataifa. Yaliyomo na/au jalada havikubaliwi kunakiliwa kwa ujumla au kwa sehemu kwa njia yoyote bila idhini ya Mchapishaji.

# YALIYOMO

**UTANGULIZI** ........ vii

**SURA YA 1:** Nuru Kung'aa Gizani? ........ 1

**SURA YA 2:** Njia Mpya Ya Kufikiri ........ 14

**SURA YA 3:** Suala La Mamlaka ........ 31

**SURA YA 4:** Je Hukumbuki? ........ 55

**SURA YA 5:** Kuwezesha Riziki Yako ........ 71

**SURA YA 6:** Imani Ndio Ufunguo ........ 97

**SURA YA 7:** Onyo: Kaa Ndani Ya Imani Yako Uliyokuza! ........ 113

**SURA YA 8:** Unahitaji Mpango! ........ 129

**SURA YA 9:** Ni Wakati Wa Kwenda! ........ 141

# UTANGULIZI

Kichwa cha kitabu hiki kinaweza kuonekana kama kauli rahisi, jambo lisilo na mashaka yoyote. Ni nani anaweza kupinga uhalali wake? Nafikiri sote tutakubali kwamba kuwa na riziki, kuwa na vitu tunavyohitaji maishani, ni muhimu. Lakini wengi hawana riziki wanayohitaji. Wengi, kwa kweli, hupigania kupata vitu vya kutosha ili kuishi. Wanaishi maisha ya utumwa ya kulipa bili na madeni yanayoonekana kana kwamba hayaishi. Badala ya kutimiza ndoto zao, wanaishi katika hali ya kukata tamaa, wakiwa wamejawa na hofu ya kwenda kufanya kazi wasiyoipenda, na hata vibaya zaidi kuishi bila kusudi lolote la maana.

Utafiti wa hivi majuzi unasema kwamba 48% ya Wamarekani hupata takriban $31,561 kwa mwaka, au chini ya $2,630 kwa mwezi, na 40% ya watu hawawezi kumudu kuandika hundi ya $400 bila kuwa na mpango kwanza.

Je, unaweza kuwazia shinikizo la kulazimika kulinda kila senti unayotumia, huku ukitumaini kwamba utafika siku ya malipo inayofuata juma hadi juma, mwezi hadi mwezi, bila mwisho? Badala ya kupiga hatua kwenda mbele, unaona kwamba unazidi kuingia katika madeni bila njia ya kutoka. Ninaelewa jambo hilo, kwa sababu ndivyo nilivyoishi kwa miaka tisa mirefu. Lilikuwa tukio halisi maishani mwangu.

### Aibu ya Kuwa na Ukosefu

Mimi na mke wangu, Drenda, tulifunga ndoa na tulitarajia kuanza maisha ya ajabu, lakini tulijikuta tukiwa na madeni na kuishi maisha ya shinikizo la kifedha. Katika miaka michache tu, tulijikuta tukiwa na kadi 10 za mkopo tulizokuwa tumetumia kupita kiwango kilichokubalika na hivyo zikaghairiwa; mikopo ya kampuni tatu za fedha kwa riba ya 28%;

malipo ya magari mawili ovyo, yote yakiwa na zaidi ya maili 200,000; madeni ya kulipa shirika la serikali la ushuru; na madeni mengine mengi ambayo hatungeweza kulipa. Tulidaiwa na wazazi wetu maelfu ya dola, hadi wakaacha kutukopesha pesa.

Sio kwamba tulikuwa tumedhamiria kuharibu maisha yetu na madeni; tulikuwa tukijaribu kuishi tu. Ingawa hili linasikika kama jambo la kichaa, kazi yangu ilikuwa ya kuwasaidia watu na mahitaji yao ya bima na uwekezaji. Nilikuwa nikilipwa kamisheni ya asilimia 100 kulingana na mauzo niliyoyafanya, lakini kamisheni hazikutosha. Tuliendelea kutumaini kwamba biashara ingeimarika, lakini majuma yaligeuka kuwa miaka bila mabadiliko.

Hatimaye, baada ya miaka tisa mirefu ya kutegemea madeni kulipa bili, tulifika mwisho wa kila njia ambayo tungeweza kufikiria kukopa pesa. Tulitumia karibu kila kitu chenye thamani ambacho tungeweza kupata kama dhamana ya mikopo, na shinikizo hili la kuishi katika mtafaruku huu wa kifedha lilianza kunidhuru sana na familia yangu.

Nilianza kuwa na mashambulio ya hofu kwa hivyo daktari aliniandikia dawa za kupunguza shida hiyo, ambazo hazikusaidia na badala yake zilianza kusababisha athari mbaya zaidi. Pia niliambiwa na madaktari wangu kwamba ningepata ugonjwa wa kisukari kulingana na jinsi damu yangu ilikuwa ikionekana.

Jambo mbaya zaidi kuliko maswala yangu ya kiafya nilikuwa na hofu iliyotawala maisha yangu ambayo ilinifanya niogope kutoka hata nyumbani kwangu. Ulimwengu wangu ulikuwa umezungukwa na mateso ya hofu ya kizimu iliyonipooza! Tulikuwa tukichelewa kulipa bili zetu zote, na kila mwezi, changamoto ilikuwa kubaini ni ipi tulipaswa kulipa na ipi tungelipa mwezi uliofuata.

Nafikiri mojawapo ya vipengele vilivyodhoofisha zaidi katika janga hili la kifedha ni aibu niliyohisi. Hofu ilinishambulia kila nilipotumia kadi ya mkopo huku nikitumaini kwamba ingefanya kazi. Nilijipata nikitoa visingizio kila mara, nikiwadanganya wakusanya madeni ambao walinipigia simu karibu kila siku. Pengine jambo gumu zaidi kustahimili lilikuwa kuona familia yangu nzuri ikiwa bila vitu walivyohitaji, jambo lililosababisha maumivu katika nafsi yangu. Kusema kweli, nilihisi kuwa mtu asiyefaa karibu kila siku nilipokabiliana na tatizo moja baada ya jingine.

Janga hili la kifedha halikuwa changamoto ndogo tu ya muda mfupi. Liliendelea kwa miaka tisa mirefu!

Ikiwa unashangaa, ndio, tulikuwa kanisani kila wiki. Nilikuwa na digrii

ya theolojia na biashara na nilikuwa nimeenda kwa shule ya Biblia kwa mwaka mmoja. Nilikuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na nilimpenda Mungu, lakini jambo halikuwa sawa mahali fulani. Nilijua hilo, lakini je! mbona hadithi nilizosoma katika Biblia hazikuwa zikitukia maishani mwangu?

Tulikuwa washirika katika kanisa kubwa ambapo tulifundishwa kwamba mapenzi ya Mungu yalikuwa kwamba tufanikiwe, lakini sikuona hilo likitukia, na sikujua kwa nini. Kwa kweli, sikuona rafiki yangu yeyote akifanikiwa kwa kiwango kikubwa pia.

### Wito wa Uamsho

Kila kitu kiliharibika wakati wakili, mmoja kati ya wengi waliokuwa wakinifuatilia ili kupata pesa, aliponipigia simu tena. Wakati huu, alizungumza moja kwa moja na kuwa wa kumaanisha. "Bw. Keesee, nitakupa siku tatu za kunitumia dola 1,600 unazodaiwa na mteja wangu la sivyo nitalazimika kuanzisha kesi dhidi yako kuhusu kiasi hicho cha pesa." Kisha akakata simu.

Nilijua nilikuwa nimekwisha. Hakukuwa na mahali pa kugeukia ambapo sikuwa nimekopa awali. Hatukuwa na pesa, wala chakula. Jokofu yetu ilionekana tupu kama akaunti yetu ya benki. Nilikuwa nikitumaini kwamba wiki moja nzuri ya biashara ingetutoa katika hali hii, lakini kamwe haikuja.

Nikiwa na moyo uliokata tamaa sana, nilipanda hadi kwenye chumba changu kidogo cha kulala katika nyumba yetu nzee hapo mashambani ambayo tulikuwa tunakodisha kwa $300 kila mwezi. Nilijua kwamba hayakuwa mapenzi ya Mungu kwamba tuishi katika utumwa huo wa kifedha, hata hivyo tulikuwa tukifanya kila jambo vyema ila hatukuona fanaka.

Nilipojitupa kitandani mwangu nikiwa nimejawa machozi, nilimlilia Mungu. Cha kustaajabisha ni kwamba nilipokuwa nikimlilia kwa sauti, ghafla nilimsikia akijibu. Kutoka rohoni mwangu, nilisikia Maandiko haya:

> *Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri Wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.*
>
> —Wafilipi 4:19 (Tafsiri ya 'NASB')

Nikasema kwa sauti, "Ninajua Maandiko hayo, lakini sioni hilo maishani mwangu." Kisha nikasikia Roho Mtakatifu akisema:

> "Sina uhusiano wowote na changamoto uliyo nayo. Uko katika hali hii kwa sababu hujui jinsi Ufalme Wangu unavyofanya kazi." Aliendelea kuniambia kwamba kanisa Lake lilikuwa likiishi kama vile Israeli walivyoishi wakati wa Farao, kama watumwa. Alisema, "Nataka watu Wangu wawe huru kifedha!"

Ingawa sikujua maana hasa ya Ufalme, nilielewa kwamba kuishi katika madeni halikuwa jambo nzuri, na alikuwa akimaanisha kulikuwa na njia bora maishani ambayo sikuwa nimejifunza. Sikujua maana ya hilo au jinsi lilivyofanya kazi, lakini nilijiambia lazima nijue.

Kitu cha kwanza nilichokifanya ni kutoka mle chumbani na kumshika Drenda. Nilimwambia kile Mungu alichokuwa ameniambia, na ninakumbuka nilisimama pale, huku nikiwa nimemshika mkono, na kutubu kwa Mungu na kwake kwa sababu ya shida niliyokuwa nimesababisha. Tulijitolea pale pale kwamba ingawa hatukuelewa Mungu alimaanisha nini aliposema Ufalme, tungetafuta ili kujua maana yake. Pia tulijitolea kutoendelea na mtindo wa madeni maishani inga wa ilitubidi tukubali kwamba hatukujua jinsi ya kufanya hivyo. Tulipoomba, amani ilinijia, na nilijua kwamba Mungu angetuonyesha jinsi ya kutekeleza hilo kwa njia Yake.

Lakini kurudi kwa lile neno Ufalme, kwa kweli sikujua alikuwa akizungumzia nini. Nilifahamu ningeenda mbinguni, na nilikuwa na mafunzo mengi sana ya Kibiblia, lakini bado sikujua alimaanisha nini. Kwa kweli, neno Ufalme halikuwa neno ambalo nilijua sana. Wakati pekee ambao nilikumbuka neno hili likitajwa katika Biblia ni katika Sala ya Bwana.

> *Ufalme Wako uje, mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.*
>
> — Mathayo 6:9b-10

Wakati huo nilifikiri kwamba hili lilirejelea Ufalme wa wakati ujao ambao Yesu angeimarisha siku moja duniani, lakini sikujua maana yake hasa. Lakini baada ya kuchunguza andiko hili, nilitambua kwamba nilikuwa nimekosea. Yesu alikuwa akituambia jinsi ya kuomba hapa, sasa hivi. Tunapaswa kuomba mapenzi ya Mungu yatimie duniani. Lakini Ufalme wa Mungu ni nini?

Iwapo umesoma vitabu vyangu vya awali, unaweza kuruka kwenda kwenye sura ya 1 kama unataka, lakini ninaamini kwamba mapitio

huhitajika kila mara unapokaribia kufanya mtihani. Mtihani wako, mchezo wa kuishi maisha yako, tayari umeanza, lakini usijali. Bado kuna muda mwingi wa kupata majibu sahihi na kuupita. Lakini ikiwa wewe ni msomaji wa mara ya kwanza, kinachofuata ni muhimu!

### Njia Mpya ya Kuishi

Mungu aliponiambia kwamba sikuwa nimejifunza jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi, nilichanganyikiwa kusema kweli. Drenda na mimi hatukujua alichomaanisha. Tuliomba na kumuuliza Mungu atufundishe alichomaanisha aliposema hatukujua jinsi Ufalme Wake ulivyofanya kazi.

Kwa hiyo jambo la kwanza nililopaswa kujifunza ni maana asili ya ufalme. Nafikiri wazo hili ni gumu kwa akili za watu wa Magharibi kuelewa, maana tunaishi na mtazamo wa Kimarekani wa kidemokrasia na uhuru wa kujieleza. Ufalme wa Mungu si demokrasia; ni ufalme wenye mfalme. Mamlaka ya mfalme hupitia mamlaka iliyokabidhiwa, kupitia kwa mashirika mbalimbali ya serikali na watu wanaofanya kazi chini ya mamlaka hiyo. Kuwa na kundi kubwa la watu sio ufalme. Unaweza kuwa na kundi la watu milioni moja, lakini huo sio ufalme. Ufalme ni kundi la watu wanaounganishwa pamoja na sheria au serikali.

Katika kamusi maana ya ufalme ni: “jimbo au serikali iliyo na mfalme au malkia kama mkuu wake.”

Ingawa huwa tunasherehekea kuja kwa Yesu Duniani wakati wa Krismasi, huwa hatuelewi kwamba alikuwa akileta serikali pamoja Naye. Biblia inazungumzia serikali hii katika Isaya 9:6-7:

> *Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani Mwake; naye ataitwa jina Lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi Yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme Wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo.*

Yesu ndiye kichwa cha serikali hii, na tunapomkubali Yesu kuwa Mwokozi wetu binafsi, tunakuwa wanufaika wa serikali hiyo; tunakuwa raia. Sio tu kwamba tunakuwa raia, lakini pia tunakuwa sehemu ya nyumba ya Mungu kama wana na binti.

*Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina Lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu.*

— Yohana 1:12-13

*Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani Mwake Mungu.*

— Waefeso 2:19

Kama washiriki wa nyumba ya Mungu, tunafanyika sehemu ya familia Yake na hivyo kumiliki au kuwa sehemu ya kila kitu anachokimiliki. Pia, tunafanyika raia wenye haki na faida za kisheria katika Ufalme Wake mkuu.

**Ufalme Mpya**

Ili kuelewa vyema zaidi kile ninachomaanisha, hebu nizungumzie kuwa raia wa asili wa Marekani. Kama raia wa Marekani, una haki za kisheria. Haki zako za kisheria zimeandikwa katika Katiba yetu na katika sheria ambazo zimepitishwa na serikali yetu. Sheria na manufaa haya hupitishwa kwa kila raia, bila kujali ni nani. Haki hizo hazitokani na hisia au akili zetu. La, zimeimarishwa na sheria na zinapatikana kisheria kwa kila raia anayeita Amerika nyumbani kwao. Inawezekana kwamba raia hata hajui haki zake kisheria, lakini hata hivyo, zipo kwa ajili ya kila raia wa Amerika.

Sasa, hapa kuna jambo la kutafakari, na ninatumai litabadilisha mtazamo wako wote kumhusu Mungu na jinsi unavyopokea kutoka Kwake. Hapa Marekani, ikiwa tunajua kwamba kitu au mtu fulani anajaribu kutunyang'anya haki zetu za kisheria au kwamba tumetendewa isivyo haki, tunatafuta haki (haki maana yake ni utekelezaji au usimamizi wa sheria), mchakato unaotekeleza haki zetu za kisheria. Tunaenda mahakamani, na hakimu hajali sura yetu, au jinsi tulivyo tajiri au maskini. Anaangalia sheria. Anapaswa kuamua kwa kupendelea sheria kila wakati. Sheria na hakimu yupo kama dhamana zetu.

Tuna haki za kisheria, na serikali yetu itahakikisha na kutekeleza haki zetu za kisheria kupitia kwa mchakato wa haki ndani ya mfumo wa kisheria wa Marekani. Ukiwa na hilo akilini, angalia kwa makini Isaya 9 inapozungumza kuhusu serikali hii mpya ambayo Yesu alileta duniani.

*Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme Wake (Yesu); kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki....*

— Isaya 9:7

Andiko hili linasema kwamba Ufalme wa Mungu umethibitishwa na kutegemezwa kwa haki, usimamiaji wa sheria ya Mungu. Usimamiaji unamaanisha mchakato wa kutekeleza au kutumia haki zako za kisheria. Haki zako za kisheria ni kile Mungu anachokiita wema au kile anachosema ni haki, yaani sheria Yake. Ili kuhakikisha kuwa unapata kile Mungu anachosema ni sahihi katika Ufalme Wake, kile kilicho chako kisheria kama raia katika Ufalme, Mungu amekupa fursa ya kufikia haki, mchakato au dhamana inayohakikisha kwamba utapata kile alichokuahidi.

Mungu ametujulisha mapenzi Yake kupitia kwa Neno Lake, Biblia, ili tujue haki zetu za kisheria katika Ufalme Wake. Hii ni habari njema! Kila kitu unachosoma katika Biblia kuhusu kile Mungu amekuahidi tayari ni chako kisheria kama raia wa Ufalme Wake!

Wakorintho wa pili 1:20 inasema waziwazi kwamba kila ahadi—KILA AHADI—ni "Ndio" na "Amina." Uamuzi tayari umefanywa; tayari ni zako kisheria.

*Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika Yeye ni "Ndio;" tena kwa hiyo katika Yeye ni "Amin;" Mungu apate kutukuzwa kwa sisi.*

— 2 Wakorintho 1:20

Msingi hasa wa Ufalme wa Mungu ni haki na uadilifu—wala hauwezi kuyumba-yumba. Kwa hivyo lifikirie hivi: ikiwa najua sheria ya Ufalme wa Mungu (mapenzi Yake), na najua kwamba nina fursa ya kupata haki, yaani mchakato wa utekelezaji ambao unanihakikishia kile ambacho sheria inasema, basi ninakuwa jasiri wala siogopi.

*Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*

— 1 Yohana 5:14-15

Aya hii inaposema anatusikia, haizungumzii kusikia sauti kama vile kusikia maneno yetu tunayonena; inazungumzia Yeye kushughulikia kesi yetu.

Fikiria hakimu anayesikiliza kesi ili kuhakikisha haki imetendeka. Chumba cha mahakama na hakimu wapo kuhakikisha kuwa haki imepatikana kwa kila raia. Uamuzi wa jaji hautokani na hisia zake bali unatokana na sheria anayosimamia kutekeleza kwa kila mwananchi. Jaji yuko pale kuhakikisha kwamba haki (utekelezaji wa sheria) imetendeka kwa mujibu wa sheria iliyoandikwa.

Kwa habari ya Mungu, kiti Chake cha enzi (mahali pa mamlaka) na nguvu Zake zipo ili kuhakikisha haki (kutekelezwa kwa mapenzi Yake) kwa wanadamu wote wanaokuja kwa Yesu na Ufalme Wake.

Tafadhali soma kauli hii tena polepole, na iache ibadili mtazamo wako kumhusu Mungu. Watu wengi huhisi kwamba Mungu hufanya maamuzi Yake kesi hadi kesi, lakini sivyo. Yeye ni Mfalme wa Ufalme wenye sheria ambazo hazibadiliki. Hafanyi na hatafanya maamuzi nje ya sheria Yake. Tunaweza kujua jibu Lake ni nini kabla ya kuuliza, na tunaweza kuwa na uhakika kwamba tuna kile ambacho sheria Yake inasema kabla ya kukiona kwa sababu ana uwezo wa kutekeleza sheria Yake.

### Hakuna Kuomba-omba Tena

Mimi na Drenda tulipoanza kujifunza kuhusu haki zetu za kisheria katika Ufalme, jambo hilo lilibadili sana maoni yetu kumhusu Mungu na Biblia. Matokeo ya ufahamu wetu mpya yalibadilisha jinsi tulivyoishi. Hatukuwa tukiomba-omba tena. Hatukuwa tukimsihi tena. Tulijifunza kile ambacho tayari tumepewa kisheria kama raia wa Ufalme Wake. Na tuliendelea kujifunza jinsi ya kudai ahadi hizo na kuona zikitimizwa hapa duniani. Ulikuwa ufunuo mkubwa sana kujifunza kwamba sisi ni wamiliki wa vyote vilivyo mbinguni. Kama raia, tuna fursa kisheria kutumia sheria za Ufalme. Lakini kama washiriki wa familia Yake, sisi ni wamiliki na tuna madai ya kisheria juu ya urithi wa yote yaliyo mbinguni.

> *Na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu,* ***warithio*** *pamoja na Kristo.*
>
> — Warumi 8:17

Tazama andiko linasema sisi ni warithio pamoja na Kristo! Maana yake kila alicho nacho Kristo ni chetu pia!

Mungu aliponena nami katika ile nyumba yangu nzee kule mashambani na kuniambia kwamba sikujua kuhusu utendaji wa Ufalme Wake, alikuwa

akimaanisha sheria na muundo wa kisheria wa Ufalme Wake. Alikuwa sahihi. Sikujua ufalme ni nini au kuhusu utendaji wake. Lakini jambo moja nililoshika haraka, ambalo lilinisaidia kuelewa ufalme, ni kwamba falme hufanya kazi kupitia kwa sheria zisizobadilika. Sheria hazina upendeleo. Hazibadilishwi ili kumpendelea mtu fulani. La, ziko imara na zinadumu.

Hebu nikupe mfano. Leo tunafurahia umeme na mwanga unaotoa katika nyumba zetu. Utakubali kwamba sheria zinazosimamia umeme zimekuwapo tangu dunia ilipoumbwa. Hata hivyo, kwa maelfu ya miaka, hakukuwa na taa! Sababu gani? Hakuna aliyekuwa amegundua sheria zinazosimamia umeme na jinsi ya kuzitumia kuwasha balbu. Ingawa radi na umeme unaotokana na kusuguliwa kwa vitu viwili pamoja vilizingatiwa kama sehemu ya kawaida ya maisha, vilikuwa uchunguzi tu. Hakuna aliyefikiria hakika kunakili kile walichokuwa wakiona kwa sababu hawakutambua kwamba walichoona kilitokana na sheria ya asili ambayo wangeweza kujifunza.

Ukosefu huu huu wa ufahamu umeenea kanisani leo. Watu husoma kuhusu mambo makuu ambayo Mungu alifanya katika Biblia lakini kamwe hawapiti kiwango cha uchunguzi kuhusu kile wanachosoma.

Wengi wamemwona Mungu akifanya mambo ya kustaajabisha sana maishani mwao, lakini kama watu watazamao mwanga mkuu wa radi katika dhoruba ya msimu wa kiangazi, wao husimama hapo na kusema, "Ajabu, je, uliona hilo?" Wala hawawezi kuona hilo likirudiwa kwa sababu hawaelewi sheria zinazosimamia kile walichokiona. Kwa mfano, leo, tunaweza kuweka taa mahali popote tunapotaka duniani, kwa sababu tunaelewa sheria zinazosimamia umeme.

Vivyo hivyo, leo tunafurahia pia uwezo wa kusafiri maelfu ya maili kwa siku kwa ndege popote duniani. Ndege hupata uwezo wake wa kupaa kwa sababu ya ufahamu wetu na hutumia sheria inayosimamia kuinuliwa kwa vitu. Hata hivyo, sheria hii imekuwa duniani tangu kuumbwa kwa dunia, kama inavyothibitishwa na ndege wanaotumia sheria hiyo kila siku. Lakini hakuna mtu aliyeendesha ndege kwa maelfu ya miaka tangu kuumbwa kwa mwanadamu kwa sababu hakuna mtu aliyegundua sheria hii na kujifunza jinsi ya kuitumia.

Tena, ni vivyo hivyo katika Ufalme wa Mungu. Watu wengi huomba, hulia, na huendelea kujaribu kumshawishi Mungu awafanyie jambo. Lakini wasichojua ni kwamba walipookoka, sheria na manufaa yote ya Ufalme yalifanyika yao kutumia na kufurahia, bila kuomba-omba.

Tuseme nimealikwa kuhubiri kanisani mwenu. Je, timu yenu ya maombi

itahitajika kuomba na kufunga kwamba taa ziwake jioni hiyo nitakapokuja? Bila shaka la! Ikiwa nimefika kanisani mwenu na labda taa hazijawashwa, je, kila mtu ataanza kumlilia Mungu, na kujaribu kumshawishi awashe taa? La, watu watatafuta kibonyezi, wakifinye kuelekea upande wa juu, na taa zitawaka. Hakuna hofu, wala kuchanganyikiwa, ni kuziwasha tu!

Lakini kwa sababu moja au nyingine, Wakristo hawaukaribii Ufalme na Neno la Mungu wakiwa na mtazamo huu. Tena, huwa wanatumia muda wao mwingi kuomba-omba, huku wakitumaini kitu kitatokea. Wakati hakitokei, mara moja wanamlaumu Mungu, wakiamini kwamba Mungu amechagua kutowatimizia ombi lao. Kutoelewa huku ndiyo sababu Wakristo wengi leo wanaamini kwamba Mungu anaruhusu mambo mabaya yatukie, au kwamba Yeye anajua vyema zaidi msiba unapotokea. Rafiki, hivi SIVYO jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi!!!! Hebu tena tuangalie Maandiko yetu katika 1 Yohana.

> *Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*
>
> — 1 Yohana 5:14-15

Kwa kuwa tunajua tunaomba kulingana na haki yetu ya kisheria, na kwamba Yeye hushughulikia ombi letu, tuna uhakika kwamba tuna kile ambacho tumeomba! Cha kusikitisha ni kwamba ukweli unaofichuliwa katika andiko hili haueleweki na waumini wengi. Kupitia kwa uzoefu wangu, lazima niseme waumini wengi. Lakini ni ufahamu huu uliobadilisha maisha yangu kabisa!

### Maono Dhidi ya Unusuru

Nilianza kusoma hadithi za Biblia kwa umakini mpya. Nilifahamu kwamba katika kila hadithi kulikuwa na sheria za kiroho nilizohitaji kugundua. Nilifanyika mwanasayansi wa mambo ya kiroho. Katika kila hadithi, niliuliza maswali. “Kwa nini hili lilitokea?” “Ni sheria gani inayoonyeshwa katika hadithi hii?” Polepole, nilianza kujifunza kanuni na sheria zilizopo kwa ajili yangu katika Ufalme wa Mungu, na hilo lilibadili maisha yangu kihalisi.

Tulipoanza kutumia sheria hizi, tulitoka kwa madeni kabisa baada ya miaka miwili na nusu. Tulianza kulipia magari yetu kwa pesa taslimu,

tulijenga nyumba ya ndoto yetu kwenye ekari 55, na mengi zaidi. Habari nzuri zaidi ni kwamba sasa hatuna shinikizo la kifedha. Nyumba yetu imelipiwa, na sasa tunaweza kukaza fikra zetu kwa kazi ya mwito wetu, na kusudi letu, badala ya kuishi maisha ya unusuru.

Tulisisimka sana na yale tulikuwa tukijifunza lakini hatukuwaona marafiki wetu na watu wengi tunaowafahamu wakiyafurahia mambo yaleyale tuliyoyaona yakitukia. Kutokana na nia yetu ya kuwasaidia watu kujifunza kile tulichokuwa tumejifunza, tulizindua Kanisa la Faith Life mwaka wa 1995. Tulizingatia kushiriki sheria na kanuni ambazo Mungu alikuwa ametufundisha, kushiriki na watu jinsi wanavyoweza kuwa huru na kuishi maisha mazuri ya Ufalme.

Kisha mwaka wa 2005, tulizindua Faith Life Now, ambayo ni huduma yetu ya vyombo vya habari. Faith Life Now huonyesha vipindi vyetu viwili vya televisheni kila siku—*Fixing the Money Thing* na *Drenda*—katika kila eneo ulimwenguni pamoja na Habari Njema ya Ufalme.

Leo, hatutafuti shilingi zilizoingia ndani ya viti vya magari yetu tukitumai kutoa humo pesa za kutosha kuwanunulia na kuwagawanyia watoto wetu watatu mlo mmoja wa kujifurahisha. Sasa sisi hutumia mamilioni kufanya chochote tunachofanya, na tuna shauku ya kuwasaidia watu kujifunza jinsi tulivyoweza kufanya hivyo.

Ghafla tuliacha fikra za unusuru tukaanza kuwa na fikra zenye msingi wa maono na kuanza kuota kuhusu yale tunayoweza kuunda na kufanya na maisha yetu. Tulitoka kwenye matatizo ya kifedha na utumwa na kuingia katika uhuru wa kifedha.

Katika siku zetu za ukosefu na utumwa, kila suala dogo la kifedha lilikuwa jambo la dharura kuu. Wakati wowote tulipokuwa chini ya dhiki kubwa, kwa kawaida tungejaribu kutafuta mtu wa kukopa pesa, au tungetembelea duka la mkopo ambapo tungebadilishana vitu vyetu na kupewa pesa tena! Lakini leo, tunafurahia Nguvu ya Kuwa na Riziki.

Labda unaweza kuuliza, "Gary, Nguvu ya Kuwa na Riziki ni nini?" Nguvu ya kuwa na riziki ni uwezo wa kugundua kusudi la maisha yako na kuepuka unusuru. Daima kumbuka kwamba riziki inapaswa kuwepo kwa ajili ya kutimiza maono yako. Soma maneno haya tena polepole ili kupata maana yake kwa udhahiri.

Kutokuwa na riziki huleta maisha ya utumwa, na watumwa hawaoti ndoto kubwa! Na kumbuka daima kwamba wewe si mtumwa! Wewe ni mshiriki wa nyumba ya Mungu, mrithi wa mali yote pamoja na Yesu. Kwa hivyo inua macho yako na uone mustakabali mpya. Ninataka uwe huru

kuota, huru kufurahia kuunda maono yako, na kuishi maisha mazuri. Ninaamini unaposoma kitabu hiki utatiwa moyo, lakini sio kutiwa moyo tu, bali utapata ujasiri. Sheria zilezile za Ufalme zilizobadili maisha yangu ni zako pia.

— Gary Keese

Hiki ni kitabu cha nne katika mfululizo wa vitabu vitano wenye kichwa, "Mapinduzi Yako ya Kifedha." Ninakutia moyo usome vitabu vitatu vilivyotangulia ili kupata ufahamu mzuri wa sheria ninazorejelea na zaidi kuhusu jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi. Navyo ni: Mapinduzi Yako ya Kifedha: *Nguvu ya Kuwa Mwaminifu, Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kupumzika, na Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa na Mkakati*. Unaweza kuvipata kwenye GaryKeesee.com.

SURA YA 1

# NURU KUNG'AA GIZANI

Nilikuambia katika utangulizi kuhusu simu niliyopigiwa na wakili ambayo ilinifanya nikabiliane uso kwa uso na ukweli wa hali yetu na hatimaye kumlilia Mungu. Pia nilikwambia kile ambacho Bwana aliniambia nilipokuwa nimelala kitandani mwangu nikilia, kwamba nilikuwa katika hali mbaya kwa sababu sikuwa nimejifunza jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi. Lakini je, unafanyaje kazi? Alikuwa akijaribu kunionyesha nini? Sikujua, lakini nilikuwa karibu kujifunza.

Ikiwa unakumbuka, nilipaswa kumpa wakili dola 1,600 kabla ya siku tatu kuisha ili niepuke kesi. Wakati huo, hatukuwa na pesa na hatukuwa na matarajio ya kupata pesa haraka kutoka kwa biashara yetu ili kulipa $1,600. Nilikuwa katika hali ngumu sana, au ndivyo nilivyofikiri. Lakini nilikuwa karibu kujifunza somo langu la kwanza kuhusu Ufalme.

Wakati huo, nilikuwa na gari nzee aina ya Dodge Caravan ambalo lilitoa moshi kama bomba la moshi lilipoendeshwa barabarani. Jioni hiyo, nilikuwa nimepanga kukutana na familia fulani ili kuzungumzia mahitaji yao ya bima, na mkutano wetu ulikuwa nyumbani kwao, ambapo palikuwa umbali wa takriban dakika 15 kutoka ofisini kwangu.

Katika nyakati hizo, nilikuwa nikiegesha gari langu barabarani kimakusudi au pembeni karibu na nyumba ya mteja wangu. Sababu ni wazi. Kila nilipoliwasha, lilijaza hewa na moshi mweupe, na sikufikiri kwamba hiyo ilikuwa picha nzuri kwa biashara yangu maana nilikuwa mtu aliyeitwa mtaalamu wa masuala ya fedha aliyewashauri wateja jinsi

ya kuwekeza na kununua bima.

Kwa kweli jioni hiyo kama kawaida, niliegesha gari pembeni karibu na nyumba ya mteja wangu. Tulikuwa na wakati mzuri kisha nikawaaga, lakini niliingiwa na wasiwasi wakati bwana huyo alipoendelea kutembea pamoja nami nilipokuwa nikielekea kwenye gari langu. Ingawa nilisikitishwa kidogo, sikuwa na shida na hilo mradi tu asibaki karibu kuona nilipowasha gari langu, jambo ambalo alifanya. Ijapokuwa nilichukua muda wangu kuandaa mkoba wangu na vitu vingine ndani ya gari huku nikijaribu kumpa muda wa kuondoka, alisimama kwa subira hadi nilipoona ni vyema kuwasha gari. Kweli, kama ilivyotarajiwa, barabara ilijaa moshi mweupe.

Nilipotaka kuanza kuondoka, aliniashiria nilizime na akaja dirishani. Kisha akaniambia kwamba alikuwa akifanya kazi ya ufundi wa magari kama kazi ya ziada, na angependa kuangalia sehemu ya mbele ya gari. Nilikubali na nikamfungulia sehemu ya mbele. Nilijua haikujalisha alichopata. Sikuwa na pesa za kutumia kwa gari hilo nzee wakati huo.

Baada ya dakika chache, alisema, "Kama vile nilivyoshuku, kifaa kinachozuia uvujaji wa mafuta ya injini kimepasuka. Endesha gari hadi nyumbani, kisha ukirekebishe kabla ya kuliendesha tena. Kitakugharimu takriban $700 tu."

Nilimshukuru kwa ushauri wake na kuondoka kurudi ofisini kwangu. Kile tu nilichosikia akilini mwangu ni, "Kitakugharimu takriban $700 tu!" Kwangu wakati huo, dola 700 zilionekana kama dola milioni moja, na bado nilikuwa na hitaji la dola 1,600 ili kutuma kwa wakili. Kando na hilo, nilikuwa na rundo la bili nyingine zilizohitaji kulipwa.

Sikuwa na jibu, lakini nilikumbuka maombi ambayo mimi na Drenda tulikuwa tumeomba awali, "Mungu, tufundishe jinsi Ufalme Wako unavyofanya kazi, na utuonyeshe jinsi ya kuishi bila madeni."

Nilipokuwa nikiendesha gari kurudi ofisini, nilianza kuzungumza na Bwana kuhusu hali yangu ya kifedha. "Bwana, unajua yote kuhusu pesa ninazohitaji. Wewe unajua ningali na deni la gari hili, na sasa $700 zinahitajika. Bwana Mungu, kwa kweli tukihesabu pesa ninazodaiwa na benki juu ya gari hili na gharama ya kulikarabati, pengine ingekuwa bora liteketee tu ili yote yalipiwe na shirika la bima!" Nilisema hivyo kwa sauti ya kuchanganyikiwa, kwa njia ya kejeli, wala haikuwa sala halisi.

Mara niliposema hivyo, kitu kilikamata usikivu wangu. Sikuwa na hakika kama kilikuwepo wakati wote, lakini kulikuwa na tone ya kitu kilichokuwa kikichemka juu ya kifuniko cha sehemu ya mbele ya gari. Nilipotazama, ilionekana kwamba tone hilo lilikuwa likiongezeka polepole.

Na nilipoendelea kutazama tone hilo, kwa kweli lilikuwa likiongezeka kwa ukubwa. Nilishtuka kusema kweli. Sikuona moshi wowote ila ule uliofuka nyuma ya gari kila siku, kwa hiyo niliendelea kuelekea ofisini.

Nilipokuwa nikiingia katika mahali pa kuegesha magari ofisini, sehemu ya mbele ya gari langu ilipasuka ghafla na kuwaka moto! Miale ya moto ilikuwa ikiruka futi sita hewani kutoka kwa injini. Kisha nikasema kwa sauti, "Bwana, umenisikia nikisema hivyo?"

Siku iliyofuata, kampuni ya bima ilishughulikia hilo, nami nikawa na pesa za kutosha kumlipa wakili $1,600 nilizomwia, na kulipa deni la gari na bado nikawa na pesa za kutosha kununua chakula. Tulifurahi na kushtuka kwa wakati mmoja ingawa sasa hatukuwa na gari, ambalo familia yetu ya watu sita ilihitaji kwa ajili ya usafiri.

SAUTI, "BWANA, JE, ULISIKIA NILIPOSEMA HIVYO?"

Kwa kweli sikuweza kueleza kilichotokea wakati huo, lakini ukweli kwamba nilisema kwa sauti kuwa gari hilo liungue ulivutia umakini wangu. Ilinibidi nikiri kwamba sikuwa nimewahi kumiliki gari lolote hapo awali ambalo lilishika moto. Kwa upande mwingine, sikuwa nimewahi kusema kwa sauti kwamba nilitaka gari lolote langu lishike moto.

Je, hili lilihusiana na Ufalme? Je! nilifanya kitu kilichosababisha hili kutokea, au ilikuwa bahati mbaya tu? Hatukuwa na uhakika. Ingawa tulisherehekea ushindi wa kulipa deni la gari na pia mkopeshaji, bado tulihitaji gari, lakini vipi?

### Kutafuta Gari Mpya

Babangu alinipigia simu kuona jinsi tulivyokuwa tukiendelea na kutoa msaada wa kubadili gari letu lililoteketea. Baba alikuwa tajiri, na nilitumai kisiri-siri kwamba bila shaka angetununulia gari. Alipendekeza twende tukaangalie wauzaji fulani wa magari katika eneo hilo ili kununua gari zuri lililotumika. Bila shaka, nilikubali hilo kwa moyo wote.

Tulienda kwa wauzaji wa magari kadhaa, na nikapata gari nzuri aina ya Caravan Dodge. Lilikuwa limetumika kwa mwaka mmoja na lilikuwa katika hali nzuri sana. Nilimwambia babangu kwamba nilifikiri hili ndilo Drenda angetaka, gari la kifahari lenye rangi ya hudhurungi-nyekundu, nikitumaini kwamba angesema kitu kama, "Vema kabisa! Naam, twende tuiandikie hundi." Lakini hakusema hivyo. Badala yake, alisema, "Nitakupa mchango wangu wa $5,000 kwa ajili ya kuinunua." Ndio, kwa kweli hilo

lilikuwa toleo la ukarimu sana, lakini alikuwa akijitolea kugharamia malipo ya mwanzo, huku akiniacha nigharamie pesa zilizosalia.

Ghafla nilishtuliwa na ukweli uliokuwepo. Sikuwa na ukadiriaji wa mkopo ambao ungeshawishi benki yoyote kunikopesha pesa. Na hadi wakati huo, nilikuwa nimeweza kuficha hali yetu mbaya ya kifedha kutoka kwa babangu. Pili, nilihisi kutochukua madeni mengine.

Walakini, kwa kuwa sikuwa na chaguo lingine, nilifanya uamuzi wa haraka angalau kujaza fomu ya ombi la mkopo. Walakini, nilijua katika kufanya hivyo, ingenibidi kukiri hali yangu kwa babangu na angelazimika kutia saini. Nilimwambia babangu kuhusu hali yetu nzima bila kupenda, naye akajitolea kusaini mkopo, kisha tukauwasilisha. Muuzaji aliniambia wangenipa taarifa asubuhi iliyofuata.

Bila shaka, nilijua kwamba benki ingeidhinisha mkopo huo kwa vile babangu alikuwa na ukadiriaji mzuri wa mkopo. Nilipokuwa nikielekea nyumbani, kuidhinishwa kwa mkopo halikuwa jambo lililonisumbua. Nilijua sikutaka kuchukua mkopo huo, lakini nilikuwa na hitaji la kweli na sikuwa na pesa. Niliwaza nifanye nini? Nilichanganyikiwa na kufadhaika kidogo.

Nilipofika nyumbani na kumweleza Drenda hali ilivyokuwa, alijua pia hatukutaka kusaini fomu nyingine ya madeni, lakini tulikuwa na chaguo gani jingine? Sote wawili tulishindwa kulala usiku huo, lakini asubuhi tulikuwa na hakika kwamba kukopa pesa hakukuwa suluhisho letu.

Kwa hiyo nilimpigia babangu simu na kumshukuru kwa toleo lake, kisha nikamwambia hatungeweza kugharimikia deni la gari. Kisha nikampigia simu muuzaji wa gari na kumfahamisha kwamba hatungeenda huko kulichukua. Waliniambia, bila shaka, kwamba mkopo wa gari ulikuwa umeidhinishwa na lilikuwa safi na tayari kuchukuliwa. Niliwashukuru lakini nikasisitiza singeweza kuchukua gari.

Nilipokata simu, nilikuwa na amani, lakini wakati huohuo, sikujua jinsi tungeweza kununua gari kubwa la kutosha familia yetu yote ya watu sita. Nilikuwa na gari lingine aina ya coupe yenye viti vitano ambayo nilikuwa nikiendesha nilipokuwa nikienda kufanya biashara ambayo ingebidi tuitumie hadi tufikirie suluhu. Takriban majuma mawili yalipita, nasi tukaitumia gari hiyo yenye viti vitano, huku tukifanya safari mbili wakati tulipohitaji kufika mahali fulani.

Kisha siku moja, nilipokea simu kutoka kwa bwana mmoja kwamba alikuwa amekutana na Drenda miezi michache awali. Drenda alikuwa akitafuta vitu vichache vya kuuza katika mnada wa wazazi wake wa kuuza

vitu vya kale, ambao ulifanyika kila mwezi huko Atlanta, walipokuwa wakiishi. Walikuwa wakija Ohio mara moja kwa mwezi kununua vitu vya mnada wao, na Drenda alikuwa macho kwa kitu chochote alichofikiri kingewavutia wazazi wake. Kufanya hivyo kulileta kiasi kidogo cha pesa zaidi kila mwezi maana walimlipa Drenda kamisheni kwa chochote alichopata.

Alikuwa amekutana na mtu huyo mahali fulani, kisha wakaanza mazungumzo kuhusu kazi ya Drenda na kazi ya mtu huyo. Drenda alimwambia ikiwa angekuwa na kitu cha kuuza, huenda akapendezwa. Inavyoonekana, alikuwa na nyumba kubwa ya kuwatunzia wazee, na kila baada ya muda fulani, mgonjwa fulani angehitaji kufilisi mali yake alipohamia huko. Iwapo hakukuwa na wanafamilia wa kutunza vitu vya nyumbani ambavyo hawakuvihitaji tena, alikuwa akivihifadhi katika sehemu fulani ya ziada aliyokuwa nayo na hatimaye kuviuza.

Sikumfahamu, kwa hivyo alipopiga simu niliandika hilo na kumwambia Drenda. Ili kufupisha hadithi ndefu, Drenda alipompigia simu, mtu huyo alimwambia kwamba alikuwa na vyumba vitatu vya samani na vitu vya nyumbani ambavyo alihitaji kuondoa huko na kumuuliza kama angependezwa navyo. Alivitoa vyote kwa bei ya chini sana.

Mimi na Drenda tulienda kuona vitu hivyo, ingawa hatukuweza kupita vyumbani ili kuona kila kitu, maana vyumba vilikuwa vimesheheni sakafu hadi darini, tuliona vitu vichache ambavyo tulihisi kwamba ikiwa vingeuzwa vingefidia bei aliyowapa. Tuliwapigia simu wazazi wake, nao wakatutumia pesa, wakaleta lori lao, na kupeleka kila kitu huko Atlanta kwa mnada wao wa kila mwezi.

Mnada huo ulikuwa na mafanikio makubwa, na kama kamisheni yetu, walikubali kutupa gari lao aina ya Peugeot Station Wagon ambalo lilikuwa limetumika kwa miaka michache tu na lilikuwa katika hali nzuri sana. Sasa najua kwa watu wengi, kupata gari lililotumika kunaweza kusiwe sababu ya sherehe kubwa. Lakini wakati huo, hii ilikuwa mara yetu ya kwanza kuendesha gari lisilo na deni. Gari lilikuwa limepakwa rangi upya na lilionekana jipya kabisa. Tulifurahi sana.

Ghafla, nilianza kuona jambo. Ningeweza kumtumaini Mungu anisaidie na kile nilichohitaji bila deni.

## Mabadiliko ya Dhana

Tukio lingine nililokuwa nalo na Bwana mwaka mmoja awali, tulipokuwa tukiishi Oklahoma, sasa lilifanyika wazi zaidi kwangu.

Ninapotazama nyuma, ninaweza kuona kwamba Bwana alikuwa akijaribu kupata usikivu wangu, lakini tulikuwa na madeni mengi na chini ya shinikizo kubwa sana kiasi kwamba kwa sababu moja au nyingine, hatukuona kile ambacho Mungu alikuwa akijaribu kutufundisha.

Napenda kuwinda, hasa kulungu. Lakini pia napenda kula nyama ya kulungu na kuwa na matokeo ya kuonyesha juhudi zangu za kuwinda. Kwa miaka mingi ilikuwa kawaida kwangu kuwinda na kukosa kupata chochote cha kuonyesha kama matokeo ya jitihada zangu zote. Nilikuwa nikitoka, ninakaa kwa baridi, siku baada ya siku bila kumuona hata kulungu mmoja. Hili lilinikatisha tamaa kidogo maana nilikuwa na watoto waliohitaji chakula na hakika ningeweza kuwalisha na nyama ya kulungu. Ingawa hapo awali nilikuwa na kiasi cha mafanikio, miaka mingi ilikuwa imepita tangu niwe na msimu mzuri wa kuwinda kulungu na kupeleka nyama nyumbani.

Siku moja, nilipokuwa nikifikiria kuhusu msimu wa kulungu uliokuwa ukija, nilisikia sauti ya Bwana. Alisema, "Kwa nini usiniruhusu nikuonyeshe jinsi ya kumpata kulungu wako mwaka huu?" Hilo lilinishangaza. "Unionyeshe jinsi ya kumpata kulungu wangu?" Hiyo ina maana gani?

Nilipokuwa nikiomba kuhusu maneno haya, nilihisi Roho Mtakatifu akinisisitizia kutoa toleo la kifedha kama mbegu au karama kwa madhumuni hasa ya kuvuna kulungu. Hapo awali sikuwa nimewahi kutoa toleo la kifedha huku nikitarajia kuvuna kulungu, kwa hivyo mwanzoni nilihisi isivyo kawaida kidogo. Lakini nilihisi waziwazi kwamba Bwana alikuwa akiniongoza kutoa toleo hilo kwa maelekezo ya kina sana. Nilipaswa kuandika hundi ya kiasi nilichohisi kuongozwa kutoa. Ilitupasa mimi na Drenda tuweke mikono yetu juu ya hundi hiyo na kutangaza kuwa tumepokea kulungu wetu wa mwaka wa 1987 papo hapo, tulipoomba, wala sio baada ya kuvuna.

Ingawa sisi kama Wakristo, sikuzote tulitoa matoleo na kulitegemeza kanisa letu, kutoa kwa njia hii kwenye nia fulani na kuamini kwamba tumepokea tulipoomba lilikuwa jambo jipya kwangu.

Kwa hiyo nilichukua hundi na kuandika katika sehemu ya kumbukumbu, "Kwa kulungu wetu wa mwaka wa 1987." Mimi na Drenda tuliweka mikono yetu juu yake, kisha nikaituma kwa huduma ambayo nilikuwa na imani nayo, na kutangaza kwamba nilikuwa nimepokea kulungu wangu wakati nilipoituma. Nilichukua kipande cha karatasi na kuandika juu yake siku na wakati ambao niliamini kuwa nilimpokea

kulungu na kukiweka kwenye mfuko wangu wa koti langu la kuwinda.

Maana nilikuwa ninaishi katika mpaka wa jiji la Tulsa, Oklahoma wakati huo, kwa kweli sikuwa na mahali pa kuwinda, lakini rafiki yangu kutoka kanisani alinialika nyumbani kwa nyanyake mashambani wakati wa sherehe ya Kutoa Shukrani; na akasema kulikuwa na kulungu wachache karibu na shamba hilo.

Kwa hivyo asubuhi ya sherehe hiyo familia yangu ilielekea huko ili kufurahia siku kuu ya kula chakula na ushirika na sasa kumpata kulungu wangu. Rafiki yangu hakujua mahali nilipaswa kuelekea, lakini palikuwa na malisho yaliyokuwa yamepakana na pori kwenye mali hiyo, akanishauri nitoke nje niende malishoni na kukaa karibu na mti mkubwa uliokuwepo pale.

Sasa, nataka upate picha hii. Jua lilipoangaza mazingira yangu taratibu, niliona nimeketi katikati ya shamba lililokuwa limekatwa nyasi ambapo kulikuwa na mti mmoja mkubwa katikati yake. Nilihisi kwamba nilikuwa mahali pasipofaa kabisa maana nilijua kwamba hakuna kulungu timamu ambaye angejitokeza wakati niko mahali palipo wazi katika uwanja huo wa nyasi.

Nilikuwa karibu kuinuka ili kuelekea msitu ambao ulikuwa takribani yadi 130 mbele yangu, wakati nilisikia kitu kikisonga kwenye msitu kando ya uzio upande wangu wa kushoto. Nilisikia majani yakipepesuka kwa mbali, nikajua ni kulungu.

Ghafla, kulungu watatu wa kike walijitokeza huku wakitembea ndani ya msitu kando ya uzio. Niliwaona kidogo tu walipokuwa wakipita kwenye kichaka. Walikuwa mbali sana, lakini hilo lilinifanya nisimame na kungoja dakika chache kabla ya kuanza kuingia msituni mahali ambapo nilihisi kulungu walikuwa wakielekea. Kisha bila mimi kutarajia, kulungu dume alikuwa akikimbia kwenye uwanja nyuma yangu moja kwa moja kuelekea kwa mti wangu.

Nilikuwa nyuma ya mti ule huku dume kulungu akivuka shamba kuelekea upande wa pori lililokuwa mbele yangu, wala hakuniona. Fahamu alikimbilia ule mti, na aliponusa harufu yangu, alisimama akikoroma vikali, jambo ambalo lilinishtua. Nilipotazama upande wangu wa kulia ambapo sauti ile ya ghafla ilitoka, nilishtuka kuona dume kulungu mwenye pembe sita akinitazama kwa umbali wa takriban yadi tano tu. Papo hapo, dume huyo, ambaye sasa alitambua kilichokuwa kikiendelea, aliondoka mbio kuelekea msituni huku akirukaruka.

Sasa, kujaribu kukimbiza kulungu mwenye mkia mweupe ambaye

anakimbia kwa kasi huku ukiwa umelenga bunduki sio kitu rahisi, na nilijua kwamba ningeweza kufyatua risasi moja tu kabla hajaingia msituni. Singeweza kulenga shabaha kwa uangalifu kwa sababu kulungu alikuwa akiruka kwa hatua kubwa. Akiwa amebakiza yadi 20 tu kabla ya kulungu kufika porini, nilivuta kifyatulio cha bunduki. Risasi hiyo moja ilimwangusha huyo kulungu wala hakusonga. Nilishtuka! Je, hili kweli limetokea? Yote yalifanyika haraka sana! Nilinyanyuka taratibu na kuelekea pale ilipolala kulungu. Harakaharaka nilikitoa kile kipande cha karatasi kutoka kwa mfuko wa koti kisha nikaanza kumshukuru Mungu kwa kunipa kulungu wangu.

Aliposikia mlio wa bunduki, rafiki yangu alitoka na kunipongeza kwa kumpata kulungu wangu maana alimwona akiwa pale. Sikuwa nimemwambia rafiki yangu kuhusu kile ambacho Bwana alikuwa ameniambia, lakini nilimtazama na kusema, “Sidhani kumpata kulungu huyu kulitokana na uwezo wangu mkuu wa kuwinda.” Kisha nikamuonyesha kile kipande cha karatasi nilichokiandika siku ambayo mimi na Drenda tuliomba kuhusu kulungu. Kilisema, “Ninaamini kwamba nimepokea kulungu wangu wa mwaka wa 1987 katika tarehe ya leo ambapo nimeomba katika jina la Yesu.” Niliinua kikaratasi hicho ili rafiki yangu aweze kukiona kisha nikaanza kumwambia kuhusu yale ambayo Bwana alikuwa ameniambia nifanye.



Tukio hili lilivutia umakini wangu. Nilijua bila shaka lilitoka kwa Mungu. Lakini kwa sababu moja au nyingine, bado sikuwa nimeunganisha nukta. Bado sikuwa nimeona jinsi dhana ya sheria ya Ufalme na kile kilichotokea na kulungu kilivyobadili fedha zangu. Kumpata yule kulungu lilikuwa jambo la kushangaza, lakini je, hilo lingetokea tena? Bila dhana ya sheria ya Ufalme, singejua ni jinsi gani au ni sheria gani zilizosababisha kulungu kujitokeza. Lakini nilitazamia kujaribu tena katika msimu wa kulungu uliofuata.

**TUKIO HILI LILIVUTIA UMAKINI WANGU. NILIJUA BILA SHAKA LILITOKA KWA MUNGU.**

**Imani Hufanya Kazi Kila Wakati**

Msimu wa kulungu uliofuata ulileta mabadiliko maana tulihamia Ohio kutoka Tulsa. Hatua hii ilichochewa siku moja tulipokuwa tukifanya zoezi la kukimbia. Roho Mtakatifu alinena nami kwamba ulikuwa wakati wetu wa kuhamia nyumbani Ohio, na huko ningefanya kazi yangu ya mwisho.

Wakati huo nilikuwa nimeishi Tulsa kwa miaka kumi, na nilipapenda, lakini nilifurahishwa zaidi na matarajio ya kuondoka. Mgogoro wa mafuta uliokumba Tulsa mwaka mmoja awali uliikumba sana kwa sababu msingi wa uchumi wake ulikuwa wa mafuta. Tulikuwa katika hali mbaya kifedha, na tulijikuta tukipata riziki kwa shida. Mwanzo mpya ulikuwa kitu nilichofurahishwa nacho. Sikujua kwamba miaka tisa iliyofuata ingeleta mafadhaiko zaidi kifedha ambayo yangepita kwa mbali yale tuliyoyaona huko Tulsa.

Tulihamia Ohio mwanzoni mwa msimu wa kiangazi, na nilitazamia kwa hamu yale ambayo Ohio ilikuwa imetuandalia. Tuligundua haraka sana kwamba kuzindua biashara yetu tena huku tukiwa na madeni yetu yote kulikuwa na shinikizo kubwa sana.

Bila shaka, msimu wa kulungu ulikuwa unakuja pamoja na kuzaliwa kwa mtoto wetu wa tatu, Tom. Tom alizaliwa siku ya pili ya msimu wa kulungu wa Ohio, kwa hivyo ni wazi, sikuwa na wakati wa kuchunguza mahali popote maana mtoto alikuwa karibu kuzaliwa na nilihitaji kuanzisha biashara tena. Nilijua sehemu moja tu ya kuwinda.

Upande ule mwingine wa barabara kutoka kwa nyumba niliyolelewa, nilikuwa nimeweka mfululizo wa mitego nilipokuwa katika shule ya upili. Shamba la wazazi wangu lilikuwa na kidimbwi kilichoingiwa na maji kutoka kwa kijito kidogo kilichopita kwenye shamba la jirani. Lazima nikubali

kwamba ingawa nilipita kando ya kijito hicho kwa miaka mingi nilipokuwa nikikua, sikuwa nimewahi kuona kulungu au hata nyayo moja ya mguu wa kulungu kwenye ardhi hiyo. Lakini nakumbuka nilipokuwa chuoni nilipigiwa simu na ndugu yangu ambaye aliniambia jinsi alivyoshtuka kumuona kulungu huko siku moja na kwamba alikuwa amepanga kuwinda huko katika msimu wa vuli uliofuata. Sote tulishangaa. Niliweka mazungumzo hayo akilini mwangu, jambo ambalo tulikuwa tumefanya miaka tisa au kumi awali.

Nilikumbuka sehemu haswa aliyosema alimuona kulungu, maana nilikuwa ninakifahamu sana kijito hicho. Alisema alikuwa amemwona kulungu mahali ambapo mkondo wa maji uligawanyika na mti mkubwa sana wa mikoko ulikuwa. Kisha akaniambia kwamba kulikuwa na mti mdogo sana wa mipororo karibu na ule mti mkubwa, na kwamba angeweza kutumia mti ule mdogo kupanda juu ya mti huo mkubwa, ambao alifikiri ungekuwa mahali pazuri pa kuwinda kulungu.

Kweli, ndugu yangu hakuwa amewahi kumuua kulungu karibu na kijito hicho, ingawa alisema alikuwa amemkosa kulungu mara moja. Lakini pia hakuwa amerudi huko kwa miaka mingi, kwa hiyo sikujua kama mti ulikuwa bado upo au kama ningeweza kuupata gizani asubuhi ya kuwinda kama nilivyokuwa nimepanga.

Jambo lililofanya mambo kutokuwa rahisi ni kwamba Ohio ilikuwa na sheria ambayo haikuruhusu watu kutumia silaha yoyote nyingine kuwinda ila bunduki ndogo pekee. Bunduki ndefu hazikuruhusiwa hata kidogo wakati wa msimu wa kulungu, ni aina fulani ya kipande kidogo cha chuma nzito tu cha kumpiga kulungu kilichoruhusiwa kufyatuliwa kutoka kwa bunduki hiyo ndogo. Nilikuwa na bunduki ndogo yenye sehemu mbili za kuweka risasi wakati huo na sikuwa na imani ningeweza kumpiga kulungu nayo isipokuwa nikiwa katika umbali wa yadi 20. Lakini hiyo tu ndiyo niliyokuwa nayo wakati huo, na huo ndio uliokuwa mpango wangu.

Mimi na Drenda tulitoa toleo letu, tukaweka mikono yetu juu ya hundi ile jinsi tulivyofanya mwaka uliopita, kisha tukadai kwamba tulikuwa na kulungu wetu kulingana na Marko 11:24. Ili kufupisha hadithi ndefu, katika siku ya nne ya msimu wa bunduki ndogo wa Ohio, siku yangu ya kwanza kwenda kuwinda, nilimuua kulungu wa kike na wa kiume katika dakika 40, wote wawili nikiwa umbali wa yadi 75, jambo ambalo lilikuwa nje ya uwezo wangu unapolinganisha na ile bunduki ndogo niliyokuwa nayo. Ohio iliruhusu watu kuua kulungu wawili tu wakati huo, ndiyo sababu niliua kulungu wawili mwaka huo. Hiyo ni kweli, nilikuwa na

kulungu wangu wawili baada ya dakika 40.

Tena, nilitambua kwamba nilikuwa nimepata ufahamu fulani. Lakini wakati huo hali yetu ya kifedha ilikuwa mbaya sana, na matatizo yalikuwa mengi sana. Kwa kweli sikufikiria kutumia kanuni hii hii kwa fedha zetu.

**"Matukio Mengi Sana Yenye Upatanifu"**

Msimu huo kwanza wa baridi na miezi 12 iliyofuata huko Ohio ilikuwa ya kutisha nilipopambana na matatizo makubwa ya kihisia-moyo, mshtuko wa hofu, na mshuko wa moyo, kama nilivyoshiriki katika utangulizi wa kitabu hiki.

Ilikuwa Novemba iliyofuata, kabla ya msimu wa kulungu, ambapo gari letu liliteketezwa na moto. Ingawa nilikuwa nimepata mavuno ya ajabu ya kulungu katika misimu miwili ya kulungu iliyotangulia, bado sikuwa na ufunuo kuhusu Ufalme. Kuteketea kwa gari na Mungu kunena nami juu ya Ufalme, yote yalinifanya nitambue kwamba kulikuwa na mengi zaidi kuhusu matukio haya kuliko nilivyofikiria mwanzoni. Nilitiwa moyo sana, lakini hata wakati huo, sikujua sheria ya Ufalme.

**KWA KWELI, MUNGU HUTUMIA CHOCHOTE KUPATA UMAKINI WAKO.**

Msimu uliofuata wa kulungu ulikuja, na nilimuua kulungu wangu katika dakika 40 tena, ni kama nilikuwa nimewekewa saa. Tulianza kuona Ufalme ukifanya kazi katika fedha zetu pia, jambo ambalo nitazungumzia katika sura ya 2. Lakini katika miaka hiyo ya mwanzoni, nilikuwa nikiona mambo fulani ya ajabu.

Bila shaka, kila mara nilipoenda kuwinda kulungu ilionekana kwamba Mungu alikuwa akinifundisha jambo jipya. Nafikiri sababu ni kwa sababu msimu wa kulungu unahusu mavuno, na hutokea kwa muda uliodhibitiwa na mfupi sana. Msimu wa kutumia bunduki ndogo huko Ohio kawaida hufunguliwa kwa majuma mawili tu. Ukiwa katika msimu wa mavuno mfupi hivyo, kamwe hutaki kupoteza wakati. Wawindaji wengi wa kulungu huwa makini sana na wenye kusudi wanapoelekea msimu huo. Wengi hutumia masaa mengi kukusanya taarifa na kujiandaa kwa fursa hiyo ya majuma mawili. Kwa hivyo hii inakuwa maabara nzuri ya kujifunza kuhusu Ufalme.

Samahani kwa hadithi zote za kuwinda kulungu, lakini zilikuwa muhimu sana kwangu. Zilifichua sheria zilizofichwa ambazo nisingezijua

vinginevyo. Kwa kweli, Mungu hutumia chochote kupata umakini wako. Alitumia uvuvi kuvutia umakini wa Petro, Yakobo, na Yohana katika Luka sura ya tano walipovua samaki wengi sana mashua zao zilikuwa karibu kuzama. Ilikuwa tu kwamba kwangu alitumia uwindaji wa kulungu.

Baada ya Mungu kunena nami juu ya Ufalme katika chumba changu cha kulala siku ile, na baada ya kuona gari letu likiteketea na kukumbuka uwindaji wangu wa kulungu, na kisha jinsi Mungu alivyotufungulia mlango wa kupata lile gari kubwa bila deni, ghafla, niliona tulikuwa tumeelewa jambo. Mimi na Drenda tulijitoa kulifuatilia.

Nilianza kusoma Biblia kwa njia mpya kabisa. Nilijiita mwanasayansi wa kiroho. Nilianza kuuliza maswali. "Kwa nini hili lilitokea hivi? Kwa nini halikutokea?" Nilikuwa nikitazama kwa ukaribu dalili za msingi wa sheria za kiroho katika hadithi nilizokuwa nikisoma katika Biblia.

Mungu aliendelea kunionyesha mambo; na tena, alitumia uwindaji wa kulungu kunionyesha mengi zaidi kuhusu Ufalme. Hadithi hii inayofuata ilivutia umakini wangu sana. Lilikuwa moja ya matukio ya nyakati tuliposema, "Je, uliona hilo?"

Ilikuwa jioni siku ya sherehe ya Halloween, na familia yetu ilikuwa na kama dakika 45 kabla ya kuelekea kanisani kuhudhuria karamu tuliyokuwa nayo kama njia mbadala ya sherehe ya kidesturi ambayo huchochewa na mashetani.

Majuma mawili awali Mimi na Drenda tulikuwa tumetoa toleo letu kwa ajili ya kulungu dume mmoja, tukaweka mikono juu ya hundi hiyo, tukaituma kwa huduma tuliyoamini kwamba Mungu alituonyesha, na kutangaza kwamba hilo limetimia kulingana na Marko 11:24. Hiyo ilikuwa mara yangu ya kwanza kwenda kuwinda katika msimu huo, na nilikuwa nikitumia upinde kuwinda katika shamba tulilokuwa tumekodisha.

Ingawa sikuwa na muda, kwa kuwa Mungu alikuwa ameniambia jinsi ya kuwinda kwa imani, kwa kawaida ningempata kulungu wangu katika dakika 40, kwa hiyo nilihisi ningekuwa na muda mchache lakini nilikuwa na wakati wa kupata kulungu wangu. Siku hii mahususi, nilipanda mti uliokuwa nyuma ya miti ya misonobari ambayo ilikuwa nyuma ya nyumba yetu nzee kule mashambani. Sikuwa pale kwa zaidi ya dakika 10 nilipomwona kulungu dume ambaye alikuwa umbali wa yadi 200 akielekea kwenye msitu wa jirani yangu. Nilijua kwamba huyo alikuwa kulungu wangu, lakini alikuwa akielekea njia nyingine!

Huu ulikuwa mwaka wangu wa pili tu kuwinda nikitumia upinde, na kwa kweli sikujua mengi juu yake. Sikuwa nimevaa mavazi ya kujificha,

sikuwa na kifaa kinachotoa sauti ya mguno ili kuita kulungu, wala sikuwa nimesikia kuhusu kutumia manukato ili kuvutia kulungu. Kisimamo changu pale mtini kilikuwa ubao ambao nilikuwa nimeupigilia misumari kati ya mashina mawili ya mti umbali wa futi 12 kutoka ardhini, ambao ikiwa unajua chochote kuhusu kuwinda na upinde kutoka kwa mti, kwa kweli haukuwa juu vya kutosha. Lakini mwaka uliotangulia, mwaka wangu wa kwanza wa kuwinda na upinde, nilivuna kulungu wawili mara mbili nilipoenda kuwinda kwa imani, na sikutarajia chochote tofauti mwaka huu.

Nilipomtazama yule kulungu dume akielekea upande usiofaa, sikujua la kufanya, kwa hiyo nikaanza kuomba. Ghafla, nilimsikia Roho Mtakatifu akizungumza nami. Akasema, "Mwambie huyo dume aje kwako." Nilishtushwa kidogo na hilo. Mwambie kulungu aje kwangu? Nilijua singeweza kupiga kelele kwa nguvu, kwa hiyo nilinena kwa sauti ya kawaida, "Kulungu, simama! Geuka, njoo usimame chini ya mti wangu." Jambo la kichaa, sivyo? Sikuwa na kifaa cha kuguna, sikuwa na chochote. Lakini mara ya pili niliposema hivyo, kulungu alisimama, akatazama pande zote mbili, kisha akageuka na kuanza kutembea yadi 200 kuelekea kwangu. Ingawa msitu niliokuwemo ulikuwa na upana wa takriban yadi 400, dume huyo alitembea moja kwa moja hadi kwenye mti wangu, akatembea moja kwa moja chini yake, kisha akasimama tuli.

Bila shaka, singekosa kumpiga risasi. Ajabu! Je, nilikuwa nimeliona hilo? Kulungu alianguka chini yangu na risasi safi. Niliangalia saa yangu ya mkononi na kutambua ikiwa nilitaka kufikia sherehe ingekuwa bora nimuache yule kulungu pale mpaka nirudi na kumpeleka ghalani. Inanibidi nikubali kwamba nilifikiria juu ya kile nilichoona kwa wiki kadhaa baada ya hapo. Lakini Mungu hakuwa amemaliza kupata umakini wangu.

Shamba tulilokuwa tumekodisha lilikuwa na kijito kilichopita ndani yake chenye nyasi nyingi kando yake. Kila wakati tulifaulu katika uwindaji wa sungura. Siku hiyo mahususi, theluji iliyoanguka usiku ilifanya iwe rahisi kuwaona sungura. Singeweza kujizuia, kwa hiyo mimi na mwanangu Tim tulianza kuteremka kuelekea kwa kijito, huku tukipiga teke mirundo ile ya nyasi, na ghafula, ndege dume anayefanana kuku aliruka kutoka kwa nyasi.

Ohio ilikuwa na msimu wa kuwinda ndege hawa, ingawa kamwe sikuwa nimewaona katika shamba letu, labda moja kwa mwaka. Naam, huyu alipokuwa akitoroka, nilifurahi sana kumpiga risasi. Nilipompiga, ndege huyo alianguka chini lakini akaanza mbio. Mara moja nilijua nilichokuwa nimefanya. Nilikuwa nimepiga bawa lake. Ndege huyo alikuwa akikimbia

kutoka kwa kijito kuelekea juu ya kilima kwa nguvu zake zote, na huyo ndege dume anaweza kukimbia hadi kasi ya maili 35 kwa saa. Bila shaka, kwa sababu ya theluji, hakuwa akienda haraka sana, lakini alikuwa akienda haraka.

Kwa kuwa kijito kilikuwa chini ya bonde refu, niliona kikamilifu kila sehemu ya kilima hicho. Kilikuwa kimetumiwa kupanda nyasi mwaka mmoja awali, kwa hiyo kilikuwa tambarare huku nyasi zikiwa hapa na pale.

Maana ndege huyo alikuwa akikimbia kwenda kwa kilima hicho kwa kasi, nilijua singeweza kumkamata, na bunduki yangu haingefyatua risasi hadi hapo. Lakini ghafla, nilikumbuka dume kulungu, jinsi alivyojileta kwangu niliponena. Kwa hivyo nilisema kwa sauti kubwa, "Ndege, SIMAMA!" Papo hapo niliposema hivyo, yule ndege alitoweka. Kilima chote ambacho kilikuwa kimefunikwa na theluji na nyasi zilizoonekana juu ya theluji hapa na pale, kilikuwa wazi kwangu, lakini ndege huyo alikuwa ametoweka. Tim akapaza sauti, "Alienda wapi, Baba?" "Sijui," nikajibu.

Kwa hiyo tulianza kufuata nyayo zake kwenda juu ya kilima, na hapo ndipo alikuwa ameketi na kichwa chake kidogo kuingizwa ndani ya theluji. Nikawaza, "Je, nilimpiga kisha akakimbia mpaka ikafa?" Niliinama chini na kumshika ndege, naye akaanza kupiga kelele kingi, huku akipigapiga mabawa yake, ndege wazimu. Alikuwa hai kikamilifu! Usiku huo nilipomchinja yule ndege, nilimtazama kwa makini sana. Hakuwa na alama zozote za kupigwa, bali niliona mahali nilipomkata kidogo kwa bawa la kulia. Kwa hiyo ndege huyo alikuwa hai kabisa lakini alisimama sekunde ileile niliposema kwa sauti, "Simama!"

Ndio, Bwana, una usikivu wangu kamili!

SURA YA 2

# NJIA MPYA YA KUFIKIRI

Mimi na Drenda tulipoanza kuona Ufalme ukitenda kazi maishani mwetu, hatukuwa na uwezo wa kuacha kuwaambia watu kuuhusu. Tulifahamu kwamba tulikuwa katika safari ya kusisimua ya ugunduzi na ukombozi. Bado nilikuwa nikiuza bima na dhamana, lakini nilihisi kulikuwa na mabadiliko fulani. Sikujua ni nini, lakini nilifahamu kwamba lazima kulikuwa na suluhisho kuhusu fedha zangu kama vile nilivyoona katika uwindaji wa kulungu na jinsi nilivyopata lile gari kubwa. Nilifahamu nilihitaji zaidi ya umiliki wa gari kubwa tu, ingawa hakika nilifurahi kuwa nalo.

Bado nilikuwa na madeni mengi wakati huo. Nilitaka kutoka kwa madeni lakini sikujua nilichohitaji kubadili. Ingawa sikujua nibadilishe nini, nilikuwa na uhakika kwamba ningegundua. Nilijua kwamba nilikuwa nimepata jibu langu, lakini nilihitaji kujifunza zaidi kuhusu jinsi ya kuona yale yaliyotokea kwa Biblia katika maisha yangu. Biashara yangu ilivyokuwa wakati huo, haikuwa ikitosheleza mahitaji yetu maishani. Lakini ilikuwa afadhali zaidi kuliko ilivyokuwa awali tulipokuwa tukiingia kwa madeni zaidi kila mwezi.

Mimi na Drenda tuliendelea kusoma Biblia na kutafuta vidokezo zaidi kuhusu utendaji wa Ufalme. Tulitoa matoleo yetu kwa ajili ya fedha tulizohitaji pia.

Kisha usiku mmoja, niliota ndoto. Katika ndoto, niliona kiwavi akitambaa polepole juu ya bua la mmea. Kisha akatambaa juu ya shina na kusuka koko. Ghafla, kipepeo cha kupendeza kikatoka kwenye kifukofuko

hicho, na kikaruka. Ndipo sauti ikasema, "Hivyo ndivyo biashara yako itakavyokuwa."

Niliamka na kuelewa maana ya ndoto hiyo. Kiwavi ana uwezo wa kutambaa tu na ana finyu sana katika jinsi anavyoishi maisha yake, kwa kawaida huishi kwenye mmea mmoja maisha yake yote. Lakini mabadiliko huja ambayo hubadilisha uwezo na maisha yote ya kiwavi huyo. Anajigeuza kuwa kipepeo, jambo ambalo linamruhusu kuruka popote anapotaka kwenda. Baadhi yao, kama yule anayeitwa Monarch kwa lugha ya kimombo, wanaweza kuruka maelfu ya maili ili kuepuka miezi ya baridi katika maeneo ya kaskazini. Ingawa wakati wa ndoto hiyo sikujua jinsi mabadiliko hayo yangetokea, nilijua kwamba Mungu alikuwa akinionyesha kwamba yangetokea. Nilitiwa moyo.

## Ugunduzi wa Kushangaza

Kama ilivyokuwa kawaida yangu tangu niliporudi Ohio, nilikuwa nikipiga simu 90 kila asubuhi. Natamani ningekuambia nilikuwa na mfumo mzuri wa kufanya hivi, lakini kusema kweli, nilipitia kitabu cha simu kila siku (hii ilikuwa kabla ya serikali kuanzisha mfumo wa kuruhusu watu kudhibiti idadi ya simu za uuzaji walizopokea kwa kusajili nambari zao za simu).

Kwa kuwa nilikuwa makamu wa rais wa mkoa katika kampuni niliyoifanyia kazi, kazi yangu kuu ilikuwa kuajiri na kutoa mafunzo kwa wawakilishi wapya wa mauzo. Nilikuwa nikipiga simu na kusema kwamba kampuni yangu ilikuwa ikipanuka hapo Ohio, na nilikuwa nauliza ikiwa walifahamu mtu yeyote ambaye labda angependelea hilo. Mara nyingi, nilijibiwa na mashine na ningeacha ujumbe. Ikiwa walipendelea hilo, wangenipigia simu. Kwa kupiga simu 90 kila siku, nilitarajia kuhoji watu wawili au watatu na labda kuuzia mtu mmoja.

Ni kupitia kwa mchakato huu ambapo nilikutana na Dave. Katika kuzungumza naye kwa simu, alieleza nia yake ya kutafuta kazi mpya na kwamba angependezwa kuona kile nilichokuwa nacho. Nilijitolea kwenda nyumbani kwake jioni hiyo, naye akasema ingekuwa sawa. Nilipoketi naye na mke wake, nilianza kuuliza maswali yote ya kawaida kuhusu mahali alipokuwa akifanya kazi wakati huo, kwa nini alitaka mabadiliko kikazi, na hali yao ya kifedha. Kwa kawaida kila mara ningewauliza wafanyi kazi watarajiwa kuhusu fedha zao za kibinafsi kwa sababu ikiwa, kwa kweli, wangeamua kwamba hawakutaka kazi katika kampuni, basi ningeshughulikia hilo kama uwezekano wa kuuza. Kwa hivyo kukusanya taarifa zao za kifedha

kulinipa fursa ya kujua ni kiasi gani cha bima walichopaswa kuzingatia na kuona ni bidhaa gani zingine za bima walizokuwa nazo.

Kwa mshangao wangu, tulipokuwa tukijadili hali yao ya kifedha, mke alianza kulia huku akiwa amekata tamaa. Fedha zao zilikuwa katika hali mbaya sana, na hawakujua wafanye nini au wabadilishe nini. Niligundua kwamba shida yao haikuhusu bima. Walihitaji kuongeza pesa zao na kuondoka kwa madeni, kwa hiyo nilitaja pia Ufalme wa Mungu na jinsi mimi na Drenda tulivyokuwa tukijifunza kuhusu utendaji wake. Niliwahakikishia kwamba ningefanya kila niwezalo kuwasaidia na kwamba ningekutana nao tena baada ya wiki moja ili kujadili mabadiliko yoyote ambayo wangehitaji kutekeleza.

Nikiwa njiani kuelekea ofisini baada ya kukutana nao, nilikuwa na wasiwasi. Lazima kungekuwa na kitu ambacho ningeweza kufanya!

Niliporudi ofisini, nilikaa kwenye meza yangu na ghafla nikapata wazo. Ningefanya utafiti kuhusu aina kadhaa za bidhaa au huduma walizokuwa nazo kwa matumaini ya kupata zilezile lakini kwa bei ya chini. Lengo langu lilikuwa ni kuona ni kiasi gani cha pesa ningeweza kuokoa ambacho wangeweza kutumia kupunguza madeni. Wakati huo hakukuwa na Mtandao, kwa hivyo ilinibidi nitafute katika kurasa za manjano za saraka ya simu na kupiga simu.

Baada ya wiki moja, nilikuwa nimekagua bei ya kila bidhaa au huduma waliyokuwa nayo na kwa kweli nilishangazwa sana na kile nilichogundua. Nilipopanga upya au kubadili wachuuzi waliokuwa nao na kutumia makampuni ambayo hayakuwa ghali, niliwaokolea zaidi ya $600 kila mwezi. Nilichukua kikokotoo changu cha fedha na kugawa fedha hizo katika madeni waliyokuwa nayo kisha nikabofya kitufe cha kikokotoo.

Hesabu zilipoonekana kwenye skrini ya kikokotoo, niliketi pale nikiwa nimepigwa na butwaa. Hesabu yangu ilionyesha kuwa wanandoa hawa wangeweza kutoka kwa madeni kabisa katika chini ya miaka saba, likiwemo deni la rehani yao ya nyumba, bila kubadili mapato yao. *Haiwezekani*, niliwaza. Hakika, nilikuwa nimefanya makosa mahali fulani. Kwa hivyo nilipiga hesabu tena na nikapata matokeo yaleyale.

Kisha nilienda kwenye droo yangu ya faili na kuvuta faili chache za wateja wangu wengine na kuwafanyia hesabu hiyohiyo juma hilo. Kama mteja wangu huyu, kila mmoja wao angeweza kutoka kwa madeni kabisa kati ya miaka mitano hadi saba, pamoja na rehani yao, bila kubadili mapato yao. Ikiwa hii iliwezekana, na sasa nilijua ingewezekana, kwa nini hakukuwa na mtu ambaye alikuwa akitangaza kuhusu hili kila mahali? Nilimwandikia

mteja wangu taarifa iliyomwonyesha jinsi wangeweza kutoka kwa madeni katika chini ya miaka saba. Nilifurahi sana kukutana nao na kuwaonyesha kile nilichokuwa nimegundua, na nilikuwa na hamu ya kujua jinsi wangepokea habari hiyo.

Nilipoketi pamoja na Dave na mkewe, nilipitia hesabu moja baada ya nyingine nikiwaeleza jinsi pesa zingeweza kuokolewa. Nilificha matokeo ya mwisho kimakusudi hadi nilipokuwa nimewaonyesha kila kitu ambacho kingeweza kuokoa pesa. Wakati huo wote, wateja wangu waliketi pale wakiwa wamepigwa na mshtuko. Kwa mtazamo wao, hakukuwa na pesa na hawakuwa na njia ya kutoka kwa madeni—kamwe! Nilipofungua ukurasa wa mwisho na kufichua kwamba wangeweza kuwa huru katika muda usiozidi miaka saba, ikiwemo rehani ya nyumba yao, ghafla, mume aliruka juu huku machozi yakimtoka. Alisisimka sana. Wote wawili sasa waliangua kilio na kunishukuru tena na tena kwa kuja nyumbani kwao. Kisha nilichukua muda kuwaeleza yote ambayo Mungu alikuwa amenifunulia na yale niliyokuwa nimejifunza kufikia wakati huo kuhusu Ufalme wa Mungu. Wote walitega masikio!

Sikupata hata senti moja kutoka kwa mteja huyo, lakini nilifurahia zaidi kuweza kupata mteja; na sasa akili yangu ilikuwa ikizunguka maili milioni kwa saa. Nilitaka kumfanyia kila mteja niliyemwona hivyohivyo, na nilimwomba Bwana hekima juu ya jinsi ya kuchuma mapato kwa kufanya hivyo. Nilijua huu ungekuwa mfumo wangu mpya wa biashara ikiwa ningeweza kujua jinsi ya kupata pesa kwa kufanya hilo. Baada ya majaribio na hitilafu kadhaa, tulipata njia ya kutoa mpango wetu bila malipo kwa mtu yeyote ambaye aliuliza na pia kupata pesa kwa biashara yetu kupitia kwa mfumo wa rufaa tuliounda. Mpango huu ulikuwa mzuri sana kupita kiasi, na mimi na Drenda tulifurahi sana.

Nilijua haya ndiyo mabadiliko niliyokuwa nimeona kwenye ndoto. Ingawa nilijua tulikuwa tu kwenye hatua ya kifukofuko katika ndoto yetu, nilikuwa tayari kuruka! Bado kulikuwa na mengi niliyopaswa kujifunza ili kuruka, lakini nilifahamu nilikuwa katika njia sahihi.

Tuliijumuisha kampuni yetu mpya na kuiita *Faith-Full Family Finances* kwa sababu tulifahamu kwamba ukiwa na imani, fedha zako zingeendelea kuwa kamili; na huo ndio ujumbe tuliotaka kuwasilisha, hata zaidi ya suluhu ya kifedha tuliyoitoa. Tulihifadhi jina hilo kwa zaidi ya miaka 20 lakini kwa maana lilikuwa la Kikristo, na tulitaka kufikia watu wengi zaidi wasioamini, tuliamua kubadili jina letu kuwa Forward Financial Group, ambalo lipo hadi leo. (Kumbuka, tungali tunatoa mpango uleule wa kutoka kwa madeni bila

malipo na pia huwa tunasaidia watu kuepuka hatari ya soko katika akaunti zao za kustaafu. Unaweza kufikia Forward Financial Group kwa nambari 1-(800)-815-0818 au mtandaoni katika Forwardfinancialgroup. com.)

Ingawa bado tulikuwa na madeni mengi tulipozindua kampuni yetu, tulijua katika njia sahihi. Kampuni yetu ilifanikiwa sana, na mimi na Drenda tulitoka kwa madeni katika muda wa takriban miaka miwili na nusu. Siwezi kukueleza jinsi hilo lilivyosisimua! Ghafla, maisha yetu hayakuwa katika hali ya unusuru tena, na maono yalianza kuibuka ndani yetu.

Kulipia gari jipya pesa taslimu lilikuwa jambo la kupendeza. Kununua na kulipia pesa taslimu ekari 55 za ardhi nzuri sana hapo Ohio kulitustaajabisha. Kujenga nyumba ya ndoto yetu ya futi za mraba 7,700 na kuilipia lilikuwa jambo la kushangaza zaidi! Sitasahau mimi na Drenda tuliposimama na kutazama wakati msingi wa ghorofa ya chini ya nyumba yetu mpya ilikuwa ikichimbwa. Chumba hicho cha chini kilikuwa kikubwa kuliko nyumba ile ndogo nzima ya mashambani ambapo tuliishi. Sote tulisimama pale huku machozi yakitiririka nyusoni mwetu tulipotazama hilo. Tulipoona mwisho wa miaka tisa ya kuwa katika hali mbaya sana Duniani na kuwa na ufahamu kwamba mambo sasa yalikuwa yamebadilika, tulifahamu tulikuwa tumegundua kuhusu Ufalme wa Mungu, na kuelewa kwa nini uliitwa habari njema na nabii Isaya.

> *Roho ya Bwana MUNGU i juu Yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema.*
>
> — Isaya 61:1

Kusema kweli, mimi na Drenda tulipigwa na butwaa tena na tena kwa sababu ya mambo makubwa sana yaliyokuwa yakitokea. Kutoka kwa madeni kabisa wakati mmoja ilikuwa ndoto isiyowezekana, lakini sasa ilikuwa ukweli!

Sikiliza, mimi si mzuri hivyo! Umeona utendaji wangu wa awali. Nilijaribu kufaulu kwa njia yangu binafsi kwa miaka mingi na nilifanya kazi kwa bidii bila chochote ila kuumia moyoni na shinikizo. Nilikuwa nikijifunza jinsi ya kuishi maisha kupitia kwa njia ya Kiungu, na hilo lilikuwa likifanya kazi vyema. Na ndio maana unasoma kitabu hiki, ili kujua nilichogundua, na bila shaka utajua. Lakini kwanza lazima utambue kwamba nilikuwa nimeingia mfumo mpya, Ufalme mpya, na njia mpya kabisa ya kuishi maisha. Hili ndilo jibu lako pia. Hili ndilo jibu unalohitaji. Hii ndio habari njema ambayo umekuwa ukingojea. Najua, najua, kanisa

lako halifundishi mambo haya. Naam, langu pia halikufanya hivyo, lakini yote yamo humo humo ndani ya Biblia.

## Mungu Ni Mwema—Sikuzote

Basi ngoja nikupe jambo muhimu ili kuelewa ninachosema—tupilia mbali dini! Hili si suala la kidini. Ni kuhusu Mungu, kile anachotaka uwe nacho, na jinsi alivyolipa gharama kupitia Yesu ili kukupa Ufalme. Kwa hiyo, hebu tuchimbue Ufalme huo na tuone jinsi unavyofanya kazi.

Mimi na Drenda tulipoanza kuona Ufalme wa Mungu ukitenda kazi maishani mwetu, mara nyingi, tulishtushwa na kile tulichoona. Tuligundua kwamba waumini wengi hawakujua jinsi unavyotenda kazi.

Kwa mfano, hivi karibuni nilisoma kichwa cha habari kuhusu binti wa umri wa miaka saba ambaye alikufa alipokuwa akifanyiwa upasuaji wa kifuko cha koo. Ingawa huu ni upasuaji wa kawaida na kwa kawaida ni salama sana, moyo wake ulisimama, na kukawa na matokeo ya kuhuzunisha sana. Nafikiri mioyo yetu sote iliumia kidogo tuliposikia kwamba hilo lilifanyika. Walakini, ingawa tukio hili lilikuwa la kusikitisha, kulikuwa na sehemu nyingine ya hadithi ambayo itaathiri familia hii maisha yao yote. Hebu ninukuu kile baba alichomwambia mwandishi.

> "Huwezi kuelewa kwa nini mambo haya hutokea, lakini tunajua ulikuwa ni mpango wa Mungu. Na hilo ndilo jambo pekee linaloweza kutuvusha, kwa sababu tunajua ilikuwa ni Mungu."

Acha nimnukuu mchezaji Aaron Rodgers wa timu ya Green Bay Packers, ambaye hadithi yake ilikuwa katika jarida la *People* mnamo Januari 22, 2020.

> Rodgers alieleza kuwa alitilia shaka dini akiwa mtoto na tangu wakati huo amekuwa akihusiana na mambo ya "kiroho kwa njia tofauti" kadri anavyozidi kuwa mkubwa. "Watu wengi niliowajua, kanisa lilikuwa ... lazima uende." Pia alisema, "Sijui jinsi unavyoweza kumwamini Mungu anayetaka kuhukumu karibu dunia nzima kwenye moto wa jehanamu. Ni kiumbe wa aina gani mwenye upendo, nyeti, aliye kila mahali, na mwenye uwezo wote anayetaka kuhukumu uumbaji wake mzuri kwenda kwa jehanamu ya moto mwishoni mwa haya yote?"

Maoni ya kichaa! Lakini ikiwa hivi ndivyo wanavyoamini kumhusu Mungu, itabidi ukubali, ni nani anaweza kumtumaini au kutamani kumtumikia Mungu ambaye anataka kumchukua bintiye mwenye umri wa miaka saba? Hakuna mtu! Na ni nani anayetaka kumtumikia Mungu ambaye "anataka" kuhukumu karibu dunia nzima kwenda kwa moto wa mateso? Hakuna mtu! Lakini ndivyo Wakristo wengi wanavyoamini. Maisha yako yote umesikia watu wakisema: "Mungu aliruhusu hilo," "Mungu alifanya hivi," "Huo ulikuwa mpango wa Mungu," "Ulikuwa ni wakati wao wa kwenda," na kauli nyingi zaidi kama hizo. Kwa kweli, nitaweka dau kwamba labda unafikiria vivyo hivyo. Kwa hivyo nitakuwa mkweli. Ikiwa unaamini kweli kwamba Mungu yuko hivyo, kwamba anaweza kuua mtoto kwa hiari au kumpa mtu ugonjwa wa saratani, basi tunahitaji kuwa na mazungumzo mazito. Acha niseme hivi:

**KAMWE HUWEZI KUMWAMINI MTU USIYEMTUMAINI!**

Ikiwa umefundishwa kutomwamini Mungu, kwamba Yeye huwaua watu wasio na hatia, na ikiwa unakubali kwamba Yeye ndiye Muumba mwenye uwezo wote ulimwenguni, basi afadhali sisi sote tufanye kila tuwezalo kubaki upande wa kuwa na kibali mbele Zake. Hivi ndivyo watu walivyofanya zamani katika tamaduni nyingi za kale. Walitoa matoleo ya kila aina ili kumridhisha Mungu mwenye ghadhabu. Walijiweka chini ya kila aina ya vizuizi, hata kujinyenyekeza kwa aina mbalimbali za maumivu, ili kuonyesha kwamba kweli walikuwa wamejisalimisha Kwake, wakiwa na matumaini ya kuepuka ghadhabu Yake. Lakini je, hii kweli ni tabia ya Mungu wa Biblia? Je, tunapaswa kumwogopa Mungu? La, bila shaka sivyo. Dhana ya kwamba Mungu yu kinyume nasi au haaminiki, yote hayo ni matokeo ya mafundisho mabaya yaliyoanzia kwenye bustani ya Adamu na Hawa.

> *Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, "**Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu**, msile matunda ya miti yote ya bustani?"*
>
> *Mwanamke akamwambia nyoka, "Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, msiyale wala msiyaguse, msije mkafa."*
>
> *Nyoka akamwambia mwanamke, "Hakika hamtakufa, kwa maana*

*Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya."*

*Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.*

*— Mwanzo 3:1-6*

Shetani amekuwa akitilia shaka tabia ya Mungu tangu zamani. Ajabu ni kwamba, Hawa tayari alikuwa na hekima yoyote ambayo huenda alihisi hakuwa nayo kupitia kwa uhusiano wake na Mungu, Mwenyewe. Hata hivyo Shetani aliweza kumsadikisha kwamba kuna kitu alikosa ambacho Mungu alikuwa akimzuilia. Adamu na Hawa waliamini uwongo juu ya Mungu na kwa hiari wakatupilia mbali vyeo vyao katika Ufalme Wake ili kufuata ufalme tofauti. Waliamini kwamba Shetani alikuwa na hatma nzuri zaidi kwao. Bila shaka, uamuzi wao ulileta maumivu, huzuni, na kifo tu.

Mbinu za Shetani kamwe hazijabadilika, na haishangazi kwamba shabaha yake kuu ni kanisa lenyewe. Kwa sababu kanisa tayari lina mamlaka ya kumweka Shetani chini ya miguu yake na kumshinda kila upande, silaha za shetani ni kama zilivyokuwa zamani, udanganyifu na uongo.

## Tabia ya Mungu

Suala la tabia ya Mungu ndilo tunalohitaji kushughulikia kwanza inapohusu mustakabali wako na riziki yako. Ikiwa hatutasuluhisha suala hili, basi unaweza kuweka kitabu hiki kando kama kitabu chochote kingine cha kusaidia watu kupata utajiri. Matumaini yangu ni kwamba utanipa muda wa kutembea nawe katika hili. Natumai unataka kuwa huru kifedha na unatamani hekima na maarifa. Wakati huu, mafundisho hayatokani na mwongo, Shetani, ambaye aliwadanganya Adamu na Hawa, bali kutoka kwa Mungu, Mwenyewe.

Kwanza, ninaweza kuelewa kwa nini unahisi kwamba Mungu huruhusu mambo mabaya yatukie. Yaani ikiwa Yeye ni Mungu, basi ana uwezo wa kufanya chochote, sivyo? Kwa hiyo ikiwa mtoto wa miaka saba alikufa na Mungu alikuwa na uwezo wa kuzuia hilo, basi lazima iwe kwamba aliliruhusu. Naam, taarifa hiyo ni kweli kwa kiwango fulani. Ingawa Mungu alikuwa na uwezo wa kukomesha hilo, hakuwa na mamlaka ya kisheria ya

kulizuia. Nitazungumzia suala hili la mamlaka katika sura inayofuata, lakini nahitaji kushughulikia suala la tabia kwanza na nihakikishe umeelewa, bila kuyumba au shaka yoyote, kwamba Mungu ni mwema na Neno Lake ni kweli.

Labda unaweza kujiuliza kwa nini jambo hili ni muhimu sana. Tunapoendelea zaidi katika kitabu hiki, nitajadili sheria za Ufalme, kazi zao, na jinsi sheria hizo zilivyoniweka huru kutoka kwa mateso ya kifedha niliyokuwa nayo. Ikiwa humwamini Mfalme, Mwenyewe, basi sheria Zake hazitakuwa na maana kwako.

Kumbuka, uvumbuzi wangu wa kwanza katika safari hii ulikuwa kwamba Ufalme wa Mungu ni serikali. Serikali hii ina Mfalme anayeweka sheria za Ufalme Wake. Sheria hizi zinaonyesha faida na wajibu wa raia wanaoishi katika Ufalme huo. Zinalinda na kuhakikishia kila raia katika Ufalme mapenzi ya Mfalme kwa ajili ya maisha yao. Kuelewa tabia ya Mfalme ni sharti la kuelewa sheria zenyewe.

Kama nilivyosema hapo awali, nilipoelewa kwamba Ufalme wa Mungu ni serikali yenye sheria na manufaa ambayo kisheria ni ya kila raia wa Ufalme huo, nilifanyika mwanasayansi wa mambo ya kiroho. Kisha nilitambua kwamba kuna sheria ya kiroho nyuma ya kila utendaji wa Ufalme. Basi nikapata tumaini. Ningejifunza sheria hizo! Mtu yeyote anaweza kufanya hivyo pia! Hivi ndivyo Keith na Kathy walivyogundua.

### Miaka Minne Ilibadili Maisha Yao

Keith na Kathy walikuwa na kazi yenye mshahara wa kawaida, na waliishi maisha ya kawaida. Mara tu waliponunua nyumba mpya Keith alisimamishwa kazi. Hata hivyo, Keith alipata habari kuhusu kipindi chetu cha televisheni cha Fixing the Money Thing muda zaidi ya mwaka mmoja awali na alikuwa ametumia wakati kujifunza na kutafakari baadhi ya nyenzo zangu, na kujifunza kuhusu Ufalme na haki zake za kisheria kama raia.

Alipopoteza kazi yake, aliomba kuhusu jambo hilo na kuamua kwamba badala ya kutafuta kazi nyingine, aanzishe kampuni yake ya lori. Alikiri kwamba kweli hakujua mengi kuhusu biashara hiyo, lakini alihisi angeweza kujifunza. Alianza biashara yake ya kuvuta malori akiwa na lori moja na alikokota magari na chochote alichopata. Keith na Kathy walipoendelea kujifunza, walipata fursa mpya ya kuvuta malori katika kampuni ya kitaifa iliyohitaji msaada. Hii ilikuwa hatua kubwa kwa Keith ambayo ilimhitaji yeye kumiliki lori kubwa na kujifunza sheria nyingi zaidi kuhusu biashara

ya usafiri wa malori—lakini aliichukua kazi hiyo na kuamini kwamba Mungu alikuwa akimuongoza.

Tangu wakati huo, kampuni yake imenawiri tu. Sasa, ana lori kubwa nane za usafirishaji wa kila siku. Keith aliniambia kwamba katika kazi yake ya ofisi, alikuwa akipata $1,500 kwa wiki. Katika mwaka wake wa kwanza wa kumiliki kampuni yake ya lori, Keith alisema alikuwa akipata karibu $4,000 kwa wiki. Mwaka wa pili, mapato yake yaliruka hadi zaidi ya $15,000 kwa wiki. Mwaka uliofuata, yaliruka hadi $25,000 kwa wiki, na mwaka uliofuata hadi zaidi ya $38,000 kwa wiki. Keith alitoka kwa mapato ya $78,000 kwa mwaka hadi milioni mbili kwa mwaka katika miaka minne!

Nilipata ujumbe mfupi kwa simu kutoka kwa Keith nilipokuwa nikiandika sura hii. Alisema ilimbidi kuajiri madereva wengine wanne, na mapato yake sasa yalikuwa $70,000 kwa wiki. Kutoka $78,000 kwa mwaka hadi $70,000 kwa wiki katika kipindi cha miaka minne! Hilo linavutia umakini wangu! Keith na Kathy wanatarajia kwamba mambo makubwa zaidi yako mbele yao maana sasa wanapanga kuanzisha kampuni mbili zaidi.

**CHOCHOTE AU MTU YEYOTE ANAYEKWAMBIA MUNGU SI MWEMA ANAKUAMBIA UONGO!**

Ukiuliza Keith na Kathy sababu ya kufaulu kwao, wao hutoa sifa zote kwa kujifunza jinsi Ufalme unavyofanya kazi

Jambo la kwanza ambalo Keith na Kathy watakuambia ni kwamba iliwabidi waache mafunzo mengi yasiyofaa ya kidini ambayo walikuwa wamefundishwa maisha yao yote kumhusu Mungu na jinsi anavyofanya kazi. Jambo moja muhimu ambalo walipaswa kuzingatia ni kwamba Mungu ni mwema, MWEMA DAIMA, na HADANGANYI KAMWE. Chochote au mtu yeyote anayekuambia Mungu si mwema anakuambia uwongo!

> *Ndugu zangu wapenzi, msidanganyike. Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; Kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka.*
>
> — Yakobo 1:16-17

Pili, watasema walipaswa kujifunza kuwa watoaji kwa njia mpya kabisa. Kusaidia kazi ya Mungu kupitia kwa fedha wanazotoa ni jambo muhimu katika mafanikio yao.

Biblia iko wazi. Kumlaumu Mungu kwa mambo ya kutisha

yanayowapata watu si sahihi. Biblia inasema kwamba Shetani ndiye huja kuua, kuiba na kuharibu.

> *Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.*
>
> — Yohana 10:10

Na tazama kile Yesu alichosema baada ya kauli ya kwanza, "Mimi nimekuja ili wawe na uzima na wawe nao tele," au tafsiri zingine zinasema uzima "kwa wingi zaidi." Mungu si adui yako. Lakini ikiwa unafikiri hivyo, basi kulingana na Yakobo 1:16, umedanganywa na mtu fulani. Itabidi ujiulize ni nani alikuambia kwamba Mungu ni mdanganyifu. Ni nani alikuambia kwamba Mungu alimuua yule mtoto wa miaka saba? Ni nani alikuambia kwamba wakati fulani Mungu huponya na wakati mwingine Yeye huchagua kutofanya hivyo? Labda naweza kukisia—ni mhubiri fulani ambaye hakuwa na ufahamu sahihi. Lakini hapa kuna kauli ambayo unahitaji kushikilia ikiwa utapokea kutoka kwa Mungu. Mungu hasemi uongo! Kwa kweli, Biblia inasema kwamba haiwezekani Kwake kusema uwongo (Waebrania 6:18).

Tena, sababu inayofanya watu kuamini kwamba Mungu si mwema sikuzote ni kwa sababu hawaelewi mfumo wa kisheria wa Ufalme wa mbinguni hapa duniani. Kama nilivyotaja hapo awali, tutazungumzia hilo kwa kina katika sura inayofuata, na itajibu maswali yako mengi. Lakini ukitaka kuelewa jinsi Ufalme unavyofanya kazi, lazima ujue kwamba Mungu ni mwema na hasemi uwongo.

### Mambo ya Ufalme wa Mungu Yasiyobadilika

Katika shule ya upili, nilijifunza somo ambalo nafikiri linatumika hapa. Tulifundishwa kwamba inapohusu vitu vya kiasili, kuna sifa fulani zisizobadilika na ni za milele. Umekisia vyema! Sheria hizi katika fizikia zinaitwa yale yasiyobadilika. Kwa mfano, halijoto inayosababisha maji kuganda ni digrii 32. Hilo halibadiliki kamwe. Vivyo hivyo, ukweli kwamba Mungu ni mwema unadumu milele. Kwa hivyo inapohusu maji, utatumia halijoto ya kugandisha maji katika milinganyo yako yote kuhusu maji.

Ndivyo ilivyo katika kuelewa tabia ya Mungu. Ukijua kwamba Mungu ni mwema na habadiliki kamwe, utaweza kutafsiri kifungu cha Maandiko kupitia kwa macho ya yale yasiyobadilika. Kwa mfano, hebu tuangalie

kitabu cha Kutoka 4:11-12 katika tafsiri ya Biblia ya King James.

> *Bwana akamwambia, "Ni nani aliyekifanya kinywa cha mwanadamu? Au ni nani afanyaye mtu kuwa bubu au kiziwi, au mwenye kuona, au kuwa kipofu? Si mimi, Bwana?"*
>
> — Kutoka 4:11-12

Unapotazama andiko hili mara ya kwanza, inaonekana kana kwamba Mungu huwafanya watu kuwa vipofu na viziwi kimakusudi. Lakini tunapaswa kukumbuka daima—kwamba Mungu ni mwema sikuzote. Hebu tuangalie Maandiko yale yale katika tafsiri tofauti.

> *Kisha Mwenyezi-Mungu akamuuliza Musa, "Ni nani afanyaye kinywa cha mtu? Ni nani anayeamua ikiwa watu watanena au kutonena, kusikia au kutosikia, kuona au kutoona? Je, si mimi, Bwana?"*
>
> — Kutoka 4:11 (Tafsiri ya 'NLT')

Muktadha wa kifungu hiki ni kwamba Mungu alimwita Musa kwenda kwa watu Wake binafsi, Wayahudi, na kuwaambia kwamba Mungu alimwita aende kwa Farao kudai kwamba Wayahudi waachiliwe. Lakini Musa alimjibu Mungu, "Itakuwaje Wayahudi wasipoamini kwamba umenitokea?" Mungu alimwambia njia chache za kuwathibitishia hilo. Lakini Musa akamsihi Bwana,

> *"Ee Bwana, mimi si mzuri sana kwa maneno. Sijawahi kuwa wala siko sasa, ingawa umesema nami. Mimi huchanganyikiwa na maneno, na maneno yangu huvurugika."*
>
> *Kisha Mwenyezi-Mungu akamuuliza Musa, "Ni nani afanyaye kinywa cha mtu? Ni nani anayeamua ikiwa watu watanena au kutonena, kusikia au kutosikia, kuona au kutoona? Je, si mimi, Bwana?*
>
> *Sasa nenda! Nitakuwa pamoja nawe unapozungumza, nami nitakufundisha la kusema.*
>
> — Kutoka 4:10–12 (Tafsiri ya 'NLT')

Hebu nifafanue kile ambacho Mungu alikuwa akimwambia Musa. Je! niliumba mdomo wa mwanadamu unene au usinene? Je! niliumba macho ya mwanadamu yaone au yasione? Jibu ni dhahiri. Kinywa kiliumbwa kunena, na macho yaliumbwa yaone. Hayo tu ndiyo Mungu alikuwa

akijaribu kumwambia Musa kusema. Kimsingi, Mungu alisema, "Ikiwa niliumba kinywa, basi hakika naweza kukusaidia kukitumia!" Mungu alikuwa akijaribu kumfanya Musa aelewe kwamba angeweza kumtumaini kumsaidia kunena alipoenda kwa Wayahudi.

Lakini bila kuwa na mtazamo sahihi kumhusu Mungu, tunaweza kutafsiri vibaya kusudi lililo hapa. Nafikiri sote tumesikia kwamba Musa alikuwa kigugumizi. Watu wengi wanaweza kusema kwamba ni ukweli mtupu, lakini je, ni kweli? Kwa kujibu, unaweza kusema, "Hakika kabisa. Musa, mwenyewe alisema kwamba hakuwa na uwezo wa kunena vyema." Ninakubali, alisema hivyo, lakini alimaanisha nini? Ikiwa Musa hakuwa na uwezo wa kuzungumza vyema, basi tunahitaji kueleza Matendo 7:22.

> *Musa alifundishwa hekima yote ya Wamisri, naye alikuwa hodari katika usemi na matendo.*
>
> —Mdo. 7:22 (Tafsiri ya 'NLT')

Kwa kweli, tunaona kwamba Musa alikuwa kinyume kabisa na mtu mwenye wakati mgumu katika kunena. Alikuwa na nguvu katika hotuba. Kwa hiyo Musa alimaanisha nini aliposema, "Ee Bwana, mimi si mzuri sana kwa maneno. Sijawahi kuwa wala siko sasa, ingawa umesema nami. Mimi huchanganyikiwa na maneno, na maneno yangu huvurugika."

Kitabu cha Kutoka 4 kinapozungumza kuhusu Musa kuwa mpole wa kusema, kilirejelea ukweli kwamba Musa hakujua lugha ya Kiebrania vyema. Hakulelewa pamoja na Wayahudi. Alilelewa kama Mmisri na kimsingi alizungumza lugha ya Kimisri. Mungu alimhakikishia Musa kwamba kwa kuwa aliumba kinywa cha mwanadamu, angemsaidia kuzungumza na Wayahudi. Lakini tena, Musa alirudi nyuma.

> *Akasema, "Ee Bwana, nakuomba, tuma kwa mkono wake huyo utakayemtuma." Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Musa, akasema, "Je! Hayuko Haruni, ndugu yako, Mlawi? Najua ya kuwa yeye aweza kusema vizuri. Pamoja na hayo, tazama, anakuja kukulaki; naye atakapokuona, atafurahi moyoni mwake. Nawe utasema naye, na kuyatia maneno kinywani mwake; nami nitakuwa pamoja na kinywa chako, na pamoja na kinywa chake, na kuwafundisheni mtakayofanya. Naye atakuwa msemaji wako kwa watu, hata yeye atakuwa mfano wa kinywa kwako, nawe utakuwa mfano wa Mungu kwake."*
>
> — Kutoka 4:13-16

Hitimisho ni kwamba Haruni alijua lugha ya Kiyahudi vyema sana, alilelewa kama Myahudi, na angeweza kuzungumza nao kwa niaba ya Musa, si kwamba Musa alikuwa kigugumizi. Kwa hivyo sasa unaona jinsi ilivyo muhimu kuwa na mtazamo sahihi na wa kudumu kuhusu tabia ya Mungu. Kuwa na ufahamu kwamba Yeye ni mwema kila wakati kunapaswa kutufanya tuhoji maana inayokusudiwa na maandishi haya na kuchimba zaidi ili kupata utafsiri sahihi. Kwa hivyo tena, msingi wako katika Ufalme ni kujua tabia ya Mfalme mwenyewe. Ikiwa hilo halijulikani, basi Shetani anaweza kukudanganya, kama alivyofanya Hawa, ili uamini kwamba Mungu hasemi ukweli wote au, hata vibaya zaidi, kwamba Mungu amekudanganya.

**KUNA ZAIDI YA AHADI 7,000 KATIKA BIBLIA ZINAZOFAFANUA HAKI ZAKO ZA KISHERIA KAMA MTOTO WA MUNGU**

### Kuelewa Ahadi za Mungu

Kuna zaidi ya ahadi 7,000 katika Biblia zinazofafanua haki zako za kisheria kama mtoto wa Mungu. Kila ahadi umepewa na Mfalme Mwenyewe na inaweza kuaminiwa. Au sivyo? Ikiwa unaweza kushuku wema wa Mungu, basi unaweza kushuku ahadi Zake pia.

Hebu nikupe mfano. Tuseme nimekupa hundi ya $1,000. Utanishukuru, na katika akili yako, utakuwa na $1,000. Utatenda kama mtu mwenye $1,000, utanena kama mtu aliye na $1,000, na tena utanishukuru kwa kukupa dola hizo. Lakini ukweli wa mambo ni kwamba hutakuwa na $1,000; utakuwa na hati ya ahadi. Hundi ni ahadi ambayo nimekupa kusema kwamba una haki kisheria kupokea $1,000 kutoka kwa benki yangu. Lakini lazima utoe hundi ili uwe na pesa! Lakini kwa kuwa nia yangu kwako imejulikana, kwa vile nimekupa hundi kwa hiari na nikaitia saini, na kwa sababu umeamini kwamba nina $1,000, utasema una $1,000 wakati kile ulicho nacho tu ni ahadi.

Hakika Mungu ni mkuu kuniliko. Neno Lake halisemi uongo. Ametupa ahadi Zake kuu na za thamani. Mungu akikupa ahadi Yake, ni sawa na kukamilika! Kitu pekee ambacho Shetani anaweza kufanya ili kuzuia ahadi hiyo isitimie ni kukufanya utilie shaka Neno la Mungu. Ndiyo maana ni muhimu kujua kwamba Mungu ni mwema na hasemi uongo.

Nikupe mfano mwingine. Najua wengi wamesikia kwamba miujiza imepita na Mungu hafanyi yale yale ambayo Yesu alifanya alipokuwa duniani. Nililelewa katika kanisa la kitamaduni sana, na kusema kweli,

sikumbuki nikiona nguvu za Mungu zikidhihirishwa. Kwa hiyo kwa sababu sikuona watu wakiponywa, je, hiyo inamaanisha kwamba Mungu haponyi tena? Ili kujibu hilo, hatuwezi kutegemea uzoefu wetu. Tunahitaji kujua Biblia inasema nini, sheria ya Mfalme inasema nini kuhusu uponyaji.

> *Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu **alivyomtia** mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu Naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; **kwa maana Mungu alikuwa pamoja Naye**.*
>
> — Mdo. 10:38

Kama tunavyoona, uponyaji ulikuwa jambo mkuu katika huduma ya Yesu. Andiko linasema kwamba Yesu aliwaponya wote kwa sababu Mungu alikuwa pamoja Naye. Sasa maneno hayo, "Mungu alikuwa pamoja Naye" ni kauli ambayo unahitaji kuelewa. Bila shaka, Mungu alikuwa pamoja na Yesu maisha Yake yote duniani. Lakini kauli hii hakika inarejelea wakati Yesu alikuwa akibatizwa kwa maji na Roho Mtakatifu akamshukia kama njiwa. Kufikia wakati huo, Yesu alikuwa hajafanya miujiza yoyote. Hatuna rekodi ya Yesu kuzidisha kifungua kinywa Chake au kuponya hata mtu mmoja alipokuwa mtoto. Ilikuwa tu baada ya kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu ndipo huduma Yake ilipoanza. Mungu alikuwa pamoja Naye alipokuwa akifanya kazi hiyo.

Vema, labda unaweza kusema, "Ndio, Yesu aliponya, lakini hayupo hapa tena." Kweli, ninakubali, uko sahihi, lakini alipatia kanisa kazi hiyo. Wajua, nguvu zile zile zilizomjia Yesu pia zilitolewa kwa kanisa. Yesu alipokaribia kuondoka duniani, aliwaambia wanafunzi Wake mambo yafuatayo.

> *Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*
>
> — Mdo. 1:8

Nguvu hizo hizo, za Roho Mtakatifu, zilikuja juu ya kanisa ili kufanya miujiza ile ile ambayo Yesu alifanya.

Huwezi kuniambia chochote kingine. Binti yangu Amy alikuwa na uvimbe wa kilo 13 tumboni mwake. Sote tulimuombea uponyaji kwa msingi wa Neno la Mungu, alilala kisha akaamka asubuhi akiwa mzima kabisa. Uvimbe wa kilo 13 ulikuwa umetoweka, na mgongo wake (ambao

ulikuwa na fundo na kupinda) ulijengwa upya kabisa. Unaweza kuona na kusoma hadithi yake katika kitabu chake *Healed Overnight*.

Binti-mkwe wangu alikuwa na uvimbe wa saizi ya chungwa katika upande wake mmoja ambao madaktari walisema ingebidi utolewe kwa upasuaji. Walisema alikuwa na aina adimu ya ugonjwa wa saratani na alikuwa na mwezi mmoja hadi miwili kuishi. Pia aliamini ahadi za Mungu na aliamka asubuhi akiwa mzima kabisa. Uvimbe ulikuwa umetoweka.

Mke wangu, Drenda, pia alikuwa na uvimbe mkubwa mgongoni mwake. Alianza kuuamuru uondoke mwilini mwake, na katika wiki mbili, ulikuwa imetoweka kabisa.

Je, Mungu alichagua kuwaponya wanawake hawa? Je, lilikuwa ni jambo ambalo Mungu alipaswa kuchagua kufanya? Je, aliwapenda wanawake hawa watatu kukuliko wewe? La! Walielewa sheria na faida za Ufalme na kuzidai tu. Unaweza kuuliza, "Basi, kwa nini watu wengi ni wagonjwa? Kwa nini hatuoni watu wakiponywa mara nyingi katika makanisa yetu?"

Ninafurahi umeuliza. Hebu tuangalie hilo kwa kina katika sura inayofuata.

SURA YA 3

# SUALA LA MAMLAKA

Kama nilivyosema awali, ninaishi mashambani kwenye ekari 60 zenye ardhi ya kupendeza sana huko Ohio. Hapo awali nilikuwa na ekari 55, lakini jirani yangu aliniuzia kipande cha shamba lililopakana na langu, jambo ambalo lilinisababisha kuwa na jumla ya ekari 60. Hakika tumefurahia shamba hili kwa miaka 22 iliyopita. Kuwa na msitu wa kuwinda kulungu, bwawa la kuwinda bata, na shamba la kuwinda sungura na ndege, na pia kuendesha magari yetu humo ni baraka. Lakini ukiangalia mali yangu kwa ukaribu, utaona kwenye uzio la shamba alama zinazosema HAKUNA KUINGIA. Alama zipo ili watu wajue ni wapi mstari wa mali yangu unapoanzia.

Sheria katika Ohio inasema kwamba yeyote anayetaka kuingia katika shamba langu lazima awe na fomu ya kibali wakati wowote aingiapo. Asipofanya hivyo, hilo linaitwa kuingilia mali, na anaweza kuondolewa kisheria, kuadhibiwa na kulipa faini katika mchakato huo. Suala ni kwamba mtu yeyote atakayechagua kuingia shambani bila mimi kujua hana mamlaka kisheria kufanya uamuzi huo, kwa vile si ardhi yake. Nikimwambia aondoke shambani mwangu, hana chaguo lingine!

Kwa hivyo kwa ufupi, huwezi kumiliki kitu usicho na mamlaka juu yake kisheria.

Mfano huu wa kuingilia mali kitajibu maswali mengi sana ambayo watu wanayo kuhusu kwa nini mambo hutokea au kutotokea katika Ufalme wa Mungu. Kuelewa suala la mamlaka katika Ufalme ni sharti la

kuwa na ufanisi katika Ufalme.

### Kwa Nini Hawakuponywa?

Nina hakika labda umesikia hadithi kama hii. Mtu mashuhuri anaugua sana, na watu wanaambiwa wamwombee. Mamilioni ya watu wanajiunga katika maombi kwa ajili ya uponyaji wa mtu huyu, na bado mtu huyu anakufa. Kwa nini? Au mtu anakuambia bibi yake alifariki japo walikuwa wakimuombea, na anataka kujua kwa nini. Au mtu anakuambia kwamba ametoa matoleo kwa sababu ya hitaji la kifedha, na bado anaendelea kuwa na ukosefu. Je, kuna majibu kwa maswali kama haya?

Kabla sijajibu hilo, hebu tukubali kwamba hatujui kila kitu kinachofanyika katika ulimwengu wa Roho, na sijifanyi kwamba ninajua. Hata hivyo, kwa kutegemea Neno la Mungu, tunajua kwamba ikiwa mtu fulani alikuwa mgonjwa, Yesu alilipa gharama ya uponyaji wao. Tunajua kwamba tukiwa wakarimu na kutoa, Biblia inasema tutapokea. Hata hivyo kila siku, tunaona kile kinachoonekana kama kushindwa dhahiri kwa Maandiko katika maisha ya watu wengi. Je, ni Mungu anayepaswa kulaumiwa?

Tunapotazama yale tuliyojifunza katika iliyopita, na kujadili mada hii katika sura hii, utapata jibu ni la hasha! Ikiwa ni la, basi shida ni nini? Hili ni suala kuu. Kwa watu wengi wasio na ufahamu wa kimsingi kabisa kwamba Mungu ni mwema siku zote, wanapoulizwa kama Mungu ndiye anayepaswa kulaumiwa misiba inapotokea, wao hufikiri Yeye ndiye sababu. Tena, kwa sababu wanajua ana uwezo wa kukomesha mambo mabaya yasitokee, na inaonekana hakufanya hivyo, basi wanafikiri aliyaruhusu. Lakini ikiwa una ufahamu kwamba Mungu ni mwema na hawezi kusema uwongo, utajua lazima tatizo liwe mahali pengine, na utaanza kutafuta jibu.

Wanafunzi walionyesha walikuwa na mawazo ya aina hii wakati hawakuweza kutoa pepo kutoka kwa mvulana aliyepagawa. Badala ya kuuliza, “Kwa nini Mungu aliamua kumwacha pepo huyo mchafu hapo?” walimwuliza Yesu, “Kwa nini hatukuweza kumtoa?

**UFALME WA MUNGU NI UFALME NA UNAFANYA KAZI KWA SHERIA NA KANUNI ZISIZOBADILIKA**

Hili linapaswa kuwa swali letu la kwanza hali zinapoonekana kana kwamba zinapingana na Neno la Mungu. Kwa hiyo tena, ni muhimu kwamba lazima, kwanza kabisa, tujue Mungu ni mwema, na pili, kwamba hasemi uwongo.

Hii pia ndiyo sababu nimetumia muda mwingi kueleza kile kinachoonekana kwangu kuwa wazi, lakini cha kushangaza ni kwamba kwa wengi walio kanisani ni fumbo. Ikiwa unataka kujifunza jinsi Ufalme unavyofanya kazi unapaswa kuuliza maswali unaposoma Biblia.

Kumbuka, hadithi hizi za ajabu katika Biblia zipo kwa sababu fulani. Yesu anajaribu kukuonyesha kitu. Kwa hiyo, hebu tuendelee na sababu mtu hapokei kile ambacho Neno la Mungu linasema. Naam, kunaweza kuwa na masuala mengi yanayodhoofisha mamlaka ya mbinguni. Masuala mengine si dhahiri mara moja, na mengine ni ya kibinafsi na huwa yamefichwa.

Ufalme wa Mungu ni ufalme na unafanya kazi kwa sheria na kanuni zisizobadilika kamwe. Kama nilivyosema, unaweza kujifunza kanuni hizo, na kuzitumia kama vile mkulima anavyoelewa sheria za wakati wa kupanda na kuvuna katika ulimwengu wa asili na hutumia sheria hizo ili kufanikiwa. Kwa sababu Ufalme unatumia sheria kufanya kazi ambazo zimetolewa kwa kila raia kuelewa na kutumia, mtu yeyote anaweza kujifunza kuzihusu. Wakati mwingine, kujua au kutojua jinsi sheria hizi zinavyofanya kazi kunaweza kuwa jambo linaloleta uzima au mauti.

### Uamuzi kati ya Uzima na Mauti

Mark na Hannah walikuja kanisani kwetu wakiwa na hitaji la kupata mtoto. Hadi wakati huo, Hannah aliambiwa na madaktari kwamba kutokana na masuala mbalimbali ya mwili wake, ingekuwa vigumu kwake kupata mimba au kubeba mtoto. Alipoendelea kusikia kuhusu wema wa Mungu na kujifunza sheria za Ufalme katika Kanisa la Faith Life, aligundua kwamba alikuwa mjamzito. Alifurahi kupita kiasi. Lakini muda si muda, alianza kupata maumivu makali ya tumbo. Mara mbili, yalikuwa makali sana kiasi cha kumfanya Hannah kuzimia.

Baada tukio moja kama hili, alitaka mambo yakaguliwe kwa hivyo alienda kwa daktari wake. Daktari wake hakuwa kazini, lakini yule aliyekuwepo alitaka kumfanyia uchunguzi ili kuona shida ilikuwa wapi. Alichokiona daktari ni ganda kubwa la damu, kisha akamwambia mimba ilikuwa imetoka, na hakusikia mapigo ya moyo wa mtoto. Daktari alipendekeza aje siku iliyofuata ili mtoto wake aliyekufa atolewe tumboni mwake, lakini Hannah alikataa. Mume wake, Mark, alimtia moyo Hannah kupitia kwa Neno la Mungu na ahadi za Mungu na kumshawishi asitupilie mbali imani yake kuhusu mtoto huyo. Wikendi hiyo, aliombewa kanisani na alikuwa na hakika kwamba angekuwa na mtoto mwenye afya njema

licha ya yale ambayo daktari alikuwa amemwambia.

Jumatatu hiyo, aliingia kuonana na daktari wake binafsi, maana hakuwepo ile siku alipoenda kumwona. Daktari wake alipendekeza afanyiwe uchunguzi mwingine. Hannah alisema daktari alikuwa na sura ya kupigwa na mshtuko usoni mwake alipokuwa akitazama matokeo katika skrini ya kompyuta na mara moja kutazama skanisho zilizofanywa siku chache awali. Kisha akamwambia Hannah maneno yafuatayo: "Nimekuwa nikifanya kazi hii kwa miaka 30, na sijawahi kuona jambo hili likitukia hapo awali. Ninaona ganda kubwa la damu kwenye matokeo ya wiki iliyopita na kutokuwepo kwa mapigo ya moyo. Ninapokutazama leo, ganda lote la damu limetoweka, na kuna mtoto mkamilifu, aliye hai, mwenye mapigo kamili ya moyo." Baada ya miezi michache, Hannah alizaa mtoto msichana mwenye afya njema, ambaye alimwita Evelyn. Siku moja akiwa na hamu ya kutaka kujua maana ya jina hilo, alitafuta maana yake na kushangaa kwamba lilimaanisha uhai!

Hadithi hii ya kushangaza kwa hakika ilikuwa kazi ya Mungu, lakini kama mwanasayansi wa mambo ya kiroho, unapaswa kufikiria maswali machache kama haya sasa hivi. Kwa nini hili lilitokea? Je, Hannah ni mmoja wa watu wanaopendelewa na Mungu? Je, Mungu alichagua kwa nasibu tu kumponya mtoto wake? Haya ni maswali ambayo yanapaswa kujibiwa. Tena, kwa Mkristo wa kawaida huo ulikuwa muujiza. Lakini ninawahimiza watu kufikiria upya neno muujiza maana linamaanisha kitu kisicho cha kawaida. Katika Ufalme, hii ilikuwa tu kazi ya sheria ya Ufalme.

Iwapo ningedondosha jiwe na likaanguka chini, ungefikiri mimi ni wazimu ikiwa ningesema kwa sauti, "Ajabu! umeona hilo? Jiwe limeanguka chini; huo ni muujiza!" Hungekubali ni muujiza kwa sababu unajua hiyo ni kazi ya sheria ya mvuto, na inafanya kazi kwa njia sawa kwa kila mtu wakati wowote. Lazima jiwe lianguke chini. Kwa hivyo kama mwanasayansi wa mambo ya kiroho, lazima utafute vidokezo juu ya kile kilichotokea katika hadithi, vidokezo vya kiroho vitakavyofunua sheria za Ufalme zilizopo.

## Jambo Muhimu Lafunuliwa

Hebu tuendelee na hadithi nyingine ambapo tutajifunza zaidi kuhusu Kazi ya Ufalme kuhusiana na maswali haya. Moja ya hadithi nzuri katika Biblia itakayotusaidia kupata majibu inapatikana katika Luka sura ya nane.

*Na alipokuwa akienda makutano walimsonga. Na mwanamke mmoja,*

*ambaye ametokwa na damu muda wa miaka kumi na miwili, [aliyekuwa amegharimiwa mali zake zote kwa kuwapa waganga] asipate kuponywa na mtu ye yote, alikwenda nyuma yake, akaugusa upindo wa vazi lake; na mara hiyo kutoka damu kwake kulikoma.*

*Yesu akasema, "Ni nani aliyenigusa?"*

*Basi, watu wote walipokana, Petro alimwambia, "Bwana mkubwa, makutano haya wanakuzunguka na kukusonga."*

*Yesu akasema, "Mtu alinigusa, maana naona ya kuwa nguvu zimenitoka."*

*Yule mwanamke, alipoona ya kwamba hawezi kusitirika akaja akitetemeka, akaanguka mbele Yake, akamweleza mbele ya watu wote sababu yake ya kumgusa, na jinsi alivyoponywa mara. Akamwambia "Binti, imani yako imekuponya; enenda zako na amani."*

— Luka 8:42-48

Katika hadithi hii, tunapata mwanamke ambaye alikuwa mgonjwa sana kwa miaka mingi wala hakuweza kupona. Alipokuja nyuma ya Yesu, na kugusa vazi Lake alipona mara moja. Sasa, kuna vidokezo vya kina sana vya utendaji wa Ufalme katika hadithi hii ambavyo tunaweza kujifunza hapa na ambavyo vitadhihirisha baadhi ya majibu tunayotafuta.

Kwanza kabisa, umati wote uliokuwa umemzunguka Yesu ulikuwa ukimgusa. Kama hadithi inavyosema, alikuwa karibu kupondwa na umati uliokuwa ukimsonga. Yesu alipouliza, "Ni nani aliyenigusa?" Petro alishangazwa na swali hilo kwa sababu, tena, kila mtu alikuwa akimgusa. Lakini Yesu alisema mtu huyu alikuwa amemgusa kwa njia tofauti maana alihisi nguvu za Roho Mtakatifu zikimtoka.

Baada ya kusoma hadithi hii, unapaswa kuwa na hamu kubwa rohoni mwako kukoma na kufikiria kile ambacho kilikuwa kimetokea. Akili yako inapaswa kuingia mara moja katika hali ya uchunguzi na kujawa na maelfu ya maswali. Kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, tunahitaji kujua kwa nini mwanamke huyu aliponywa na hakuna mtu mwingine aliyeponywa. Ninaweza kukisia kwamba kulikuwa na wagonjwa wengine wengi pale ambao walikuwa wakimgusa kimwili lakini hawakuponywa. Kwa hiyo tunahitaji kuuliza, "Kwa nini upako ulitiririka kwa mwanamke huyu tu na

si kwa kila mtu mwingine aliyemgusa wakati huo?”

Jibu la jadi la kidini ni kwamba aliponywa kwa sababu Yesu alimponya. Lakini je, Yesu alikuwa akimhudumia kimakusudi alipoponywa? Je! Aliweka mikono Yake juu yake? Je, aliamuru ugonjwa uondoke kwenye mwili wake? Jibu ni la. Kwa kweli, Yesu hakujua kwamba mwanamke huyo alikuwa pale. Ilimbidi aulize ni nani aliyemgusa. Je, Yesu alichagua kumponya wakati huo? Tena, hakujua alikuwa pale. Kwa hiyo, aliponywaje? Kwa nini aliponywa?

Kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, tunaweza kuondoa wazo kwamba alikuwa mmoja wa watoto maalum wa Mungu au kwamba alikuwa na uhusiano maalum na Yesu, kwa sababu Matendo 10:34 inasema kwamba Mungu hana upendeleo. Tunaweza kusema maana Yesu hakujua kwamba alikuwa pale, hakuwa na sehemu katika uamuzi wake wa kuponywa siku hiyo. Tunakubali kwamba Yeye alikuwa hifadhi la upako, lakini hakuwa sehemu ya uamuzi alioufanya wa kuponywa.

Yesu alituambia hasa jinsi alivyojiingiza katika mamlaka na nguvu za Ufalme. Alisema, “Binti, imani yako imekuponya. Enenda zako na amani.” Sentensi hii inatuambia kila kitu tunachohitaji kujua na kujibu swali letu la kwa nini na jinsi alivyopokea siku hiyo. Kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, hebu tuanze kuchunguza hadithi hii kwa kina ili tuone ikiwa tunaweza kupata dalili za sababu zilizomfanya apokee.

Kwanza kabisa, Yesu alimwita binti Yake, kumaanisha kwamba alikuwa sehemu ya taifa la Israeli, mzao wa Ibrahamu. Kama mtoto wa Ibrahimu, alikuwa na baraka na faida za agano alilofanya Mungu na Ibrahimu.

> *Akawaambia, “Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele Zake, na kutega masikio usikie maagizo Yake, na kuzishika amri Zake, Mimi sitatia juu yako maradhi yoyote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.”*
>
> — Kutoka 15:26

Kwa hiyo, Yesu alipomwita binti Yake, hilo lilimaanisha kwamba alikuwa na haki ya kisheria ya mambo yote yaliyokuwa katika agano alilolifanya Mungu na Ibrahimu. Hata hivyo, ukweli huu pekee hauwezi kuwa sababu tu iliyomfanya apokee maana kila mtu pale siku hiyo alikuwa na uhalali huo huo. Ilibidi kuwe na kitu kingine ambacho kilikuwa kimesababisha nguvu za Ufalme wa Mungu kutiririka. Kisha Yesu ametuambia sababu moja zaidi iliyomfanya apokee. Kwa kweli, Yesu alisema hii ndiyo sababu haswa iliyofanya yule mwanamke kupokea kibinafsi. Alisema imani yake ilimponya.

Kwa hivyo, sasa tunajua sababu iliyomfanya aweze kupokea. Ilikuwa ni haki yake kupokea kihalali kwa vile alikuwa binti wa Ibrahimu, na pili, imani yake ilikuwa kibonyezi kilichofungulia nguvu hizo kutiririka kibinafsi ndani ya mwili wake wakati huo. Ukweli kwamba alikuwa binti unaweza kulinganishwa na kampuni ya umeme inayowasha nguvu za umeme zinazoingia kupitia kwa nyaya katika nyumba yako. Nguvu zipo, lakini hiyo haimaanishi kwamba taa zako zitawaka. Lazima pia ufinye kibonyezi kabla ya kuwasha taa.

Kwa hiyo, yeye kama mzao halali wa Ibrahimu, alikuwa na haki ya kisheria ya kuponywa. Walakini, kwa sababu alikuwa na mamlaka juu ya dunia na maisha yake mwenyewe, ilimbidi kuwasha swichi ili kuachilia nguvu hizo. Lakini swichi iko wapi? Je, tunaiwashaje? Ili kujua, tunahitaji kufafanua masharti yetu.

### Imani Ni Nini?

Imani ni neno ambalo Wakristo hutumia kiholela. Na nina hakika kwamba wengi hawajui imani kwa kweli ni nini, kwa nini inahitajika, jinsi ya kujua kama wako katika imani, na jinsi ya kupata imani. Ikiwa imani ndiyo swichi iliyofungulia upako uliomponya yule mwanamke, basi tunahitaji kuchunguza imani kwa ukaribu sana! Tunapata ufafanuzi wetu wa imani katika Warumi 4:18–21.

**IMANI NI NENO AMBALO WAKRISTO HUTUMIA KIHOLELA.**

> *Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonenwa, "Ndivyo utakavyokuwa uzao wako." Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, (akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara. Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu; <u>huku akijua hakika</u> ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*
>
> — Warumi 4:18-21

Hebu tuelewe mpangilio wa hadithi hii. Ibrahimu na Sara hawangeweza kupata watoto. Simaanishi walikuwa na shida kupata mtoto na walipaswa kuendelea kujaribu. Namaanisha walikuwa karibu miaka 100, na kamwe haingewezekana. Miili yao haingeweza kupata watoto; haingewezekana

kabisa! Lakini Mungu alimwahidi Ibrahimu mtoto ingawa katika hali ya asili haingewezekana kabisa. Biblia inasema kwamba Ibrahimu alikuwa amesadiki kikamilifu kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kufanya yale aliyosema licha ya mambo ya asili yaliyodhihirisha ukweli tofauti.

Huu hapa ni ufafanuzi wetu wa neno imani: "kuwa na hakika kabisa kwamba Mungu ana uwezo wa kufanya yale ambayo ameahidi." Ninaliweka hivi: "**Moyo wako unapokubaliana na mbingu**." Si kukubaliana tu kiakili na kile anachosema Mungu bali kusadiki kikamilifu.

**Ufafanuzi wetu wa maana ya imani:**

Hebu nirudie mara moja tena ili kuwa na uhakika kwamba umeelewa jambo hili. Imani ni kusadiki kikamilifu kile anachosema Mungu! Ni wakati mioyo na akili zetu zinakubaliana na mbingu, kushawishiwa kikamilifu.

## Kwa Nini Imani Inahitajika?

Mbona Mungu huwa hamponyi kila mtu hospitalini anapotaka? Kwa nini huwa hakomeshi vita? Kwa nini huwa hatumi malaika kutuhubiria Injili? Nina hakika umesikia maswali haya yote hapo awali. Jibu ni kwamba hawezi kufanya hivyo. Si kwamba Mungu hana uwezo wa kufanya hivyo, lakini hana mamlaka ya kufanya hivyo. Ili kuelewa ninachosema, tunapaswa kuangalia Waebrania 2:6-8.

> *Ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema,*
>
> *"Mwanadamu ni nini hata umkumbuke, ama mwana wa binadamu, hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake."*
>
> *Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu <u>kisichowekwa</u> chini yake. Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake.*
>
> — Waebrania 2:6-8

Mungu alimpa mwanadamu mamlaka kamili ya kisheria juu ya ulimwengu wote alipowekwa hapa. Hakuna kitu ambacho hakikuwa chini ya mamlaka yake. Alitawala juu ya eneo hili kwa mamlaka kamili. Uwezo wake wa kutawala kwa mamlaka uliungwa mkono na serikali iliyomweka hapa. Kimsingi, alitawala akiwa na mamlaka aliyokabidhiwa na Ufalme

wa Mungu. Alivaa taji ya serikali hiyo, ambayo iliwakilisha utukufu wa Mungu, upako, na cheo cha heshima au mamlaka aliyokuwa nayo.

Sasa, bila shaka, hakuwa amevaa taji halisi ya chuma, lakini alikuwa na taji kwa maana ya kile ambacho taji inawakilisha. Ili kupata picha nzuri ya jambo hili, tafakari kuhusu mfalme wa asili. Ingawa yeye ni mtu wa asili na hana nguvu halisi katika utu wake wa asili, yeye huvaa taji, ambayo inaashiria kwamba hajiwakilishi mwenyewe tu bali ufalme mzima na serikali. Maneno yake yanabeba mamlaka kwa sababu yanaungwa mkono na nguvu na maliasili zote za serikali na ufalme anaowakilisha.

Ukifikiria polisi anayeelekeza magari barabarani, yeye husimamisha lori kubwa na mamlaka yanayosema, "Simama kwa jina la sheria." Ndio, lori hilo ni kubwa zaidi kumliko—naye mwenyewe, hawezi kulinganishwa na lori—lakini lori hilo husimama, si kwa sababu ya mtu mwenyewe bali kwa sababu ya beji aliyo nayo, ambayo inawakilisha serikali. Katika hali hii, serikali ni kubwa zaidi kuliko mtu mwenyewe. Dereva wa lori huwa hamhofu mtu mwenyewe, lakini anaihofu serikali ambayo mtu huyo anawakilisha, na hilo humfanya dereva wa lori kusimama.

Vile vile ni kweli hapa. Adamu alitawala kila kitu kilichoumbwa katika ulimwengu. Nguvu na enzi ya Mungu, iliyowakilishwa na taji ya utukufu na heshima, ilimpa mwanadamu uhakikisho kwamba maneno yake yalitawala kwa niaba ya Ufalme wa Mungu.

Ni muhimu sana kutambua kwamba Adamu alipopoteza uwezo wake wa kutawala juu ya dunia kwa kufanya uhaini dhidi ya serikali ya Mungu, alipoteza taji yake, cheo chake cha mamlaka katika Ufalme wa Mungu, lakini hakupoteza dai lake la kisheria duniani. Mwanadamu bado alikuwa msimamizi wa dunia kisheria. Mungu alikuwa amempa dunia aitawale. Tukirudi kwenye kifungu chetu cha Waebrania, tunaweza kuona hili.

> *Ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema,*
>
> *"Mwanadamu ni nini hata umkumbuke, ama mwana wa binadamu, hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake."*
>
> *Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu <u>kisichowekwa</u> chini yake. Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake.*
>
> — Waebrania 2:6-8

Ingawa andiko hili linazungumzia wakati Adamu na Hawa waliumbwa, andiko linasema, "Mungu hakusaza kitu kisichowekwa chini yao."

*Mbingu ni mbingu za Bwana, bali nchi* ***amewapa wanadamu****.*
— Zaburi 115:16

**Mwanadamu Alimfukuza Mungu Nje**

Ingawa mwanadamu ana mamlaka ya kisheria juu ya dunia, amepoteza mamlaka yake ya kutawala kiroho. Hakika Adamu alimfukuza Mwenyezi Mungu kutoka kwa mambo ya watu kule Bustanini; na kupitia kwa dhambi ya asili, ulimwengu ulichafuliwa na kubadilika. Kifo kiliingia ulimwenguni, na sasa Shetani akawa na dai la kisheria la kuwa na ushawishi katika mambo ya wanadamu. Lakini ingawa haya yote yalitokea, ni lazima uelewe kwamba mwanadamu bado ni mkaaji halali duniani. Hata katika hali yake ya dhambi, bado ndiye msimamizi. Ndio, hana taji yake ya serikali ya Mungu ya kumtegemeza. Hana mamlaka ya kutawala kwa nguvu na utukufu wa Mungu, na amepoteza cheo chake cha heshima. Lakini bado ndiye kiumbe hai pekee ambaye ana haki ya kisheria ya kuutawala ulimwengu.

**HII NDIYO SABABU INAMBIDI MUNGU KUTUMIA WATU WALIOJAZWA NA ROHO ILI KUTIMIZA MAPENZI YAKE KATIKA MAISHA YA WANADAMU.**

Hii ndiyo sababu inambidi Mungu kutumia watu waliojazwa na Roho ili kutimiza mapenzi Yake katika maisha ya wanadamu. Vivyo hivyo, Shetani hutumia watu waliovuviwa na roho waovu kuathiri ulimwengu kutekeleza mpango wake kwa mwanadamu. Kanuni hii ya mamlaka ya mwanadamu juu ya dunia ni muhimu kwa uelewaji wako wa sheria ya Ufalme na, hasa, kwa nini imani inahitajika ili Mungu apate mamlaka ya kisheria katika hali fulani.

Unaweza kusema, "Lakini nilifikiri Mungu ndiye anayemiliki dunia na yote yaliyomo?" Ni kweli, ndivyo ilivyo. Natumai mfano huu utakusaidia kuelewa ninachosema. Nikikodisha nyumba ninayoimiliki kwako, ingawa ninaimiliki kihalali, huwa sina haki kisheria ya kuja wakati wowote ninapotaka. Kuna kifungu katika ukodishaji wa nyumba kinachobainisha wakati wenye nyumba wanaweza kuingia kihalali katika majengo yao—kwa mfano, kushughulikia jambo la dharura au kufanya matengenezo—na kiasi cha notisi kinachohitajika. Nikijaribu kuingia katika jengo langu nje ya

mkataba huu, itakuwa ni kama nimevunja na kuingia, hata kama mimi ni mmiliki. Iwapo nitakiuka sheria kama ilivyobainishwa katika ukodishaji, basi ninaweza kulazimishwa kisheria kuondoka katika jengo hilo.

Hiyo inaonyesha kwa nini ilimbidi Shetani kupitia kwa Adamu ili kuupata ulimwengu. Adamu pekee ndiye aliyekuwa na ufunguo! Ilimbidi Shetani apitie mlangoni na ilibidi awe amepewa ufunguo kutoka kwa yule aliyeumiliki kihalali au angelazimika kutoka kisheria.

Kwa njia hiyohiyo, mara tu Adamu alipoifukuza serikali ya Mungu kutoka ulimwenguni, ilimbidi Mungu atafute njia ya kuirejesha kisheria katika ulimwengu. Tena, ilimbidi apitie kwa mwanadamu. Katika kisa hiki, ni mtu aliyeitwa Abramu ambaye alifungua mlango.

> *Bwana akamwambia Abramu, "Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; Nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; <u>na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.</u>"*
>
> — Mwanzo 12:1-3

Ibrahimu anaitwa baba wa imani yetu kwa sababu yeye ndiye mtu aliyemfungulia Mungu mlango wa ulimwengu ambao kupitia kwake mataifa yote duniani yangebarikiwa. Bila shaka, hii inazungumzia Yesu Kristo na mpango wa Mungu wa kuwaokoa wanadamu. Imani ya Ibrahimu ilifungulia Mungu mlango wa kudumu kisheria kwa kufanya mapatano ya kisheria kati yake na Mungu Mwenyewe. Makubaliano haya pia yalikuwa yanafungamana na uzao wa Ibrahimu, na hili ndilo lililomaanishwa katika Mwanzo 12 Biblia inaposema, <u>"na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa."</u> "Watabarikiwa katika wewe" inarejelea kuja kwa Yesu kupitia kwa ukoo wa Ibrahimu na kurejesha kile Adamu alichopoteza.

Hebu nifafanue ninachosema. Mwanamume au mwanamke aliye na mamlaka ya kisheria katika ulimwengu lazima asimame katika mapatano na mbingu ili mbingu ziweze kuingia kisheria duniani. Makubaliano haya na mbingu yanaitwa imani. Hii ndiyo kanuni ileile ambayo Shetani alitumia kuingia kisheria katika ulimwengu kupitia kwa mtu aliyekuwa na ufunguo, Adamu.

> *Akampandisha [Yesu] juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, "Nitakupa wewe enzi hii yote, na*

> *fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako."*
>
> — Luka 4:5-7

Unaweza kuona katika mstari huu kwamba Shetani anadai kwamba mamlaka na fahari (mali) ya falme za wanadamu amepewa yeye. Anadai mamlaka kamili juu ya dunia inapohusu wanadamu. Kwa hivyo ni nani aliyempa mamlaka haya? Ni yule aliyekuwa nayo, ambaye ni Adamu! Hivyo Mungu hawezi kuingilia mambo ya wanadamu bila mlango wa kisheria, au itakuwa ni kinyume cha sheria. Shetani atadai kutofanyiwa haki. La, Mungu hana budi kupitia mlango uleule ambao Shetani alitumia, kupitia kwa mwanamume au mwanamke aliye duniani.

## Yesu Hangeweza Kuwaponya—Somo Lenye Nguvu Lafunuliwa

> *Yesu akawaambia, "Nabii hakosi heshima, isipokuwa katika nchi yake mwenyewe, na kwa jamaa zake, na nyumbani mwake." Wala* ***<u>hakuweza kufanya mwujiza wowote huko</u>****, isipokuwa aliweka mikono Yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya. Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao. Akazunguka-zunguka katika vile vijiji, akifundisha.*
>
> — Marko 6:4-6

Nikiuliza watu barabarani ikiwa Yesu angeweza kufanya chochote, labda watasema angeweza. Lakini nikiwauliza kama kuna mahali popote katika Biblia ambapo Yesu alijaribu lakini hakuweza kufanya miujiza, watasema nini? Ninakuhakikishia wataniambia kwamba hakukuwa na tukio kama hilo katika Biblia. Lakini umesoma kuhusu tukio moja kama hilo, sivyo? Yesu hakuweza kuwaponya. Kama mwanasayansi wa mambo ya kiroho, ninataka kujua kwa nini. Jibu ni rahisi kwamba hakuweza, na sasa unajua ni kwa nini. Ilikuwa ni kwa sababu hawakuwa na imani, ambayo ina maana kwamba hapakuwa na makubaliano na mbingu, na hivyo mbingu haikuwa na mamlaka ya kisheria katika hali hiyo. Hakikisha una ufahamu dhahiri wa kile ambacho tumegundua.

**Mbingu hazina mamlaka juu ya dunia isipokuwa moyo wa mwanamume au mwanamke umeshawishika kabisa juu ya kile mbingu inachosema, ambayo ni IMANI.**

Tukirejea maswali niliyouliza katika sehemu ya kwanza ya sura hii

kuhusu maombi yasiyojibiwa, sasa tunapata majibu yetu. Kumbuka, nilitaja hali inayoweza kutokea ambapo mamilioni ya watu wanaweza kuwa wakiomba kwa ajili ya mtu fulani na bado anakufa. Kwa nini? Sababu ya msingi tena ni, hakuna imani. Watu wengi wanakosea wanapofikiri kelele kingi ndicho imani.

> *Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba.*
>
> — Mathayo 6:7-8

Watu wengi huamini kwamba watu wengi wanapoomba, ndivyo uwezekano wa Mungu kusikia na kusukumwa kusaidia unavyokuwa mkubwa zaidi. Natumai tumeshughulikia mengi ya kutosha hadi sasa kiasi cha kukufanya ujue kwamba huu ni uwongo kabisa. Na tunaposema hapakuwa na imani, kimsingi, tunazungumza juu ya yule anayehitaji kupokea kutoka kwa Mungu kuwa na imani.

Kulingana na hadithi yetu ya Marko 6, itabidi ukubali kwamba Yesu alikuwa na imani nyingi, lakini hakuweza kuwaponya. Kwa hivyo ikiwa mimi na wewe tunazungumza kuhusu rafiki mgonjwa ambaye mamilioni ya watu wanamwombea, nitakuuliza, "Mgonjwa anasema nini?" Wajua, hakuna kiasi cha watu ambacho kinaweza kuwa na mamlaka ya kiroho juu ya mtu mwingine. Tunaweza kuwa na watu bilioni 20 wanaomwombea mtu fulani, lakini ikiwa mtu huyo hana imani na anasema atakufa, basi atakufa.

Tena, hebu tufikirie mfano wetu tulioutazama hivi punde katika Marko 6. Tunajua kwamba Yesu alikuwa na imani ya kuponya, lakini hangeweza kuwafanyia watu chochote bila imani yao.

Watu wengi wamekuja kwangu wakisema kwamba bibi yao au babu yao au jamaa ni mgonjwa na kusema kwamba wamekuwa wakimwombea, lakini hakuna mabadiliko. Mimi kila mara huuliza, "Bibi anasema nini? Babu anasema nini? Ana imani?" Wajua, huna mamlaka ya kiroho juu ya mtu mwingine. Unaweza kumhudumia, lakini yeye anapaswa kutumia imani yake mwenyewe. Kwa hivyo kitu cha lazima ninachowaambia watu wafanye kama wanataka kuhudumiwa kwa ufanisi ni kubadilisha mtazamo wao kwanza. Ninazungumza juu ya picha aliyo nayo mgonjwa kuhusu hali yake mwenyewe. Usitoe nukuu nyingi za kidini; wape picha. Hebu nikuonyeshe ninachozungumzia.

*Wanafunzi wa Yohana wakamletea habari za hayo yote. Ndipo Yohana alipowaita wawili katika wanafunzi wake, akawatuma kwa Yesu akiuliza, "Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?"*

*Nao walipofika Kwake, walisema, "Yohana Mbatizaji ametutuma kwako, akisema, 'Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?'"*

*Na saa ile ile aliwaponya wengi magonjwa yao, na misiba, na pepo wabaya; na vipofu wengi aliwakirimia kuona. Ndipo alipojibu, akawaambia, "Nendeni mkamweleze Yohana hayo mliyoyaona na kuyasikia; vipofu wanapata kuona, viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakasika, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, maskini wanahubiriwa habari njema."*

— Luka 7:18-22

Tazama kwamba Yesu hakurejelea Maandiko. Angesema,

"Nyinyi rudini mkamwambie Yohana Andiko hili ama lile." Lakini la, aliwaambia kuhusu mambo yote mazuri yaliyokuwa yakitendeka katika Ufalme wa Mungu. Fanya vivyo hivyo. Mwambie rafiki yako ambaye ni mgonjwa hadithi ya jinsi Yesu alivyomponya mtu mwingine. Ikiwezekana, mwambie hadithi kuhusu mtu ambaye aliponywa kutokana na ugonjwa uleule ulio mwilini mwao. Picha hii itamtia moyo na kuleta matumaini. Matumaini daima huwa na picha, na hii ndiyo picha unayotaka rafiki yako aone, kwamba uponyaji wa ugonjwa huo upo.

**"BASI IMANI, CHANZO CHAKE NI KUSIKIA; NA KUSIKIA HUJA KWA NENO LA KRISTO." – WARUMI 10:17**

Mara rafiki yako atakapoona kwamba anaweza kuponywa, basi atakuuliza jinsi hilo linavyowezekana. Huu ndio wakati ambao umekuwa ukingojea. Badala ya kumhubiria, sasa yuko tayari kupokea maagizo kuhusu Neno la Mungu na kanuni za Ufalme. Kwanza, utataka kumleta katika Ufalme ikiwa hawajazaliwa mara ya pili; na pili, utahitaji kutumia muda pamoja naye kumweleza Maandiko kuhusu uponyaji. Ikiwezekana, mwachie nyenzo fulani ili kusisitiza yale ambayo umemwambia.

Sasa tunajua imani ni nini (makubaliano na mbingu) na kwa nini imani inahitajika kisheria, lakini bado tunahitaji kujua jinsi ya kupata imani na jinsi ya kujua ikiwa tunayo.

## Je, Tunapataje Imani?

*Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*
— Warumi 10:17

Imani hujaje kwa kusikia Neno la Mungu? Mchakato ni upi? Je, kusikia tu Neno ndilo jambo pekee linalohitajika ili imani isitawishwe katika roho ya mwanadamu? Ili kuelewa jinsi imani inavyokuja na kile ambacho Warumi 10:17 inazungumzia, tunaweza kutazama Marko sura ya 4. Sikuzote mimi husema ukirusha Biblia yako hewani, inapaswa kutua kwenye Marko sura ya 4; andiko hili ni muhimu hivyo! Yesu alisema katika Marko 4:13 kwamba usipoelewa kile alichokuwa akifundisha katika sura hiyo, huwezi kuelewa mfano mwingine wowote katika Biblia. Hili ni jambo muhimu sana!

Kwa nini sura hii ni muhimu sana? Kwa sababu inatuambia jinsi mbingu inavyoingiana na ulimwengu, jinsi inavyopata mamlaka, na mahali hilo hutukia. Hakuna kitu muhimu zaidi katika maisha yako kuliko kujua sura hii yote inazungumzia nini.

Katika sura hii, Yesu anatuambia mifano mitatu kuhusu jinsi imani inavyokuja katika roho ya mwanadamu, ambayo ni, kama unavyojua sasa, hitaji la mbingu kuivamia Dunia kihalali. Hadithi tatu katika sura hii ni mfano wa mpanzi, mfano wa mtu anayetawanya mbegu, na hadithi ya mbegu ya haradali. Hebu tuanze kwa kutazama hadithi ya pili ambayo Yesu anasimulia katika Marko sura ya 4, hadithi ya mtu anayetawanya mbegu.

> *Akasema, "Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana nchi huzaa yenyewe; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika."*
>
> — Marko 4:26-29

Jambo la kwanza tunalohitaji kufanya ni kufafanua masharti yetu. Je, ni mbegu gani ambayo Yesu alizungumzia na ardhi ni nini? Yesu alifafanua maneno hayo mawili katika mfano uliotangulia wa mpanzi katika sura hii hii. Mbegu ni Neno la Mungu, na ardhi ni moyo wa mwanadamu au roho ya mwanadamu.

Kwa hiyo katika mfano huu, Yesu alisema mtu hutawanya Neno

la Mungu moyoni mwake. Kisha peke yake, udongo, au moyo wa mwanadamu, huanza kutokeza imani, au mapatano, na mbingu. Sasa, huu ni mchakato wa asili na kazi ya roho yako ya kibinadamu. Utasindika kile ulichoweka humo. Kabla sijaendelea, ni muhimu kukumbuka maana ya imani ni nini: ni wakati moyo wa mwanamume au mwanamke umeshawishika kwa uthabiti kuhusu kile mbingu inasema. Sasa, jambo gumu kukumbuka hapa ni kwamba kukubaliana na mbingu si kitu sawa na kukubaliana kiakili na Neno la Mungu. Biblia inasema kwamba Abrahamu alisadiki kabisa.

**Kusadiki Kikamilifu**

Ili kukusaidia kupata picha dhahiri ya maana ya kusadiki kikamilifu, hebu tuseme nimekuambia uruke kutoka juu ya jengo la Empire State katika Jiji la New York. Ili kukushawishi kujaribu, nikwambie kwamba ukipigapiga mikono yako juu na chini kama ndege kwa nguvu, utaweza kuruka kwa usalama hadi ardhini. Utanicheka waziwazi kwa sababu UNAJUA kitakachokupata. Unajua matokeo bila shaka yoyote. Huko ndiko kusadiki kikamilifu. Unasadiki; hakuna uwezekano mwingine. Utakufa ukiruka.

Hebu tutazame hali nyingine na tuone jinsi utakavyoishughulikia. Tuseme una uvimbe mkubwa sana kwa mwili wako, na daktari amesema una takriban mwezi mmoja wa kuishi: una ugonjwa wa saratani. Daktari kwa kweli amesema kwamba aina yako ya saratani ni nadra sana hivi kwamba hakuna mtu ambaye amewahi kuishi ambaye amegunduliwa kuwa nayo. Sasa, tuseme unajua kile 1 Petro 2:24 inachosema.

> *Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili Wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa Kwake mliponywa.*
>
> — 1 Petro 2:24

Maandiko yanatuambia jibu, lakini wewe na mimi tuna tatizo kubwa. Tulikulia katika ufalme wa giza, na upotovu na kifo vilikuwa vimetuzunguka. Tumekulia katika ufalme wa hofu, tukiwa na hakika kabisa ya kile ambacho hofu inasema. Kwa hiyo katika kielezi kilicho hapo juu, tumezoezwa kwamba saratani inaweza kuua. Tuna ushahidi katika kila matangazo ya vyombo vya habari kwamba hii ni kweli. Kwa hivyo tutabadilishaje makubaliano

yetu; tutasadikije kikamilifu kile Mungu anachosema? Naam, kwa kweli, hatuwezi peke yetu. Lakini Neno la Mungu li hai na limejaa nguvu, na kwa kulipanda katika roho yako, roho yako na Neno huanza kukubaliana na kile ambacho mbingu inasema.

### Makubaliano na Mbingu

*Akasema, "Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana nchi huzaa yenyewe; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika."*

— Marko 4:26-29

Udongo (moyo wako) peke yake, huanza kukubali. Tambua kwamba huwezi kuomba kupata imani; ni kazi ya moyo wako na Neno. Tunapotazama andiko hili, tunaweza kuona kwamba mapatano ya moyo wetu na mbingu ni mchakato; si jambo linalotokea mara moja.

Mfano huu unatuambia kwamba mwanzoni moyo wetu unapopokea Neno, imani huanza kukua, kama vile jani au chipukizi la mbegu iliyopandwa hivi karibuni hukua. Kisha huendelea na kukua kama bua, na kisha huunda kichwa. Kichwa ni mahali ambapo mbegu au matunda yanaanza kuundwa. Mmea unapokuwa katika awamu hii, bado huna chochote cha kula. Mmea haujazaa matunda yake yaliyoiva na kukomaa, lakini unakua.

Ndivyo ilivyo na Neno la Mungu. Hakuna mabadiliko yanayoonekana katika ulimwengu wa asili wakati imani inakua. Bado hakuna makubaliano, lakini hakika mmea unakua, imani itaingia, na makubaliano yatafanyika. Yesu anaendelea kueleza kwamba mbegu katika kichwa inapokomaa au kuiva, wakati wa mavuno umefika, makubaliano yapo, na sasa imani ipo.

Kwa hivyo elewa hili. Unapopanda mbegu kwenye ardhi, kupitia kwa mchakato wa kuchibuka, mmea huanza kukua, ingawa bado hakuna matunda. Mmea unaendelea kukua kwa muda mrefu ikiwa uko katika mazingira sahihi; nao unapokomaa, huzaa matunda yake. Tuseme umelima mahindi. Mmea wa mahindi huchipua suke la mahindi, lakini mwanzoni, ni suke dogo tu la mahindi lisilo na mahindi usiyoweza kula. Lakini baada ya muda, nafaka kwenye sikio hukomaa na kuiva. Sasa pata hili! Wakati huo punje ya mahindi kwenye sikio inalingana na punje ya mahindi iliyopandwa ardhini, kuna makubaliano.

**Mbegu iliyo kwenye kichwa cha mmea inapokomaa, huonekana sawasawa—SAWASAWA—na ile iliyopandwa.**

Panda mmea wa mahindi, na mbegu iliyokomaa kwenye sikio itafanana na ile uliyoipanda. Zinafanana. Zinafanana na zina ladha sawa; huwezi kuzitofautisha.

Kwa hivyo hebu nifafanue kile Yesu alichosema. Tunaposikia Neno la Mungu (Warumi 10:17), tunalitawanya ndani ya utu wetu wa roho, yaani mioyo yetu. Tukiliweka Neno hilo mioyoni mwetu, litakua na kukomaa; na litakapokomaa, mioyo yetu itasadikishwa kikamilifu kuhusu kile ambacho mbingu imesema. Mbingu na nchi zinalingana, na mbingu sasa zimepata mamlaka ya kisheria katika ulimwengu kupitia kwa mtu ambaye amesadiki kikamilifu. Mawazo na imani yetu vyote vinalingana kabisa na kile mbingu inasema kwa ujasiri kamili. Hili si jambo la kiakili. Hiki sasa kimekuwa kile tunachoamini kwa hakika kama vile tunavyoamini kwamba jiwe huanguka linapoangushwa. Mbingu hupanda Neno katika ulimwengu ambapo litasababisha makubaliano na mapenzi ya Mungu. Mbingu zikisema umeponywa, basi hilo Neno likikomaa moyoni mwako, utakachokiona ni kile mbingu zinachosema. Hakuna hofu tena. Ukifumba macho utajiona umepona! Hii ndiyo sababu Waebrania 11:1 inasema:

> *Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni <u>bayana ya mambo yasiyoonekana.</u>*

Unaweza kukosa kuyaona katika hali ya kawaida, lakini umeyaona katika roho yako, na ni halisi, ni kama umeyashikilia mkononi mwako. Makubaliano hayo yanaitwa imani, na imani hiyo husababisha picha hiyo kutokea hapa duniani, katika maisha yako!

## Kubonyeza Swichi

Lakini subiri; Marko sura ya nne haimalizii hapo. Baada ya kutufundisha jinsi mioyo yetu inavyokubaliana na mbingu na imani kuingia, inatupa maelekezo ya jinsi ya kuvuna matunda hayo.

> *Hata matunda yakiiva, mara **<u>atapeleka mundu</u>**, kwa kuwa mavuno yamefika.*
>
> — Marko 4:29

Tambua kwamba ingawa moyo unakubaliana na mbingu na kuna imani, bado hakuna kinachotokea. Kwa nini? Vile tumekuwa tukisema wakati wote, una mamlaka ya kisheria hapa katika ulimwengu. Je, unakumbuka mazungumzo yetu juu ya Luka 8 kuhusu mwanamke aliyetokwa na damu? Kumbuka Yesu alisema, "Binti, imani yako imekuponya"? Nilisema basi binti huyo alitambua mbele za mbingu, ya kwamba kwa sababu alikuwa binti wa Ibrahimu, alikuwa na haki za kisheria.

Nililinganisha hili na kuwa na nyaya kutoka kwa kiwanda cha nguvu za umeme zilichounganishwa na nyumba yako. Umeme upo lakini unapaswa kuwasha taa kibinafsi. Ndivyo ilivyo pia katika hili. Imani inapoimarika, nguvu zipo, lakini hakuna kitakachotokea hadi ubonyeze swichi. Unapaswa kuachilia nguvu za Ufalme wa Mungu hapa duniani kwa sababu ni wewe tu, mwanamume au mwanamke uliye duniani, unayeweza kufanya hivyo kisheria. Kanuni hii haswa ndiyo uliyoitumia ulipookoka, kama Warumi 10:10 inavyosema.

**UNAPASWA KUACHILIA NGUVU ZA UFALME WA MUNGU HAPA DUNIANI KWA SABABU NI WEWE TU, MWANAMUME AU MWANAMKE ULIYE DUNIANI, UNAYEWEZA KUFANYA HIVYO**

*Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*

— Warumi 10:10

Kwa moyo mtu huamini Neno na kupata haki. Kupata haki kunamaanisha kushughulikiwa kisheria. Kwa hiyo wakati moyo wa mwanamume au mwanamke unakubaliana na mbingu, wakati anaamini kile mbingu zimesema, yeye huhesabiwa haki mbele za mbingu na nchi. Sasa ni halali kwa mbingu kuingilia maisha yake na kuathiri dunia kwa niaba ya Ufalme wa Mungu. Lakini cha ajabu, ingawa sasa ni halali na ana imani, bado hakuna kinachotokea. "Lakini, Gary, nilifikiri ulisema ikiwa nina imani, italeta mamlaka ya kisheria ya mbingu hapa." Sahihi, lakini mtu anapaswa kuachilia mamlaka ya mbinguni hapa mara imani inapokuja. Hebu tuangalie Maandiko yetu kwa mara nyingine.

*Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa* ***<u>kinywa hukiri hata kupata wokovu</u>****.*

— Warumi 10:10

Sasa ukiwa na imani au kuhesabiwa haki, ni halali kwa mbingu kuivamia Dunia, lakini angalia kwamba andiko linasema kwamba ni kwa kinywa chako utakiri na kuokolewa. Je, unaona sehemu hizo mbili? Sehemu ya Mbingu ni kuleta Neno ndani ya moyo wako ambapo litaleta mapatano hapa ulimwenguni. Kisha makubaliano au imani vikishakuwepo, lazima utende kulingana na makubaliano hayo na uachilie mamlaka ya mbinguni katika hali yako ili kupokea kile ambacho mbingu imesema. Maandiko yetu katika Marko 4:29, yanasema mavuno yanapokuja, mtu (aliye duniani) huweka mundu ndani. Yeye ndiye anayepaswa kutenda kulingana na Neno la Mungu mara imani inapokuja na kupokea mavuno hayo.

## Kupokea katika Ufalme wa Mungu

Hebu nirudi nyuma nizungumze kwa muda kuhusu mundu iliyo hapa katika Marko nne. Ninaamini kwamba wengi katika kanisa hawajafundishwa jinsi ya kutumia mundu, maana yake hawajafundishwa jinsi ya kuvuna kile wanachohitaji. Sikujua hilo pia hadi Bwana alipoanza kunifundisha kuhusu utendaji wa Ufalme. Hapa kuna hadithi ya jinsi nilivyopata ufunuo wangu wa kwanza wa mchakato huu muhimu katika Ufalme.

Nilialikwa kuhubiri katika kanisa moja huko Atlanta. Ilikuwa ibada ya Jumatano jioni; kanisa halikuwa kubwa, na hilo lilikuwa sawa kwangu. Nilipenda sana kuwafundisha watu kuhusu Ufalme. Nilipofika kanisani, niliona ajabu kwamba milango ilikuwa imefungwa na hakukuwa na mtu. Ilikuwa dakika kumi kabla ya ibada kuanza. Nilisikia lori kubwa sana nyuma yangu, na nilipotazama, niliona lori kuukuu likiingia nyuma ya uchochoro wa kanisa. Sikufikiria chochote juu yake; maana, nilikuwa jijini Atlanta.

Nilipokuwa nikingoja, mwanamume mmoja alikuja kutoka nyuma ya jengo na kujitambulisha kuwa mchungaji. Alisema anasikitika kwa kuchelewa, lakini lori lake kuukuu lilimpa shida kuwaka. Aliniambia ni lazima aliwashe kwa kuliviringisha chini ya kilima maana kifaa fulani cha injini kilikuwa kimeharibika. Aliendelea kusema kwamba wakati mwingine haikuwa ikiwaka kabisa, na ilimlazimu kutembea maili tano hadi kanisani. Inabidi nikiri kwamba nilishangazwa kidogo na mazungumzo haya.

Aliendelea kueleza kwamba kanisa hili kwa kweli lilikuwa huduma ya uenezi na kwamba alilisha maelfu ya watu kila mwezi, kwa kawaida jumla ya milo 10,000 kwa mwezi, kutoka mahali hapo. Mchungaji alipokuwa akizungumza nilifadhaika sana. Hapa kuna mtu wa Mungu anayelisha watu 10,000 kwa mwezi, na hana hata gari la heshima? Ningeweza kutatua shida

hiyo. Nilikuwa na gari mpya sana yenye maili 20,000 nyumbani ambayo ningempa. Nilimweleza mpango wangu na kwamba ningemtuma mmoja wa wafanyakazi wangu kumletea gari. Yeye, bila shaka, alifurahi sana.

Nilitumia jioni hiyo kumfundisha yeye na kanisa lake dogo kuhusu Ufalme wa Mungu na jinsi unavyofanya kazi kuhusiana na pesa. Nilijua ilikuwa muhimu waanze kuonyesha jinsi Ufalme ulivyo kwa wale waliouhitaji sana.

Niliporudi nyumbani, nilipanga gari lipelekwe hadi Atlanta. Wakati mfanyakazi wangu alipokuja kuchukua gari, nilijua kwamba nilikuwa nikifanya shughuli ya kiroho mbinguni. Nilijua kwamba nilipoachilia gari hilo katika Ufalme wa Mungu, ningeweza kumwamini Mungu kupata gari nililohitaji pia. Mimi sio mtu wa magari, maana yake sivutiwi na magari. Kuna watu wanaovutiwa, lakini si mimi. Kwa hiyo mfanyakazi wangu alipokuja kulichukua niliweka mkono wangu juu ya gari hilo, na nikasema, "Baba, ninaachilia gari hili kwa kazi yako huko Atlanta. Ninapoliachilia, ninalipanda kama mbegu na ninaamini kwamba nimepokea____________________." Sikuweza kufikiria gari ambalo nilitaka. Kwa hivyo nikasema, "Nitarudi kwako juu ya hilo!"

Kweli, kwa miezi michache iliyofuata, sikufikiria gari sana, lakini asubuhi moja, nilimuuliza mke wangu Drenda aina ya gari ambalo angependa. Baada ya kufikiria kidogo, alisema kuwa gari lenye paa la kukunja au linaloweza kutenganishwa lingekuwa nzuri. Naam, nilimuuliza ni aina gani alitaka, na hakuna hata mmoja wetu ambaye angeweza kufikiria aina yoyote ya magari yaliyopo. Kwa vile nilitaka kumnunulia Drenda gari, nilitaka kuhakikisha kwamba alipata gari alilolipenda. Nilimwambia aangalie mtandaoni au atazame kote na anijulishe ikiwa alipata ile aliyoipenda. Hatukumwambia mtu yeyote kuhusu shauku yetu ya kupata gari jipya, lakini wakati huohuo, tulikaa macho tulipokuwa tukizunguka huku na huko, tukitafuta gari ambalo lingeweza kutuvutia.

Siku moja, tulikuwa tukiingia kwenye mkahawa fulani katika eneo hilo kwa ajili ya kupata chakula cha mchana, na ghafula, Drenda akapaza sauti, "Ndiyo ile! "Ndiyo ile nini?" Nikauliza. "Gari ninalopenda." Alikuwa akielekeza kidole upande wa sehemu ya maegesho, kwa hivyo nilizungusha gari letu katika eneo hilo na kusimama nyuma ya gari aina ya BMW 645Ci, gari nzuri bila shaka. Na ninaweza kuongeza gari la gharama kubwa pia. Nilimpongeza kwa chaguo lake na kumwambia lilikuwa gari zuri.

Sasa, unahitaji kujua kwamba mimi na Drenda huwa hatutumii pesa

nyingi kununua magari. Kama nilivyosema, sijawahi kuwa mtu wa magari. Maana ninafanya kazi katika eneo la fedha, nilijua pia jinsi zinavyopungua thamani haraka na kwamba ilikuwa bora sikuzote kununua gari ambalo lilikuwa na umri wa mwaka mmoja hadi miwili. Kwa hiyo huo ndio uliokuwa mpango wangu; ningetafuta gari nzuri iliyotumika.

Vema, baada ya juma moja, kijana mmoja kutoka kanisani alinipigia simu na kusema maneno haya, "Nimepata gari la Drenda!" Nilishangaa kwa sababu hatukuwa tumemwambia mtu yeyote kuhusu BMW tuliyoiona siku ile katika chakula cha mchana. Kwa hivyo nilimuuliza ni gari aina gani, akasema ni gari aina ya BMW 645Ci, ile haswa tuliyoitaka. Alisema alipokuwa akizunguka huku na kule, aliliona, na Bwana akamwambia ni gari la Drenda. "Sawa, sasa una usikivu wangu," nilimwambia. Gari lilikuwa limetumika kwa mwaka mmoja na lilikuwa katika hali nzuri sana. Nilililipia pesa taslimu, na Drenda akapata gari lake.

Ajabu, hilo lilitendekaje?

Hebu tulinganishe hadithi hii na yale tuliyojifunza kuhusu kuwa na imani na kutumia mundu. Nilipotoa gari langu, nilikuwa na imani. Lakini Drenda aliposema kwa sauti, "Ndiyo ile!" alikuwa akitumia mundu, kisha baada ya siku chache, gari likatokea. Ingawa nilimsikia akisema kwa sauti, "Ndiyo ile!" Sikuhusisha tamko lake na Marko sura ya nne na kutumia mundu. Lakini tukio hili linalofuata lilifanya jambo hili liwe wazi kabisa.

## Nguvu ya Maneno Yako

Kama nilivyosema, ninamiliki ekari 60 na takriban ekari 10 ni ardhi yenye majimaji. Ninapenda kuwinda katika msimu wa joto, na hata ingawa nilikuwa nimewinda bata katika shule ya upili, kwa kweli sikuwa nimefanya uwindaji wowote wa bata kule Ohio. Lakini mwaka huo, bwawa lilikuwa limejaa maji, na makundi makubwa ya bata yaliendelea kurukaruka ndani yake. Mamia kwa siku yalikuwa yakija kulala usiku. Kwa hiyo nilichukua bunduki yangu usiku mmoja na kwenda nje na kuwa na wakati mzuri wa kuua bata wachache kwa ajili ya chakula cha jioni.

Katika msimu wa vuli mwaka huo, mimi na vijana wangu tulifurahia uwindaji mzuri wa bata. Jambo moja nililoona, hata hivyo, ni kwamba wakati mwingi, bata walikuwa umbali ambao risasi zangu hazingewafikia vizuri. Wakati wa kuwinda bata, kisheria unaruhusiwa kutumia risasi za chuma kinyume na risasi za jadi. Risasi za kawaida ni nzito na huhifadhi nishati yake mbali zaidi kuliko risasi ya chuma, na hivyo basi kukawa na

tatizo la kupiga risasi wakati wa kuwinda bata.

Lakini wakati huo nilipokuwa nikizungumza na wawindaji-bata wenzangu wachache, waliniambia kuhusu bunduki mpya ambazo zimeundwa kwa ajili ya kuwinda bata tu. Walikuwa na uwezo wa kufyatua risasi nzito zaidi na walikuwa wamevaa mavazi ya kuwaficha pia. Nilipendezwa sana na uwezekano wa kununua moja ya bunduki hizo, lakini ilikuwa Desemba, na msimu wa kuwinda bata ulikuwa unakaribia kuisha, kwa hivyo sikufikiria zaidi juu jambo hilo.

Mapema Januari, kwa bahati nilikwenda kwa duka la bidhaa za michezo liitwalo Cabela kutafuta kitu fulani, na nikakumbuka bunduki zile za bata. Nilitaka kuona moja. Kwa hiyo nilipokuwa nikitoka nilipitia sehemu ya bunduki hizo, na nikaona sehemu kamili ya bunduki mpya za kuwinda ndege wa majini. Nakumbuka, bila kufikiria juu yake, nilinyoosha kidole changu kwa ile iliyoonekana bora na kusema kwa sauti kubwa, "Bwana, nitaichukua hiyo." Sikuwa nimefikiria juu yake nilipotamka hilo; maneno yalitoka mdomoni mwangu tu. Msimu wa bata haukufunguka tena hadi msimu wa vuli, kwa hivyo sikupanga kununua bunduki hadi msimu ulipokaribia kidogo.

Baada ya majuma mawili, nilialikwa kuwa mnenaji katika mkutano fulani wa biashara. Nilipomaliza, Mkurugenzi Mtendaji alinishukuru na kusema walikuwa wameninunulia zawadi. Na cha kushangaza ni kwamba, alileta bunduki ileile, muundo haswa, niliokuwa nimeona wiki mbili awali katika lile duka. Kwa kweli, nilishangazwa kabisa na zawadi hiyo ya ukarimu, lakini nilijua hii haikuwa bahati tu. Nilikumbuka nilichosema nilipokuwa kwenye lile duka na kugundua nilichokuwa nimefanya. Nilikuwa nimetumia mundu!

> *Akasema, "Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana nchi huzaa yenyewe; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. Hata matunda yakiiva, <u>mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika</u>."*
>
> — Marko 4:26-29

Kupeleka mundu kunaonyesha kanuni ileile kuhusu imani ambayo tulizungumzia awali katika Warumi 10:10.

> *Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa*

*hukiri hata kupata wokovu.*

— Warumi 10:10

Kwa moyo wangu niliamini, na kwa kinywa changu niliachilia Ufalme ulimwenguni. Nilikuwa nimetoa zaidi ya bunduki 30, lakini hii ilikuwa mara ya kwanza ambapo nilikumbuka kusema kwa sauti, "Nitaichukua hiyo." Lakini nilipofikiria jambo hilo kwa dakika moja, kulikuwa na wakati mwingine mmoja tu ambao nilikuwa nimefanya jambo lilelile—lakini wakati huo, sikujua kuhusu utendaji wa Ufalme.

Mimi na Drenda tuliporudi Ohio, tulikuwa tumetoka Oklahoma ambapo uwindaji wa kulungu ulifanywa kwa bunduki ndefu. Lakini huko Ohio, hizo bunduki ndefu hazikuwa halali; bunduki ndogo tu zinazotumia vipande vidogo vya chuma kama risasi ndizo zilizoruhusiwa. Mwaka wa kwanza tulipohama nilikuwa na bunduki ndogo yenye sehemu mbili za kuweka risasi ambayo nilitumia na kufanikiwa kuvuna kulungu wawili. Lakini kwa kweli nilitaka bunduki nzuri ambayo imeundwa mahsusi kuwinda kulungu. Nilikumbuka kwamba baada ya msimu huo wa kwanza wa kulungu huko Ohio, nilikuwa nimetoa maoni kwa Drenda kwamba nilitaka sana bunduki aina ya Remington 11-87 yenye mwili mweusi wa plastiki kwa ajili ya kuwinda kulungu. Krismasi ilikuwa baada ya majuma machache, na nilishangaa wakati babangu alinipa bunduki hiyohiyo kama zawadi ya Krismasi. Hata sikuwa nimemtajia hitaji langu la bunduki. Nakumbuka nikiwaza, "Ajabu, hili linashangaza." Nilikuwa nimeitumia mundu bila kujua.

SURA YA 4

# JE, HUKUMBUKI?

Ikiwa utaishi maisha yaliyojaa mikakati na ushindi unaoongozwa na Roho Mtakatifu, kwanza, lazima uzaliwe mara ya pili, kisha ubatizwe na Roho Mtakatifu. Ndio, ni kazi mbili tofauti kabisa za Roho yule yule. Ikiwa hili ni jambo geni kwako, hamna shida. Nitakueleza mambo yote. Lakini wacha niende moja kwa moja kwenye hoja muhimu, Yesu alisema ni bora sana kuwa na Ubatizo wa Roho Mtakatifu kiasi cha kusema kwamba mtu hapaswi kuondoka nyumbani bila hilo! Tena, sikusema hivyo; Yesu ndiye aliyesema hivyo katika Matendo 1:4-5.

Nilikuwa Tulsa, Oklahoma, wakati Mungu aliponionyesha jinsi ya kuwinda kwa imani nilipomuua yule dume mwenye pembe sita. Na kama nilivyowaambia, tulihamia Ohio mwaka uliofuata. Ohio ilikuwa kulungu wengi na uliruhusiwa kuua kulungu wawili ambao mmoja tu ndiye alipaswa kuwa dume. Kwa hivyo nilipohamia Ohio, nilianza kutoa matoleo kwa ajili ya kuvuna kulungu wawili, dume mmoja na kulungu wa kike mmoja kila mwaka. Na kama saa inavyofanya kazi, ndivyo nilivyowapata.

Lakini mwaka mmoja, niliona jambo lililonishangaza. Niliwaza, "La, hii haiwezekani." Msimu wa kulungu ulipokwisha, niliona kwamba kulungu alikuja kwa utaratibu niliokuwa nimewaandika kwenye hundi yangu nilipopanda mbegu yangu. Kwa mfano, ikiwa niliandika "kwa ajili ya kulungu dume na kulungu wa kike," dume alikuja kwanza kisha wa kike. Nilipotafakari misimu michache ya awali huko Ohio, niliwaza kwamba jambo hili lilikuwa likitokea kila mwaka. Sikuwa na uhakika kwa vile sikuwa nimetilia maanani sana, lakini kwa sababu moja au nyingine, nilijiuliza ikiwa hii ilikuwa kweli.

Kwa hiyo mwaka uliofuata, niliamua kuwa makini ili niweze kujua. Ninakubali lilikuwa wazo la kichaa, lakini niliona lilifanya kazi, na nisingejua kamwe isipokuwa ningefanya majaribio machache. Kwa hiyo nilibatilisha agizo hilo nilipotoa matoleo mwaka huo. Wakati huu, niliweka kulungu wa kike kwanza kwenye orodha. Hadi wakati huo nilikuwa nikiandika matoleo ya dume kwanza wakati wa kupanda mbegu yangu. Kwa hakika, huo ulikuwa utaratibu waliofuata walipokuja. Kwa hiyo mwaka uliofuata, nilifanya hivyo tena, na walikuja kwa utaratibu ambao niliandika. Sikuwa nimewahi kufikiria kwamba kitu kama hiki kingeweza kutokea. Je, Ufalme ni mahususi hivi?

Ili kujua ikiwa hili lilikuwa kweli linafanyika au ilikuwa bahati tu, niliamua kujua kwa uhakika kwa hivyo nilifanya jaribio la kina zaidi. Mwaka huo, nilitoa matoleo yangu kwa ajili ya dume mwenye pembe saba. Nilijua kwamba kulungu wa kawaida, angekuwa na pembe sawa pande zote mbili, kwa hivyo nilichagua nambari isiyo ya kawaida na nambari kamili. Kwa hivyo mimi na Drenda tulitoa matoleo kulingana na hilo, ingawa hili linasikika kama jambo la kushangaza sana. Tuliomba na kuachilia mbegu yetu kwa ajili ya dume mwenye pembe saba.

## Imani Ni Hususa Vipi?

Oktoba hatimaye ilifika, na msimu wa kutumia upinde katika uwindaji ukafunguliwa. Kwa kawaida, nilitazamia sana kuingia msituni na upinde wangu, lakini niligundua kwamba nilihisi isivyo kawaida msimu ulipofunguliwa. Sikuwa na hamu ya kwenda. Hisia ilikuwa yenye nguvu, na cha ajabu, nilijua wakati wa kwenda kuwinda haukuwa umefika. Wakati huo, niliwaza kwamba ukosefu huu wa hamu ya kwenda kuwinda ungeondoka kadiri msimu ulivyoendelea na majani kuanza kuanguka. Lakini hilo halikufanyika na singeweza kueleza kwa nini; sikuwa na hamu ya kwenda hata kidogo. Nakumbuka nikifikiria, “Hivi ndivyo inavyokuwa unapozeeka, unaacha kufanya mambo?” Yaani sikuweza kueleza hisia hii niliyokuwa nayo. Ilikuwa ni kama sikujali kama ningeenda tena kuwinda kulungu. Kweli, sasa Novemba ilikuwa imefika, na nilikuwa na wasiwasi kidogo. Tayari nilikuwa nimekosa wakati mzuri zaidi msituni na hali-joto nzuri zaidi ya hewa, ikiwa naweza kuongeza. Ilikuwa katikati ya Novemba, na bado sikuwa na hamu ya kwenda kuwinda kulungu. Nilijiuliza kama ningetoka hata kidogo; ndivyo nilivyohisi.

Wazazi wa Drenda walikuwa wameanza safari kwa gari kutoka

Alabama ili kuja kukaa nasi kwa siku kadhaa. Tulipokuwa tumeketi sebuleni tukizungumza, ghafla nilipata ufahamu kwamba siku iliyofuata ndiyo iliyokuwa ya kwenda porini. Ni kama swichi iliwashwa. Niliwaambia wote kwamba nilipaswa kwenda kumchukua kulungu wangu asubuhi iliyofuata. Ghafla, nilisisimka na kuwa na matarajio huku nikitayarisha vifaa vyangu kwa ajili ya asubuhi iliyofuata.

Nilijua kwamba kulungu wangu mwenye pembe saba angekuwepo. Kisha nikaelewa. Kulungu wenye pembe saba huenda hawakuwepo mnamo Oktoba, na hawakuwepo siku iliyotangulia. Huenda ndiyo sababu sikuhisi kwenda kuwinda kulungu. Naweza kufikiria jinsi ingekuwa vigumu kusubiri kwa mwezi mmoja na nusu ikiwa ningetazama nje ya dirisha langu kila siku kwa mwezi na nusu nikitamani kuwa huko. Hilo lingekuwa la kukatisha tamaa. Kwa wakati huu, kila kitu kilikuwa nadharia tu, lakini nilikuwa karibu kufanya jaribio asubuhi iliyofuata.

Kulikuwa na giza nilipoamka asubuhi hiyo, na nilikuwa nimesali usiku kuhusu kisimamo cha mti ambacho kingenifaa. Nina visimamo kadhaa kwenye shamba langu, na nilipokuwa nikisali kuhusu jambo hilo, nilihisi kwa hakika kwamba nilipaswa kwenda kwenye eneo la kinamasi. Tunakiita kisimamo cha kinamasi kwa sababu kinapakana na takriban ekari kumi za kinamasi upande mmoja na kichaka cha nyasi upande ule mwingine. Nilijua kwamba kulungu wakati fulani hupita kando ya ukingo ili kuepuka bwawa. Kisimamo hicho kilikuwa kimenipa matokeo mazuri katika siku za nyuma, na nilitarajia kabisa kuona kulungu wangu kwenye eneo hilo siku hiyo.

Nilipokuwa nikielekea huko, nilijikumbusha yale ambayo Mungu alikuwa amenionyesha katika nyakati za awali kuhusu Ufalme Wake kupitia kwa kuwinda kulungu, na nilihisi alitaka kunifundisha mambo zaidi. Nilifurahia kuona matokeo ya jaribio langu.

Mwangaza wa asubuhi ulikuja polepole, na sauti za kawaida na harufu za asubuhi ya msimu wa vuli zilikuwa mabadiliko mazuri katika maisha yangu. Kwa kweli nilikuwa nimeyakosa yote. Ilikuwa karibu saa moja asubuhi, na hakukuwa na dalili ya kulungu. Lakini nilijua kutokana na kutazama kawaida ya kulungu katika shamba langu kwamba kulungu walikuja katika eneo hilo baada ya asubuhi maana lilikuwa eneo nzuri la matandiko. Ingawa nilikaa kwenye kisimamo kwa muda wa saa moja, mwanga wa kuwinda kisheria ulikuwa wa takriban dakika 40 tu.

Nilipokuwa nimeketi pale nilisikia mlango wa gari ukifungwa kwa nguvu pale nyumbani. Kisha nikakumbuka kwamba wazazi wa Drenda walikuwa wakiondoka asubuhi hiyo ili kurudi Alabama, na nilitaka

kuwaaga. Kwa hiyo, kwa kusitasita, nilishuka kutoka kwenye kisimamo changu, nikifikiri kwamba ingenibidi nitoke siku nyingine ili kumwinda kulungu wangu mwenye pembe saba.

Nilipofika nyumbani, kila mtu alikuwa ameamka na kuwa tayari kunywa kifungua kinywa. Mimi ndiye mpishi wa kiamsha kinywa katika familia yangu kila wakati, na huwa ninapikia kila mtu aliye kwetu kiamsha kinywa karibu kila siku. Basi nikaenda kazini kupika kifungua kinywa huku wazazi wa Drenda wakimaliza kufungasha mizigo yao kwenye gari lao. Bila shaka, waliuliza kuhusu kulungu wangu, na ilibidi niwaambie kwamba niliamua kuacha mpango wangu ili kuwa pamoja nao asubuhi hiyo. Ndio, nilikatishwa tamaa kidogo. Nilitarajia kwamba wangeondoka baadaye kidogo, ili niweze kupata muda wa kumwinda kulungu wangu.

Lakini nilipokuwa jikoni nikikoroga mayai yaliyochanwa, nilitazama nje ya dirisha la jikoni ambalo lilitazama upande wa msitu na mashamba yetu ya nyuma. Nilimwona dume akimkimbiza kulungu wa kike upande wa nyuma wa uwanja, kuelekea moja kwa moja kwenye eneo la kinamasi ambapo kisimamo changu kilikuwa. Nilijua huyo alipaswa kuwa dume wangu. Ghafla nilipiga kelele kwa sauti kubwa kwamba mtu aje kupika na kwamba nilikuwa nimemwona kulungu wangu, na nilikuwa ninaenda kumchukua. Nilijua sikuwa na wakati mwingi.

Ilinibidi nikimbie na kuzunguka shamba kutoka kwa upande tofauti ili kuepuka kuonwa na dume huyo. Niliwaza kwamba labda alikuwa akielekea upande wa kisimamo changu. Nilikimbia haraka niwezavyo kuzunguka uwanja na kufika katika kisimamo changu wala sikumwona kulungu yoyote, jambo ambalo lilinifaa. Nilijua basi kwamba nilikuwa nimewatangulia pale ikiwa, kwa kweli, wangechagua kuelekea upande wangu. Kwa haraka nilipanda kisimamo changu huku moyo ukidundadunda na kijasho kikinitoka.

Ghafla, nilipoketi, walikuja. Kulungu wa kike alikuja akitembea moja kwa moja chini ya kisimamo changu, na nikajitayarisha maana nilijua dume hakuwa mbali nyumaye. Hakika, alikuja. Sikuwa na wakati wa kuthibitisha ikiwa kweli alikuwa na pembe saba au la. Sikuwa na wakati wa kuinua upinde wangu ili kumpiga mshale. Nilipoachilia mshale, nilijua kwamba nilikuwa nimepiga dume lakini chini kidogo, jambo ambalo lilinitia wasiwasi. Dume aliruka ndani ya magugu. Nilingoja kwenye kisimamo kwa takriban dakika 20 na hatimaye nikashuka mti, nikiwa na shauku ya kuangalia mshale ili kuona ikiwa kulikuwa na dalili za kumpiga yule kulungu. Kwa bahati mbaya, kulikuwa na damu kidogo sana kwenye mshale na ardhini.

Nilikasirishwa kidogo, lakini nilifahamu kwamba dume huyo angelala chini kwenye magugu, wala sikutaka kumwondoa hapo haraka. Nimewapiga kulungu katika nyakati za awali na kuona damu kidogo na hivyo kujifunza kwamba jambo bora ni kuwaacha wakae hapo kwa muda fulani. Kwa hiyo nilirudi nyumbani na kumaliza kula kifungua kinywa, huku nikisimulia kila mtu hadithi hiyo, kisha nikawaambia vijana wangu jinsi nilivyohitaji wanisaidie kutembea shambani ili kuona kama tungeweza kumpata yule dume. Matumaini yangu yalikuwa kwamba tupate dume amepigwa vizuri zaidi kuliko jinsi mshale uliovyoonyesha na kwamba huenda tayari alikuwa amekufa. Lakini nilijua kulikuwa na uwezekano ya kwamba nilikuwa nimempiga chini sana na alikuwa amejeruhiwa tu.

Baada ya kungoja kwa masaa mawili, tulitoka nje, na kutapakaa kote shambani. Nilikuwa na upinde wangu tayari ikiwa ningeuhitaji. Ghafla, katika upande wa mbali wa shamba, Tim alimruka yule dume. Hakuwa ameniona na alikuwa akikikimbia kuelekea upande wangu. Alipokuwa akikimbia, ghafla alimwona Tom, kisha akasimama ili kupata athari kuhusu upande wa kuelekea.

Kulungu alikuwa umbali wa yadi 65 hadi 70, mbali sana kwa mishale ya nyakati hizo, lakini mimi nilijua hiyo ilikuwa fursa yangu pekee. Niliinua upinde haraka na kulenga juu ya kulungu na kuuachilia ule mshale. Kwa mshangao wangu, mshale huo uliinama kuelekea kwa dume na kumpiga sawasawa katikati ya shingo yake. Alitoka mbio kuelekea chini ya kilima, mahali asipoonekana. Nilipigwa na butwaa. Ajabu! Tulisogea polepole kuelekea upande ambao dume alikuwa amekimbia, na nikamwona akiwa amelala karibu yadi 100 mbele yetu. Alikuwa imeinua kichwa lakini hakutuona, kwa hiyo tulirudi nyuma na kuamua kurudi baadaye.

**NDIO, UFALME ULIKUWA HUSUSA HIVYO! HAKUNA MTU ALIYEWAHI KUNIAMBIA KWAMBA UFALME HUFANYA KAZI HIVI, KWAMBA UFALME NI MAALUM, NA KWAMBA KWA KWELI TULIKUWA NA MAMLAKA KAMA**

Kweli, baadaye ilikuwa baadaye sana maana nilikuwa na siku nzima mbele yangu kanisani na sikuweza kurejea nyumbani hadi giza lilipoingia. Mimi na Tim tulibeba tochi kisha tukarudi mahali tulipomwona kulungu akiwa amelala. Tulimkuta yadi chache kutoka mahali alipokuwa awali na upesi nikazitazama pembe, na hakika mbele yangu palikuwa na kulungu mwenye pembe saba. Nilimtazama yule dume

kwa mshangao. Mimi na Tim tulimshukuru Mungu kwa ajili ya kulungu huyo, na tulipokuwa tukimkokota hadi nyumbani, tulizungumza kuhusu Ufalme na yale ambayo tulikuwa tumeona.

Ndio, Ufalme ulikuwa hususa hivyo! Hakuna mtu aliyewahi kuniambia kwamba Ufalme hufanya kazi hivi, kwamba Ufalme ni maalum, na kwamba kwa kweli tulikuwa na mamlaka kama haya.

## Ugunduzi Mwingine

Ninakumbuka uwindaji mwingine wa kulungu ambapo nilikuwa nimetoa matoleo yangu kwa ajili ya kulungu dume mdogo. Huyu ni kulungu mwenye umri wa mwaka mmoja, ambaye ana pembe ndogo sana. Kwa sababu ni wadogo sana, kwa mbali, anaweza kuonekana kama kulungu wa kike. Kwa sababu hii, dume hawa wadogo huhesabiwa kama wa kike katika jimbo la Ohio. Tafadhali fahamu, wao sio kulungu watoto. Ni wakubwa kiasi lakini si kama kulungu aliyekomaa.

Kwa hiyo siku hiyo mahususi, nilikuwa kwenye kisimamo changu cha miti, na kundi kubwa la kulungu likaja, wapata kulungu tisa au kumi. Walikuwa mbali kidogo ya uwezo wa upinde wangu lakini walikuwa wakielekea kwangu polepole. Ghafla, jirani yangu akaanzisha gari lake kubwa na sauti hiyo iliwafanya wote wakimbie moja kwa moja kutoka kwangu. Nilisema kwa sauti, "Dume mdogo, nakuamuru urudi na usimame chini ya mti wangu." Kwa hivyo pata picha hii. Lilikuwa shamba la nafaka lililokuwa limevunwa, na kulungu wote tisa walinikimbia mara moja. Kwa neno langu, dume mdogo aliacha kundi, akaanza kukimbia nyuma kwa mzunguko, kisha akaja moja kwa moja chini ya kisimamo changu cha miti, na kusimama! Nilimpeleka yule kulungu nyumbani, na ndio, alikuwa dume mdogo.

Haya ndiyo mambo ambayo nilikuwa nikiyaona mara kwa mara. Nitajadili zaidi kuhusu jinsi Ufalme ulivyo wa kina na mahususi baadaye katika kitabu hiki, lakini kwa sasa, hebu tutambue kwamba jambo la ajabu lilikuwa likiendelea hapa.

Ufalme ulibadili maisha yetu, na hatungeweza kuacha kuwaambia watu kuuhusu. Tuna hadithi nyingi, na tumeona mengi. Tumewaona wafu wakifufuka, uvimbe ukitoweka mara moja, hadithi za ajabu za kifedha, na hadithi za ajabu za ukombozi na mwongozo. Tulipokuwa na njaa ya kuwaambia watu juu ya wema wa Ufalme wa Mungu, mimi na Drenda tulihisi mwongozo wa kuanzisha Kanisa la Faith Life mnamo 1995 ili

kuwasaidia watu kuelewa Ufalme. Kisha Mungu akatuelekeza kuzindua Faith Life Now, ambayo ni huduma yetu ya vyombo vya habari, mnamo 2006, ambayo huonyesha huduma yetu ya runinga katika kila eneo ulimwenguni kila siku. Tuligundua kwamba watu kila mahali wanataka kujua jinsi ya kuishi maisha haya ya Ufalme ya uhuru na ushindi.

## Ufalme wa Mungu Hufanya Kazi kwa ajili ya Kila Mtu

Nilipoketi kuandika sura hii asubuhi ya leo, niliangalia barua pepe zangu. Huwa tunapokea barua pepe kila siku kutoka kwa watu wanaotueleza jinsi Ufalme wa Mungu unavyobadili maisha yao pia. Niliwaza nikuruhusu uwe sehemu ya siku yangu maana barua pepe hii imeingia dakika chache zilizopita.

> Mimi ni nani Mungu anikumbuke? Miaka michache iliyopita, nilianza kusikiliza mafundisho yako, na nimeona miujiza tangu wakati huo. Nimeona uponyaji na miujiza ya kifedha. Hivi sasa, mawazo yangu yameshangazwa kweli ninapotazama huku na huku na kuona wema Wake. Ninaona watu wenye uhitaji na milango iliyofunguliwa kwa Injili na ukweli. Milango imefunguliwa kwa ajili ya ukweli! Na kinachonistaajabisha ni kuona ghala langu limejaa. Amenitajirisha ili niweze kutoa, ili wengine wamwone! Mimi ni mkaguzi wa nyumba aliyejiajiri. Mara kwa mara mimi huwashauri wakaguzi wa nyumba wachanga, na nilianzisha kikundi cha biashara cha Wakristo ambapo tunazungumza juu ya wito wa kuwa wakarimu na kuinua kizazi kijacho... kwamba mfumo wa Ufalme sio mashindano bali utele. Kwa kweli, mafundisho yako yamebadilisha maisha yangu, na sasa yanapitishwa kwa wengine; na kwa kuwa Mungu ameniimarisha, wengine sasa wanasikiliza na kuona utukufu Wake. Inafedhehesha sana kuona kile alichofanya Mungu na jinsi anavyoendelea kutoa. Asante kwa huduma yako!
>
> Kwa unyenyekevu,<br>B.F.<br>Knoxville, TN

Hii ni mojawapo ya aina ya barua pepe tunazopokea kila wakati. Lakini pia sisi huulizwa maswali mengi kuhusu utendaji wa Ufalme. Watu huuliza

jinsi ya kufanya kazi katika Ufalme na kuwa na matokeo kama yale ambayo mimi na Drenda tumeona. Hayo ndiyo madhumuni ya kitabu hiki cha nne katika mfululizo wangu wa "Mapinduzi Yako ya Fedha." Ikiwa una vitabu vyangu vingine, basi unajua nimechukua muda hadi sasa kuzungumzia baadhi ya dhana muhimu ambazo mtu yeyote anayetaka kufanya kazi katika Ufalme anahitaji kujua.

Lakini sasa ninataka kuchimba kwa undani zaidi kazi ya Ufalme na, natumai, kukusaidia kuelewa zaidi jinsi ya kuishi maisha yenye matokeo katika Ufalme. Ninataka kuanza kwa kuweka kile ninachokiita hatua tano za msingi ili kupokea riziki unayohitaji kutoka kwa Ufalme wa Mungu, kama vile Mungu alivyonifundisha.

## Hatua 5 za Kimsingi za Kupokea Riziki Unayohitaji

Hebu tuanze na hadithi katika Marko 8:14–21.

> *Wakasahau kuchukua mikate, wala chomboni hawana ila mkate mmoja tu. Akawaagiza, akasema, "Angalieni, jihadharini na chachu ya Mafarisayo na chachu ya Herode."*
>
> *Wakabishana wao kwa wao, kwa kuwa hawana mikate.*
>
> *Naye Yesu akatambua, akawaambia, "**Mbona mnabishana kwa sababu hamna mikate?** Hamfahamu bado, wala hamjaelewa? Je! Mioyo yenu ni mizito? Mna macho, hamwoni; mna masikio, hamsikii? Wala **hamkumbuki?** Nilipoivunja ile mikate mitano na kuwapa wale elfu tano, mlichukua vikapu vingapi vimejaa vipande?"*
>
> *Wakamwambia, "Kumi na viwili."*
>
> *"Na ile saba kuwapa wale elfu nne, mlichukua makanda mangapi yamejaa vipande?"*
>
> *Wakamwambia, "Saba."*
>
> *Akawaambia, "Hamjafahamu bado?"*
>
> — Marko 8:14-21

Kimsingi, Yesu alikuwa akisema, "Jamani hamkumbuki? Tayari tumeshughulikia hili, na tayari mmeona jinsi tulivyoshughulikia uhaba wa mikate hapo awali. Lakini wanafunzi hawakuweza kuelewa jambo hilo. Kwa hiyo, Yesu aliwaambia wafikirie matukio ya awali. Alikuwa akiwapa dokezo zito. "Fikiria mara ya mwisho tulipokabiliana na hali hii, na hapo ndipo mtapata jibu." Ningependekeza kwamba hili ni jibu letu pia. Ndio, tunaona kwamba mikate na samaki viliongezeka, mtu yeyote angeweza kuona hilo, lakini kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, tunahitaji kuchunguza kwa kina zaidi. Haya yalitokeaje? Kwa hiyo, turudi kwenye hadithi ambazo Yesu alikuwa akirejelea na kutafuta madokezo.

> *Hata zilipopita saa nyingi za mchana, wanafunzi Wake walimwendea, wakasema, "Mahali hapa ni nyika tupu, na sasa kunakuchwa; uwaage watu hawa, ili waende zao mashambani na vijijini kandokando, wakajinunulie chakula.*
>
> *Akajibu, akawaambia, "Wapeni ninyi chakula." Wakamwambia, "Je! Twende tukanunue mikate ya dinari mia mbili ili tuwape kula?"*
>
> *Akawaambia, "Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame." Walipokwisha kujua wakasema, "Mitano, na samaki wawili."*
>
> *Akawaagiza wawaketishe wote, vikao vikao, penye majani mabichi. Wakaketi safu safu, hapa mia hapa hamsini. Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akashukuru, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi wake wawaandikie; na wale samaki wawili akawagawia wote. Wakala wote wakashiba. Wakaokota vipande vilivyomegwa vya kuweza kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia. Na walioila ile mikate wapata elfu tano wanaume.*
>
> — Marko 6:35-44

Nina hakika kwamba wanafunzi walishtuka walipomwomba Yesu awaachilie watu waende kutafuta chakula, aliwageuzia hilo na kusema, "Wapeni ninyi chakula." Katika tukio hili walikuwa zaidi ya watu 5,000. Biblia inasema kulikuwa na wanaume 5,000 huko, kwa hiyo naweza kukisia kwamba kulikuwa na wanawake na watoto huko pia, na wakafanya idadi halisi kufikia watu 15,000 hadi 20,000. Nafikiri mtu yeyote atakubali

kwamba ni watu wengi wa kulisha, haswa bila onyo lolote la haki au maandalizi yaliyofanywa hapo awali.

Bila shaka, ninaamini kwamba Yesu alikuwa na nia ya kuwalisha watu, lakini nafikiri pengine alikuwa na nia ya kuwafundisha wanafunzi Wake katika hali hii kuliko kitu kingine chochote. Ninaamini hii ndiyo sababu aliwaambia, "Wapeni ninyi chakula." Walikuwa wamemwona Yesu akifanya miujiza mingi, lakini sasa ilikuwa zamu yao. Baada ya yote Yeye angeondoka, na Yesu alitaka kuwa na hakika kwamba walijua jinsi ya kushughulikia maisha kwa mtazamo tofauti, mtazamo wa Ufalme.

**YESU ALITAKA KUWA NA HAKIKA KWAMBA WALIJUA JINSI YA KUSHUGHULIKIA MAISHA KWA MTAZAMO TOFAUTI, MTAZAMO WA UFALME.**

### Hatua #1: Una Nini?

*"Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame."*

*Walipokwisha kujua wakasema, "Mitano, na samaki wawili."*

Hapa kuna jambo muhimu. Yesu hakusema, "Hebu tugeuze mawe yawe mkate." Hilo lingekuwa kinyume cha sheria kiroho. Badala yake, aliwauliza walichokuwa nacho tayari. Hasa, alikuwa akiuliza ni kiasi gani cha kile walichohitaji ambacho walikuwa nacho tayari. Alijua kwamba hapakuwa na mikate na samaki wa kutosha kulisha umati huo, na hiyo haikuwa nia ya swali Lake. Sasa, kwa akili ya asili, matarajio yote ya kulisha wale watu yalisikika kama jambo la kichaa. Wanafunzi walijua, bila kuangalia, kwamba hakungekuwa na chakula cha kutosha kulisha watu 20,000 popote walipotafuta. Je, unaweza kuwazia walichokuwa wakifikiria Yesu alipowaambia waende waone ni kiasi gani cha mikate na samaki kilichokuwepo? Kisha warudi na kumpa taarifa kwamba wangeweza kupata mikate mitano na samaki wawili tu? Jambo la kichaa, sivyo?

Hebu nifafanue mazungumzo haya kwa kutoa mfano halisi. Kama mchungaji, nimesaidia familia katika hali ngumu ya kifedha hapo awali, labda kwa kuwasaidia kulipa rehani ya mwezi mmoja au malipo ya kodi, kulipa bili chache za matumizi, au kununua chakula. Lakini hebu tuseme nilijua jibu la kweli halikuwa kuwapa kitini, bali nilijua jibu ni Ufalme.

Mazungumzo yetu yangekuwa kama haya. "Habari Mchungaji Gary,

tumekuwa na upungufu mwingi mwezi huu, na tuko karibu kufukuzwa nyumbani kwetu. Je, kanisa linaweza kutusaidia?" "Hakika, naweza kukusaidia. Huu hapa ndio ushauri wangu. Lipa malipo yote ya nyumba, kisha hamtakuwa na malipo yoyote ya kuwapa wasiwasi." Wangenitazama na kusema, "Mchungaji, hatudhani unaelewa. Hatuna pesa za kulipa malipo ya nyumba yanayofuata, tupilia mbali kuilipia kikamilifu." "Najua," ninajibu, "ndiyo maana niliwaambia mlipie nyumba ili msiwe na malipo yoyote ya nyumba."

Kisha ikiwa ningewauliza waende kuona ni pesa ngapi walizo nazo ambazo zingeweza kutumika kulipia nyumba, wangefikiri kwamba siwajali. Lakini ikiwa katika kunitii walienda na kuangalia na kurudi na kusema, "Tumechunguza maradufu, Mchungaji. Tulichoweza kupata ni $20, lakini salio kwenye rehani ni $360,000." Nafikiri umeelewa jambo hili. Wangefikiri nimerukwa na akili, sivyo?

Lazima iwe hivi ndivyo wanafunzi walihisi siku ile, walikuwa wamechanganyikiwa kabisa. Mikate mitano na samaki wawili kuwalisha watu 20,000?

## MTU HUVUNA ALICHOPANDA

Vema, kabla hatujaingia ndani zaidi katika hadithi hii, ninahitaji kukengeusha kwa muda mfupi ili kufichua sheria nyingine ya Ufalme itakayodhihirishwa sasa hivi. Mkate huzidisha na kuwa mikate, na samaki huzidisha na kuwa samaki wengi. Kwa hivyo andika hili.

**LAZIMA UACHILIE KIASI FULANI CHA KILE UNACHOHITAJI KATIKA UFALME ILI KUKIZIDISHA!**

Hebu nitoe mfano mwingine katika Biblia, kisha nitarudi kwa hadithi yetu katika Marko 6. Hebu tuangalie 2 Wafalme 4:1-7.

> *Basi, mwanamke mmoja miongoni mwa wake za wana wa manabii alimlilia Elisha, akasema, Mtumishi wako mume wangu amekufa; nawe unajua ya kuwa mtumishi wako alikuwa mcha Bwana; na aliyemwia amekuja ili ajitwalie wana wangu wawili kuwa watumwa.*
>
> *Elisha akamwambia, **"Nikufanyie nini? Niambie; una kitu gani nyumbani?"***
>
> *Akasema, "Mimi mjakazi wako sina kitu nyumbani, ila chupa ya mafuta."*

*Akasema, "Nenda, ukatake vyombo huko nje kwa jirani zako wote, vyombo vitupu; wala usitake vichache. Kisha uingie ndani, ukajifungie mlango wewe na wanao, ukavimiminie mafuta vyombo vile vyote; navyo vilivyojaa ukavitenge."*

*Basi akamwacha, akajifungia mlango yeye na wanawe; hao wakamletea vile vyombo, na yeye akamimina. Ikawa, vilipokwisha kujaa vile vyombo, akamwambia mwanawe, "Niletee tena chombo."*

*Akamwambia, "Hakuna tena chombo." Mafuta yakakoma.*

*Ndipo akaja akamwambia yule mtu wa Mungu. Naye akasema, "Enenda ukayauze mafuta haya, uilipe deni yako; nayo yaliyosalia uyatumie wewe na watoto wako."*

— 2 Wafalme 4:1-7

Tazama nabii hakusema, "Vema, hebu twende kwenye hazina tuone kile tulicho nacho." La, alifahamu njia bora ya kutatua jambo hilo. Alisema, "Nikufanyie nini?" Huenda mwanamke huyo alichanganyikiwa kidogo kwa kujibu, "Unaweza kunisaidiaje? Nahitaji pesa!" Lakini nabii hakuwa akijaribu kumdharau. Alikuwa akiuliza swali muhimu sana ambalo alijua lingemletea jibu. Swali hili hili ndilo litakalokupa jibu lako pia.

**"Nikufanyie nini? Niambie, una kitu gani nyumbani?"**

## Una Kitu Gani?

Una kitu gani nyumbani? Nina hakika alishtushwa kidogo na swali hilo kwa sababu alikuwa ameshaeleza kwa nini alikuwa pale.

"Mimi mjakazi wako sina kitu nyumbani," akasema, "ila chupa ya mafuta."

Tazama alichosisitiza, "sina kitu nyumbani." Lakini ni kweli kwamba hakuwa na chochote?

La, kauli yake haikuwa sahihi kikamilifu. Alisema kwamba alikuwa na chupa ya mafuta ya mzeituni. Vizuri sana! Hicho ndicho nabii alikuwa akisubiri kujua.

Na hilo tu ndilo unalohitaji kujiuliza pia. Mungu anahitaji tu kile kilicho chini ya mamlaka yako ya kisheria kufanya kazi nacho.

Basi hebu tuangalie hatua ya kwanza. Utahitaji kumpa Mungu baadhi

ya yale unayohitaji. Unapoyatoa kwa Ufalme wa Mungu, unayabadilishia mamlaka, na kuyaweka chini ya utawala wa kisheria wa Mungu ili yaweze kuongezeka. Tukumbuke kwamba kuzidisha hakumaanishi haswa kile tulichoona katika hadithi hii, kwamba mkate wako utazidisha peke yake ukiwa kwenye kabati lako, ingawa nimeona kitu kama hicho kikitokea. Lakini kwa kawaida, Mungu hufanya njia kwa mkate kuongezeka kupitia kwa mahusiano na watu wengine. Huenda mtu akawa mkarimu kwako, au upate nyongeza hiyo kazini, au utarejeshewa pesa usizotarajia. Mungu anaweza kukuzidishia mkate wako kupitia kwa njia nyingi.

**UNAPOYATOA KWA UFALME WA MUNGU, UNAYABADILISHIA MAMLAKA, NA KUYAWEKA CHINI YA UTAWALA WA KISHERIA WA MUNGU ILI YAWEZE KUONGEZEKA.**

### Unaweza Kutamka Kusudi la Pesa Zako

Ninataka kutaja jambo muhimu sana kuhusu pesa.

**Pesa zinaweza kutumika kama mbegu kwa ajili ya jambo lolote.**

Huwa unatamka kusudi la pesa zako kila siku maishani mwako kila unaponunua kitu. Kwa mfano, ukiwa kwenye duka la chakula kununua mkate, unabadilisha pesa zako na kupewa mkate, au kwa kweli, unaita pesa zako "mkate." Hebu tuchunguze ninachomaanisha. Ikiwa unahitaji mkate, sasa unaelewa sheria ya Ufalme inayoitwa kupanda na kuvuna. Kwa kutumia sheria hiyo, unajua kwamba ukipanda mkate, utavuna mkate. Lakini hebu tuseme kwamba unahitaji mkate, lakini huna mkate wa kupanda. Utafanya nini? Unaweza kupanda pesa na kutaja mkate unapozipanda. Kumbuka, pesa ni mfumo wa kubadilishana tu. Huwa tunazitaja kila siku tunapohitaji chochote iwe ni maziwa, kulipa kodi, kununua viatu au hata chakula. Kwa hivyo unaweza kuzipa pesa zako jina unapozitoa pia.

**Unaweza kutamka kusudi la pesa zako unapozitoa.**

Faith Life Church, hapa New Albany, Ohio, ndilo kanisa ambalo mimi na Drenda tulianzisha zaidi ya miaka 25 iliyopita. Mnamo 2008, tulijenga kituo tunachokiita The Now Center, mahali ambapo Kanisa la Faith Life linapatikana. Ulikuwa mradi wa kutisha ambapo tulitumia dola milioni 6.5, mradi mkubwa kwa watu wapatao 550 kutekeleza.

Kweli, kwa miaka 10 iliyopita, tumelijaza jengo hilo kupita kiasi. Hatuna nafasi ya zaidi ya watu elfu tatu kwa wikendi na kuhudumu katika

ibada nne za moja kwa moja kila wikendi ndiko tu ninakoweza kufanya. Tuliamua kupanua jengo letu la sasa. Ulikuwa mradi wa dola milioni 10 na ungetuwezesha kukua kwa kuongeza ukubwa wa ukumbi wetu na kuongeza nafasi ya watoto. Wakati huohuo, tuligundua kwamba wakati uliohitajika ili kukusanya pesa na kisha wakati uliohitajika kujenga jengo hilo ungekuwa suala. Ilimaanisha kungojea kwa kipindi cha miaka miwili na nusu kabla ya kutumia nafasi hiyo iliyoongezwa.

Kwa kuzingatia hilo, tulihisi kuendelea mbele katika kupanua jengo la kanisa lakini wakati huo huo pia tulianza kutafuta maeneo mengine kwa ajili ya kuanzisha shule, ambalo tulihisi lingekuwa tayari baada ya takriban miezi sita. Tuliamini kwamba kufanya hivyo kungeondoa shinikizo kutoka kwa kanisa kuu na wakati huo huo kulipa fursa ya kuendelea kukua. Kwa hivyo tuliweka timu pamoja ili kuanza kutafuta eneo jipya. Tulichunguza maeneo tofauti na idadi ya watu waliopo na tukapenda eneo fulani ambalo tulihisi lingekuwa nzuri jijini mwetu. Lakini tuliendelea kutafuta na mara kadhaa karibu tufanye uamuzi kuhusu maeneo kadhaa tofauti, lakini tulipoketi chini ili kukubaliana, sote tungehisi kwamba kila kitu hakikuwa sawa. Sisi sote tulihisi tahadhari mioyoni mwetu.

Sasa hebu tusonge mbele muda wa miezi sita, na tukatambua kwamba hatukuwa tumepata mahali pa kuweka shule, tulikuwa jinsi tulivyokuwa siku ya kwanza tulipoanza. Itabidi nikubali, mimi na Drenda tulijaribiwa kukata tamaa kidogo tulipokuwa tukitafuta. Tulikuwa tumeangalia kila mahali katika eneo letu na hatukupata jengo ambalo lingefaa kabisa. Ndio, tulikuwa tumetoa matoleo yetu kama mbegu mwanzoni, na hilo lilitufanya tujue kwamba Mungu alikuwa na jengo kamilifu kwa ajili yetu, lakini hatukutarajia kutumia muda mrefu sana kulitafuta. Hapa kuna kidokezo: jambo kamili wakati mwingine huchukua muda mrefu kupatikana!

Wakati huo nilikuwa nimewekwa kwenye ratiba ya kuhusika katika kipindi kirefu cha runinga ambacho madhumuni yake yalikuwa ni kuchangisha pesa ili kuzindua mtandao mpya wa televisheni. Hiki kilikuwa kipindi cha siku tatu ambacho kingekuwa hewani asubuhi na jioni siku zote tatu. Nafikiri ilikuwa siku ya tatu, wakati nilikuwa nimeketi mbele ya kamera nilipomsikia Bwana akinena nami. Alisema, “Chukua hundi ya $100,000 kutoka kwa kanisa lenu na uipe huduma hii kwa ajili ya kazi yao ya ufikiaji kupitia kwa runinga kama njia ya kuvunja ule mkwamo wa kupata mahali kwa ajili ya shule yetu mpya. Peleka hundi hiyo kwa kila moja ya ibada zenu nne, na kanisa liombee zawadi hiyo unapoitoa, na kutangaza kwamba mahali penu pa shule mpya pamekamilika!” Aliendelea kusema

kuwa nilipoomba nimkemee Shetani na kuamuru kuchanganyikiwa na kuchelewa kukome. Basi tulifanya hivyo katika wikendi iliyofuata katika ibada zetu za Jumamosi na Jumapili.

Siku iliyofuata, ambayo ilikuwa Jumatatu, timu yetu iliyokuwa ikitafuta mahali pa kuweka shule yetu mpya ilisema kwamba wakala wa mali alikuwa amepiga simu na kusema alikuwa amepata taarifa kuhusu chuo cha shule ya upili cha kibinafsi ambacho kilikuwa kikiuzwa. Waliamua kwenda kukikagua. Walipoenda walipata majengo kamili yenye vyumba vya darasa la kwanza hadi kidato cha mwisho cha shule ya upili, pamoja na shule ya chekechea. Mali hiyo ilikuwa imeorodheshwa kwa zaidi ya kiasi cha pesa tulizokuwa tukitaka kutumia, kwa kuwa tulitaka kukodisha ili kuhifadhi pesa za kupanua jengo letu la kanisa kuu. Ingawa bei haikuwa kitu ambacho tungeweza kuzingatia, mimi na Drenda tuliamua kukagua mali hiyo Jumanne asubuhi.

Tulichoona ni mali safi ajabu ya chuo chenye futi za mraba 88,000, majengo manne, mahali pa mazoezi ya kukimbia, chumba cha mazoezi ya kuinua uzani, viwanja vinne vya tenisi, jengo maalum la sanaa, maabara ya sayansi, na kimsingi kila kitu ambacho chuo cha shule ya K-12 kingehitaji. Sehemu ya kushangaza ya hadithi hii ni kwamba ilikuwa imejazwa kamili na vifaa. Drenda na mimi tulishangazwa lakini hatungeweza kununua mali hiyo.

Ilitokea tu kwamba tulikuwa na miadi jioni hiyo na mmoja wa washirika wetu ili kukutana na kuwa na mazungumzo naye. Tulikuwa tumepanga miadi hii ya chakula cha jioni tena na tena pengine mara tatu au nne katika kipindi cha miezi miwili kwa sababu sisi sote tulikuwa na shughuli nyingi. Lakini jioni hiyo tulifanikiwa. Tulipokuwa tumeketi pale katika chakula cha jioni, tulianza kuzungumza juu ya upanuzi wa kanisa kuu. Wenzi hao walituuliza kuhusu jinsi mambo yalivyokuwa yakiendelea, nasi tukawaambia jinsi vibali na ramani vilivyocheleweshwa sana na masuala mengine tuliyokuwa nayo. Tuliwaambia ilionekana kama sehemu hiyo mpya iliyokuwa ikiongezwa haingekuwa tayari hadi mwisho wa 2022 au katika msimu wa masika wa 2023 kadri ya jinsi mambo yaliyvokuwa yakienda.

Mara moja waliuliza ikiwa tulikuwa tumewahi kufikiria kuanzisha shule, na tukasema ndio. Tulieleza jinsi tulivyokuwa tukitafuta kwa muda wa miezi sita awali bila kufanikiwa. Kisha tukawaambia kuhusu ile shule tuliyoikagua asubuhi siku hiyo, huku tukisema kwamba kitu kama hicho kingekuwa sawa, lakini mali hiyo ilikuwa ikikodishwa kwa mamilion ya dola.

Wanandoa hao waliketi hapo na bila wasiwasi walisema, "Naam, vipi yakiwa ya bure?" Kwa kweli mara ya kwanza hatukuelewa walichosema, kwa hivyo waliuliza tena, "Je, vipi yakiwa ya bure?" Tena, tulifikiri walikuwa wanafanya utani, lakini wakati huu bwana huyo akasema, "Drenda, vipi ikiwa mali yangekuwa bila malipo?" "Unamaanisha nini?" tuliuliza. Wakasema, "Tutaandika hundi!" Tulipigwa na butwaa kwa muda tukiwa tumeketi pale. Lakini ili kufupisha hadithi ndefu, walitimiza hilo.

Siku mbili baada ya kutoa matoleo kama mbegu kwa ajili ya shule yetu, Mungu alituelekeza kwenye eneo kamili. Sasa tunamiliki mali ya dola milioni 12 bila kuyalipia wala kuwa na deni juu yake! Ni nani angewahi kufikiria au, kusema kweli, kuwaza hivyo? Baada ya kuona hilo, mimi na Drenda tulikubaliana kwamba hata kwa yote tuliyoyaona, tulipaswa kuwa na mawazo makubwa zaidi. Mungu anaweza kufanya mambo ya ajabu sana!

Nafikiri lazima wanafunzi walihisi hivyo siku ile baada ya kuwalisha watu 20,000 kwa mikate mitano na samaki wawili. Niliweka dau kuwa walienda kulala wakisema, "Ajabu, uliona hilo?"

SURA YA 5

# KUWEZESHA RIZIKI YAKO

Tulizungumza katika sura ya mwisho kuhusu hatua ya kwanza ya kuhusisha sheria ya Ufalme kwa ajili ya riziki yako.

**LAZIMA UYACHILIE BAADHI YA YALE UNAYOHITAJI KATIKA UFALME ILI YAZIDISHWE!**

Nilikuambia kwamba ningejibu maswali kadhaa kuhusu kauli hii, la kwanza likiwa, "Ina maana gani kuachilia kitu katika Ufalme ili kiongezeke?"

Tena, hebu turudi kwenye hadithi yetu katika Marko 6 ili kupata ufahamu zaidi.

> *Hata zilipopita saa nyingi za mchana, wanafunzi Wake walimwendea, wakasema, "Mahali hapa ni nyika tupu, na sasa kunakuchwa; uwaage watu hawa, ili waende zao mashambani na vijijini kandokando, wakajinunulie chakula.*
>
> *Akajibu, akawaambia, "Wapeni ninyi chakula." Wakamwambia, "Je! Twende tukanunue mikate ya dinari mia mbili ili tuwape kula?"*
>
> *Akawaambia, "Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame." Walipokwisha kujua wakasema, "Mitano, na samaki wawili."*
>
> *Akawaagiza wawaketishe wote, vikao vikao, penye majani mabichi. Wakaketi safu safu, hapa mia hapa hamsini. Akaitwaa ile mikate mitano*

*na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akashukuru, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi wake wawaandikie; na wale samaki wawili akawagawia wote. Wakala wote wakashiba. Wakaokota vipande vilivyomegwa vya kuweza kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia. Na walioila ile mikate wapata elfu tano wanaume.*

— Marko 6:35-44

Nataka utambue mambo machache katika hadithi hii usije ukayapuuza. Yesu alipowaambia, "Wapeni ninyi chakula," jibu lao na mwitikio Wake hutuonyesha mojawapo ya funguo muhimu zaidi katika kuelewa Ufalme inapohusu riziki. Walipomjibu, walisema ingechukua zaidi ya mshahara wa nusu mwaka kulisha watu wengi kiasi hicho. Tazama jinsi akili zao zilivyohusisha hitaji lao la riziki na kazi walipokabiliwa na tatizo hilo. Ukweli ni kwamba sote hufanya hivyo. Lakini mawazo haya ya kulipwa dola kiasi fulani kwa kufanya kazi kwa masaa fulani hayakuwepo katika fahamu za mwanadamu kila wakati. Yalikuja wakati wa Dhambi ya Asili. Nahitaji kukurudisha katika Dhambi ya Asili ambapo tunaweza kuona jambo hili likitendeka wazi.

### Mtazamo wa Kulipwa Pesa Fulani kwa Masaa Fulani

*Akamwambia Adamu, "Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, 'Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.'"*

— Mwanzo 3:17-19

Ikiwa unakumbuka, Adamu na Hawa waliwekwa duniani ili kuitawala kwa niaba ya Ufalme wa Mungu. Walitawala kwa mamlaka iliyokabidhiwa. Shetani, ambaye alikuwa duniani tayari, aliwadharau na kutamani mamlaka waliyokuwa nayo. Ingawa Adamu na Hawa walikuwa na mamlaka kamili juu yake, alifaulu kuwadanganya ili waamini kwamba Mungu hakuwa upande wao na hakuwa wa kutegemewa. Aliwaahidi kile kilichoonekana kuwa hatma iliyo bora zaidi, hivyo wakaamua kumfuata yeye badala ya Mungu. Kwa sababu ya uasi wao, walipoteza vyeo vyao vya kisheria katika

Ufalme wa Mungu na kimsingi walimfukuza Mungu kutoka kwa maisha yao, na hivyo kumpa Shetani mamlaka ya kisheria juu ya ulimwengu wote inapohusu wanadamu. Paulo alimwita Shetani mungu wa dunia hii hapa katika 2 Wakorintho.

> *Ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya Injili ya utukufu Wake Kristo aliye sura yake Mungu.*
> — 2 Wakorintho 4:4

Mungu alipomkabili Adamu kuhusu dhambi yake, Mungu alimwambia, "Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa taabu utakula chakula chako siku zote za maisha yako." Kisha ukiruka sentensi moja, andiko linasema, "Kwa jasho la uso wako utakula chakula chako."

Mungu alimwambia Adamu kwamba kwa sababu ya uasi wake, dunia haingezaa kama ilivyokuwa awali. Mikono ya Mungu sasa ilifungwa, na Adamu alilazimika kujitafutia jinsi ya kuishi kwa jasho lake mwenyewe na kazi chungu. Tafadhali kumbuka kwamba Adamu ndiye aliyeilaani dunia, si Mungu. Adamu alikuwa na mamlaka kamili ya kisheria juu ya dunia, na alipoasi dhidi ya Mungu, baraka ya Mungu ililazimika kujiondoa. Ndio maana Mungu akamwambia Adamu, **"Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako."** Bustani aliyoumbwa Adamu kuishi, ambayo ilikuwa imejaa riziki, ilikuwa imetoweka. Kabla ya uasi wake, Adamu kamwe hangekuwa na wazo au wasiwasi juu ya riziki; ilikuwa imetolewa kwa wingi kila mahali alipotazama. Lakini sasa ingemlazimu kutafuta riziki yake mwenyewe kupitia taabu yake mwenyewe yenye uchungu na jasho. Nauita huu mfumo chungu wa taabu na jasho.

**Kazi chungu na jasho sasa vilihitajika ili kuzalisha chakula!**

Dunia sio kitu pekee kilichobadilika. Adamu na wanadamu wote sasa walibadilika. Adamu alipoteza utambulisho wake, kusudi lake, na riziki yake na sasa alikuwa mtumwa wa unusuru. Hivi ndivyo mimi na wewe tulivyolelewa pia, chini ya mfumo chungu wa taabu na jasho.

Kila uamuzi chini ya mfumo huu wa laana ya dunia ni wa unusuru,

**TANGU WAKATI WA ADAMU, WANAUME NA WANAWAKE WAMEKUWA WATUMWA WA UNUSURU, AMA KUKIMBILIA RIZIKI AU KUTUNZA RIZIKI, KWA SABABU KUWA NA PESA NDIO NJIA PEKEE YA KUTOROKA KUTOKA KWA MBIO ZA PANYA.**

na kwa kawaida hutegemea kutafuta pesa au kushughulika na masuala ya pesa. Mahali na jinsi ya kupata riziki tunayohitaji hutawala mawazo na maisha yetu. Kutambulika kwetu, ambako hapo awali kulibuniwa kwa njia ya kipekee na Mungu kwa ajili ya makusudi na kazi zetu hapa duniani sasa kumetekwa nyara na mahali pake pamechukuliwa na hitaji letu la kupata pesa tunazohitaji ili kuishi, sikuzote tukitazamia maandalizi ya siku inayofuata.

## Mfumo wa Utumwa

Uchunguzi wa hivi majuzi nilioona ulisema kwamba zaidi ya 70% ya watu nchini Marekani hawapendi kazi zao. Unaweza kuuliza, "Basi kwa nini wanaenda kazini ikiwa hawazipendi?" Kwa maneno rahisi, wao ni watumwa wa mshahara!

Chini ya laana ya dunia ya kazi chungu na jasho, kila mtu ana ndoto ya kuwa milionea, kutoroka kutoka kwa mbio za panya zisizo na mwisho na shinikizo la kutafuta riziki. Watu huota ndoto ya kushinda bahati nasibu, ndoto ya kuwa tajiri ambapo watakuwa huru kufanya kile wanachotaka kufanya badala ya kile wanachopaswa kufanya. Tangu wakati wa Adamu, wanaume na wanawake wamekuwa watumwa wa unusuru, ama kukimbilia riziki au kutunza riziki, kwa sababu kuwa na pesa ndio njia pekee ya kutoroka kutoka kwa mbio za panya.

Nikupe mfano wa jinsi mfumo huu umetuzoeza sisi sote jinsi ya kufikiri. Nikikuambia kwamba unapaswa kutoka kwa madeni kabisa katika kipindi cha miezi 12 ifuatayo, utaanza moja kwa moja kukokotoa jinsi ya kufanya kazi chungu zaidi na kutokwa jasho ili kutimiza hilo. Utahesabu jinsi unavyoweza kufanya kazi mbili au tatu, ikiwa itahitajika, chochote kitakachohitajika. Na kitakachohitajika ni kazi chungu zaidi na jasho. Taabu yenye uchungu na jasho huhusishwa katika kila ndoto. Ikiwa unahitaji gari jipya, utagawanya gharama ya kazi na jasho na kusema, "La, hatuwezi kuimudu." "Nyumba kubwa zaidi? La, hatuwezi kuimudu."

## Mungu Huona Mambo Yanayowezekana Katika Yale Yasiyowezekana

Chini ya mfumo wa laana ya dunia, ndoto hubadilishwa na safari fupi za kwenda kwa maduka makubwa kisha kula mkate uliowekwa nyama njiani kwenda nyumbani. Na ikiwa huna wakati wa kutosha au hutaki

kufanya kazi ngumu ya kutimiza ndoto yako, unaiacha ndoto na kukubali kwamba unapaswa kuendelea na kazi unayoichukia kama watu wengine wanavyofanya. Kwa watu wengi, taabu chungu na mlinganyo wa kutokwa jasho kwa kawaida huwa na neno *haiwezekani* baada ya ishara ya usawa.

Na hivi ndivyo wanafunzi walivyoona hali yao, "Tuwalishe watu hawa 20,000? Haiwezekani! Hilo lingegharimu zaidi ya mishahara ya miezi sita!" Mshahara hapa ulimaanisha taabu na kazi chungu zaidi kuliko ilivyowezekana ili kukidhi hitaji hilo. Tena, mtazamo wao pekee wa kupata riziki ulikuwa kupitia kwa kufanya kazi. Hivi ndivyo mambo yanavyofanya kazi ulimwenguni. Kila mtu alijua hilo, lakini Yesu alitaka kuwaonyesha njia mpya ya kuishi, Ufalme mpya wenye sheria mpya. Ndio, kuna njia ya kutoroka kutoka kwa mfumo wa kazi chungu na kutokwa jasho. Kunayo kweli!

Hebu turejee wakati wanafunzi waliposema haingewezekana kuulisha umati na tuone jinsi Yesu alivyojibu. Labda unapaswa kuwa na bangili ya ngozi iliyoandikwa FAY (Fanya Alichofanya Yesu) ili usisahau kile atakachotuonyesha kama wanafunzi Wake. Badala ya kukubaliana na utambuzi wa wanafunzi Wake kuhusu hali hiyo, Yesu alichukua mamlaka kwa kuwapa maagizo, "Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame." Sasa, walijua kabla hata ya kutazama kwamba haingetosha kuulisha umati mzima. Hii ndiyo sababu walimwendea Yesu kwanza na kumwomba awaruhusu watu waende kutafuta chakula wao wenyewe. Lakini ili kutii, walienda wakatazama, wakarudi na ripoti kwamba walipata mikate mitano na samaki wawili.

Sasa, jambo lilitokea hapa ambalo lazima uone, kidokezo kingine kikuu! Ili kukiona, nataka kuangalia hadithi hiyo hiyo lakini katika toleo la Mathayo.

> *Yesu akawaambia, "Hawana haja kwenda zao, wapeni ninyi vyakula."*
>
> *Wakamwambia, "Hamna kitu hapa ila mikate mitano na samaki wawili."*
>
> *Akasema, <u>"Nileteeni hapa."</u> Akawaagiza makutano waketi katika majani; akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni, akabariki, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi, wanafunzi wakawapa makutano. Wakala wote wakashiba; wakayaokota masazo ya vipande vya mikate, vikapu kumi na viwili, vimejaa. Nao waliokula walikuwa wanaume wapata elfu tano, bila wanawake na watoto.*
>
> — Mathayo 14:16-21

Angalia katika mstari wa 18 kwamba Yesu aliwaambia wanafunzi wamletee mikate hiyo na samaki. Kisha mwishoni mwa mstari wa 19, tunaona kwamba aliwarudishia wanafunzi Wake mikate ile na samaki. Jambo fulani lilitokea kati ya kauli hizo mbili za Maandiko ambalo lilipaswa kuvutia usikivu wako na kuibua swali: "Kwa nini Yesu aliwaambia wanafunzi Wake wamletee mikate na samaki ikiwa angewarudishia baada ya muda mfupi?" Yesu huwa hafanyi jambo lolote la kidini, kwa hiyo lazima kuwe na sababu aliomba aletewe mikate ile na samaki. Kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, tunahitaji kujua ni nini kilifanyika alipopokea mikate na samaki kutoka kwa wanafunzi.

> ***Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni, akabariki, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi, wanafunzi wakawapa makutano.***

Biblia inasema alivibariki. Baadhi ya matoleo yanasema alitoa shukrani. Lakini hiyo inamaanisha nini? Neno shukrani au kubariki ambalo limetumiwa hapa katika lugha ya Kiyunani linamaanisha kuweka wakfu, kuomba baraka za Mungu juu ya jambo fulani, au kumwomba Mungu abariki kitu fulani kwa ajili ya matumizi ya mtu. Maana nyingine ya kuweka wakfu ni kutangaza kitu kuwa kitakatifu, kutengwa kirasmi kwa kusudi la kimungu.

Kwa hiyo kimsingi, Yesu alipobariki samaki na mikate, vilitengwa na mamlaka ya ulimwengu na kuwekwa chini ya mamlaka ya mbinguni.

**Aliponena juu ya samaki na mikate na kuvibariki, vilibadili falme.**

## Kuweka Vitu Chini ya Mamlaka Mpya

Mikate na samaki hapo awali vilikuwa chini ya mamlaka ya wanadamu hapa duniani na nje ya uwezo wa Mungu kuvitumia. Lakini sasa tunaona kwamba kupitia kwa ukarimu wa mvulana mdogo, vilitolewa kwa Yesu, na hivyo kuhamishwa kwenda chini ya mamlaka ya Ufalme. Ni lazima pia tutambue kwamba ikiwa vingeachwa chini ya mamlaka ya dunia, kamwe havingeweza kuongezeka.

Kama wanasayansi wa mambo ya kiroho, tunahitaji kuzingatia kwa karibu yale yaliyotokea. Kuhamishwa huku kulifanyika lini haswa? Huenda mwanzoni ukafikiri kwamba mamlaka ilibadilika wakati yule mvulana mdogo alipowapa wanafunzi samaki na mikate. Hiyo bila shaka ilikuwa

sehemu ya mchakato, na kwamba mvulana huyo alifanya hivyo kwa hiari pia ni kidokezo muhimu cha kuzingatia. Lakini kuhamishwa huku hakukufanyika wanafunzi walipopokea mikate na samaki. Kulifanyika kihalisi kisheria Yesu alipotamka baraka juu ya chakula hicho. Ninasema kwamba ingawa Yesu alikuwa amemiliki mikate na samaki na alikuwa amevishika mikononi Mwake, havingezidisha hadi alipotamka maneno na kutoa mwongozo maalum.

Hebu tuliweke hili katika mtazamo wa somo letu kuhusu imani ambalo tulijifunza hapo awali. Tuligundua kwamba ingawa moyo wako unaweza kuwa na imani, jambo linalohalalisha mbingu kuivamia Dunia, hakuna kitakachotokea mpaka wewe, mwenye mamlaka ya kisheria duniani, uachilie mamlaka ya mbinguni hapa.

> *Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*
>
> — Warumi 10:10

Ingawa maneno aliyoyatamka Yesu alipoibariki mikate ile na samaki hayakuandikwa katika Biblia, nina hakika kwamba huenda yalikuwa kama ifuatavyo: "Baba, nakushukuru kwa ajili ya riziki Yako, na ninapokea mikate hii na samaki katika Ufalme Wako kwa ajili ya utukufu Wako. Mikate hii na samaki sasa vitaongezeka ili viweze kulisha umati huu mkubwa na viwe zaidi ya kutosha, ili wapate pumziko, nguvu na kuona utukufu Wako." Bila shaka, kama nilivyosema, maneno Yake hayakuandikwa. Lakini nina hakika alitoa agizo kwa mikate na samaki baada ya kuviwekwa mikononi Mwake. Ninajuaje hilo? Kwa sababu tayari alifahamu mpango aliokuwa nao na tayari walikuwa wameketishwa katika vikundi.

> *Yesu akawaambia, "Hawana haja kwenda zao, wapeni ninyi vyakula."*
>
> *Wakamwambia, "Hamna kitu hapa ila mikate mitano na samaki wawili."*
>
> *Akasema, "Nileteeni hapa." Akawaagiza makutano waketi katika majani; akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni, akabariki, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi, wanafunzi wakawapa makutano.*
>
> — Mathayo 14:16-19

Tambua kwamba tayari alikuwa amewapa maagizo ya kuketi kwenye nyasi kabla ya kubariki mikate na samaki. Alijua kabisa mpango Wake ulikuwa ni nini. Nina hakika alitoa maagizo baada ya kuwekwa chakula hicho mikononi Mwake. Kutoa maagizo unapoachilia mbegu yako ni kipengele muhimu katika kuachilia mbegu. Nilisema muhimu? Ndio, kwa hivyo kaa makini. Ninataka kuzungumzia papa hapa kuhusu kutoa maagizo unapopanda mbegu yako.

> *Akawaambia, "Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?"*
>
> *Simoni Petro akajibu akasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."*
>
> *Yesu akajibu, akamwambia, "Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa Langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda. <u>Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni."</u>*
>
> — Mathayo 16:15-19

Maandiko haya yanatuambia wazi kwamba uwezo wetu wa kutawala duniani kwa niaba ya Ufalme wa Mungu sasa umerejeshwa kupitia kwa Yesu Kristo. Tumepewa mamlaka ya kumfunga shetani na kuachilia mapenzi ya mbingu duniani. Sasa, ninaamini, au angalau natumai, kwamba Wakristo wengi tayari wanajua maana ya kumfunga shetani. Kwa maneno rahisi, kumfunga shetani maana yake ni kumzuia asitekeleze mipango yake miovu. Hilo linaweza kutokea kwa kutoa pepo kutoka kwa watu, kuweka mikono yako juu ya wagonjwa na wao kupata nafuu, au kwa kusema, "Koma, katika jina la Yesu!" Unachukua mamlaka yako katika Ufalme wa Mungu na kuyatumia kutekeleza ushindi ambao Yesu alishinda juu ya shetani.

**TUMEPEWA MAMLAKA YA KUMFUNGA SHETANI NA KUACHILIA MAPENZI YA MBINGU DUNIANI.**

**Kutumia Mamlaka Yako**

Katika uchunguzi wangu, ni watu wachache sana wanajua jinsi ya kufungulia mbingu hapa duniani. Tayari nimezungumza kuhusu 1 Yohana 5:14-15 kama muhtasari wa maombi yenye matokeo.

> *Huu ndio ujasiri tulio nao katika kumkaribia Mungu, ya kwamba, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na ikiwa tunajua kwamba anatusikia—chochote tunachoomba—tunajua kwamba tunayo tuliyomwomba.*
>
> — 1 Yohana 5:14-15

Kuamini moyoni mwako au kuwa na imani sio mwisho wa mlinganyo. Kama tulivyoona tayari, unapoamini kile ambacho mbingu zinasema, unahesabiwa haki. Mbingu zinapata uhalali wa kutiririka duniani, ingawa hakuna kitakachotokea hadi utakapoiachilia mamlaka hiyo duniani. Umeketi pamoja na Kristo katika ulimwengu wa roho kwenye mkono wa kuume wa Baba. Maneno yako ni maneno ya kifalme, na mbingu haziwezi kuachiliwa hapa hadi utakaposema! Hili linaweza kuwa tangazo au mapatano yanayotamkwa katika maombi, lakini una funguo za Ufalme. Mungu hawezi kufanya chochote bila wewe!

Sio kujua jinsi ya kuomba kunakofanya mambo kutokea; bali ni kujua kutoa mwongozo unapofanya hivyo. Kumbuka, usipozifungulia mbingu hapa duniani, hakuna litakalofanyika. Kwa hivyo ni muhimu kwamba tuelewe jinsi ya kuachilia mapenzi ya mbinguni katika maisha yetu na ulimwengu wetu.

Mojawapo ya mifano bora kuhusu kutoa mwongozo inafunzwa katika Sala ya Bwana. Kuna baadhi ya mambo muhimu hapa katika Sala ya Bwana unayohitaji kufahamu. Kwanza, andiko linasema kwamba Mungu tayari anajua unachohitaji, kwa hiyo acha kuombaomba. Kuombaomba si imani, na kunaonyesha kutojua kwako kuhusu jinsi Ufalme unavyofanya kazi na haki zako kama raia wake. Kutoa mwongozo katika maombi ni kuwasilisha ombi. Ni orodha ya kina ya kile unachohitaji. Sio kuomba kupokea vitu hivyo; bali ni kuvidai vitu hivyo.

> *Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla*

*ninyi hamjamwomba. Basi ninyi salini hivi; "Baba yetu uliye mbinguni, jina Lako litukuzwe, Ufalme Wako uje, mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu."*

— Mathayo 6:7-11

Yesu alianza kwa kusema, "Baba yetu uliye mbinguni, jina Lako litukuzwe (listahiwe na kuheshimiwa) (kutafakari enzi na mamlaka Yake)." Yesu aliweka wazi mtazamo wa kisheria wa maombi katika sentensi hii ya kwanza. Hebu tulinganishe na sentensi ya kwanza inayosemwa mahakamani.

Mhudumu wa dhamana husimama na kusema, "Tafadhali inuka. Mahakama ya (kisha anaitaja mahakama)…." Huwa inapata jina lake kutoka kwa yale inayoyashughulikia. Lakini mambo kadhaa hutokea hapo mwanzoni. Mdhamini husema, "Wote wainuke," huku akiipa mahakama heshima inayostahili na pia hakimu atakayeiongoza mahakama. Jina la mahakama hutajwa ili kuweka mamlaka sahihi, na kukujulisha kwamba uko katika chumba cha mahakama chenye mamlaka juu ya kesi yako.

Hebu tuendelee na anachosema mhudumu wa dhamana. "Tafadhali inuka. Mahakama ya Mashtaka ya Kawaida ya Kaunti ______________ (jina la Kaunti) sasa imeanza, Mheshimiwa Jaji Smith ndiye anayeongoza."

Sentensi hii yote ya kwanza, "**Baba yetu uliye mbinguni, jina Lako litukuzwe,**" hutangaza cheo cha Yule atakayeongoza kesi hiyo na kutupa mamlaka ya kuwepo. Yeye ni Baba yetu, na tunaweza kuingia katika mahakama hii kisheria. Sentensi hii ya kwanza pia huweka wazi mamlaka ya mahakama kwamba ni ya mbinguni, ambayo iko juu zaidi ya mamlaka yote.

Kisha, Sala ya Bwana inasema, "**Ufalme Wako uje, mapenzi Yako yatimizwe.**"

Kifungu hiki cha maneno kinaweka hitaji kwa mahakama kutawala kulingana na sheria ya Ufalme. Uko karibu kuwasilisha ombi au kuleta suala mahakamani, na unamwomba Jaji atekeleze kile ambacho mapenzi Yake (sheria) inasema kuhusu suala hilo. Kisha linasema, "**Duniani kama huko mbinguni**." Tena, hapa unasema kwamba unataka uamuzi wa mbinguni utekelezwe duniani jinsi ilivyo huko. Sasa, haya yote yalikuwa ni kukusimamisha katika mahakama. Bado hakuna chochote kimeombwa au kuwasilishwa. Lakini kinachofuata ni maombi.

"Utupe leo riziki yetu." Tafsiri nyingine inasema, "Utupe leo mkate wetu wa kila siku." Kauli hii kwa kweli haihusu mkate isipokuwa hilo haswa ndilo hitaji lako. Inakuambia ujaze pengo na kile unachohitaji. Kumbuka, mazungumzo haya yote yalianzia pale Yesu alipokuwa akiwaagiza wanafunzi

Wake jinsi ya kuomba ili kupokea mahitaji yao. Hapa ndipo unapokata rufaa, lakini kama nilivyosema, maneno bora ya kutumika hapa ni kuweka madai. Bila shaka, yote mawili hufanya kazi, na Wafilipi 4 inazungumzia kukata rufaa. Lakini hoja ninayotaka uelewe ni kwamba kukata rufaa ni ombi lenye maelezo. Jambo muhimu ni kukumbuka kwamba lina maelezo. Unatoa agizo katika maombi; linapaswa kuwa la kina na halisi. Wafilipi 4:6-7 inatuambia jambo hili haswa.

**"AH, CHOCHOTE AMBACHO MUNGU ANATAKA KUNILETEA NI SAWA. YEYE ANAJUA VYEMA ZAIDI." MAKOSA, MAKOSA, MAKOSA!**

> *Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*
>
> — Wafilipi 4:6-7

Tambua kwamba sala na maombi ni tofauti. Sala zetu hubeba maombi yetu na kuyapeleka kwa Baba yetu. Tena, maombi yanapaswa kuwa na maelezo mengi na halisi. Lakini Wakristo wengi husema hivi, "Ah, chochote ambacho Mungu anataka kuniletea ni sawa. Yeye anajua vyema zaidi." Makosa, Makosa, Makosa!

**Mungu amekupa WEWE funguo za Ufalme!**

Ikiwa umesoma nyenzo zangu nyingi, utaona hadithi nyingi za kina za Ufalme. Kuna mengi katika kitabu hiki ambayo natumai yatakusaidia kuona jinsi Ufalme ulivyo wenye maelezo mengi na maneno yako yanapaswa kuwa vivyo hivyo. Ili kufafanua hoja yangu, niruhusu nikuchoshe na hadithi kadhaa za zamani ambazo huenda umesikia hapo awali. Lakini ninahisi nahitaji kutumia wakati mwingi kadiri inavyohitajika ili uelewe vizuri jinsi Ufalme ulivyo hususa. Hebu nikukumbushe kifupi kuhusu hadithi ambazo tumezungumzia tayari.

## Ufalme Kazini

Ulisoma hapo awali jinsi gari langu lilivyoungua niliposema kwa sauti, "Bwana, inaweza kuwa bora ikiwa gari hili lingeteketea tu." Je, hii ilikuwa bahati mbaya? Hebu tuendelee. Nilikuambia kuhusu kulungu,

jinsi Bwana alivyonionyesha kutoa matoleo kama mbegu kwa ajili yao, na jinsi hakuna kulungu ambaye amekuja chini ya kisimamo cha mti wangu ambaye sijatoa matoleo kwa ajili yake. Kulungu sahihi, yule haswa niliyetoa matoleo kwa ajili yake alijitokeza kila wakati. Kisha nikakueleza jinsi Mungu alivyonionyesha kwamba kulungu walikuwa wakija kwa mpangilio haswa niliotoa matoleo. Je, umewahi kusikia kitu kama hicho hapo awali? Najua sijawahi mpaka nilipoona na macho yangu. Ufalme ni hususa sana nilikuambia kuhusu jaribio alilofanya Tim kwa kutoa matoleo kwa ajili ya kulungu mwenye pembe saba. Nilikuambia jinsi Mungu alivyonifundisha kunena kwa mamlaka, na yule dume ambaye alikuwa akiondoka kwangu kwa umbali wa yadi 200 alisimama sekunde ile ile nilipozungumza, kisha akaja na kusimama moja kwa moja chini ya kisimamo changu. Nilikuambia juu ya ndege ambapo niliamuru asimame, na akasimama mara moja.

Nilikuambia kuhusu bunduki niliyonyooshea mkono kwenye duka la vifaa vya michezo huku nikisema, “Nitaichukua hiyo,” na baada ya majuma machache, nilipewa bunduki hiyo hiyo. Nilikuambia pia kuhusu gari aina ya BMW 645Ci ambayo Drenda aliiona kwenye eneo la maegesho na kusema, “Ndiyo ile!” Hatukumwambia mtu yeyote, lakini baada ya wiki chache, mtu mmoja kanisani alinipigia simu na kusema, “Nimeona gari la Drenda leo.” Nilishtuka na kumuuliza alimaanisha nini. Aliendelea kusema kuwa alipokuwa akiendesha gari mjini, aliona gari zuri aina ya BMW 645Ci ambalo lilikuwa likiuzwa; na alipoliona, Bwana alimwambia ni gari la Drenda. Hilo lilivutia umakini wangu, gari lile lile haswa!

Nitakusimulia hadithi katika sura ya 7 ya jinsi nilivyopokea ndege haswa niliyokuwa nimetoa matoleo kwa ajili yake kutoka mahali ambapo sikutarajia kabisa na jinsi nilivyopata pesa za kuilipia. Nina hadithi nyingi zinazoonyesha jinsi Ufalme unavyofanya kazi.

Nakumbuka nilipomuua kulungu wangu mkubwa mwenye pembe 26. Ilikuwa siku yenye hali-joto isivyo kawaida katika mwezi wa Novemba. Nilimwacha kulungu kuning’inia siku hiyo nzima, na siku iliyofuata nilimpeleka kwa mtu ambaye kazi yake ni kuandaa ngozi za wanyama na ndege waliokufa na kuzijaza na nyenzo maalum kuwafanya waonekane kama wako hai, ili aweze kuunda kichwa chake kionekane kuwa hai. Alitazama manyoya na kusema, “Samahani; inaonekana hali ya hewa ya joto imeharibu manyoya. Sidhani nitafaulu kuunda hii, lakini nitajaribu nione.” Sasa, sikuwa tayari kuruhusu kulungu wa ushindi wangu ambaye nilikuwa nimevuna kwa imani kutokuwa muundo mzuri unaosimama katika ofisi yangu. Mara alipokwenda ofisini mwake kuniletea fomu ya kuagiza,

niliweka mkono wangu juu ya dume yule na kutangaza kwamba manyoya yake yalikuwa kamili na umbo la kichwa chake ungetokea kikamilifu. Basi nilirudi baada ya mwezi mmoja, kisha yule muundaji akasema, "Unajua, nilikuambia nilifikiri manyoya yake yalikuwa yameharibika, lakini umbo lilitokea vizuri na manyoya ni laini."

Ninaweza kuendelea hivi kwa masaa mengi, lakini kimsingi ni maneno unayotamka. Kila neno unalotamka huanzisha utendaji wa sheria fulani ya kiroho! Huenda hukujua hilo. Sikujua pia, lakini ni kweli. Ufalme ni mahususi sana. Hebu nikusimulie hadithi nyingine, na utaona hadithi nyingi zaidi katika sehemu ya kitabu hiki iliyosalia ambazo zitathibitisha kile ninachosema. Kama unavyoweza kuona, nina shauku kwamba uelewe jambo hili.

### Kuanzisha Utendaji wa Sheria ya Kiroho

Ulikuwa wakati wa kongamano moja la wanawake la Drenda. Tulikuwa tumekodisha gari aina ya Cadillac Escalade ili kumtembeza mgeni mmoja mjini. Mwishoni mwa kongamano, gari hilo halikupaswa kurudishwa hadi asubuhi iliyofuata, kwa hivyo mimi na Drenda tuliamua kuliendesha hadi nyumbani kwetu usiku huo ili kuona ni gari aina gani. Hatukuwa tumewahi kuendesha Escalade hapo awali. Kweli, lilikuwa gari zuri sana. Tulipokuwa tukilirudisha kanisani asubuhi iliyofuata, tulikubaliana kwamba tungependa kuwa gari kama hilo. Lilikuwa na muundo mfupi na lenye rangi nyeupe ya lulu. Sote wawili tulikubali kwamba tulipenda gari lenye muundo huo huo na rangi hiyo hiyo.

Vema, ilikuwa mwezi mmoja au zaidi baada ya tukio hilo kwamba nilipokuwa nikitoka nje kuchukua gazeti langu, simu ya yangu ya mkononi ililia, na sauti ilikuwa ya mmoja wa washiriki wa kanisa langu. Alisema virahisi, "Ningependa kukununulia Cadillac Escalade. Ungependa yenye rangi gani?" Nilishangazwa lakini nikasema lulu nyeupe. Lakini nilisahau kutaja kwamba nilipenda muundo mfupi. Naam, karibu mwezi mmoja ulipita, na nilifikiri kwamba labda alikuwa amesahau, lakini simu ililia, na akasema kwamba alikuwa nayo. Kwa hiyo tulienda kukutana naye, na alikuwa na Escalade yenye muundo mfupi na rangi ya lulu nyeupe. Tulipoikaribia kuipokea, alisema yafuatayo, "Samahani nilichukua muda mwingi kwa sababu ya kutafuta gari lenye muundo mrefu." Kile ambacho hakujua ni kwamba hatukutaka gari refu. Alipenda lenye muundo mrefu na alifikiri hilo ndilo tulilotaka, lakini alipata lile fupi tu. Tena, lile gari haswa

tulilokubaliana kuhusu katika mazungumzo kati yangu na Drenda.

Mfano wa kustaajabisha niliouona katika biashara ulifanyika katika miaka michache iliyopita. Huenda unajua au usijue kwamba bado ninamiliki ile kampuni yangu ya huduma za kifedha. Kabla ya kuanza kazi ya uchungaji miaka 25 iliyopita, ofisi yangu ilichukua nafasi ya kwanza kati ya ofisi 5,000 ambazo mmoja wa wachuuzi wangu alikuwa akitumia. Nilipozindua kanisa letu, nilijua kwamba ningekuwa na shughuli nyingi na singeweza kudumisha nafasi hiyo ya kwanza, jambo ambalo sikufanya. Katika biashara yetu, wachuuzi kwa kawaida hutoa safari za motisha ili kuwazawadia wauzaji wao kwa uzalishaji wa mwaka huo.

Kampuni mmoja nilifanyia kazi ilitoa $100,000 kwa ofisi kumi za juu kwenye kongamano lao la kila mwaka kwa muuzaji yeyote aliyeuza zaidi ya dola milioni 10 kama bonasi. Pia walilipia safari nzuri sana kila mwaka kwa muuzaji yeyote aliyefanya zaidi ya $3 milioni. Kawaida niliuzia kampuni hii takriban dola milioni 4 kila mwaka, na hivyo ningepata safari ya bure, kisha ningeketi hapo na kuwatazama wakitoa hundi za $100,000 kwa wauzaji kumi bora kila mwaka. Nilifanya hivi kwa miaka 18! Hiyo ni kweli, kwa miaka 18. Sikufikiria kamwe ningeweza kufikia kiwango hicho nikiwa mchungaji, kwa hiyo sikuweka imani yangu katika mwelekeo huo.

Lakini mwaka mmoja nilipokuwa nimekaa kwenye kongamano nikitazama wale wauzaji kumi bora wakipata hundi zao za $100,000, Bwana alizungumza nami na kusema, “Kwa nini haupo huko juu?” Kabla sijajibu, Yeye alisema, “Ninakutaka huko juu. Nataka jina Langu lionekane hapa.” Mwezi wa Machi tayari ulikuwa umefika, na kama nilivyosema, nilikuwa katika kiwango cha uuzaji cha takriban dola milioni 4 kila mwaka kwa miaka 18 ilipohusu kampuni hiyo. Kiasili, sikuona njia yoyote ya kufikia kiwango hicho, lakini nilisali kuhusu jambo hilo, kisha mimi na Drenda tukatoa matoleo kusudi tufikie kiwango hicho cha dola milioni 10. Bwana alinionyesha mabadiliko ambayo ningeweza kufanya kuhusiana na jinsi kampuni yangu ilivyoshughulikia maswali, jambo ambalo lilileta tofauti kubwa. Ili kufupisha hadithi ndefu, tulifanikiwa kufikia lengo hilo la wauzaji kumi bora na tukapata hundi hiyo ya $100,000. Lakini hapa kuna jambo ninalotaka kushiriki nawe. Tulifanya hivyo kwa kuuza mara moja tu!

Mwaka uliofuata, kampuni hiyo iliinua kiwango hadi dola milioni 12 ili kufuzu kupata hundi ya $100,000. Kwa hiyo tulitoa matoleo yetu kwa ajili ya hilo, na tukafanikiwa mwaka huo pia. Lakini ulikisia vema; tulifanya hivyo kwa kuuza mara moja tena. Miaka miwili iliyofuata, programu hiyo

ilighairiwa. Lakini mnamo 2019, walianza tena kwa kiwango cha $10 milioni. Tulitoa matoleo yetu kama mbegu na tukafikia kiwango hicho cha wauzaji kumi bora; na tena umekisia vema. Tulifanya hivyo kwa kuuza mara moja tu. Je, ilikuwa bahati tu kwamba tuliuza mara moja na kufikia kiwango hicho? La, tulikuwa tukitoa matoleo tukiwa na kusudi la kufikia kile kiwango cha hundi cha $100,000. Na ndivyo tulivyofanya. Je, tulimaanisha kufanya mauzo moja tu? Bila shaka la. Tulikuwa tukienda kwa kasi mwaka mzima na hatukujua mambo yangeenda wapi hadi siku ya mwisho ya mwezi. Tena, picha ya kushangaza ya jinsi jambo hili linavyofanya kazi.

**Umuhimu wa Kuagiza**

Katika Kongamano la Riziki la mwaka huu, Mungu alizungumza nami na kuniambia niwafundishe watu yale ambayo mimi na Drenda tumejifunza kuhusu kutoa agizo. Hiki ndicho haswa Roho Mtakatifu alichokiita, agizo. Kwa hivyo nilitumia muda kufundisha kuhusu jambo hili maana najua watu wengi hawajui mengi kulihusu. Kulingana na kamusi, agizo ni elekezo rasmi au lenye mamlaka. Tazama haikusema ni kuomba rehema, bali agizo. Ni agizo lenye mamlaka! Basi hebu tuzungumzie hili kwa kina zaidi. Ikiwa ninatoa agizo kiroho, ni nani anayelitekeleza? Ndiyo, kuna yule anayefanya hivyo; hebu tujue ni nani.

> *Yesu akajibu, akamwambia, "Mwaminini Mungu. Amin, nawaambia, Yeyote atakayeuambia mlima huu, 'Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake. Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu."*
>
> — Marko 11:22-24

Kuna mambo mawili katika kifungu hiki ambayo ninataka kuzingatia. Angalia andiko linasema, "Yeyote atakayeuambia." Hapa tunaona kile tulichogundua mimi na Drenda. Maneno yetu huachilia mbingu hapa duniani. Pili, nataka kuzingatia sehemu ifuatayo hii ya andiko hili.

> ***". . . wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake."***

Angalia andiko linasema, "Yatakuwa yake!" Si ya Mungu, bali ya yule

aombaye, yule anayenena hapa duniani.

Ajabu! Koma kisha utafakari kuhusu jambo hili kwa dakika moja! Liruhusu liingie ndani yako; linazungumza juu yako.

Kwa hivyo ni nani anayetekeleza hili? Hebu tuangalie Waebrania 1:14 ili tujue.

> *Je! Hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?*

Tazama kuna maneno mawili tofauti yanayoelezea malaika hapa, watumikao na kuwahudumu. Kutumikia kunamaanisha kutekeleza majukumu au huduma kwa mtu mwingine, katika kesi hii ni kwa ajili yako. Waziri maana yake ni afisa mkuu wa serikali aliyepewa dhamana ya kusimamia kitengo cha shughuli za kiserikali. Ili kufafanua maana ya malaika, yeye ni mwakilishi wa mahakama ya mbinguni mwenye idhini ya kutenda kwa niaba ya Ufalme wa Mungu kwa niaba yako! Tafadhali kumbuka kwamba hatuwezi kuwatawala malaika kwa vile hawako chini yetu, lakini tunaweza kuiomba mahakama ya mbingu kile tunachohitaji, na watatumwa. Ajabu kweli!

"Lazima niseme jambo? Sikujua hilo." Hadithi ifuatayo inafafanua somo hili ambalo Mungu alinifundisha.

Mwaka huo mahususi, nilikuwa nimetoa matoleo yangu kwa ajili ya kulungu mdogo. Nilikuwa na uhakika sana wa kupokea kulungu wangu. Kwa hivyo kama kawaida nilienda kuwinda nikiwa na matarajio kwamba ningemuua kulungu wangu mdogo baada ya muda mfupi. Nilipokuwa nimeketi kwenye kisimamo changu cha miti, nilimwona kulungu mdogo akitembea msituni, lakini alikuwa mbali sana kwangu singeweza kumfikia na mshale wangu. Nilijaribu kumwambia aje kwangu, wala hakufanya hivyo. Sikuona kitu chochote kingine asubuhi nzima. Nilirudi asubuhi iliyofuata na sikuona hata kulungu mmoja. Papo hapo, nilijua kabisa kwamba mambo hayakuwa sawa!

Nilipokuwa nikitoka msituni siku hiyo ya pili, nilianza kuomba katika Roho Mtakatifu ili kupata jibu. Haraka sana, Roho Mtakatifu alinionyesha ni kitu gani hakikuwa sawa. Nilipotoa matoleo yangu kwa ajili ya kulungu, niliandika hundi yangu ya mbegu tu, nikaiweka kwenye bahasha na kuituma. Sikuiwekelea mikono yangu na kuizungumzia kama kawaida. Kisha Roho Mtakatifu akanikumbusha kisa ambapo Yesu alizidisha mikate na samaki na akaonyesha kwamba Yesu aliibariki kabla ya kuzidisha.

Nakumbuka niliwaza, *lazima nifanye hivyo?* Sasa, kwa kawaida nilikuwa nikiweka mikono yangu juu ya bahasha hiyo na kuizungumzia hapo awali, lakini nilikuwa na shughuli nyingi sana siku ambayo niliituma bahasha hiyo mwaka huo na nikasahau. Nilidhani kwamba kutoa matoleo yangu ndiko kulikoleta kulungu chini ya mamlaka ya Ufalme.

Naam, nilikuwa na hamu ya kusahihisha kosa langu na kujaribu kutumia ufahamu wangu mpya wa Ufalme ili kuona kama nilikuwa sahihi. Kwa hiyo nilitoa matoleo yangu tena kwa ajili ya kulungu mdogo, lakini wakati huu nilihakikisha nimeinenea nilipokuwa nikiitoa. Ili kufafanua hili hebu nikupe mfano wa maneno ninayoweza kusema. "Baba, leo ninapotoa matoleo haya, ninapokea kulungu wangu mdogo. Ninasema jambo hili limetimizwa, kulingana na Marko 11:24, na ninakushukuru kwa hilo. Roho Mtakatifu, mlete kulungu huyo karibu ili niweze kumuua kwa urahisi, kwa jina la Yesu. Amina." Kama unavyoona, hakuna mapambo, lakini siombi wala kuombaomba kupewa kulungu. Ninatangaza, na kufanya ombi langu lijulikane. Mtu aliye kwenye mstari wa mbele katika jeshi hahitaji kuomba kupewa risasi; yeye huagiza apewe. Kwa maneno mengine, tayari sheria imempa ruhusa ya kupata chochote anachohitaji, hakuna haja ya kuomba, bali kusema tu, "Leta risasi."

Naam, asubuhi iliyofuata, nilikuwa nje kwenye kisimamo changu cha miti kabla ya mwanga, na msitu kuanza kuwa na rangi ya mvi, kisha nikaona kulungu mmoja akielekea upande kwangu. Giza lilikuwa kubwa singeweza kurusha mshale, lakini niliweza kuona kulungu akija moja kwa moja kwenye mti wangu. Alipokaribia mti wangu, alisimama, na kwa dakika 15 zilizofuata, alizunguka mti wangu polepole. Kwa ufupi nilishangaa. Kulungu alikaa ndani ya yadi 20 za mti wangu na kuuzunguka polepole tu.

Nuru ya msitu ilipozidi kuongezeka kwa utaratibu, niliweza kuona kwamba hakuwa dume mwenye pembe. Kwa kweli, alionekana kama kulungu wa kike maana singeweza kuona pembe ndogo kwa kichwa chake. Bado hakukuwa na mwangaza kabisa, lakini sasa ilikuwa halali kuwinda kwa sababu Ohio ina wakati halali wa kuwinda asubuhi. Sikuweza kutambua kama alikuwa dume mdogo, kama nilivyodhani, lakini pia nilijua kwamba mara nyingi, pembe ndogo huwa chini ya manyoya. Nilifikiri kwamba jinsi kulungu huyo alivyokuwa amefanya jambo la ajabu, lazima alikuwa kulungu wangu, kwa hiyo nilirusha mshale nikamwangusha yule kulungu. Nilipomkaribia nilifurahi kuona vitufe vidogo vya pembe na nikajua kwamba hakika huyo alikuwa dume wangu mdogo. Nilimuacha pale alipoangukia kwa sababu niligundua sikuwa nimeleta kisu changu, kwa

hivyo nilirudi hadi nyumbani kukichukua.

Niliporudi nilimwona Tim akinifuata. Aliniuliza ikiwa nilikuwa nimeona chochote, na nikamweleza yaliyotokea. Tulipokuwa tukienda mahali alikuwa amelala, Tim alisema kwamba hakuwa ameona kulungu katika siku tatu tulizokuwa tumeenda kuwinda. Tim alikuwa amekuja nami siku hizo zote tatu, na aliposema hivyo, sasa nilijua tatizo lilikuwa nini. Nilikumbuka siku ambayo alikuja ofisini kwangu na kunikabidhi hundi ya matoleo yake ya kulungu, ambayo alikuwa akiitoa kwa kanisa. Nilikumbuka kwamba hakutamka chochote kuhusu matoleo yake. Nilichukua muda na kueleza kile ambacho Mungu alikuwa amenionyesha kuhusu kutamka juu ya matoleo yalipokuwa yakitolewa.

Usiku huo, mimi na Tim tulikuwa na shughuli fulani kule Columbus, na njiani kurudi nyumbani, tungepita karibu na kanisa. Tim aliuliza kama tungeweza kupitia kanisani ili aweze kutoa matoleo yake tena, na wakati huu angetamka juu yake alipokuwa akiiachilia. Tulipokuwa tumeketi katika ofisi yangu, aliandika hundi yake, na nikaona matoleo yake yalikuwa ya kulungu mwenye pembe sita. Niliwaza kwamba hilo lilikuwa tamko la ujasiri na mahususi.

Asubuhi iliyofuata, Tim alienda kwenye mti uleule niliokuwa nimeutumia siku moja awali. Alipitia jambo lile lile nililokuwa nimepitia. Kabla ya mwanga wa asubuhi kudhihirika, dume alikuja kwa mti moja kwa moja, na kuuzunguka hadi mwanga wa kuwinda ulipodhihirika. Tim alimpiga mshale na akahisi alikuwa amemgonga dume huyo vizuri. Lakini kwa bahati mbaya, dume huyo alitoweka, na ingawa tulimtafuta kwa masaa mawili hatukuweza kumpata. Ajabu ni kwamba baadaye siku hiyo, rafiki yetu, ambaye anaishi karibu robo tatu ya maili kutoka kwetu, alituambia kwamba jirani yake alikuwa ameamka asubuhi hiyo na kumpata dume mwenye pembe sita ambaye alikuwa amekufa akiwa amelala kwenye kibarabara cha gari lake. Dume alikuwa na mshale ndani yake. Nyumba hii ya jirani ilikuwa upande haswa ambapo kulungu alikuwa amekimbia kutoka kwa msitu wetu. Rafiki yangu alituambia kwamba jirani yake, ambaye hakujua ni nani alimpiga kulungu, alimchinja mwenyewe asubuhi hiyo. Najua ni hadithi ya kichaa, lakini somo kwetu.

**Nenea matoleo yako unapoyaachilia, kama vile Yesu alivyofanya**. Hata hivyo, Tim alitoa matoleo upya na juma lililofuata alipoenda kuwinda alimpata kulungu wake.

## Unaponena, Kuwa Mahususi

Najua kwamba kulungu mwenye pembe sita ni mahususi sana, lakini kama tulivyogundua, ndivyo Ufalme ulivyo! Kwa mfano tazama ulimwengu wa asili.

> *Kwa sababu mambo Yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi Zake; yaani, uweza Wake wa milele na Uungu Wake; hata wasiwe na udhuru.*
>
> — Warumi 1:20

Biblia inasema kwamba sifa za Mungu zisizoonekana ziko dhahiri katika ulimwengu wa asili. Kwa hivyo, nikuulize swali, "Ulimwengu wa asili una maelezo gani?" Ya kina sana! Ikiwa ningekuambia kwamba nitanunua gari, swali lako kwangu lingekuwa, "Gari la aina gani?" sivyo? Huwezi kuona gari akilini mwako ninaposema gari. Utaona "gari" kama gari aina fulani kama vile Ford au Chevy, gari lenye muundo na rangi fulani. Neno gari halina picha fulani: daima lazima limaanishe gari fulani. Hivi ndivyo unavyotakiwa kuwa katika maombi.

Je, umewahi kusoma hati ya kisheria? Nina hakika umefanya hivyo. Huwa ni ya kina sana. Ndivyo ilivyo na yale unayoachilia na maneno yako, hata wakati humaanishi. Tazama jinsi Yesu alivyohudumu. Alielewa umuhimu wa maneno.

> *Naye aliposhuka mlimani, makutano mengi walimfuata. Na tazama, akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia, akisema, "Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa."*
>
> *Yesu akanyosha mkono, akamgusa, akisema "Nataka, takasika." Na mara ukoma wake ukatakasika.*
>
> — Mathayo 8:1-3

Tazama hakuna kilichotokea mpaka Yesu aliposema, "Nataka, takasika!"

> *Naye alipofika ng'ambo, katika nchi ya Wagerasi, watu wawili wenye pepo walikutana naye, wanatoka makaburini, wakali mno, hata mtu asiweze kuipitia njia ile. Na tazama, wakapiga kelele, wakisema, "Tuna nini nawe,*

*Mwana wa Mungu? Je! Umekuja kututesa kabla ya muhula wetu?"*

*Basi, kulikuwako mbali nao kundi la nguruwe wengi wakilisha. Wale pepo wakamsihi, wakisema, "Ukitutoa, tuache twende, tukaingie katika lile kundi la nguruwe."*

*Akawaambia, "Nendeni!" Wakatoka, wakaingia katika nguruwe. Kundi lote wakatelemka kwa kasi gengeni hata baharini, wakafa majini.*

— Mathayo 8:28-32

Tafadhali kumbuka kwamba pepo alikuwa akizungumza na Yesu na hakuwa akitoroka! Walikuwa na mazungumzo! Pepo hao waliondoka tu Yesu aliposema, "Nendeni!" Wewe ndiye msimamizi, una funguo, lakini lazima unene! Sema kitu. Tena, Ufalme ni ufalme ulio na sheria zinazotiririka kwa njia ifaayo ya mamlaka. Maneno yako ni muhimu!

Kabla hatujaendelea, hebu tujikumbushe yale ambayo tumejifunza. Yesu alipobariki mikate na samaki, vilibadilisha falme. Na kama Yesu, unapaswa kutoa agizo kwa matoleo yako unapoyaachilia. Je, unapaswa kuwa na matarajio gani mara unapotoa matoleo yako? Kila toleo lina picha inayopaswa kuambatanishwa nalo. Kila ahadi ina picha pia. Tutazungumzia hili baadaye, lakini swali linalofuata ambalo ninataka kushughulikia ni mahali unapopaswa kutoa matoleo yako.

**WEWE NDIYE MSIMAMIZI, UNA FUNGUO, LAKINI LAZIMA UNENE!**

### Unapaswa Kutoa Matoleo Yako Wapi?

Kwanza kabisa, utataka kutoa matoleo kwa huduma nzuri ya Mungu. Tafadhali kumbuka sizungumzii mtindo wako wa maisha wa kawaida wa ukarimu kwa wale walio na mahitaji.

*Anayemhurumia maskini humkopesha Bwana, Naye atamlipa kwa tendo lake jema.*

—Mithali 19:17, Tafsiri ya 'NASB'

Ni kweli kwamba ukiwa mkarimu Mungu atakulipa!

*Lakini nasema neno hili, apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu. Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema; kama ilivyoandikwa,*

*Ametapanya, amewapa maskini, Haki yake yakaa milele.*

*Na yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, Naye atayaongeza mazao ya haki yenu;*

*Mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu.*

*Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu; kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote. Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu. Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo.*

— 2 Wakorintho 9:6-15

Ni wazi kwamba Mungu huwapa thawabu wale walio wakarimu. Lakini aina ya utoaji ninaozungumzia ni **utoaji wenye malengo** na **hulenga mavuno**. Kumbuka, ninapaswa kutamka kusudi la matoleo yangu katika kutoa kwa aina hii. Kuwa mkarimu ni kitendo cha huruma, na kwa kawaida huwa sitamki chochote ninapokuwa mkarimu, bali huwa ninadai yale ambayo tumesoma hivi punde katika 2 Wakorintho 9, kwamba Mungu atanipa mbegu ya kuwa mkarimu na kwamba ninapoendelea kuwa mkarimu, atanizidishia mali ili niongeze utoaji wangu.

### Utoaji Wenye Malengo

Nimetaja kwamba ninapotoa matoleo, ninajishughulisha na kile

ninachokiita utoaji wenye malengo. Tena, utoaji huu huwa na lengo la mavuno. Hiki ndicho hasa Yesu alichofanya pale katika Marko sura ya 6. Alikabiliwa na hitaji maalum sana na alihitaji jibu mahususi sana. Alihitaji chakula ili kulisha watu hao 20,000, na hivyo alihitaji mbegu maalum sana ya kutumia. Sasa hakuwa akitoa matoleo; alikuwa akipokea matoleo. Na hayakuwa matoleo ya hiari, ya kutoa unachotaka. Alihitaji kumpata mtu ambaye angetoa matoleo maalum ili yazidishe mikononi mwa Mungu. Ndiyo maana alisema, "Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame." Mikate na samaki ndivyo alivyohitaji wakati huo, si kuni au vazi bali, mikate na samaki haswa.

Hakikisha umetoa agizo unapotoa matoleo ili kukidhi hitaji hususa ulilo nalo. Ninapohitaji kitu mahususi, kwa kawaida mimi hutumia aina hii ya utoaji, nikiwa dhahiri katika kile ninachohitaji, na kutamka kusudi la matoleo yangu ninapoyatoa. Ninapotoa matoleo, huwa ninaandika hundi au kutoa mtandaoni. Ikiwa ninatoa matoleo kwenye Mtandao, huwa ninanukuu kile nimetoa ili kuhifadhi katika rekodi zangu maagizo ambayo nimetoa katika utoaji huo, tarehe na wakati. Kumbuka, hutarajii kupokea kile ambacho umeomba au kutangaza katika siku zijazo; bali unapokea vitu hivyo unapoomba!

> *Kwa hiyo nawaambia, yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*
>
> — Marko 11:24

Sasa, utoaji huu wenye malengo hutolewa kwa huduma ya Ufalme, kazi Mungu aliyo nayo duniani. Kawaida ni huduma ambapo Mungu amempa mhudumu kazi inayohitaji ufadhili. Tena, hii ni tofauti na kusaidia maskini au wahitaji, ambayo pia ni ajenda ya Mungu, bila shaka, na Mungu yuko wazi sana kuhusu malipo kwa ajili ya aina hiyo ya utoaji. Tunazungumzia utoaji wenye malengo. Bila shaka, unaweza kutoa matoleo aina hii katika kanisa lako la mtaa, na, kwa hakika, sehemu kubwa ya utoaji wako wenye malengo inapaswa kuwa kwa kanisa lako la nyumbani.

Zaka zako zinapaswa pia kulipwa katika kanisa lako la nyumbani. Nina watu wengi wanaoniuliza ikiwa wanaweza kulipa zaka zao kwa huduma yetu kwa sababu wao ni sehemu ya kanisa letu la mtandaoni. Huwa nawajibu, "Bila shaka mnaweza kufanya hivyo." Lakini pia huwa nawahimiza kutafuta kanisa zuri la nyumbani katika eneo lao wenyewe. Lakini ikiwa kanisa letu ndilo kanisa lao kuu, basi ndio, wanaweza kutoa zaka kwetu. Hata

hivyo, mimi kama mchungaji, najua watu hukua kwa kasi na nguvu zaidi wanapohusika katika kanisa zuri la mtaa. Kwa upande mwingine, kuhusika na kanisa linalofundisha mashaka na kutoamini ni kanisa usilotaka kuunga mkono au kuhudhuria.

Kwa hiyo kuhusu kutoa matoleo kwa ajili ya kazi ya Mungu, unahitaji kutoa katika makubaliano, yaani mtu au huduma inayoelewa imani na kufahamu maana ya makubaliano. Jihadhari na watu wanaosema, "Tutaenda chini msipotoa matole." Hakuna imani katika kauli hiyo. Biblia iko wazi kabisa kwamba tusitoe matoleo kwa kulazimishwa. Ikiwa mtu yeyote wa Mungu anakufanya ujisikie kuwa na hatia ikiwa hutoi matoleo au anakuwekea shinikizo ufanye hivyo, ingekuwa bora kushikilia pesa zako tu. Imani haihitaji kusukumwa.

Ikiwa unataka kutoa matoleo lakini hakika huna mwongozo wa kutoa katika mahali popote maalum, basi toa katika kazi unayohisi ina matokeo na inafundisha imani katika kile Mungu anachosema. Kamwe usitoe matoleo katika kanisa linalosema kwamba Mungu huua watu au kuwapa ugonjwa wa saratani ili kuwafundisha jambo fulani au upuuzi wa aina hiyo. Bali panda katika huduma inayofundisha Neno la Mungu.

Sasa, kumbuka kukiri au kutamka juu ya matoleo yako unapotoa. Mimi na Drenda tumefanya hivi tangu Bwana aliponielekeza jinsi ya kupata kulungu wangu katika mwaka wa kwanza. Bila shaka, kulikuwa na mwaka ambao nilikuambia juu yake katika sura hii ambapo sikutamka chochote juu ya matoleo yangu, na unajua matokeo yalivyokuwa. Tulitamka maneno juu ya matoleo yetu kwa miaka mingi bila kufikiria au hata kujua kwamba ni sehemu muhimu ya kutoa matoleo. Nilifikiri kwamba kutoa tu ndiko kulikohitajika ili kuleta matoleo yangu chini ya mamlaka ya Ufalme, na kweli, hilo hufanyika. Lakini bila agizo dhahiri, hujui unachotarajia, hujui mavuno halisi ni yapi; na usipojua hilo, basi utakosa majira ya mavuno pia.

Nimejifunza masomo mengi kupitia uwindaji wangu wa kulungu, na tunapomalizia sura hii ya jinsi ya kuachilia imani yako, ninataka kuongeza hadithi moja.

Ilikuwa miaka michache tu baada ya kujifunza jinsi ya kuwinda kwa imani wakati kwa sababu nisiyoijua niliamua kwamba singetoa matoleo ya kulungu mwaka huo. Sikumwambia mke wangu kuhusu jambo hilo; sikuzungumza kuhusu kutoa matoleo wala kuomba kuhusu kulungu wakati msimu wa kutumia bunduki ulikuwa ukikaribia. Miaka kadhaa awali nilikuwa nimevuna kulungu kwa njia za ajabu kwa kutumia yale ambayo Mungu alikuwa amenifundisha, lakini yote yalikuwa mapya kwangu; na

nilihisi wakati huo kwamba nilikuwa na imani ya kumpata kulungu wangu na sikuhitaji kurudia kitendo cha kuachilia imani yangu. Hata hivyo, unaweza kukisia kilichotokea.

Kitu cha kwanza asubuhi, nafikiri niliona dume ambaye alikuwa yadi 300 kutoka kwangu akikimbia, na ndivyo ilivyokuwa. Sikufaulu pia katika uwindaji wa jioni. Nilipoingia nyumbani bila kitu siku ile ya kwanza, Drenda alikuwa na rafiki yake pale nyumbani na nilimwambia mambo hayakuwa yakienda sawa kwangu katika kuwinda kulungu. Nilimwambia kwamba sikufuata maagizo ambayo Mungu alinipa kuhusu kupata kulungu wangu. Drenda alisema, "Nilishangaa kuhusu hilo wakati ulipotoka kwenda." Naam, nilikubali kosa langu na kuwauliza ikiwa wangeniombea kuhusu hilo. Niliandika hundi kama mbegu yangu kwa ajili ya kulungu, bila kubainisha jinsia yoyote. Sote tuliweka mikono yetu juu ya hundi, tukaomba, na kumpokea kulungu huyo kwa imani.

Siku iliyofuata, sikuweza kutoka asubuhi, kwa hiyo nilitoka jioni. Nilikuwa nimefikiria mti mkubwa wa mchororo kwenye mpaka wa shamba letu ambao nilifikiri ungekuwa kisimamo kizuri, na hapo ndipo nilipoelekea. Ilikuwa jioni yenye joto jingi isivyo kawaida katika mwezi wa Desemba, na ikiwa nakumbuka vyema, joto lilikuwa karibu digrii 70, na kulikuwa na upepo. Dakika chache tu katika uwindaji, kulungu mkubwa alitoka msituni na kwenda kwenye uwanja mbele ya ule mti mkubwa. Kulungu alikuwa amesimama mbele yangu kwa njia ambayo ningeweza kumuua virahisi. Nilipokuwa nikidadisi mambo, niligundua kulungu huyo alikuwa karibu yadi 75 kutoka kwangu, lakini sikuwa na uhakika na umbali huo maana nilikuwa nikitumia bunduki ambayo haingefikisha risasi vyema. Lakini nililenga kwa uangalifu na kufyatua risasi, na kulungu akaanguka. Jamani, nilifurahishwa na hilo. Nilirudi nyumbani kabla ya giza kuingia, na rafiki wa Drenda alikuwa amerudi kututembelea; na sote tulifurahia sheria za Ufalme na wakati huohuo nilihisi nilikuwa nimejifunza somo.

Katika sura hii, tumepitia kanuni ya pili ya kupokea kutoka kwa Ufalme:

### Hatua #2: Kuachilia Mbegu yako katika Ufalme wa Mungu

Tulijifunza kwamba tunapotoa mbegu zetu kwa kazi ya Ufalme, huwa zinabadili falme. Pia tulizungumzia jinsi tunavyotoa mbegu zetu, kwa matamshi na maagizo. Hapa kuna mambo mengine machache tunayohitaji kukumbuka kwenda mbele.

1. Tunaweza kutaja pesa.
2. Tunaweza kutaja hitaji maalum.
3. Hatupaswi kutumia zaka kama matoleo.
4. Kutoa sio fomula; lazima kufanyike kwa imani.
5. Utoaji maalum una mavuno maalum.

**Tunapaswa kuachilia mbegu yetu na matamshi.**

## SURA YA 6
# IMANI NDIYO UFUNGUO

Miaka michache baada ya kuzindua kanisa letu, nilikuwa nikiendesha gari kuelekea nyumbani na nilikuwa karibu kufika kwa kibarabara chetu cha kuingia nyumbani kule mashambani nilipoona mbele yangu taa za polisi zilizokuwa zimewashwa barabarani. Hakuna jipya, nilidhani mtu alikuwa ameshikwa kwa kuendesha gari kwa mwendo wa kasi. Hakika nilipopunguza mwendo, niliona gari mbele ya gari la polisi likitoka taratibu na kuelekea barabarani. Nilipokaribia gari la polisi na kupunguza mwendo ili kulipita, jambo lilivutia umakini wangu. Pale kando ya barabara palikuwa na dume mzuri mwenye pembe nane. Nilijua mara moja kilichotokea. Dume huyo alikuwa amegongwa na gari ambalo nililiona likiondoka.

Nilisimamisha gari mbele ya dume na nikatembea kwenda kwa gari la polisi na kumuuliza afisa huyo kile ambacho angefanya na dume huyo. Kwa kuwa kibarabara changu cha kuingia nyumbani kilikuwa yadi 400 tu kutoka hapo na nilikuwa na watoto wa kulisha, niliwaza niulize kama ningeweza kumchukua kulungu. Afisa wa polisi alionekana kufarijika kuwa na mtu aliyemtaka. Aliandika jina langu na anwani yangu na kunipa tagi kwa ajili ya kulungu.

Kabla ya kuagana, aliniambia kwamba kulungu walikuwa wakigongwa kila wakati, na ikiwa ningependezwa, angeandika jina langu kwenye orodha ya watu watakaopigiwa simu ikiwa kulungu yeyote aligongwa barabarani na hakuna mtu aliyemdai. Niliwaza kwamba hilo lilikuwa jambo zuri. Ulikuwa mwanzo wa msimu wa vuli, na bado sikuwa nimeenda kuwinda. Wakati huo sikuwa nimeanza kutumia upinde na mshale kuwinda, na msimu wa bunduki haukuwa hadi wiki ya kwanza ya Desemba, kwa hivyo niliwaza kwamba kuwa na nyama ya kulungu lilikuwa jambo zuri. Naam,

haikuchukua muda nilipigiwa simu na idara ya polisi kuhusu kulungu mwingine. Kwa hiyo kabla ya msimu wa bunduki kuanza, nilikuwa tayari nimechinja kulungu wanne au watano. Siwezi kukumbuka idadi kamili, lakini najua ilikuwa angalau nne. Jambo la msingi ni kwamba jokofu zangu tayari zilikuwa zimejaa msimu wa bunduki ulipoanza.

Ajabu ni kwamba, Drenda alikuwa na safari nje ya jiji katika wiki nzima ya msimu wa bunduki. Sikumbuki kwa nini aliondoka, lakini najua haikuwa kawaida yetu kutokuwa pamoja na kwa wiki nzima. Kwa hiyo sikusali naye kuhusu kuwinda kulungu, wala kutoa matoleo. Nafikiri niliwaza kwamba haikujalisha ikiwa nilipata kulungu maana jokofu langu lilikuwa limejaa. Lakini nilienda kuwinda; unaweza kuwa na uhakika kuhusu hilo. Ili kufupisha hadithi ndefu, niliwinda kwa wiki nzima wakati wa msimu wa bunduki na sikufyatua hata risasi moja. Drenda aliporudi nyumbani, alinikumbusha yale ambayo Mungu alikuwa amenifundisha tayari kuhusu kutoa matoleo yetu na kuomba pamoja ili kuwapokea kulungu wetu.

Naam, mwaka uliofuata ulifika, na wakati huu, sikufanya kosa kama lile tena. Ingawa idara ya polisi ilitupigia simu mara kadhaa kuhusu kulungu waliokufia barabarani, nafikiri nilichukua mmoja tu maana nilikuwa nimeamua kupata mawindo yangu mengi kutoka kwa uwindaji wangu mwenyewe. Wakati huu, mimi na Drenda tulitoa matoleo yetu na kusali huku tukitoa matamshi yetu kuhusu kulungu dume. Hatukutaja ukubwa wa dume, lakini tulimtaka dume tu. Sikuweza kwenda kuwinda asubuhi lakini nilifurahi kwenda jioni hiyo. Lakini cha kusikitisha ambacho lazima nikuarifu ni kwamba, tena, hakukuwa na kulungu. Hakika nilichanganyikiwa nilipokuwa nikielekea nyumbani jioni hiyo baada ya kukaa porini.

Nilipokuwa nimeketi mezani kula chakula cha jioni, ghafla, simu ililia. Ilikuwa ni idara ya polisi iliyokuwa ikisema kulikuwa na kulungu aliyegongwa barabarani ikiwa nilimtaka. Niliwauliza mahali alipokuwa nao wakanipa anwani. Sikuamini masikio yangu. “Unaweza kurudia anwani hiyo tena?” Nikauliza. Walirudia anwani, na nikagundua kuwa ilikuwa anwani yangu mwenyewe! Nilishtuka. Kwa hiyo nilienda kwenye dirisha, na hakika, kulikuwa na taa nyekundu zilizokuwa zinawaka mwishoni mwa kibarabara changu cha kuingia nyumbani, kwa hiyo nikawaambia ningefika hapo mara moja. Kibarabara chetu kilikuwa zaidi ya futi 900 kutoka kwa barabara kuu, na nakumbuka nilitembea umbali huo bila kuamini kabisa. Nilipofika huko, nilimwona kulungu dume mdogo lakini mnene sana mwenye afya. Nilijaza baadhi ya fomu, nikamshukuru ofisa huyo, kisha

nikamvuta kulungu kwenye kibarabara changu kuelekea kwenye ghala. Je, umechanganyikiwa? Lazima uwe! Sikufikiria tena kuhusu uwindaji wa kulungu hadi Septemba au Oktoba ya mwaka uliofuata.

**Chanzo Chako Ni Nini?**

Sikumbuki sasa ulikuwa mwezi gani, lakini nilikuwa nikikimbia nikizunguka katika uwanja wangu wa nyuma ya nyumba kama nilivyofanya mara kwa mara ili kufanya mazoezi. Nilikuwa nikikimbia huku nikisali kuhusu kile kilichotukia miaka miwili awali. Sikuelewa. Ghafla, maneno, "orodha ya polisi" yalinijia kwa udhahiri sana. Niliwaza kwa muda. Je, Mungu alikuwa anataka kuniambia jambo fulani? Kisha nikapata ufahamu. Nilitambua kwamba tumaini langu halikuwa katika Neno la Mungu au Ufalme Wake. Imani yangu ilikuwa katika orodha ya polisi! Nilitarajia kwamba ikiwa singepata kulungu wangu mwenyewe, orodha ya idara ya polisi ingenipa mmoja.

Kisha pia nilielewa kwa nini mwaka awali nilikuwa nimepokea dume wangu mwishoni mwa kibarabara changu badala ya mwishoni mwa bunduki yangu. Imani yangu ilikuwa katia orodha ya polisi. Wakati mimi na Drenda tulipotoa matoleo yetu kwa ajili ya dume wa mwaka huo, dume alijitokeza kwa mara ya kwanza mwaka huo lakini katika mahali pasipofaa, au sivyo? Nilisimama pale nikiwa na mshangao huku Roho Mtakatifu akinidhihirishia mambo. Kisha nikaelewa kwamba dume alijitokeza mahali ambapo imani yangu ilikuwa, katika orodha ya polisi. Nilipotambua hivyo, nilikimbia moja kwa moja hadi nyumbani, nikapigia idara ya polisi mara moja, na kuliondoa jina langu kwenye orodha hiyo. Nilijifunza kwamba mpango wako wa chelezo ni mpango wako binafsi! Tangu mwaka huo, sijawahi kukosa kuona kulungu wakijitokeza kila mara.

Lakini mioyo yetu hudanganyika rahisi. Ujasiri wetu hupelekwa kwa vitu vya asili virahisi. Hili ni jambo ambalo tunapaswa kufahamu na kuchunga kila wakati. Imani haihitaji mpango wa chelezo. Bado ninashangaa kwamba ingawa imani yangu ilikuwa katika orodha ya polisi, kulungu yule alijitokeza mwishoni mwa kibarabara changu siku ile ya mwanzo wa uwindaji. Na hii inatuleta katika kanuni ya tatu ambayo Mungu alinionyesha.

**Hatua #3: Achilia Mbegu Yako Ukiwa na Imani!**

Hili ni suala muhimu, maana tuliona hapo awali wakati wanafunzi hawakuweza kumtoa pepo yule mvulana mwenye pepo. Yesu alisema ni kwa sababu ya kutoamini kwao au kukosa imani. Tumeshashughulikia suala la maana ya imani na jinsi ya kuipata, lakini ni jambo muhimu kujifunza kujihukumu mwenyewe, ikiwa uko na imani au la. Basi hebu nikupe mtihani rahisi unaoweza kujipa ili ujione ikiwa kweli una imani au la. Funga macho yako. Je, umeona nini?

> *Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*
>
> —Waebrania 11:1

Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo. Matumaini daima huwa na picha. Ikiwa ningekuahidi koni ya aiskrimu, mara moja ungekuwa na picha ya koni ya aiskrimu akilini mwako. Ikiwa uliamini kwamba mimi ni mwaminifu katika ofa yangu na nina na uwezo wa kuilipia, ungejiona na hiyo koni ya aiskrimu, kukiwa na ushahidi wa kuwa na msisimko na kufanya haraka.

Ndivyo ilivyo na Neno la Mungu. Unapoamini ahadi ya Mungu na kushawishika kabisa kwamba Mungu ana nia na njia ya kutimiza ahadi Yake, utaona picha yako mwenyewe ukiwa na ahadi. Ingawa huna mkononi kile ulichoahidiwa, utatenda kana kwamba unacho, kwa sababu kwa njia moja unacho. Ahadi ni halali, nia ni halali, na ni yako. Basi imani, yaani kushawishika juu ya nia na nguvu za Mungu, ndiyo hakika ya ahadi kwako. Pia ni ushahidi wa mambo ambayo bado hayajaonekana.

**UNAPOAMINI AHADI YA MUNGU NA KUSHAWISHIKA KABISA KWAMBA MUNGU ANA NIA NA NJIA YA KUTIMIZA AHADI YAKE, UTAONA PICHA YAKO MWENYEWE NA AHADI.**

Bado unahitaji kupeleka hundi yako kwenye benki ili kupewa pesa taslimu, ambao ni mchakato wa kisheria unaotumika katika ulimwengu wa kiroho kama ilivyo katika ulimwengu wa asili. Kwa hiyo ninaposema, “Funga macho yako. Je, umeona nini?” ninachomaanisha ni hiki. Usichoweza kukiona huwezi kukikamata. Hebu nifanye hili kuwa rahisi kuelewa zaidi. Ukifumba macho na usione ahadi

hiyo ikiwa nawe, huna imani. Ikiwa wewe ni mgonjwa na ufumbe macho yako, na ujione ukiwa umepona—bila hofu yoyote, na uhakikisho kamili kwamba umepona—hiyo ni imani. Lakini ukifumba macho na bado unajiona mgonjwa, ukingoja kuponywa, basi huna imani. Ikiwa unahitaji pesa na unaamini ahadi ya Mungu, basi huna wasiwasi tena juu ya pesa bali unajiona na riziki unayohitaji.

### Hofu Ni Kinyume cha Imani

Hofu haipo wakati kuna ujasiri kama huu. Ikiwa bado una hofu juu ya matokeo, hauko katika imani. Unapaswa kujua jinsi ya kutambua ikiwa uko katika imani au la. Hupaswi kufanya maamuzi makubwa ikiwa huna imani, kwa sababu ikiwa huna imani, uko katika hofu. Hofu daima hutaka usalama na ni kutoamini. Ndiyo maana nikasema panda matoleo yako kila wakati ukiwa katika imani. Hutakiwi kuyatoa kama fomula, kwa kufanya kitendo cha kutoa tu, kwa sababu hilo halitaleta chochote. Unatakiwa kuwa na uhakika wa kile anachosema Mungu ili ukifumba macho, unachokiona ni wewe na ahadi hiyo. Tayari unayo, unaimiliki, ni yako, na amani imechukua mahali pa wasiwasi wowote ambao huenda ulikuwa nao.

> *Msijisumbue kwa neno lolote, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*
>
> — Wafilipi 4:6-7

Ukiwa katika imani, kuna amani ambayo haitokani na hali bali ahadi.

Kisha, ushahidi wa imani ni uwezo wako wa kujitetea katika mahakama ya sheria ya kiroho. Kwa kuwa imani hutegemea Neno la Mungu, lazima ujue ni kwa nini unaamini kile unachoamini. Tuseme uko katika chumba cha mahakama na wewe ni wakili wa utetezi. Upande wa mashtaka unasema kuwa mteja wako anaishi katika nyumba ya mteja wao kinyume cha sheria na anasema kuwa nyumba hiyo si ya mteja wako bali inamilikiwa na mteja wao. Je, ungefanya nini? Ungesema samahani na kwamba mteja wako ataondoka huko mara moja? Ikiwa una hati iliyotiwa saini mikononi mwako, nafasi ya hofu ingechukuliwa na ujasiri, na ungemwambia hakimu awafukuze walaghai hao nje ya chumba cha mahakama. Hivi ndivyo imani inavyofanya kazi. Inajua ukweli, ina ujasiri, na huonwa kama kuwa na

kiburi. Kwa hivyo unaweza kutetea msimamo wako?

Sarah alikuja kanisani kwetu siku moja bila kujua alikuwa wapi maana alikuwa mgeni katika mji wetu ambapo alikuwa akiendesha gari tu. Yeye na mumewe walikuwa wamehamishwa kwenda Columbus, na walikuwa wamesali kuhusu kupata kanisa. Walipokuwa wakiendesha gari huku na huko, waligeuka na kuingia kwenye kibarabara chetu cha kuingia kanisani maana waliwaza wajaribu kuhudhuria ibada yetu. Kamwe hawakuondoka hadi sasa. Sarah alikuwa ameugua ugonjwa wa pumu maisha yake yote. Kwenda na kutoka hospitalini ulikuwa mtindo wake wa maisha kwa sababu maisha yake yalikuwa yameshikwa mateka na ugonjwa huo. Alijifunza jinsi ya kuepuka mazingira yaliyochochea ugonjwa huo, na alibeba kipulizio chake kila mahali alipoenda.

Katika Kanisa la Faith Life, alijifunza kwamba uponyaji ulikuwa haki yake ya kisheria na jinsi ya kujilinda kiroho. Ibada moja alipokuwa akimsikiliza mmoja wa washiriki wetu akielezea jinsi alivyoponywa ugonjwa wa kutishia maisha, alikata shauri. Mungu hana upendeleo. Alitoa kipulizia chake kwenye mkoba wake na kuweka kadi za Maandiko badala yake, zote zikieleza haki yake ya kisheria ya kuponywa. Alizisoma kila siku. Wakati wowote alipohisi shambulio la pumu likija, alitafuta kadi ya Maandiko badala ya kipulizia chake, na hajawahi kuwa na shambulio la pumu tena!

Shangazi yangu alikuja kwangu kwenye mkutano wa familia. Aliniuliza ikiwa ningemwombea kwa kuwa alikuwa na ugonjwa wa saratani ya mapafu na alikuwa na upasuaji baada ya wiki moja na nusu ili kuondoa uvimbe mkubwa. Aliendelea kuniambia kwamba madaktari wake walikuwa wakifuatilia uvimbe wa ukubwa wa balungi ambao ulikuwa kwenye mapafu yake kwa mwaka mmoja na nusu. Ulikuwa umeanza kukua kwa haraka zaidi, na madaktari walisema ilibidi utolewe. Niliposimama pale kusikiliza hadithi yake, nilitafakari maisha yake. Alikuwa mvutaji sigara maisha yake yote, na nilifahamu kwamba hakuwa ameenda kanisani kwa miaka mingi. Nilimuahidi kwamba ningemuombea lakini nilihisi hakuwa tayari kuombewa wakati huo. Nilimuuliza kama angesoma nyenzo ambazo nilitaka kumpa kuhusu uponyaji kabla sijamwombea. Nilisema ningefurahi kumwombea asubuhi ya Jumapili iliyofuata mara tu baada ya ibada. Alikubali.

Nilifahamu alikuwa ametoa moyo wake kwa Bwana miaka mingi awali lakini hakuwa akimfuata. Nilitumaini kwamba kutafakari juu ya ahadi za Mungu kuhusu uponyaji kungetia moyo imani yake. Pia nilijua tulikuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuona matokeo chanya ikiwa tungeweza kuomba

tukiwa na mapatano na Neno la Mungu kama nanga na tumaini letu.

Kwa hivyo Jumapili iliyofuata, shangazi yangu alikuja kanisani kama alivyosema angefanya. Baada ya ibada, nilimwomba ajitokeze; na alipokuwa amesimama pale, nilimuuliza ikiwa alikuwa amesoma ahadi nilizompa. Alisema alikuwa amefanya hivyo, kwa hiyo nikamuuliza, “Unajuaje kwamba utaponywa nitakapoweka mikono yangu juu yako?” Kisha akanukuu Maandiko kadhaa na kusema kwamba tumaini lake lilikuwa katika Neno la Mungu. Nilijua wakati huo alikuwa tayari kwa maombi, na niliweka mikono yangu juu yake, nikaomba, na kutangaza kwamba alikuwa ameponywa na hakuwa na ugonjwa wa saratani. Upako wa Mungu ulimjia nilipokuwa nikiomba, na akaanguka chini ya uwezo wa Mungu. Alipoinuka, alikuwa akitetemeka huku akisema, “Nimepona!”

Alikwenda kufanyiwa upasuaji Jumanne hiyo kuondoa uvimbe huo, lakini madaktari hawakupata chochote walipomkata. Hakukuwa na uvimbe, hata kovu au dalili kwamba kulikuwa na kitu chochote pale.

Inashangaza sana kuona jinsi watu wanavyoishi maisha yao. Ungefikiri kwamba shangazi yangu angeshukuru sana kwamba Mungu alimponya na hangekosa kwenda kanisani hata mara moja maisha yake yote.

Lakini haikuwa hivyo. Nafikiri nilimwona mara moja tu baada ya Jumapili hiyo. Alifariki baada ya miaka sita au saba kutokana na aina tofauti ya saratani. Lakini wakati huu, hakuniomba kamwe nimwombee.

### Shikilia Wakati Ulipoachilia Imani Yako

Jambo moja ninalowakumbusha watu ni kwamba daima kuna muda kati ya uliposema “Amina” na unapoona jibu. Kwa sababu hii, ni muhimu kwamba ushikilie wakati ulipoachilia imani. Ninape-ndekeza kwamba uandike haya katika shajara yako au mahali ambapo unaweza kujikumbusha.

Nilitaja kuhusu jambo hili awali, maana ninaamini ni muhimu sana. Kwa mfano ninaweza kuandika kama ifuatavyo. “Mnamo tarehe 12 Novemba saa saba na nusu ya mchana, ninaamini kwamba nimepokea (andika ombi husussa) kulingana na Marko 11:24, na ninaamini kwamba nilipokea nilipoomba.” Unaweza kuongeza maelezo mengine kama vile ni nani aliyekubaliana

**DAIMA KUNA MUDA KATI YA ULIPOSEMA “AMINA” NA UNAPOONA JIBU. KWA SABABU HII, NI MUHIMU KWAMBA USHIKILIE WAKATI ULIPOACHILIA IMANI.**

nawe, kiasi cha matoleo yako, na kazi ya Mungu uliyotolea. Huu ni mfano tu, lakini ni muhimu kuandika kwa sababu unaweza kutumia hilo kupigana.

Wakati hali zinakujaribu kurudi nyuma kwa hofu, unaweza kujikumbusha tarehe na wakati ulipopokea jibu lako. Hofu ilipojaribu kuniingia, nilikuwa nikichukua kikaratasi changu na kukisoma kwa sauti kama tangazo. "La hofu, wewe ni mwongo. Tayari nimepokea hilo tarehe na wakati huu kulingana na (andiko linalohusu jambo hilo.)" Wakati mwingine ilinibidi kusoma maandishi hayo mara kadhaa ili kuufanya moyo wangu utulie na kuwa na amani. Usiruhusu kile ambacho kinaweza kuonekana kama kushindwa kukushawishi kuacha imani yako. Kwa hakika, kanuni hii ilikuwa muhimu sana watoto wangu walipokuwa wakikua kwamba katika mkutano wetu wa kila wiki wa maombi ya familia tungekuwa na shajara ya familia ambapo tuniandika kile tulichokuwa tumeombea na kile tulichokuwa tunaamini kuwa tumepokea. Tuliita hii daftari yetu ya Yakobo 4. Tunaziuza katika huduma yetu ikiwa ungependa moja.

Wakati fulani, kuna mambo ya kiroho yanayotokea ambayo huyajui. Mungu hufanya kazi kupanga kila kitu, lakini inaweza kuchukua muda. Kunaweza kuwa na vipande vingi vya fumbo ambavyo lazima viwekwe. Kwa mfano, ikiwa Mungu atatosheleza mahitaji yako ya kifedha, huenda ikambidi kuzungumza na mtu fulani ili kushughulikia hilo au kukuletea fursa ya kupata pesa unazohitaji. Hayo yote huchukua muda.

> *Ndipo akaniambia, "Usiogope, Danieli; kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, maneno yako yalisikiwa; nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako. Lakini mkuu wa ufalme wa Uajemi alinipinga siku ishirini na moja; bali, tazama, huyo Mikaeli, mmoja wa hao wakuu wa mbele, akaja kunisaidia; nami nikamwacha huko pamoja na wafalme wa Uajemi. Sasa nimekuja kukufahamisha mambo yatakayowapata watu wako katika siku za mwisho; maana maono hayo ni ya siku nyingi bado."*
>
> — Danieli 10:12-14

Hebu tuangalie tena hadithi ambayo nilikusimulia hapo awali kuhusu kutafuta mahali pa kuanzisha shule la kanisa letu. Tulikuwa tumeangalia majengo mbalimbali na tukataka kukodisha mahali kadhaa lakini hatukuhisi kuchukua jengo lolote kati yao. Tulipoanza kutafuta mahali, tulitoa matoleo ili Mungu atuonyeshe mahali pazuri. Kila wakati tulipopata eneo na kulifikiria, tulihisi tahadhari mioyoni mwetu, na tulikuwa karibu

kuvunjika mioyo. Tulikagua kila jengo katika eneo ambalo tulitaka kuweka shule yetu, lakini hakukuwa na lolote tulilohisi vyema kuhusu.

Maadili yetu ya kimsingi kama kanisa ni pamoja na hamu kubwa ya kusaidia kusomesha watoto na kutunza familia. Tumezungumza mara nyingi juu ya uwezekano wa kuwa na shule siku moja iliyo na kituo cha kulelea watoto mchana, programu ya kuhudumia na kuelimisha watoto wa wazazi walio kazini, na programu nyingine nyingi za kuhudumia jamii zetu. Jengo letu limejaa kupita kiasi, kwa hivyo hatungeweza kutekeleza mambo yoyote kama haya.

Labda unaweza kusema inaonekana kana kwamba Ufalme haukuwa ukija, lakini lazima ukumbuke kwamba tayari tulikuwa tumetoa matoleo kwa ajili ya shule bora. Ukweli ni kwamba Mungu alijua kwamba shule hiyo ingeuzwa. Alikuwa na picha nzima. Wenye shule hawakuwa wameanza kuiuza mwanzoni tulipoanza kutafuta mahali.

Kando na kujua kwamba shule hiyo ingekuwa bora sana kwetu, Mungu pia alijua jinsi tungeilipia. Nilikuwa nimepanga kwa kalenda yangu kukutana na wale wanandoa waliotununulia shule hiyo ili kula chakula cha jioni nao. Lakini kutokana na hali mbalimbali, tulikuwa tumehairisha kukutana nao angalau mara nne hadi ile siku ambayo tulikutana. Tulikuwa tumetembelea hiyo shule siku ile ile tuliyokula chakula cha jioni pamoja.

Kulikuwa na watu wengine waliyoitaka, lakini sisi ndio tuliokuwa wa kwanza kuweka zabuni. Kila kitu kilikuwa katika wakati mkamilifu. Tulipotoa matoleo yetu ya $100,000 siku mbili kabla ya kula pamoja nao, kwa maelekezo ya Roho Mtakatifu, ninaamini kwamba Shetani alitaka kuficha shule hiyo tusiione au kutumia mbinu nyingine kutuzuia. Mungu aliponiambia nitoe matoleo hayo na kumkemea Shetani asituingilie tulipokuwa tukitafuta shule yetu, ninaamini kwamba mpango ambao shetani angetumia ulisitishwa.

Wenzi hao waliotoa pesa za kununua shule yetu pia walikuwa katikati ya kufanya uamuzi wa kumsaidia rafiki yao kununua mali fulani, ambapo wangetumia pesa hizo hizo taslimu walizotumia kutununulia shule. Baada ya kusikia hadithi yetu jioni ile, walisema kwamba walielewa kwa nini hawakuwa na amani ya kufadhili ununuzi wa rafiki huyo. Kwa hiyo kumbuka unapoomba kwa imani, ukijua kwamba umepokea unapoomba, kuna muda kati ya unaposema “Amina” na wakati wa kuona majibu. Kwa hivyo kuwa na nguvu na subira.

## Simama Imara katika Imani yako

*Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.*

—Yakobo 1:4

Hii ndiyo sababu ninapendekeza kwamba watu watambue tarehe na wakati walipoachilia imani yao, kwa sababu unahitaji kusimama imara.

Binti yangu alipokuwa akikabiliwa na uvimbe wa kilo 13 kwenye fumbatio lake, alichoka kustahimili matatizo ya kiafya hilo lilisababisha, kama vile: maambukizo ya mara kwa mara kwenye figo zake, kuumwa na mgongo mara kwa mara, na matatizo ya usagaji chakula. Alitosheka na akaamua kutafakari Neno la Mungu na ahadi Zake kwa siku 30 kuhusu uponyaji. Baada ya siku hizo, alituomba mimi na mamake tumwekee mikono maana aliamini amepona. Kwa hiyo mimi na mamake, pamoja na wazee wa kanisa letu tulimwekea mikono na kuamini kwamba alikuwa ameponywa kulingana na Yakobo 5:14-16.

*Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa. Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.*

— Yakobo 5:14-16

Alienda nyumbani usiku ule akiwa na hali ile ile aliyokuja nayo; uvimbe ulikuwa bado upo. Lakini akasema, "Nimepona." Alishikilia ungamo lake kwa muda wa wiki mbili bila mabadiliko yoyote, ingawa alikuwa katika maumivu makali sana kuliko wakati wowote mwingine. Aliniambia kwamba katika kipindi hicho cha majuma mawili alipokuwa katika maumivu hayo, alimwambia Shetani, "Unaweza kujaribu kuniumiza, lakini nimepona."

Baada ya majuma mawili, alilala uvimbe ule ukiwa bado upo, lakini alipoamka alikuwa mzima kabisa. Alipoteza pauni 13 na inchi 9 kiunoni alipokuwa usingizini, na mgongo wake, ambao ulikuwa na fundo na kupinda, uliumbwa upya na kuwa uti wa mgongo mkamilifu.

Unapokuwa na uhakika katika ahadi, usimruhusu Shetani akudanganye usipate uponyaji wako au kutoamini ahadi yoyote ambayo Mungu amekupa.

Christine alikuja kanisani kwetu bila ufahamu wowote kuhusu kanisa. Yote yalikuwa mapya kwake. Christine alikuwa amevaa vifaa viwili vya kumsaidia kusikia kwa miaka mingi na alikuwa amepoteza uwezo wake mwingi wa kusikia kufikia wakati huo. Mamake alikuwa na ugonjwa huo huo na alikuwa karibu kuwa kiziwi kabisa.

Christine alipohudhuria ibada yetu, alitoa moyo wake kwa Bwana, na Mungu akabadilisha maisha yake kwa kiasi kikubwa. Alisisimka na alitaka kujifunza mengi kadiri awezavyo kuhusu Ufalme wa Mungu. Tuna darasa elekezi la waumini kwa wale ambao ni wapya kwa kanisa, na Christine alikuwa na shauku ya kuhudhuria mafundisho yaliyokuwepo. Mafundisho hayo hushughulikia mada mbalimbali, lakini ikawa kwamba darasa alilohudhuria Christine lilikuwa juu ya uponyaji. Mwishoni mwa mafundisho, viongozi waliombea watu waliohitaji uponyaji. Christine alifurahi sana alipoenda mbele kufanyiwa maombi. Alipokuwa akiombewa, masikio yake yalifunguka ghafla. Kwa mara ya kwanza, aliweza kusikia kikamilifu.

Alipokuwa akiondoka kwenye ibada siku hiyo, nilihisi kumwonya kuhusu kile ninachokiita mashambulizi ya Shetani. Hakika, alisema asubuhi iliyofuata, ghafla, masikio yake yalifungika, na akaingiwa na wasiwasi. Lakini nilimwambia hili lingetukia, na lilipotokea, alipaswa kutangaza kwamba ameponywa na kumkemea Shetani. Kweli, alifanya kile nilichomwambia afanye. Alianza kumsifu Mungu na akatangaza kwamba ameponywa huku akimfunga adui. Baada ya dakika chache, masikio yake yalifunguka na yamekuwa wazi tangu wakati huo, na hiyo ilikuwa miaka minne iliyopita.

**TENA, KUSIMAMA IMARA KATIKA NENO LA MUNGU NDIKO UFUNGUO WA UHURU WAKO.**

Tena, kusimama imara katika Neno la Mungu ndiko ufunguo wa uhuru wako.

### Nitasema Tena—Kuwa Hususa

Kuhusu kuachilia imani yako, hebu nikukumbushe kwa mara nyingine, kuwa mahususi! Hadithi hii inahusu wakati Mungu alinionyesha umuhimu wa maneno yangu. Nimeizungumzia kwa miaka mingi, lakini ina nguvu leo kama ilivyokuwa wakati ilipotokea.

Ulikuwa ni msimu wa kawaida wa kulungu, na nilitazamia sana

kwenda msituni maana sikuwa nimeenda kwa sababu ya shughuli nyingi. Mwaka huo mahususi, nilikuwa nimetoa matoleo kwa ajili ya dume wawili, dume mmoja mwenye pembe nne au zaidi na wa pili dume mdogo. Mimi na Drenda tulitoa matoleo yetu kwa makubaliano na kwa imani. Asubuhi ya kwanza nilitoka kwenda kuwinda kukiwa bado na giza kidogo. Mwanga ulipokuwa ukiongezeka taratibu na kufanya anga kuwa na rangi nyekundu, tayari nilikuwa na kulungu wangu mwenye pembe nane. Muda wote niliokaa mtini ulikuwa dakika 15! Inasisimua sana! Kwa hiyo nilijiamini sana nilipoenda kuwinda dume wangu mdogo baada ya majuma mawili. Tena, nilienda asubuhi, na baada ya takriban dakika 20, nilimwona dume mwenye pembe nane ambaye alikuwa kama yadi 300 kutoka kwangu akielekea moja kwa moja kwenye mti wangu.

Hapa Ohio, unaruhusiwa kuwinda dume mmoja tu mwenye pembe. Kulungu wa pili lazima awe wa kike au dume mdogo asiye na pembe. Dume wadogo huhesabiwa kama wa kike kwa sababu pembe ni ndogo sana huwezi kuziona kwa mbali. Kwa hivyo nilipomwona dume akivuka shamba, nilidhani angeelekea kwingine kabla ya kufika kwa mti wangu, lakini hakufanya hivyo. Alikuja moja kwa moja kwenye mti wangu na kusimama tuli chini ya kisimamo changu kwa takriban sekunde 20. Nilimtazama tu maana haikuwa halali kumwinda. Baada ya kusimama pale kwa sekunde hizo 20, ghafla alianza kurudi kwenye njia ile ile aliyoipitia. Cha kushangaza ni kwamba, alirudi kwa njia ile ile na kutoweka msituni. Nilishtuka na kuchanganyikiwa.

Sasa, sikuwa nimewahi kuona kulungu akija chini ya kisimamo changu ambaye hakuwa kulungu wangu. Nilichanganyikiwa na nikaanza kuomba katika Roho huku nikirudi nyumbani. "Bwana, dume huyo alikuwa pale kwa nini?" Ghafla, nilimsikia Roho Mtakatifu akisema, "Chunguza matoleo yako." Nichunguze matoleo yangu? Hilo lilikuwa jambo la kichaa; nilifahamu nilichokuwa nimepanda. Hata hivyo, benki ninayotumia hutuma nakala za hundi zilizoghairiwa pamoja na taarifa za kila mwezi. Haraka niliisoma ile taarifa ya benki na kuchunguza kijitabu changu cha hundi. Katika sehemu ya chini ya ukurasa wa hundi hiyo, nilikuwa nimeandika, dume wawili wenye pembe nne au zaidi, na dume mmoja mdogo. Hao ni kulungu wangapi? Nilichotaka kuandika ni kwamba nilikuwa nikiamini kuvuna jumla ya dume wawili, mmoja mwenye pembe nne au zaidi na dume mdogo. Lakini nilikuwa nimeandika kwamba matoleo yalikuwa kwa ajili ya dume wawili wenye pembe nne au zaidi, pamoja na dume mdogo. Niliketi pale nikiwa nimeduwaa. Yule

dume wa pili alikuja kwa sababu nilikuwa nimetoa matoleo kwa ajili yake. Ndiyo maana alivuka uwanja ule na kusimama chini ya mti wangu. Alitakiwa kuwa hapo.

Nilipoona hilo, nilianza kupiga kelele kwa sauti kubwa huku nikikimbia huku na huku nyumbani. Nilisisimka sana, lakini wakati huo huo, tukio hilo liliniogopesha. Ni mara ngapi nilisema mambo ambayo sikutaka yatimie lakini niliyaanzisha kupitia kwa maneno yangu? Hili hakika lilifanya Yakobo 3:3-4 kuwa hai kwangu.

> *Angalieni, twatia lijamu katika vinywa vya farasi, ili wamtii, hivi twageuza mwili wao wote. Tena angalieni merikebu; ingawa ni kubwa kama nini, na kuchukuliwa na pepo kali, zageuzwa na usukani mdogo sana, kokote anakoazimia kwenda nahodha.*
>
> — Yakobo 3:3-4

Yakobo anazungumzia jinsi maneno yetu yalivyo na nguvu. Ni wazi ikiwa maneno yetu yanasema jambo moja huku tunatamani sana kuona jambo lingine, tutajikuta katika hali ngumu wala tusijue tulifikaje hapo.

Kwa hiyo kumbuka, Ufalme ni hususa sana, na maneno yako hufafanua hasa mahali unapoenda na jinsi ya kufika huko!

### Umuhimu wa Makubaliano

Bado tunazungumzia kuachilia matoleo yako katika imani, na hapa kuna jambo unalohitaji kukumbuka. Ikiwa umeolewa, kubaliana na mwenzi wako. Ikiwa huna mwenzi, nitashughulikia hilo baada ya muda mfupi, lakini hebu tuseme umeolewa. Kubaliana na mwenzi wako.

Mwanzoni katika ndoa yetu, nilichukia kumwomba Drenda akubaliane nami kuhusu uwindaji wangu. Sababu wakati wowote nilipozungumzia kuwinda, kwa kawaida alianza kuzungumzia mambo mengine kama vile: kuhusu takataka zilizohitaji kuondolewa, balbu ambayo ilipaswa kubadilishwa, au orodha ya mambo mengine ambayo yalihitaji kufanywa. Sasa, huu ulikuwa wakati ambapo nilikuwa bado mchanga na mbinafsi. Nilikuwa nikitaka kwenda kuwinda mara tu niliporudi nyumbani, lakini yeye alikuwa ameshughulikia watoto siku nzima. Sidhani Mungu anaweza kubariki tabia hiyo. Ndio, nilikuwa mbinafsi. Kabla ya kujifunza kuwinda kwa imani, nilikuwa nikiwinda siku nyingi bila mafanikio. Haishangazi aliogopa msimu wa uwindaji.

**ILINIBIDI NIJIFUNZE KWAMBA TUKIWA MUME NA MKE, TULIKUWA KITU KIMOJA KIROHO NA HAKUKUWA NA KITU CHENYE NGUVU ZAIDI KULIKO WAKATI TUNAPO- KUBALIANA.**

Lakini nilijifunza kumtanguliza Drenda. Ilinibidi kujifunza kwamba tulikuwa katika jambo hili pamoja na tulihitajiana. Nilipoanza kutanguliza mahitaji yake, alikuwa tayari kukubaliana nami kuhusu kulungu. Alifurahi sana kuniona nikifanikiwa katika uwindaji wangu wa kulungu. Ilibidi nijifunze kwamba tukiwa mume na mke, tulikuwa kitu kimoja kiroho na hakukuwa na kitu kingine chenye nguvu zaidi kuliko wakati tunapo-kubaliana. Jambo halikuwa kuhusu kuwinda kulungu tu. Niligundua kwamba tulipotembea pamoja kwa umoja, hili lilifanya kazi katika kila eneo la maisha.

> *Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe*
>
> — 1 Petro 3:7

Wanaume tambua kwamba msipowajali wake zenu maombi yenu yatazuiliwa! Kujali kunamaanisha unamwona kuwa sawa, maana wewe ni mmoja naye katika kila uamuzi. Ndio, kiroho, mume ndiye kichwa cha ndoa lakini si kama dikteta bali mtumishi, anayetoa uhai wake kwa ajili ya mkewe na kumheshimu.

## Vipi Ikiwa Mwenzi Wako Si Mwamini?

Huwa ninapokea barua pepe ambapo watu huuliza kwamba wanapaswa kufanya nini ikiwa wamefunga ndoa na mwenzi ambaye hataki kumtumikia Bwana. Wanawezaje kukubaliana? Kuelewa kwako kuhusu makubaliano si sahihi. Tuseme umeolewa na mwanaume ambaye hamtumikii Bwana. Ninyi nyote, hata hivyo, mmekubali kwamba mnahitaji gari jipya. Wajua nini? Mmekubaliana! Ikiwa nyote wawili mnakubali kwamba mnahitaji mboga, basi mmekubali. Biblia iko wazi sana kwamba ikiwa mmoja katika ndoa anaamini Neno la Mungu, basi Ufalme una mamlaka ya kisheria ya kufanya kazi katika familia hiyo!

> *Kwa maana yule mume asiyeamini hutakaswa katika mkewe; na*

> *yule mke asiyeamini hutakaswa katika mumewe; kama isingekuwa hivyo, watoto wenu wangekuwa si safi; bali sasa ni watakatifu.*
>
> — 1 Wakorintho 7:14

Siamini kwamba hii ni kusema kwamba mke asiyeamini huokolewa na imani ya mwenzi wake. Ninaamini kwamba kila mtu lazima aliitie jina la Yesu kibinafsi. Hata hivyo, ninaamini kwamba ikiwa mmoja wa wanandoa anaamini Neno la Mungu, imani yake hutakasa au kuleta familia nzima chini ya baraka za Ufalme. Sasa, ni wazi, kuolewa na mwenzi anayeamini ni bora, bila shaka. Na Biblia iko wazi katika kuwatia moyo wenzi wa ndoa waaminio kwa ukweli kwamba imani yao inaweza kuwashawishi wenzi wao wasioamini kuingia katika Ufalme.

Ikiwa hujaoa, huhitaji kutafuta mtu mwingine wa kukubaliana nawe katika maombi. Wewe amini Neno tu kwa ajili yako mwenyewe na utazame kazi ya Ufalme!

Tukiwa kwenye mada ya imani, ningependa kujadili katika sura inayofuata pengine mojawapo ya maswali ya kawaida ninayoulizwa kuhusu kutoa matoleo na makosa ambayo watu wengi hufanya.

SURA YA 7

# ONYO: KAA NDANI YA IMANI YAKO ULIYOKUZA!

"Nitakamata samaki aina ya *marlin* wa pauni 900!" Hayo yalikuwa maneno ya mmoja wa washirika wa biashara yangu ambaye tulikuwa tukisafiri naye kwenda Maui, Hawaii. Tulishinda safari hii ambayo ilikuwa imelipiwa gharama zote kwa kufanya mauzo ya kiasi cha juu ya mmoja wa wachuuzi wetu. Kabla ya kuelekea Maui, watatu kati yetu tuliamua kwamba tutavua samaki aina ya *marlin* yenye rangi ya samawati, maana sio siri kwamba mji wa Maui unasifika sana kama mji mkuu wa samaki hao dunia nzima. Tulikuwa tukizungumza kuhusu imani miezi kadhaa kabla ya tukio hili, na nilikuwa nikiwafundisha vijana hao jinsi inavyofanya kazi. Dan alikuwa mpya katika mambo ya imani, nami nakumbuka niliwaza kwamba hiyo ilikuwa fursa nzuri kwake ya kwenda na kujionea kazi ya Ufalme. Kwa hiyo nikamwambia, "Dan, ulifahamu kwamba inawezekana kujua bila shaka yoyote kwamba utakamata *marlin* mwenye rangi ya samawati tutakapoenda Hawaii?" Maneno hayo yalimvutia, na tulitumia masaa mengi kuzungumzia imani kabla ya kuondoka kwenda Maui. Dan alitoa matoleo yake kama vile nilivyomfundisha na alifurahi sana kufuatilia ndoto yake, ambayo ilikuwa ni kumkamata *marlin* mwenye rangi ya samawati.

Mshiriki wangu mwingine wa biashara ambaye alikuwa mshiriki wa kanisa langu, tayari alikuwa na ufahamu mzuri wa jinsi imani inavyofanya kazi, na alikuwa amemwona Mungu akifanya mambo ya ajabu katika maisha yake. Alitoa matoleo yake pia kwa ajili ya kumkamata *marlin*, si *marlin* yoyote tu bali *marlin* ya pauni 900. Nakumbuka niliwaza, "Lo, huyo

ni samaki mkubwa!" Nilikuwa na wasiwasi fulani juu ya uzito hususa wa samaki ambao rafiki yangu alikuwa anataka, lakini sikumwambia chochote kuhusu hilo wakati huo.

Dan, kwa upande mwingine, hakutaja ukubwa wowote hususa wa samaki alipotoa matoleo yake. Naam, ili kufupisha hadithi ndefu, Dan alikamata *marlin* ya rangi ya samawati, yenye uzito wa pauni 167, lakini yule mshirika wangu mwingine hakupata *marlin* hata kidogo. Basi kwa nini Dan alimkamata *marlin* wake lakini rafiki yangu mwingine hakufaulu? Hili ni swali zuri, na watu wengi, hata Wakristo wanaweza kushtuka hata kuliuliza. Wanaweza kucheka na kusema, "Uvuvi ni nadharia ya wakati mwingine unawakamata na wakati mwingine huwakamati samaki." Lakini nilijifunza kwamba Ufalme ni hususa na unaweza kutegemewa.

> *Ikawa makutano walipomsonga wakilisikiliza neno la Mungu, Yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti, akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavuvi wametoka, wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na pwani. Akaketi, akawafundisha makutano ali chomboni.*
>
> *Hata alipokwisha kunena, alimwambia "Simoni, tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki."*
>
> *Simoni akajibu akamwambia, "Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu."*
>
> *Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama.*
>
> *Simoni Petro alipoona hayo, alianguka magotini pa Yesu, akisema, "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana!" Maana alishikwa na ushangao, yeye na wote waliokuwa pamoja naye, kwa sababu ya wingi wa samaki walioupata; na kadhalika Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, waliokuwa washirika wa Simoni. Yesu akamwambia Simoni, "Usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu."*
>
> — Luka 5:1-10

Petro aligundua njia mpya ya uvuvi, kama ilivyokuwa kwangu kuhusu uwindaji wa kulungu. Alikuwa amejaribu kuvua samaki lakini hakupata samaki hadi Yesu alipomwambia mahali pa kuvua, ndani ya kilindi cha maji. Huko alivua samaki wengi sana hivi kwamba mashua zake mbili zilikuwa karibu kuzama. Huwa ninaambia watu, "Mtu yeyote anaweza kuvua samaki ikiwa Yesu atamwambia wapi na jinsi ya kuvua."

Kwa hiyo kuhusu rafiki yangu ambaye hakumkamata *marlin* mkubwa, ndio, ni kweli kwamba mambo yote yanawezekana kwako ukiwa na Mungu. Lakini ikiwa ulitoa matoleo yako ukiamini kumkamata *marlin* wa rangi ya samawati kwenye beseni lako la kuogea, hilo halitafanya kazi. Kama unataka kumkamata *marlin* unaweza kutoa matoleo, na Roho Mtakatifu akuongoze mahali ambapo unaweza kumkamata—bila shaka katika bahari, lakini wapi katika bahari?

Kumbuka hili: Kila mavuno yana eneo la kipekee na wakati wa mavuno! Ikiwa unataka kutoa matoleo ya kumkamata *marlin* atakayevunja rekodi ya dunia, basi huwezi kusema, "Nitaenda baharini." Lazima utaenda kwenye eneo fulani la bahari. Kwa nini? Kwa sababu *marlin* wa rangi ya samawati huhama na huwa na njia fulani wanazopitia kila mwaka. Kumkamata marlin mwenye rangi ya samawati na uzito wa pauni 900 pia ni nadra. Kwa mfano, mashindano ya kawaida ya uvuvi yanayoitwa *Emerald Coast Blue Marlin Classic* huko Miramar, Florida, yamekuwa yakiendeshwa kwa miaka 17. Katika kipindi hicho Marlin mkubwa zaidi wa rangi ya samawati aliyewahi kukamatwa alikuwa pauni 899. Je, iliwezekana kumkamata marlin wa rangi hiyo na uzito huo wa pauni 900 kwenye safari hiyo ya Maui? Ndio, kwa sababu marlin mwenye rangi ya samawati aliyevunja rekodi alikuwa na uzito wa pauni 1,376, na alikamatwa huko Hawaii.

**Kadiri lengo la imani yako lilivyo mahususi au la kipekee, ndivyo inavyokuwa muhimu zaidi kuzingatia eneo, mbinu, na wakati.**

Nahodha wa mashua siku hiyo huko Maui alituambia kwamba *marlin* wenye rangi ya samawati bado hawakuwepo. Alikuwa na mashua mbili ambazo zilikuwa zimetumiwa kwa masaa manne kila siku kwa miezi minne ya awali walakini alikuwa amemkamata *marlin* mmoja tu mwenye mistari. *Marlin* wenye rangi ya samawati walitarajiwa baadaye katika mwezi huo. Bila shaka, tulimkamata mmoja mwanzoni mwa msimu huo. Lakini rafiki yangu alipofanya mbegu yake kuwa maalum zaidi, na hasa kuiweka katika kiwango cha kitabu cha rekodi cha *marlin*, basi kuvuna kungehitaji mahali na wakati muhimu zaidi. Binafsi naamini hakukuwa na *marlin* mkubwa kama huyo katika eneo hilo wakati huo. Pia tunahitaji kutambua kwamba

inawezekana kwamba rafiki yangu hakuwa na imani ya samaki wakubwa. Lakini ikiwa ana nia ya dhati ya kumkamata *marlin* mwenye uzito wa pauni 900, na ikiwa atatoa matoleo yake na kumsikiliza Roho Mtakatifu kuhusu eneo linalohusika, na kujua wakati sahihi, atampata *marlin* wake.

### Suala la Mahali na Wakati Mwafaka

Kuwa mahususi kuhusu eneo na wakati wa mavuno ni muhimu sawa na mbegu mahususi unayopanda. Uliona hili wakati nilifanya jaribio la dume mwenye pembe saba. Ilinibidi kungoja hadi nilipopata upako kabla ya kwenda; na katika hali hiyo, nilisubiri kwa zaidi ya mwezi wakati wa msimu wa uwindaji. Kwa nini? Uwezekano mkubwa ni sababu dume wa pembe saba hawakuwa kwenye mali yangu wakati huo au labda mambo mengine ambayo yangeweza kuwa kizuizi kwa mafanikio yangu yalikuwepo, kama vile hali ya hewa na mwelekeo wa upepo.

Roho Mtakatifu alijua wakati wa mavuno hayo mahususi, na aliniweka katika kisimamo kifaacho, siku ifaayo, kwa wakati ufaao ili kuvuna kulungu huyo.

Huwa ninasikia na kuona kosa hili mara nyingi. "Gary, ikiwa Ufalme huleta kulungu kama unavyosema, kwa nini hujamuua dume wa rekodi ulimwenguni?"

Sawa, swali zuri, na tunahitaji kulishughulikia. Taarifa hiyo ni kama barua pepe ninazopokea kutoka kwa watu wanaotaka kulipa rehani ya $500,000 na wananiambia walipanda mbegu ili walipwe katika siku saba. Pesa zisipokuja katika siku saba, wanavunjika moyo na kuniuliza kwa nini pesa hazikuonekana. Swali lingine la kawaida ninalosikia ni, "Kwa nini siwezi kutoa matoleo kwa kusudi la kushinda bahati nasibu?"

**ACHA NISEME TENA—NAFIKIRI UNAHITAJI KUISIKIA TENA—MUNGU ANA MPANGO KUKUHUSU!**

Sawa, hebu tuzungumzie swali kuhusu dume wa rekodi kwanza. Ndio, ninaamini kwamba ninaweza kumuua dume wa rekodi ikiwa hiyo ndiyo shauku yangu, ambayo siyo. Kwa kawaida mimi huwinda kupata nyama, na sina motisha ya kutafuta dume wa rekodi. Mojawapo ya sababu ya kutohamasishwa kufuata rekodi hiyo ya ulimwengu ni kwa sababu ya kile ambacho nimekuelezea hivi punde; huwezi kumpata nyangumi katika beseni yako. Dume wa rekodi hapatikani kwenye shamba langu. Ikiwa nilikuwa na bidii sana juu ya kuvuna dume huyo, basi najua ingenibidi

kwenda mahali pengine kuwinda. Huenda nikahitaji kujifunza mbinu mpya dume wa rekodi kawaida hupatakina usiku na wana tabia zao za kipekee. Ingenibidi kufanya utafiti mwingi na kuomba ili kupata eneo ambalo mnyama kama huyo angepatikana. Lakini sitaki kupitia shida zote hizo. Ninapenda kuwinda katika msitu wangu mwenyewe. Ninapenda kuwinda katika uwanja wangu na kupata kulungu mzuri wa kula katika starehe ya msitu wangu mwenyewe. Lakini kujibu swali lako, ninaamini mtu anaweza kumwamini Mungu kumpata kulungu kama huyo, lakini kumbuka niliyosema. Kadiri mavuno yalivyo ya kipekee na mahususi zaidi, ndivyo eneo, wakati, na mbinu vilivyo muhimu pia.

Kwa kawaida, ninapopokea barua pepe kutoka kwa mtu anayeuliza kwa nini dola milioni moja hazikuja katika siku tano, huwa ninatambua kwamba labda, wakati mwingine ninazungumza na mtu ambaye hajajifunza tofauti kati ya kuwa katika imani na kuwa na kiburi.

Ni kama barua pepe niliyoipata siku moja ambapo mtu alikuwa akisema kwamba angepanda mbegu ya dola milioni kumi baada ya siku 30 wakati hakuwa na chakula, hakuwa amelipa kodi kwa miezi mitatu, na hakuwa na kazi. Alikuwa nje ya imani aliyokuza.

Kwa hiyo, Gary, unasema kwamba Mungu hawezi kumpa mtu dola milioni kumi? Bila shaka anaweza. Yote yanawezekana kwa Mungu. Swali sio ikiwa "Anaweza?" lakini "Je, kweli una imani kuhusu hilo?" Ikiwa imani yako haiwezi kuleta chakula unachohitaji, nina shaka una imani ya dola hizo milioni kumi katika msimu huu wa maisha yako. Lakini unaweza kufika huko! Inabidi uanzie hapo ulipo na uanze kujifunza jinsi imani inavyofanya kazi na pia kupanua uwezo wako wa kusimamia zaidi ya yale unayosimamia sasa.

## Je, Unaweza Kuamini Kushinda Bahati Nasibu?

Vipi kuhusu bahati nasibu?

Ajabu, twende mbele na tuzungumzie jambo hili. Bahati nasibu zimekuwa jambo kubwa sana katika miaka michache iliyopita. Nakumbuka mwaka uliopita zilifikia karibu dola bilioni moja! Sikuwa nimewahi kununua tikiti ya bahati nasibu maishani mwangu, lakini wakati huu, zilipofika bilioni moja, wenzi wetu ofisini walisema, "Hebu, angalau tununue tikiti kadhaa." Sikufikiria sana, kwa hivyo niliamua kutupa dola kadhaa. Nilijua jinsi ilivyo vigumu kushinda—sikuweka imani yoyote katika kushinda—lakini niliwaza tu kwamba nilikuwa nikitupa pesa zangu ndani ya sufuria.

Kila mtu alikuwa akisema, "Lazima mtu ashinde." Niliwaza kwamba ikiwa mtu angeshinda zile dola bilioni moja, sikutaka kufikiria kwamba nilikosa angalau kutumia fursa hiyo ya kushinda dola hizo. Kweli, nina aibu kusema kwamba nilikubali.

Usiku huo, Bwana alizungumza nami katika ndoto kuhusu jambo hilo. Alisema katika ndoto yangu, "Ahadi Zangu zote ni zako!" "Ndio, Bwana, nakusikia vyema kabisa," nikasema. "Naelewa." Ndio, alinisahihisha, lakini pia alinitia moyo. Alinijulisha kwamba sihitaji bahati nasibu, na ikiwa ninahitaji dola bilioni moja, atanipatia wakati ninapohitaji. Nina ahadi zaidi ya 7,000 ambazo nina dai la kisheria, na zinatosha!

Sasa, kurudi katika kujibu swali la kupanda ili kushinda bahati nasibu au shindano lolote; jibu ni huna mamlaka juu yake. Naweza kupanda kwa ajili ya kulungu kwa sababu kulungu wako chini ya mwanadamu. Nina mamlaka ya kisheria juu yao. Lakini sina mamlaka juu ya bahati nasibu; ni mchezo wa kubahatisha.

## Jinsi ya Kutambua Wakati Haupo katika Imani

Kujifunza kutambua ikiwa uko katika imani kutakusaidia unapofanya maamuzi na kukusaidia kutofanya uamuzi ikiwa una woga. Kumbuka, imani ni ujasiri, matarajio, na amani kamili. Ujasiri ni kitu ambacho sikuwa nacho nilipoamua kuvuna yule dume wangu wa kombe. Sikuwa katika imani. Je, unaweza kujua wakati hauko katika imani? Ninatumai ndio.

Kama unavyojua, mimi na Drenda tunamiliki ekari 60 zenye mchanganyiko wa miti, chemchemi na nyasi. Ni mahali pazuri kabisa pa kuwinda kulungu. Kuna mimea inayozunguka mali yetu, na msitu na mabwawa ni sumaku za asili kwa kulungu. Nilijenga ofisi yangu juu ya karakana yetu yenye rafu za mbao na mahali pa moto la gesi. Ni ofisi tulivu, ya starehe ya pango, ambapo ninapenda kufanya kazi. Kitu pekee kilichosekana ni dume mzuri aliyewekwa juu ya dawati langu. Ili kuwa mkweli kuhusu hilo, sikupenda kuua dume wakubwa kwa vile nilikuwa mwindaji wa nyama, na sikuwa nimeua dume mkubwa vya kutosha kustahili kuwekwa ofisni mwangu. Lakini kadri nilivyozidi kuwaza hilo nilikubaliana na Drenda maana yeye ndiye aliyesisitiza nimuue dume mkubwa ili awekwe ofisini mwangu.

Tulikuwa tumeishi katika shamba hilo kwa miaka mitano tulipokuwa na mazungumzo hayo, na sikuwa nimewahi kuona dume wakubwa katika eneo hilo. Nilienda kuwinda kila msimu wa kulungu na nilikuwa nimewaua

dume wazuri wenye pembe nane lakini sikuwa nimeona dume aliyestahili kusimamishwa kwa ofisi yangu. Lakini mwaka huo, nilimwambia Drenda kwamba nilifikiri ningemwinda dume mkubwa kwa kusudi la kumsimamisha kwa ukuta wa ofisi. Tena, sikuwa nimewahi kuona dume wakubwa kwenye msitu wetu. Dirisha la jikoni letu linatazama msitu na shamba, lakini sikuwa nimemwona hata mmoja.

Lakini mimi na Drenda tulipanda kwa ajili ya dume mkubwa. Niliandika kwenye hundi yangu ya mbegu kwamba nilikuwa nikipanda kwa ajili ya dume mwenye pembe 10 au zaidi. Tuliiombea mbegu hiyo, nami nikaiweka juu ya meza yangu ili kuituma. Bahasha hiyo ilikaa hapo kwa siku tatu, na sikuweza kuituma. Nilijua kwamba sikuwa na imani ya kumuua dume mwenye pembe 10. Nilikuwa na imani ya dume mwenye pembe nane, sita, au nne siku nzima. Lakini nilikuwa na shida kuona dume mkubwa nikiwa na uhakikisho huo wa imani unaosema, "Ninajua kwamba nitamuua dume mwenye pembe 10 au zaidi nitakapokwenda kuwinda." Nilikuwa na uzoefu wa kutosha katika Ufalme kujua kwamba sikuwa na imani. Kwa hivyo nilirarua hundi hiyo, nikaandika hundi iliyosema "kwa ajili ya dume mwenye pembe nne au zaidi," na kuituma.

**TAYARI YOTE NI YAKO, RAFIKI YANGU, UFALME WOTE. MUNGU HAWEZI KUONGEZA CHOCHOTE KATIKA KILE ALICHOKWISHA KUKUPA. TAYARI UNAYO YOTE!**

Usiku kabla ya kwenda kuwinda, nilimweleza Drenda kuhusu kile nilichokifanya. "Sina imani ya dume mkubwa kiasi hicho," nilimwambia. Alinitazama na kusema, "Una imani kwa ajili ya kulungu, nami nitakuwa na imani kwa ajili ya dume wa kombe. Mungu ana uwezo wa kufanya zaidi ya yote uyaombayo au uyawazayo!"

Asubuhi ilifika huku kukiwa na misukosuko ya kawaida ya panya wa msitu na ndege huku harufu ya majani ya msimu wa vuli ikirudisha akilini mwangu mawinda mengi ya kulungu. Sikuwa nimekaa hapo kwa muda mrefu sana, labda dakika 20, niliposikia sauti ya dume msituni. Dume alikuwa akielekea moja kwa moja kwenye mti wangu, na nilijitayarisha kumrushia mshale. Kadiri dume alivyokaribia, niliona alikuwa na pembe nne, sawa kabisa na wale ambao kwa kawaida niliwawinda, maana ni wazuri sana kula. Alifika takriban yadi 25 kutoka kwangu, kisha nikaachilia mshale. Kwa chukizo nilitazama mshale ukimgonga na kuruka juu, kisha nikajua kwamba ingebidi nimfuate kulungu huyo. Aliruka msituni kisha

akaruka kwenye shamba la mahindi lililopakana na msitu na kutoweka. Niliweza kuisikia akikimbia kwenye mahindi na nilijua kutokana na jinsi alivyokuwa akitoroka kwa nguvu kwamba ningekuwa na kazi nyingi ya kumfuatilia.

Nilingoja kwenye kisimamo changu cha mti kwa takribani dakika 20 kisha nikaamua kushuka chini ili kuukagua ule mshale. Hakika, nilimpiga dume, na niliona mkondo wa damu. Nilipoufuata mkondo ule, nilitiwa moyo maana ulikuwa dhahiri. Lakini baada ya takriban yadi 100, mkondo wa damu ulikauka. Nilitazama na kutafuta lakini sikuweza kupata tone lingine. Baada ya masaa mawili ya kutafuta, niligundua kwamba dume alikuwa amekwenda. Nilikata tamaa sana. Kwanza, huwa sipendi kamwe kumjeruhi kulungu na kumpoteza; na pili, nilikatishwa tamaa na jinsi nilivyorusha mshale wangu.

Nikiwa nimesimama pale kwenye shamba la mahindi, nilianza kurudi nyumbani nikiwa na mawazo. *Bado nina nafasi. Ninaweza kupata kulungu ninaporudi nyumbani kupitia shamba la mahindi na kisha eneo la kinamasi*. Niliandaa upinde wangu. Nilipokuwa nikitembea polepole kwenye korongo lililo kwenye shamba la mahindi, ghafla, kulungu aliruka na kutoka mbele yangu. Bila kujua mimi ni nini, kulungu alisimama na kutazama nyuma. Kwa vile nilikuwa nimevaa mavazi ya kujisitiri, yule kulungu ambaye nilimona alikuwa dume, alisita maana hakuweza kujua mimi ni kitu gani. Yote yalitokea kwa sekunde moja. Niliona pembe, ingawa sikuweza kujua ukubwa wake au nambari yake. Nilijua nilikuwa na sekunde moja ya kuamua kuhusu dume huyo. Alikuwa umbali ambao kwa kawaida mshale wangu haungefika, takriban yadi 55 kutoka kwangu na upande wake mmoja ulinitazama. Haraka nilimkaribia na kumlenga juu ya mgongo wake na kuuachilia ule mshale. Dume alianguka mara moja mshale ulipomgonga na kubaki ndani yake. Nilishtuka kwa njia fulani. Je, hili limetokea hivi tu?

Nilipomkaribia dume, jambo la kwanza nililosema ni, "Imani ya Drenda!" Dume alikuwa mkubwa ajabu! Nilihesabu pembe 26, na nyingine ndogo iliyokuwa ikimea kuelekea chini. Sikuwa nimewahi kuona dume mkubwa kama huyo. Kweli, kusema nilifurahishwa ni kupuuza. Umekisia vyema, dume sasa yuko juu ya meza yangu ofisini mwangu. Lakini nataka kuzungumza juu ya kulungu huyu kwa dakika moja. Vipi au kwa nini alijitokeza?

Kulungu mwenye pembe nne alijitokeza wakati uliofaa ingawa sikufyatua mshale vyema. Lakini Drenda alisema alikuwa anaamini kwa

ajili ya dume wa kombe. Sasa, alikuwa na faida zaidi yangu. Yeye hawindi kulungu, na kwake, dume wa kombe anapaswa kuwa rahisi kuua kama mwenye pembe nne. Kwake wao ni kulungu tu. Kwa sababu yeye si mwindaji, hakuzungumziwa na picha ya kutowezekana. Sikuwa nimewahi kuona dume mkubwa mwenye pembe nane kwenye mali yetu, lakini imani yake haikutegemea kile kilichokuwa kwenye mali hiyo au kutokuwemo. Aliamini kwamba Mungu angeweza kumleta.

Uwindaji huu ulifanyika wakati wa msimu wa kuzaliana wa kulungu, na dume wanaweza kusafiri maili nyingi kutafuta kulungu wa kike. Kwa hivyo daima kuna uwezekano mzuri wa kuona kulungu ambao kwa kawaida huwaoni katika shamba lako wakati huo, kama ilivyokuwa hapa.

### Kushirikiana katika Imani

Imani ya Drenda ilileta dume huyo ingawa sikuwa na imani ya dume wa kombe. Nataka usome hilo tena. Sikuwa na imani ya dume wa kombe! Najua unachofikiria. "Subiri, Gary. Nimechanganyikiwa. Ikiwa hukuwa na imani ya kumpata dume huyo, kwa nini alijitokeza?" Hebu nikuonyeshe.

> *Ikawa makutano walipomsonga wakilisikiliza neno la Mungu, Yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti, akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavuvi wametoka, wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na pwani. Akaketi, akawafundisha makutano ali chomboni.*
>
> *Hata alipokwisha kunena, alimwambia "Simoni, tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki."*
>
> *Simoni akajibu akamwambia, "Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu."*
>
> *Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama.*
>
> — Luka 5:1-7

Najua tayari tuliangalia hadithi hii hapo awali, lakini nilitaka kuashiria kitu hapa ambacho kitajibu swali letu.

> *Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; **wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama.***

Nataka kukuuliza swali. Yakobo na Yohana walitumia imani kiasi gani kujaza mashua yao na samaki? Jibu ni kwamba hawakutumia imani yoyote! Ikiwa unakumbuka, mashua ya Petro, na vilevile mashua ya Yakobo na Yohana ilikuwa ufuoni, nao walikuwa wakiosha nyavu zao Yesu alipopita. Yesu alimwomba Petro atumie mashua yake kuhubiri na kisha akamwambia ashushe wavu wake kwenye kilindi cha maji ili avue samaki. Matokeo yalikuwa kwamba Petro alivua samaki wengi sana hata nyavu zake zikaanza kukatika na mashua yake ikaanza kuzama. Petro akawaita wenzake waliokuwa ufuoni waje kuwasaidia kubeba samaki. Mashua yao ilijaa sawasawa na ile ya Petro, hata ikafurika. Swali langu kwako ni, "Yakobo na Yohana walitumia imani kiasi gani kujaza mashua yao?" Jibu ni kwamba hawakutumia imani yoyote! Basi kwa nini mashua yao ilikuwa na samaki sawa kabisa na ile ya Petro? Andiko linajibu swali hilo; inasema walikuwa washirika.

**DAIMA MIMI HUSEMA KWAMBA SIRI ZA MUNGU ZIMEFICHWA KWA AJILI YAKO, SIO KUTOKA KWAKO! SHETANI ANAISHI GIZANI NA HAJUI MIPANGO YA MUNGU.**

Ufafanuzi wa neno mshirika katika Kamusi ya Kiingereza ya Collins ni: "Mtu anayeshiriki au kuhusishwa na mwingine katika tendo au jitihada fulani; kwa kawaida kushiriki hatari na faida zake."

Ubia ni mfumo wa kisheria ambapo watu hushiriki katika hatari, gharama na faida ya biashara. Kwa hiyo, imani ya Petro ilipomfuata Yesu, kwa kweli alikuwa akimkopesha Yesu biashara hiyo kwa njia ya kisheria, si mashua pekee. Yakobo na Yohana pia walikuwa na sehemu katika mashua ambayo Petro alimruhusu Yesu atumie, na kwa sababu hiyo, mashua zote mbili zilijaa kwa usawa. Kwa hiyo ni imani ya nani iliyoleta mavuno hayo? Bila shaka, ilikuwa ya Petro. Yeye ndiye aliyesema, "Bwana, tumefanya kazi kwa bidii usiku kucha na hatukupata kitu. Lakini kwa kuwa umesema hivyo, nitazishusha nyavu."

Kwa hiyo, Yakobo na Yohana walivuna mavuno yaleyale ambayo Petro

alivuna hata ingawa hawakuonyesha imani katika hilo. Ndivyo ilivyokuwa na Drenda. Sisi ni washirika, na sisi ni kitu moja. Imani yake, yenyewe, ilileta dume huyo siku ile. Tazama kwamba dhana hii ya ushirikiano ni kanuni yenye nguvu ya kiroho, kama tulivyoona hivi punde katika hadithi hii. Paulo alizungumza kuhusu kanuni hii ya ushirikiano katika kitabu cha Wafilipi.

> *Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo, sikuzote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza Injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi. Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu;*
>
> *Vile vile kama ilivyo wajibu wangu kufikiri haya juu yenu nyote; kwa sababu ninyi mmo moyoni mwangu; kwa kuwa katika kufungwa kwangu na katika kazi ya kutetea Injili na kuithibitisha, ninyi nyote mmeshirikiana nami neema hii.*
>
> — Wafilipi 1:3-7

Paulo alisema alilikumbuka kanisa la Filipi kwa furaha kwa sababu ya kuendelea kushirikiana na huduma yake. Aliendelea kusema kwamba kwa sababu ya ushirikiano wao, sasa walishiriki neema ya Mungu iliyokuwa katika huduma yake. Neema ni uweza au uwezo wa Mungu uliokuwa juu ya Paulo kukamilisha kazi yake. Kanisa la Filipi lilikuwa likishiriki katika gharama ya kazi hiyo, na kama Yakobo na Yohana, walishiriki pia katika upako na neema iliyokuwa kwenye kazi hiyo. Hebu tuende kwa sura ya 4, na utaona matokeo ya kushangaza ambayo ushirikiano husababisha.

> *Lakini mlifanya vema, mliposhiriki nami katika dhiki yangu. Nanyi pia, ninyi wenyewe mnajua, enyi Wafilipi, ya kuwa katika mwanzo wa Injili, nilipotoka Makedonia, hakuna kanisa lingine lililoshirikiana nami katika habari hii ya kutoa na kupokea, ila ninyi peke yenu. Kwa kuwa hata huko Thesalonike mliniletea msaada kwa mahitaji yangu, wala si mara moja. Si kwamba nakitamani kile kipawa, bali nayatamani mazao yanayozidi kuwa mengi, katika hesabu yenu. Lakini ninavyo vitu vyote na kuzidi, tena nimejaa tele; nimepokea kwa mkono wa Epafrodito vitu vile vilivyotoka kwenu, harufu ya manukato, sadaka yenye kibali, impendezayo Mungu. Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya*

<u>*utajiri Wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu*</u>.

— Wafilipi 4:14-19

Sikiliza kwa makini kile ambacho Paulo analiambia kanisa la Filipi, "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji." Tazama kwamba Paulo hakusema, "Mungu wenu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa sababu mmekuwa wakarimu kwangu." LA! Alisema, "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji!" Wafilipi walikuwa washirika pamoja na Paulo, na kama washirika, walishiriki katika neema iliyokuwa juu ya kazi ya Paulo. Sasa, kama vile Yakobo na Yohana walivyovua samaki hao wote kwa sababu ya imani ya Petro, Paulo alitangaza kwamba mahitaji yao yangetimizwa kwa sababu ya imani yake! Natumai unaweza kuona faida ya kanuni hii.

Hebu tuseme unahitaji gari na unashirikiana nasi kama huduma. Pia tuseme gari linagharimu $30,000. Sasa, unapotoa matoleo katika Garykeesee.com, unaelewa ushirikiano ni nini. Unashiriki upako na neema kwenye huduma yetu. Kama huduma, tunaweza kukubaliana nawe virahisi kuhusu matoleo hayo kwa sababu tulipita kiwango cha kuhitaji $30,000 zamani. Tunaweza kuwa na imani pamoja nawe virahisi kwa sababu kila mwaka tunatumia mamilioni ya dola. Lakini zamani nakumbuka ilinibidi kumwamini Mungu kupata dola 30,000, ambazo wakati huo zilionekana kama mlima mkubwa. Kwa hiyo ukiniuliza ikiwa ninaweza kumwamini Mungu kupata dola 30,000, jibu litakuwa "Hakika." Kwa hiyo kama Paulo, tunapokubaliana nawe kama mshirika, naweza kusema kwamba hitaji lako litatimizwa si kwa sababu ya imani yako bali yangu.

Sasa ni wazi kwamba unahitaji kuwa na imani unapopanda mbegu yako ya $30,000 kwa huduma yetu, unapaswa kuamini Neno la Mungu na kuniamini pia. Unapaswa kuniamini, kuwa na uhakika kwamba nimetiwa mafuta na nimeitwa na Mungu, kwamba ninafanya kazi kwa uadilifu, na unapaswa kuona matokeo dhahiri katika maisha yangu na katika huduma yangu. Ukiangalia tunachofanya na tulikotoka, utajua nina imani ya $30,000! Huenda usiwe na imani ya $30,000, lakini tunaweza kufanya kazi pamoja kwa ushirikiano na kuona mambo ambayo ni ya kushangaza. Ilikuwa vivyo hivyo na yule dume wa kombe. Drenda alisema jioni ile, "Unaamini kumpata kulungu, nami nitaamini kumpata dume wa kombe." Hivi ndivyo ushirikiano unavyofanya kazi.

## Kuchagua Ubia wa Kimkakati

Kwa hivyo hebu nikuwekee sheria za kimsingi hapa kwa kukuuliza swali. Je, ikiwa unaanzisha kampuni ya kompyuta, ungetaka kijana aliye katika muhula wake wa kwanza wa masomo ya sayansi ya kompyuta ambaye hana pesa awe mshirika wako au mtu ambaye ameunda biashara ya kompyuta yenye thamani ya mamilioni ya dola na ana fedha za kukusaidia kuzindua kampuni yako? Kwa kweli, kuna anuwai nyingi hapa, lakini ninatoa kielelezo tu. Lakini nafikiri ni wazi kwamba utachagua mtu mwenye uzoefu, aliye na rekodi ya kuthibitishwa, na ambaye hatafilisika!

Vile vile ni kweli unapotaka kupanda mbegu katika huduma fulani. Tafadhali usichanganye ninachosema na uongozi wa moja kwa moja wa Mungu wa kushirikiana na mtu fulani. Uongozi wa aina hiyo ni wa kiwango kingine na hauhusu kile ninachozungumzia. Wakati mwingine Mungu anaweza kukuelekeza uwe mshirika katika kazi Yake, lakini kuna wakati utakuwa na fursa ya kuchagua ni ipi haswa. Ninazungumzia haswa kazi unayoichagua mwenyewe, wakati unapanda mbegu ili kwenda katika kiwango kingine. Najua mimi hutoa matoleo kwa kazi ninazoamini kwa madhumuni ya kuharakisha pesa zinazohitajika maishani mwangu. Kanuni moja ambayo huwa sivunji ni kwamba mimi hutoa matoleo ya kila mara katika huduma inayoelewa imani na makubaliano isipokuwa ninatoa matoleo kwa maskini au wahitaji. Bila shaka, hatutarajii maskini na wahitaji waelewe imani. Tunapanda upendo kwao, na Mungu atatulipa. Tena, kutoa matoleo kwa maskini ni aina tofauti ya kupanda mbegu ambako hatuzungumzii hapa. Jambo lingine ninalotafuta ninapopanda mbegu ni kupata huduma iliyo na matunda yale yale ambayo ninaamini kupata kutoka kwa Mungu.

Kwa mfano, kampuni yangu inamiliki ndege mbili. Kabla ya kuzinunua, nilipanda mbegu katika kazi ya Mungu, huduma ambayo nilijua ilikuwa imelipia ndege nyingi mamilioni ya pesa hapo awali. Ninaposema nyingi namaanisha nyingi, na zote zililipwa kwa pesa taslimu. Walikuwa na matokeo dhahiri linapokuja suala la ndege. Nilijua wangeweza kukubaliana nami virahisi kuhusu ndege na kuwa na imani ili jambo hilo litimie. Sikutaka kushirikiana na huduma iliyosema kwamba ndege ni ghali sana au hazifai kumilikiwa. Hayo si makubaliano ya maana. La, nilitaka kukubaliana na huduma iliyoelewa mahali nilikuwa, huduma iliyoelewa imani yangu kuhusu kuamini Mungu kupata ndege, na kuwa na matunda ya kuthibitisha hilo.

Nimekuwa rubani tangu umri wa miaka 19 na nilijifunza kupeleka ndege kutoka kwa barabara ya changarawe yenye urefu wa futi 3,000 kule mashambani. Nilikuwa nimekodisha ndege maisha yangu yote hadi siku moja nilipowaza, *Wajua nini? Ninahitaji kupanda mbegu na kumwamini Mungu kupata ndege yangu mwenyewe*. Naam, ndivyo nilivyofanya. Nilijua ndege niliyoitaka kwa hivyo niliandika ndege hiyo kwenye hundi yangu, na mimi na Drenda tukakubaliana kuihusu. Kisha tukatuma hundi hiyo kwa huduma niliyoizungumzia hivi punde.

Vema, karibu mwezi mmoja ulipita, na nilikuwa nimeenda kwa daktari kufanyiwa uchunguzi wa kawaida. Nilipokuwa nikizungumza na daktari siku hiyo, alisema, “Je, unamjua mtu yeyote ambaye angependa kununua ndege?” Nilishangazwa kidogo na swali hilo kwa sababu katika maisha yangu hakuna mtu amewahi kuniuliza kuhusu kununua ndege. Kwa hiyo niliuliza ni ndege aina gani, na ilikuwa ndege haswa niliyokuwa nikiamini Mungu kupata. Sasa hili lilikamata usikivu wangu. Nilikwenda nikaiona ndege, nikawasiliana na mmiliki, naye akaniendesha ndani yake. Ilikuwa nzuri sana. Kulikuwa na tatizo moja tu. Wakati huo, sikuwa na pesa za kuilipia. Lakini Mungu alikuwa na mpango.

Wajua, katika msimu wa vuli uliotangulia, na sasa ilikuwa Machi, nilikuwa nimepokea jengo kutoka kwa babangu ambalo ningelikarabati na kulifanya ofisi katika msimu wa masika. Babangu aliniambia kwamba alikuwa amefunga mabomba ya maji kabla ya msimu wa baridi kali, kwa hiyo sikuyachunguza hata kidogo. Siku chache tu baada ya kuona ile ndege, kakangu alinipigia simu na kusema kwamba jengo langu lilikuwa limeharibika. Kisha akaniambia kwamba mbao za kuta zote ndani ya jengo hilo zilikuwa zimeharibika na nyingi zao zilikuwa zimeanguka kutoka kwa ukuta. Ilikuwa dhahiri kwamba mabomba ya maji hayakuwa yamefungwa na yalikuwa yameganda wakati wa baridi. Sasa kwa sababu ulikuwa mwezi wa Machi na joto lilikuwa limeongezeka, maji yalianza kumwagika ndani ya jengo na hakuna anayejua kwa muda gani, angalau wiki chache.

Kitu ambacho kakangu hakujua ni kwamba tayari nilikuwa nimefanya mkataba na kampuni ya ujenzi ambayo ingevua kuta zote na ubavu wa nje. Hii ilikuwa sehemu ya mchakato wa ujenzi upya wa kubadilisha jengo kuwa ofisi yangu mpya. Sasa, hapa ndipo jambo la kupendeza lilipotokea. Kampuni ya bima ililipa madai ya uharibifu wa maji, na hizo ndizo pesa nilizotumia kulipia ndege yangu. Niliilipia ndege pesa taslimu!

Kwa hivyo kumbuka, ushirikiano ni kanuni yenye nguvu ya kiroho ambayo unahitaji kuifahamu na kufaidika nayo.

Hii inahitimisha mjadala wetu kuhusu kuachilia mbegu yako ukiwa na imani. Kwa hiyo sasa kwa kuwa umepanda mbegu yako, ni nini kitafuata? Niamini, watu wengi hawajui haya, kama inavyothibitishwa na Wakristo wengi wanaopanda lakini hawaoni faida yoyote kutoka kwa matoleo yao. Je, huu ni wakati wa kuketi kunywa limau hadi mavuno yako yatakapokuja?

Afadhali usifanye hivyo! Tutajadili kile unachopaswa kufanya katika sura inayofuata.

SURA YA 8

# UNAHITAJI MPANGO!

Brad na Charity walipokuja kanisani kwetu kwa mara ya kwanza, sikuwafahamu. Nakumbuka niliwasalimu na kuzungumza nao kidogo mara kwa mara. Mara ya kwanza walipokamata usikivu wangu kiroho ilikuwa katika kongamano la wanawake la Drenda. Mkutano huo ulianza Alhamisi jioni na kumalizika Jumamosi alasiri. Wengi wa watu waliohudhuria walibaki ili kuhudhuria ibada ya kanisa ya Jumamosi jioni. Ilikuwa katika ibada hiyo ambapo Brad na Charity walikuja baada ya ibada na ombi. Walitaka kuanzisha biashara na hivyo waliniomba ikiwa ningepokea mbegu yao katika huduma yetu na kuwaombea kwa ajili ya biashara hiyo.

Niligundua baadaye kuwa Charity alikuwa amekodi kibanda kwenye kongamano la wanawake ili kuuza baadhi ya dawa zake za nywele zilizotengenezwa kwa mikono kwa ajili ya nywele zilizojisokota za Kiafrika na Kimarekani. Alikuwa amekodisha meza kwenye kongamano hilo kwa dola 150, na aliuza bidhaa yenye thamani ya $350, ambayo ilimletea faida ya $200.

Katika ibada ya Jumamosi jioni, wote wawili walijitokeza na zile $200 na walitaka kuzipanda katika huduma yetu kama mbegu kwa ajili ya biashara yao kukua. Nikasema, “Bila shaka,” nasi tukaomba. Sikuwaza sana kuhusu hilo, lakini niliona shauku machoni mwao, na ningeweza kusema walikuwa katika imani walipokuwa wakitoa mbegu yao.

Ili kukupa maelezo mafupi kuhusu Brad na Charity, wakati huo, Brad alikuwa meneja katika idara ya kompyuta ya kampuni fulani, na Charity alikuwa akilipwa $10 kwa kazi ya muda, ilikuwa familia yenye mapato wastani tu. Baada ya kongamano hilo, waliendelea kuuza bidhaa zao kwa

marafiki na baadhi ya mauzo ya mtandaoni lakini walikiri kuwa biashara hiyo haikuwa ikiongezeka. Lakini Mungu alikuwa akifanya kazi nyuma yao akitayarisha ukuaji wao wa siku za usoni.

Mafuta ya mbuni, ambayo walinunua kutoka kwa mkulima wa mbuni huko California, yalikuwa kiungo kikuu katika fomula yao, na waligundua kwamba alitaka kuuza kampuni hiyo. Bei ilikuwa $40,000. Charity alijua hii ilikuwa fursa nzuri kwa ukuaji wa kampuni yao wa siku zijazo, lakini Brad na Charity hawakuwa na hela hata moja. Walikuwa na pesa za kutosha kununua tikiti za ndege kwenda kuona kampuni huko California tu. Brad alisema kadri alivyokaribia California, ndivyo wasiwasi ilivyoendelea kumwingia. Angemwambiaje mwenye mali kwamba hawakuwa na pesa ilhali alikuwa ameahidiana na Charity kutokopa pesa kwa ajili ya biashara yao? Walipofika California, mkulima huyo aliwaonyesha pande zote lakini akawaambia kwamba tayari alikuwa amepata mnunuzi wa kampuni ya mafuta. Ilionekana kana kwamba mambo hayakuwa sawa. Lakini mmiliki alimwomba Brad amfanyie kazi fulani ya kompyuta, jambo ambalo Brad alikubali.

Wakati huo, Brad na Charity walianzisha uhusiano na mmiliki; na siku moja, alisema kwamba alikuwa ameamua kuwauzia biashara hiyo. Alipokea malipo ya biashara hiyo, na Brad na Charity wakapata kampuni yao ya mafuta ya mbuni. Ilikuwa karibu wakati huu ambapo Brad na Charity walisikia kuhusu mradi wa ujenzi tuliozindua katika Kanisa la Faith Life, na wakawa na msisimko ndani yao. Walikuwa wameona mbegu ya kwanza waliyoipanda hapo awali ikibadilisha kabisa biashara yao, na sasa walijua ni wakati wa kuipeleka biashara hiyo kwa ngazi nyingine kwa kutoa mbegu nyingine kubwa. Tena, Brad na Charity walikutana nami mbele ya kanisa na kupanda mbegu kwa ajili ya biashara yao na kusudi walilokuwa nalo. Hawakuwa wakipanda kwa ajili ya pesa zao binafsi bali kwa lengo la takwimu sita walilotaka kutoa kwa mradi wa ujenzi.

Ili kufupisha hadithi ndefu, mabadiliko makubwa yalitokea tena katika bidhaa yao, na Mungu alitoa kiungo kipya ambacho kilibadilisha bidhaa hiyo na kuifanya ya kufaa hata zaidi kwa nywele za Kiafrika-Amerika. Bidhaa ilisifika. Na baada ya muda mfupi, walikuwa wametoa kwa mradi wa ujenzi hundi ya takwimu sita. Sasa, wanasaidia miradi kote barani Afrika, na mapato yao sasa yamezidi takwimu saba. Haya yote yalitokea katika kipindi cha miaka mitatu. Ni hadithi ya ajabu kama nini ya kutoka mapato ya $10 kwa saa moja hadi mamilioni katika miaka mitatu! Ajabu kweli!

Hii ni hadithi nzuri na mfano kamili wa jinsi Mungu anavyofanya kazi

nawe ili uweze kunasa riziki yako na kupanua ushawishi wako. Jambo la kwanza lililonivutia zaidi ni mioyo yao kwa ajili ya umanufaa wa Ufalme na kusudi la ushirika wao, ambalo ni kutegemeza Ufalme wa Mungu kifedha. Pili, ni jinsi walivyoshirikiana na Mungu kuendeleza muundo, bidhaa, na mpango wa kampuni bila ya chochote. Hii inapaswa kumtia moyo mtu yeyote anayetaka kufanya jambo muhimu ambalo halihusu kiasi cha pesa ulicho nacho au kile unachojua unapoanza. Mungu atafanya kazi pamoja nawe wakati wote.

Hili linanileta katika kanuni ya nne ya Ufalme ambayo Mungu alinifundisha, na hiyo ni kwamba baada ya kutoa matoleo na kuachilia imani, unahitaji kumsikiliza Mungu ili kupata mpango Wake.

**Hatua #4: Baada ya Kupanda na Kuachilia Imani Yako, Unahitaji Mpango.**

> *"Ninyi wenyewe wapeni chakula," Yesu akajibu.*
>
> *Wakauliza, "Je, unataka twende kutumia sarafu mia mbili za fedha kununua mikate ili kuwalisha?"*
>
> *Basi Yesu akawauliza, "Mna mikate mingapi? Nenda mkaone."*
>
> *Walipojua, wakamwambia, "Mikate mitano na samaki wawili."*
>
> *Kisha Yesu akawaambia wanafunzi Wake wawafanye watu wote kugawanyika katika vikundi na kuketi kwenye majani mabichi. Kwa hiyo watu wakaketi safu katika vikundi vya watu mia moja na vikundi vya watu hamsini. Kisha Yesu akaichukua ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni, akamshukuru Mungu. Akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi Wake wawagawie watu. Pia akawagawia wale samaki wawili. Kila mtu alikula na kushiba. Kisha wanafunzi wakaokota vikapu kumi na viwili vilivyobaki vya mikate na samaki. Idadi ya wanaume waliolishwa ilikuwa elfu tano.*
>
> — Marko 6:37-44 (Tafsiri ya 'GNT')

Yesu aliwapa wanafunzi mpango wa kutekeleza kabla ya samaki na mikate kuzidisha. Kwa hiyo, hakikisha unaelewa hili.

Mara tu unapopanda mbegu yako kwa imani, unahitaji kupata

mpango kutoka kwa Roho Mtakatifu. Njia bora ya kufanya hivyo ni kutumia muda mwingi katika kuomba katika Roho. Usifanye maamuzi yoyote au kuzindua jambo kwa nguvu zako mwenyewe hadi usikie kutoka kwa Mungu. Kuna sababu nyingi za kutofanya hivyo. Kwanza, utajaribu kufanya hivyo kwa nguvu zako mwenyewe na kuwa na mawazo madogo sana. Pili, unaweza kupanga kufanya kitu ambacho tayari unajua wakati Mungu anataka kukupa mwelekeo mpya. Tayari umejaribu kile unachokijua, na unahitaji wazo jipya na mpango wa kubadilisha mavuno yako. Kwa hivyo, mngojee Bwana ili upate mawazo na mpango mpya. Unaweza kutoka popote. Unaweza kuona tangazo, kukutana na mtu, au kuwa na ndoto kama mimi. Mungu akipata umakini wako atakusaidia kuunda mpango mpya. Hebu nikupe mfano kwa nini hii ni muhimu sana.

**MARA TU UNAPOPANDA MBEGU YAKO KWA IMANI, UNAHITAJI KUPATA MPANGO KUTOKA KWA ROHO MTAKATIFU.**

### Nguvu ya Mpango

Nafikiri nimezungumzia mfano huu katika kila kitabu changu kilicho katika mfululizo huu unaoitwa "Mapinduzi Yako ya Kifedha," lakini inastahili nirudie tena. Ikiwa ningekuambia kwamba ningeweza kutatua matatizo yako yote ya kifedha kwa maneno machache yafuatayo, nina hakika ungeketi kusikiliza maelezo, kalamu mkononi. Sawa, jiandae kwa sababu jibu lako liko hapa. Pata mapato ya jumla ya $ 10 milioni mwaka huu. Ndio, nimesema pata mapato ya jumla ya $ 10 milioni kabla mwaka haujaisha. Kwa watu wengi, hili litaleta suluhu katika fedha zao.

Eti nini? Je, ninasikia mtu akicheka kicheko cha dharau? Je, unacheka? Ninapowaambia watu katika mikutano yangu kufanya hivi, huwa nasikia vicheko vya madharau katika ukumbi mzima. Kisha nawauliza kwa nini wanacheka. Wanacheka kwa sababu kwao huo ni mzaha; haiwezekani. Kisha nawaambia kwamba nikipunguza lengo la mapato kwa mwaka, wataacha kucheka na kusema, "Ah, hilo naweza kutimiza."

Kwa hivyo, kicheko chako kinakoma katika kiasi gani cha mapato, $600,000 kwa mwaka? Unajiona wapi, $200,000 au $100,000 kwa mwaka? Labda kiasi chako ni kidogo sana, labda $45,000 kwa mwaka. Kati ya $10 milioni na $0 kwa mwaka, utapata kiasi ambacho utasema, "Nafikiri naweza kutimiza hilo." Lakini kuna tatizo; hapo ndipo utakapokaa. Elewa

hivi, hakuna mtu anayejaribu kitu anachofikiri kwamba hakiwezekani kwake. Kwa hiyo, shida ni hii. Umefungwa au umezuiliwa na mawazo yako mwenyewe.

Sasa, hebu nikuonyeshe nguvu ya mpango. Tutumie kauli hii hii, kwamba shida zako zote za kifedha zitatatuliwa ikiwa utapata mapato ya jumla ya $10 milioni mwaka huu. Lakini wakati huu, nikupe mkataba wa kupata pesa. Nikulipe $500 kwa kila kisanduku utakachoweka mpira ndani yake, kukifunga na mkanda, kukiweka alama ya posta, kisha kukiweka kando. Hebu tuseme unaweza kuandaa masanduku 100 kwa saa, au kuwa na mapato ya $50,000 kwa saa. Tuseme pia kwamba unafanya kazi kwa masaa 10 kila siku na hivyo kuwa na mapato ya $500,000 kila siku. Sasa nikisema tuwe na mapato ya $10 million kabla ya mwaka kuisha utasemaje? "RAHISI! Hiyo itachukua siku 20 tu za kazi." Sawa, hebu nikuulize ni nini kilibadilika. Hakuna chochote isipokuwa sasa una mpango ambao, ukifuatwa, unahakikisha kwamba utatimiza lengo lako la mapato ya dola milioni 10 kwa mwaka.

Umeelewa? Ungeachwa na mawazo yako mwenyewe, labda hungewahi kufikiria kwamba lengo lako linawezekana, na ungetosheka na chochote unachofikiria kuwa kinawezekana. Lakini huhitaji maoni yako; tayari umekuwa ukiishi katika ulimwengu huo mdogo kwa muda mrefu sana. La, unahitaji Roho Mtakatifu akusaidie kuota.

## Mungu Ana Mpango Kwa Ajili Yako

Nilikuambia awali kuhusu hali yetu mbaya ya kifedha na mashambulizi ya hofu na huzuni niliyopata kutokana na ukosefu wa fedha. Nilipoanza kujifunza maisha ya Ufalme, sikuwa na mahali pa kugeukia ila Mungu. Alinena na mimi na kunipa mpango wa kuanzisha Forward Financial Group na kuwaonyesha watu jinsi ya kutoka kwa madeni. Hilo ni jambo la kichaa! Nakumbuka nikiwa nimeketi nyumbani kwangu na kutafakari kile alichokuwa akiniambia nifanye na nikasema, "Laiti ungeniambia kwanza." Lakini alinijibu kwamba ningetoka kwa madeni ninapotekeleza mpango huo.

Wakati mimi na Drenda tulizindua mpango ambao Mungu alitupa, hatukuwa na vifaa, kompyuta, wala chochote. Lakini tulipoona mpango huo, nilijua utafanya kazi; nilijua inawezekana. Namaanisha mkakati na maelezo aliyotuonyesha kuhusiana na kuzindua mpango huo. Ningeweza kutimiza hilo! Kwa kweli, nilipenda kufanya hivyo.

Kama ilivyokuwa na Brad na Charity, Mungu alitupa vifaa vyote vya kuanzisha tulivyohitaji. Ajabu, siku moja, babangu, ambaye alikuwa na duka la pizza na hakuwa na haja ya kompyuta, aliniambia kwamba alitaka kununua kompyuta, na akaniambia twende pamoja. Kwa hiyo tulienda tukanunua kompyuta yake na programu ya kuchakata maneno ambayo alisema ningeweza kutumia. Elewa kwamba sikujua chochote kuhusu kompyuta. Nyumba yake ilikuwa maili moja mbele ya barabara iliyotoka kwangu, na nilianza kujaribu kutumia kompyuta na programu hiyo hadi nilipoweza kuandika uwasilishaji mzuri wa mteja kuhusu jinsi ya kutoka kwa madeni. Mungu alifanya njia wakati sikuwa na pesa.

Kampuni ilikua, na nilianza kuajiri wawakilishi wa mauzo. Siku hizo, tulitumia vikokotoo vyetu vya fedha vya mkononi kufanya hesabu zote za kila familia. Kisha tungeandika taarifa hiyo kwenye kiolezo, ambacho nilikuwa nimeunda kwenye programu yangu ya kuchakata maneno, na kuchapisha ili wawakilishi wetu wawapelekee wateja wao nyumbani kwao. Kichapishi chetu kilikuwa kikifanya kazi siku nzima. Hivi karibuni katibu wangu hangeweza kuendelea kufanya kazi hiyo, kwa hivyo ilinibidi niajiri mtu mwingine wa kusaidia kuandika na kuchapisha ripoti hizi za wateja.

Nilitambua kwamba nilihitaji njia bora ya kufanya biashara. Nilihitaji programu ya kompyuta ambayo ingeweza kukokotoa milinganyo yote ya kifedha ya kila mteja ambayo ilihitaji kukokotwa na pia kuichapisha. Mimi na Drenda tulimwomba Bwana msaada kwamba atupatie fundi wa kompyuta ambaye tungeweza kumudu atuandalie programu nzima ya kampuni yetu.

Miezi michache baada ya maombi haya, nilikuwa katika ziara ya kawaida kwa mteja wakati aliniuliza, baada ya kuona chapa niliyomtayarishia, "Je, unafanya hivi kwa mkono?" Nikasema, "Ndio, lakini tunataka kuhamisha haya yote kwa programu ya kompyuta ambayo itakuwa inatuandikia." Alinitazama na kunieleza kwamba alikuwa fundi wa programu za kompyuta kazini lakini angependa kutusaidia kututayarishia moja jioni katika wakati wake wa ziada. Alitaja bei, na kwamba angeniruhusu nilipe niwezavyo katika mwaka uliofuata.

Mpango huo ulibadilisha kila kitu na kuniwezesha kuajiri watu zaidi. Muda si muda, tulikuwa na wawakilishi 300 katika sehemu kubwa ya mashariki mwa Marekani, jambo ambalo lilisababisha ofisi yetu kuwa ofisi nambari moja kati ya ofisi 5,000 za mmoja wa wachuuzi wetu.

Kwa sababu ya kuanzisha kampuni yetu wenyewe na kumfuata Roho Mtakatifu, hatukuwa na madeni kabisa, na mengine ni historia, kama

wasemavyo. Ninachosema ni kwamba Mungu atakupa mpango ikiwa utamwomba na kumruhusu autimize. Atakupeleka mahali ambapo hukuwa umewahi kufikiria hapo awali.

Kwa hiyo, hebu nisisitize kwamba unahitaji mpango. Mungu ana mpango wa kukufanikisha. Kwa kweli, ana mipango mingi kwa ajili ya mafanikio yako. Mawazo na hekima Yake havina mwisho.

> *"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi," asema Bwana, "ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho."*
>
> — Yeremia 29:11

**Je, Mtu Husikiaje Kuhusu Mpango wa Mungu?**

Kwa hiyo, unasikiaje kuhusu mpango huo? Kama nilivyosema, kuomba katika Roho ndiyo njia bora ya kusikia. Sitashughulikia kuomba katika Roho kirefu hapa kwa sababu kitabu changu cha Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Mikakati kinashughulikia kumsikia Roho Mtakatifu kwa undani sana. Lakini nukuu fupi inafaa.

> *Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala ya hao wanaoitawala dunia hii, wanaobatilika; bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu; ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu;*
>
> *Lakini, kama ilivyoandikwa, "Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,)" mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho.*
>
> *Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu. Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu.*
>
> — 1 Wakorintho 2:6-12

Mambo ambayo hatujasikia, kuona, au kufikiria, kama ilivyotajwa katika Maandiko haya, ni mambo ambayo yamefunuliwa kwetu na Roho Mtakatifu. Kwangu linaonekana kama jambo la faida kubwa; ninaweza kufaidika nalo. Ulipofanyika Mkristo, Roho Mtakatifu alikuja kukaa ndani yako, na akaanza kuongoza maisha yako.

Lakini kuna kipimo kingine cha Roho Mtakatifu ambacho Yesu alilipatia kanisa, kinachoitwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Haya ndiyo tuliyoyaona yakitendeka siku ya Pentekoste wakati Roho Mtakatifu alipowashukia wanafunzi katika chumba cha juu kama vile alivyomshukia Yesu kwenye Mto Yordani. Huu ndio wakati Yesu alipoanza huduma Yake. Huu ndio wakati uweza wa Mungu ulipokuja juu yake kuwa shahidi wa Ufalme. Yesu hakufanya miujiza alipokuwa mtoto. Hakuzidisha chakula cha familia yake wala kutembea juu ya maji. Ili kuelewa ubatizo wa Roho Mtakatifu, utahitaji kuelewa kwamba kuna tofauti kati ya kuzaliwa mara ya pili (wakati Roho wa Mungu anapoingia ndani yako) na ubatizo wa Roho Mtakatifu (Roho Mtakatifu anapokuja juu yako.)

> *Ikawa jioni, siku ile ya kwanza ya juma, pale walipokuwapo wanafunzi, milango imefungwa kwa hofu ya Wayahudi; akaja Yesu, akasimama katikati, akawaambia, "Amani iwe kwenu." Naye akiisha kusema hayo, akawaonyesha mikono Yake na ubavu Wake. Basi wale wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana.*
>
> *Basi Yesu akawaambia tena, "Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma Mimi, Mimi nami nawapeleka ninyi." <u>Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, "Pokeeni Roho Mtakatifu."</u>*
>
> — Yohana 20:19-22

*Hapa katika Yohana 20, wanafunzi tayari walikuwa wamezaliwa mara ya pili, lakini Yesu aliwaambia kwamba bado walipaswa kusubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao ungewawezesha kuwa mashahidi wa Ufalme wa Mungu.*

> *Wale aliowadhihirishia nafsi Yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa Kwake, ya kwamba Yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyouhusu ufalme wa Mungu. Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo walisikia habari Zake Kwake; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali*

*ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku chache.*

— Matendo 1:3-5

*Lakini mtapokea nguvu, akiisha <u>kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu</u>; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*

— Matendo 1:8

Upako huu kutoka kwa Mungu huleta nguvu za Mungu na kukuwezesha kufanya kazi Zake. Tafadhali tambua kwamba unakuja juu yako na sio ndani yako. Unaweza pia kukumbuka kwamba katika Siku ya Pentekoste wanafunzi wote waliokuwa wakingoja Yerusalemu katika chumba cha juu walibatizwa kwa Roho Mtakatifu. Je, moja ya ushahidi wa hili ulikuwa upi? Wote walinena kwa lugha. Kunena kwa lugha kumeorodheshwa katika 1 Wakorintho 12 kama mojawapo ya karama tisa za kiroho ambazo zilitolewa kwa kanisa. Unaweza kusema kwamba karama hizo zilipita, lakini sikubaliani kabisa. Ubatizo wa Roho Mtakatifu huleta karama zote tisa za kiroho, lakini nataka kuzingatia karama hii moja tu, kunena kwa lugha.

**UPAKO HUU KUTOKA KWA MUNGU HULETA NGUVU ZA MUNGU NA KUKUWEZESHA KUFANYA KAZI ZAKE.**

Mwanzoni hili linaweza kuonekana kana kwamba halina maana kwa kuwa unaweza kudhani linahitajika tu ikiwa unahubiria watu wanaozungumza lugha tofauti. Lakini kuwa na uwezo wa kuzungumza na watu kwa lugha usiyoijua kamwe haikuwa nia ya karama ya kunena kwa lugha. Hebu nikuonyeshe kwa nini ni karama ya thamani sana na kwa nini ni muhimu kwa ufanisi wako.

*Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake. Bali yeye ahutubuye, asema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji, na kuwatia moyo. <u>Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake</u>; bali ahutubuye hulijenga kanisa. <u>Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha</u>, lakini zaidi sana mpate kuhutubu, maana yeye ahutubuye ni mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha, isipokuwa afasiri, ili kusudi kanisa lipate kujengwa.*

— 1 Wakorintho 14:2-5

Tunahitaji kuelewa muktadha wa barua ya Paulo hapa. Anazungumza

kuhusu jinsi kusanyiko la kanisa linapaswa kuendeshwa. Kimsingi anasema kunenea watu kwa lugha katika ibada hakuna faida kwa sababu wale wanaosikia hawaelewi kile kinachosemwa. Paulo alisema katika ibada ni afadhali kuhutubu kwa kuwa hilo hufanyika kwa lugha ya kawaida ya watu na litawanufaisha zaidi.

Lakini inapohusu mtu mmoja kujiombea kwa lugha, ajabu, hilo ni jambo tofauti. Kunena kwa lugha kuna faida kubwa kwa yule anenaye. Biblia inasema anatoa mafumbo kupitia kwa roho yake. Mafumbo haya ni yale usiyoyajua na unayohitaji kujua. Pili, Paulo anasema kwamba mtu anenaye kwa lugha hujijenga mwenyewe. Neno kujenga maana yake ni kuleta mafundisho. Ni wazi, ikiwa unahitaji kujua jambo, basi ni siri kwako wakati huo. Lakini kunena kwa lugha huleta mafundisho kwa yule anenaye. Wewe na mimi tunahitaji hilo kwa hakika ikiwa tutatengeneza mipango mikubwa kuliko kile tunachojua tayari. Kama 1 Wakorintho 2:9-10 inavyosema:

> *Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu.*

Ninahitaji msaada huo, na wewe pia. Swali lingine ni, "Ikiwa unanena kwa lugha na huelewi unachosema, basi unafaidikaje kutokana na hayo unayosema?" Naam, hapa kuna siri. Roho Mtakatifu anapozungumza kupitia roho yako ya kibinadamu, akili yako huanza kunyakua baadhi ya mawazo yanayotiririka ndani yako. Tunayaita ufunuo, na mzizi wa neno hili ni kufunua. Kwa hiyo, kwa kuomba katika Roho, au kunena kwa lugha, kama kunavyoitwa katika Biblia, kuna uwezo wa kunyakua mawazo na dhana zisizo zako.

Najua labda una maswali mengi kuhusu hili, kwa hivyo hebu nikutie moyo upate kitabu changu *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa na Mkakati*. Utapata majibu yako yote hapo.

### Sitisha na Uombe Kupata Mkakati

Kwa sasa, hebu tuelewe kwamba mara tu unapopanda mbegu yako kwa imani, hatua inayofuata ni kukoma na kuomba katika Roho Mtakatifu kwa muda kwa sababu unahitaji mpango. Hivi ndivyo Karla alivyofanya.

Karla na Todd walikuwa wakiishi maisha ya kawaida ya Wamarekani, mshahara hadi mshahara na kutumbukia kwenye madeni zaidi na zaidi. Karla alikuwa ameona matangazo ya kipindi chetu *Fixing the Money Thing* siku moja katika runinga na akajua kwamba walihitaji kuwa na mpango taratibu katika fedha zao. Nakumbuka barua pepe niliyopokea kutoka kwa Karla. Alisema kwamba wakati huo, hawakuwa na mpango wa kifedha. Hawakuwa na uwezo wa kumudu hata miezi kadhaa mbele yao, walikuwa wamefinyika sana. Upungufu wowote katika bajeti yao ulishughulikiwa na kadi za mkopo.

Alijua kwamba walihitaji kutoka kwa madeni, lakini vipi? Baada ya kusoma kitabu changu, Yeye na mumewe walipanda mbegu kusudi wapate wazo la kibiashara, na walipanda haswa kwa biashara ambayo angeweza kufanya akiwa nyumbani. Todd tayari alikuwa na shughuli nyingi kama mwalimu wa shule katika shule ya mtaani, kwa hiyo Karla alikuwa akijiuliza kile ambacho angeweza kufanya ili kuwa msaada. Baada ya kutoa matoleo kwa ajili ya kupata wazo, kila asubuhi Karla alitenga wakati wa kuwa mtulivu mbele za Bwana, huku akingoja kusikia mwelekeo fulani kutoka kwa Roho Mtakatifu.

Asubuhi moja, kutoka ndani ya roho yake, alisikia maneno watoto wa mbwa. Mwanzoni alichanganyikiwa kidogo. Watoto wa mbwa? Kulea watoto wa mbwa? Wakati fulani walikuwa na mbwa, lakini kulea watoto wa mbwa lilikuwa jambo ambalo hakuwa amefikiria sana. Todd aliporudi nyumbani jioni hiyo, Karla alitaka kumwambia kile ambacho Mungu alikuwa amesema. Kama ilivyotarajiwa, Todd alikuwa na hofu kidogo kuhusu mpango huo lakini alimtia moyo Karla kuchunguza uwezekano wake. Punde, Todd na Karla walinunua watoto wawili wa kike wa mbwa anayeitwa *goldendoodle* na kuanza biashara yao watoto wa mbwa. Bila shaka, walipaswa kulea watoto wao wa mbwa kwanza kisha kuanza mchakato wa kuzaliana.

Kulikuwa na vikwazo vichache njiani, lakini mwaka wa kwanza mbwa wao walikuwa na watoto 13. Mbwa hao waliuzwa kwa karibu dola 1,500 kila mmoja, na Karla anasema alitokwa na machozi alipotambua kwamba alikuwa amemsikia Roho Mtakatifu kwa usahihi aliposikia maneno watoto wa mbwa. Katika mwaka huo huo, Todd pia alipandishwa cheo hadi cheo cha mkuu wa shule ya mtaani.

Biashara ya watoto wa mbwa iliendelea kukua; na kufikia sasa, wamekuwa na watoto wa mbwa zaidi ya 300, na bei imepanda hadi karibu $2,500 kila mmoja. Maisha yao ya kifedha yamebadilika kabisa! Walimaliza

kulipia nyumba yao mwaka jana na sasa hawana deni lolote. Wamesafiri nje ya nchi kwa safari za kustaajabisha na wamemwona Mungu akifanya mambo mengi sana katika familia yao ilimpasa Karla kuwaambia watu kuhusu Ufalme Wake. Amemaliza kitabu chake cha kwanza hivi karibuni kinachoitwa, *Plans to Prosper: How God Gave Us Financial Freedom Through Puppies*.

Todd na Karla wanaishi maisha ya Ufalme, ambayo huwavutia watu na kuwafanya wasimame na kufikiria kumhusu Mungu. Nabii Isaya alizungumza kuhusu nyakati za kanisa katika Isaya 61 ambapo alituambia kile ambacho Mungu anataka kufanya na maisha yetu tukiwa duniani.

> *Wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na Bwana, ili atukuzwe.*
>
> — Isaya 61:3

Mwaloni ni mti wenye nguvu sana na kwa kawaida ni mkubwa pia. Biblia inasema maisha yetu yatakuwa kama miti ya mwaloni, yenye nanga, thabiti, na isiyotikisika. Matunda ya mti huu yatakuwa haki, ambayo ina maana kwamba watu wataona jinsi maisha yanavyopaswa kuonekana, kile ambacho Mungu anakiita sawa. Sisi ni mimea ya Bwana, ambayo inamaanisha kwamba Mungu hutuweka pale anapoona panafaa, katika sehemu mbalimbali za kazi na tamaduni, ili kuonyesha fahari Yake. Mungu anataka kuvutia umakini wa watu na wewe! Anataka watu waone matunda mazuri ya njia Zake katika maisha yako. Kama vile mti wa matunda unavyokuvuta kula matunda yake yenye ladha nzuri, Mungu anataka maisha yako yaonekane kama mbingu duniani.

Kwa hiyo Todd na Karla walifanyaje? Bila shaka, iligharimu kazi nyingi kuwalea watoto hao wa mbwa, lakini uhuru ambao hilo lingeleta kwao hakika ulikuwa wa thamani kuliko kitu chochote kingine. Uhuru huo wote ulianza kwa kusikia mpango, yaani neno kutoka kwa Mungu. Neno moja rahisi ndilo alilosikia, "Watoto wa mbwa!" Lakini hilo tu ndilo lililohitajika. Mungu atanena nawe pia. Atakuongoza kwenye malisho mabichi na maji tulivu ya amani ambayo Zaburi ya 23 inazungumzia.

Lakini kama unavyoona, kusikia mpango tu hakutoshi. Nitajadili hatua ya 5 katika sura inayofuata, na inaweza kuwa sura muhimu kuliko zote kwa sababu hatua ya 5 ndipo watu wengi hushindwa. Lakini si wewe, utaenenda katika wema wa Mungu kama hadithi ulizosoma katika kitabu hiki! Uko tayari? Hebu twende kwa hatua ya 5.

SURA YA 9

# NI WAKATI WA KWENDA!

Kila mkulima anajua kwamba kila mavuno yana wakati wa kipekee na maalum unaohusika. Kujua msimu sahihi wa mavuno kwa zao fulani ndio hutofautisha kati ya mafanikio na kushindwa. Na hebu tuwe wakweli: unaweza kukosa mavuno. Kwa hiyo, hii ni mada kubwa sana na muhimu. Je, umewahi kwenda dukani, ukaona tufaha jekundu la kupendeza sana, na ukafikiri, *Hilo ni tufaha nzuri sana*—lakini uliporudi nyumbani na kulila ukafikiri, *Lo, kitu hiki hakina ladha?* Naam, hilo ni suala la wakati.

Siwezi kukuambia ni majanga mangapi ya kifedha ya watu ambayo nimesikia na kushughulikia ambapo watu huharakisha kutekeleza wazo na kukosa wakati mwafaka. Andiko ninalopenda sana kuhusu wakati ni Mathayo 13:44.

> *Tena ufalme wa mbinguni umefanana na* ***hazina*** *iliyositirika katika shamba; ambayo mtu alipoiona, aliificha; na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote, akalinunua shamba lile.*

Katika hadithi hii, mtu huyo alikuwa na hekima ya kutosha kujua kwamba wakati huo, hakuwa na uwezo wa kumiliki hazina hiyo. Ilibidi aende na kujiandaa kuinunua.

Kwa mfano, Karla aliposikia maneno watoto wa mbwa, haikuwa na maana kwamba alipaswa kutangaza kwamba alikuwa anauza watoto wa mbwa. Bado hakuwa na watoto wa mbwa. Kulikuwa na maandalizi mengi ya kufanya. Ilibidi wanunue mbwa wao wawili wa kike kwanza. Ilibidi wajenge mahali pa kuwaweka na kujiandaa kwa ajili ya watoto wa mbwa

ambao wangekuja. Kulikuwa na masuala ya kisheria ambayo walipaswa kujifunza kuhusu chanjo zinazohitajika ambazo watoto wa mbwa lazima wawe nazo ikiwa utaziuza.

Pia kuna masuala ya leseni, uuzaji, benki, na kodi, kutaja machache. Mambo haya yanahitaji kuangaliwa kabla hujaingia kwenye msimu wa mavuno wa wazo lako la biashara.

Tuseme umefanya bidii yako, lakini sehemu ngumu bado iko mbele. Inabidi uanze kutekeleza maono ambayo Mungu amekupa. Ndio, maono yatakuwa makubwa kukuliko, na kunaweza kuwa na hofu fulani inayohusika unapoanza. Lakini hofu ilikuwa ndani ya mtu wako wa zamani. Kumbuka, sasa wewe ni mtu mpya.

Mungu aliponena nami kuhusu kuanzisha biashara yangu mwenyewe, nilikuwa na hofu nyingi. Nilianza bila chochote kabisa. Ingawa Mungu alizungumza nami katika ndoto kwamba nianze na nilikuwa nimefanya bidii, bado nilikuwa na hofu juu yake. Kila kitu sasa kilitegemea kuanza kwangu. Umewahi kuwa na rafiki au kumjua mtu ambaye alikuwa akiongea kila mara juu ya kile atakachofanya lakini hakifanyi kamwe? Nimewafahamu wengi! Kumbuka, nimefundisha wauzaji kwa zaidi ya miaka 30.

Nilipozindua biashara yangu, sikupewa miongozo. Nilikuwa nikiishi kwa kutegemea kamisheni za mauzo, na nilikuwa peke yangu. Lakini jambo moja nililokuwa nalo ni shauku. Wakati Mungu aliniongoza kuanzisha kampuni ya kuwasaidia watu kutoka kwa madeni, nilikubali kabisa. Nilikuwa nimesumbuliwa na masuala ya kifedha kwa muda mrefu maishani mwangu; na sasa kwa kuwa nilikuwa nimepata jibu, Ufalme wa Mungu, nilitaka kumwambia kila mtu kuuhusu. Pili, mara Mungu aliponisaidia kuandaa mpango ulioonyesha familia jinsi ya kutoka kwa madeni katika kipindi cha miaka mitano hadi saba, ikiwa ni pamoja na rehani zao za nyumba na bila kubadilisha bajeti zao, nilikuwa na shauku hata zaidi. Nilijua nilikuwa na mahali maalum katika soko la fedha, na nilikuwa na hadithi ya kuwaambia watu. Lakini tena, ilinibidi kuwa na mfano tayari kabla ya kuwasha swichi.

Hakika daima kuna mambo unayojifunza njiani, lakini unapoanza, unapaswa kuwa na muundo wa kimsingi tayari. Lakini haijalishi ni fursa kubwa kiasi gani, bidhaa, au malipo yanayoweza kutokea, leo, na leo ndiyo siku unayopaswa kuingia katika mpango wako.

Sasa, hili linanileta kwenye shida halisi, ninayoamini kuwa sababu kuu ambayo wengi hawafikii malengo yao, hata baada ya kusikia kutoka kwa Mungu kuhusu mwelekeo na majibu ya maswala yao ya kifedha.

## Kuahirisha mambo!

Kuahirisha mambo kunaweza kuwa na msingi wa kutokuwa na usalama, woga, au uvivu tu. Lakini jambo moja ni hakika; ni rahisi kufanya! Nilisoma maneno yafuatayo kuhusu tabia za wanafunzi wa daraja la juu inapohusu kuahirisha mambo.

> *Jenny anasafisha nyumba yake. Cathy anacheza mchezo wa hesabu. Matt anaangalia alama za michezo, na Carmen anasasisha ukurasa wake wa Facebook. Wote ni wanafunzi wa saikolojia wanaoahirisha kazi wanazopaswa kufanya. Hii ndiyo kazi ya uahirishaji haswa.*
>
> *Ni tabia ngumu kuacha, haswa siku hizi wakati Mtandao unawapa wanafunzi fursa ya kuepuka wakati wa nidhamu wa kusoma kwa kubofya kipanya. Uchambuzi mmoja wa mnamo 2007 uliofanywa na mwanasaikolojia wa Chuo Kikuu cha Calgary Piers Steel, PhD, unaripoti kwamba asilimia 80 hadi 95 ya wanafunzi wa chuo kikuu huahirisha, haswa linapokuja suala la kufanya kazi za kozi zao.*

Kweli, ninapendekeza kwamba hili haliko tu kwa wanafunzi wa daraja. Vizuizi ni vingi. Kupokea simu au kufungua barua pepe bila shaka huiba wakati. Lakini kuhairisha kuna upande wa hila zaidi, wa kishetani ambao unahitaji kufahamu. Ili kufafanua na kuangazia mada hii hatari—ndio, nilisema hatari—ninataka kwenda katika 1 Wakorintho 2:6-8.

> *Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala ya hao wanaoitawala dunia hii, wanaobatilika; bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu;* ***ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu.***
>
> — 1 Wakorintho 2:6-8

Ajabu, afadhali uandike hili mahali fulani. Shetani hubadilisha mbinu anapojua unachofanya! Hii ndiyo sababu Mungu hunena kwa mifano. Hii ndiyo sababu wakati mwingine Mungu husubiri hadi saa sita usiku kabla hajafunua jibu lako. Lazima ujue na ukumbuke kwamba tuna adui. Adui yako sio mfano wa kitu kilicho na uma kubwa mkononi na vazi jekundu.

Biblia iko wazi:

> *Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze.*
>
> — 1 Petro 5:8

Sasa, bila shaka hawezi tu kummeza mtu yeyote, lakini anataka kukutoa nje ya mamlaka ya mbinguni hadi kwenye mamlaka yake ya kisheria ili kuua, kuiba, na kuharibu. Biblia inasema, "Adui yako!" Mojawapo ya mbinu za Shetani ni kukuvuta uridhike, na uahirishe mambo. Hii itampa muda wa kujua wewe na Mungu mnafanya nini.

Nakumbuka ndoto niliyoota usiku mmoja. Picha niliyoiona ilikuwa usiku, na mwanga kutoka kwenye dirisha la chumba changu ulitoka nje kwenye nyasi hadi ukafifia gizani. Pale pale ambapo nuru ilififia, kwenye vivuli, niliona pepo wawili wamesimama wakitazama dirisha langu wakiwa na madaftari mikononi mwao. Nilijua wametumwa kutafuta mlango wa kisheria wa kuingia nyumbani kwangu. Walikuwa wakiandika kumbukumbu, wakitafuta mahali pa udhaifu ambapo wangetumia kujaribu kusimamisha kazi ya Mungu.

**KUAHIRISHA MAMBO KUNAWEZA KUWA JAMBO HATARI SANA!**

Kuahirisha mambo kunaweza kuwa jambo hatari sana! Hilo linasikika kuwa neno kali, sivyo? Linasikika kuwa kinyume kabisa na yale kishawishi cha kuahirisha kinakuambia. Sauti yake ni ya hila na yenye kusadikisha, "Haitajalisha ukifanya hivyo baadaye." Unaweza kufanya baadaye. Lakini je, hiyo ni kweli? Hebu nikushirikishe hadithi ambayo itakuonyesha jinsi kuahirisha kunavyoweza kuwa hatari.

> *Huyo Mfilisti naye akamsogelea Daudi na kumkaribia; na mtu yule aliyemchukulia ngao yake akamtangulia. Hata Mfilisti alipotazama huku na huku, akamwona Daudi akamdharau; kwa kuwa ni kijana tu mwekundu, tena ana sura nzuri. Mfilisti akamwambia Daudi, "<u>Je! Mimi ni mbwa hata umenijia kwa fimbo?</u>" Mfilisti akamlaani Daudi kwa miungu yake. Mfilisti akamwambia Daudi, "Njoo huku kwangu; nyama yako nitawapa ndege wa angani na wanyama wa mwituni."*
>
> — 1 Samweli 17:41-44

> *Ikawa, hapo Mfilisti alipojiinua, akaenda akamkaribia Daudi, ndipo Daudi naye akapiga mbio, akalikimbilia jeshi ili akutane na yule Mfilisti. Daudi akatia mkono wake mfukoni, akatwaa humo jiwe moja, akalitupa kwa kombeo lake, akampiga Mfilisti katika kipaji cha uso; jiwe hilo likamwingilia kipajini, akaanguka chini kifudifudi.*
>
> — 1 Samweli 17:48-49

Hadithi ya Daudi na Goliathi ni hadithi ya kutisha sana. Taifa zima la Israeli liliogopa liliposikia kelele za Goliathi. Lakini Daudi alisema atapigana naye kwa sharti moja: kuweza kuchagua silaha yake mwenyewe, kombeo alilokuwa ametumia kwa miaka mingi akiwachunga kondoo. Daudi alipomkaribia Goliathi, Goliathi alichanganyikiwa na kupiga kelele." "Je! Mimi ni mbwa hata umenijia kwa fimbo?" Kile Goliathi alichofikiri ni kijiti hakika kilikuwa fimbo ya Daudi. Hakuona kombeo lililokuwa chini ya ukanda wake. La, Daudi alikuwa akitumia fimbo kama hila, akivuta uangalifu wa Goliathi kuihusu badala ya kombeo. Goliathi alipomkaribia Daudi, Daudi alipiga mbio ili kukutana naye. Hii ilikuwa mbinu nyingine ambayo Daudi alitumia. Alijua ingekuwa vigumu zaidi kwa Goliathi kuona kombeo ikiwa angemwendea ghafla.

Lakini vipi ikiwa Daudi angetenda kama watu wengi wanavyofanya? Kwa kuogopa kuingia kwenye mzozo, wao huhairisha tu. Je, ikiwa Daudi angecheza dansi karibu na Goliathi hadi ajisikie yuko tayari kumshambulia? Naamini kwamba Goliathi angeona kombeo, angetambua mkakati wa Daudi, na kufidia ipasavyo. Taifa zima la Israeli lingeshindwa vita hivyo na lingechukuliwa mateka.

**HIVI NDIVYO SHETANI ANAVYOTAKA KUKUFANYIA. ANATAKA KUTEKA MIPANGO YAKO.**

Hivi ndivyo Shetani anavyotaka kukufanyia. Anataka kuteka mipango yako. Ikiwa anaweza kukufanya utulie, kusubiri mpaka ujisikie tayari, atakuwa na muda wa kubadilisha mbinu yake ya kupinga mpango wa Mungu katika maisha yako. Kwa hivyo kuhairisha ni hatari? Kabisa! Nina hakika kuwa tayari imekugharimu maelfu ya pesa katika maisha yako. Katika kisa cha Daudi, huenda ingegharimu maelfu ya maisha.

Hii ndiyo sababu, unapojua wakati mwafaka na una mpango wako, jitokeze kwa ujasiri. Naamini utakuwa na msukumo kutoka kwa Roho Mtakatifu kukusaidia kujua wakati mambo yanafaa kuanzishwa. Lakini kwa sababu ya mafundisho potofu, wengi husitasita au huanza kutekeleza

kisha, wanapopata migogoro, wanarudi nyuma na kufikiri kwamba lazima wamemkosa Mungu.

## Usiogope Migogoro

Watu huniambia kwamba walipoanza kutekeleza mpango wao, kuzimu kulizuka. Kweli, umeandaliwa kushughulikia kuzimu bila woga. Adui amepigwa kofi tu na mpango wako wa Roho Mtakatifu, na anaitikia kuuzima. Hawezi kuuzuia sasa. Amechelewa. Lakini kama anaweza kukufanya utilie shaka neno la Bwana lililokuongoza, basi hofu itakurudisha nyuma. Anataka kusababisha fujo kiasi kwamba urudi nyuma. Lakini unahitaji kusimama imara sasa kuliko hapo awali na kutumia mamlaka yako kumdhibiti. Usiogope kusema, "Hapana, hutafanya hivyo" au "Ninafunga roho ya kuchanganyikiwa ambayo inajaribu kunitesa. Ninajua kile Bwana alisema nifanye, na nitafanya, katika jina la Yesu. Sasa ondoka, Shetani!"

Cha kusikitisha ni kwamba, wengi wa Wakristo wa siku hizi ambao hawajazoezwa huitikia mashambulizi ya Shetani kwa mshangao. Wanaamini kwamba kwa kuwa Mungu amesema nao na amewapa mpango Wake kwamba kila kitu kitaenda sawa na haraka bila mashambulio ya ghafula.

Sasa, usikose kuelewa vyema ninachosema. Tuna mamlaka kamili juu ya pepo wabaya, lakini hatuna mamlaka kamili juu ya watu. Kumbuka kwamba ingawa uko chini ya mamlaka ya Mungu, huenda sivyo kwa watu wengi walio karibu nawe na hivyo wanaweza kuanguka kwenye uvumi na machafuko. Wanaweza kuhukumu nia yangu isivyofaa au kunitesa.

Lakini hawawezi kukomesha mpango wako wa Roho Mtakatifu!!! Adui ataendelea kuja akiwa amechelewa. Mungu yuko mbele yako naye atakuelekeza kwenye njia ya ushindi ukikaa imara katika imani na kukataa kuridhiana.

Awamu ya kutekeleza ni hatua ambayo itahitaji ujasiri zaidi kuliko imani ili kuitimiza. Imani ilikuleta hapa, lakini sasa itahitaji ujasiri kuanza kutekeleza. Nafikiri kwamba watu huchanganyikiwa kuhusu hadithi ya Bahari Nyekundu na hadithi ya Mto Yordani.

Katika hadithi ya Bahari Nyekundu, watu wa Israeli walikombolewa kutoka Misri na wakasafiri hadi Bahari ya Shamu ambapo walizingirwa na bahari na milima kwa vile Farao alibadili mawazo yake na kuwafuata. Ilionekana kwamba hakukuwa na njia ya kutoroka. Lakini Musa aliinua fimbo yake (mamlaka), na Bahari Nyekundu ikafunguka. Walivuka kwenye nchi kavu, na jeshi la Farao likajaribu kuwafuata. Lakini jeshi la

Farao lilipofanya hivyo, bahari iliwafunika na kuwaua wote. Israeli sasa ilikuwa huru kutoka Misri na huru kutoka utumwani. Hili ni tendo kuu la ukombozi, na sote tunapenda kuimba juu ya ukombozi wa Mungu.

Mbele kulikuwa na ahadi yao, nchi ya Kanaani. Ni nchi ya mababu zao na ilikuwa imeahidiwa kwa uzao wa Ibrahimu. Walipokuwa wakisafiri katika jangwa, maneno ya Musa yalisikika masikioni mwao: itakuwa nchi inayotiririka maziwa na asali. Ilisika kuwa nzuri sana kupita kiasi kwa watu ambao walikuwa wameishi maisha yao yote katika utumwa. Lakini kulikuwa na tatizo. Ardhi tayari ilikuwa imemilikiwa na mataifa mengine. Walipokaribia Mto Yordani, Musa aliamua kutuma wapelelezi ili wachunguze njia iliyo bora zaidi ambayo wangepitia baada ya kuvuka na kuingia katika nchi mpya na kuleta baadhi ya matunda yake ili kuwathibitishia watu kwamba ni nchi nzuri iliyojaa uwezekano mwingi.

Lakini wapelelezi hao walileta habari iliyofanya taifa la Israeli litake kurudi Misri. Walisema nchi ilikuwa imejaa majiji yenye kuta na watu wakubwa na warefu zaidi kuliko Waisraeli. Waisraeli walivunjwa moyo na kulia na kumgeukia Mungu na Musa, huku wakifikiri kwamba walidanganywa. Kwa sababu ya kutoamini kwao, Mungu hakuwaongoza kwenda kwa nchi yao ya ahadi maana alifahamu kwamba bila imani, wangeangamizwa. Kizazi hicho kiliishi na kufa jangwani, na hakuna hata mmoja wao aliyesalia.

Sasa, Yoshua aliagizwa na Mungu awavushe. Lakini tena, walipokuja kwenye Mto Yordani, kulikuwa na tatizo. Mto huo ulikuwa katika msimu wa mafuriko, na watu hawangeweza kuvuka maji yaliyokuwa yakienda kwa kasi. Lakini kwa mara nyingine tena Mungu aliyapasua maji, na Waisraeli wakatembea katika nchi kavu—wakati huu si kwa sababu ya mzozo, kama ilivyokuwa wakati walipotoka Misri, bali walikuwa wakiingia ndani ya mzozo ili kunyakua ahadi yao.

Hili ndilo unapaswa kujua. Kunaweza kuwa na masuala au matatizo ya kutatua unapoanza, lakini usiogope. Mungu atakusaidia na kukulinda unapotekeleza maono yako. Daima kumbuka kwamba nyuma ya tatizo hilo kuna ahadi. Kamwe usisahau hilo.

Nitasema jambo hapa ambalo linaweza kukushtua. Fahamu maeneo yaliyo na matatizo. Sio kwamba utafakari matatizo yako binafsi kwa hofu. Ninazungumzia wewe kutafuta fursa. Wajua, watu hulipa pesa nyingi kusuluhisha au kurekebisha matatizo. Biashara kweli ni jibu kwa shida fulani ya mtu. Kwa mfano, ikiwa watu wana tatizo la njaa—suluhu ni kuanzisha duka la kuuza chakula. Nina hakika labda umepika chakula hapo awali,

lakini hukufanya hilo kuwa dhana ya biashara. Lakini leo, kuna makumi ya maelfu ya maduka ya chakula duniani kote kwa sababu yanatatua tatizo la mtu. Labda utasema, "Ningefanya hilo," na ndio ungefanya. Lakini unahitaji kufikiria kwa njia tofauti.

Mimi na Drenda ni mamilionea leo, si kwa sababu sisi ni werevu au wazuri. Tulijifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi, na Mungu akatuonyesha jinsi ya kutatua tatizo tulilokuwa nalo. Kisha Mungu akatuonyesha jinsi ya kuwasaidia watu wengine kutatua tatizo lilelile. Si vigumu sana!

### Mahali pa Maandalizi

Kwa hivyo, baada ya kutoa matoleo kwa imani na baada ya kupata mpango, usianze bila kutafakari. Kumbuka Andiko letu katika Mathayo 13.

> *Tena ufalme wa mbinguni umefanana na **hazina** iliyositirika katika shamba; ambayo mtu alipoiona, aliificha; na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote, akalinunua shamba lile.*
>
> — Mathayo 13:44

Mungu huwa anakuita ujiandae kwanza. Kwa hivyo, hata kama umesikia kutoka kwa Mungu na amekupa wazo litakaloanzisha biashara mpya nzuri, kuwa na uhakika kuhusu wakati mwafaka. Mungu daima hufunua hazina ili kukutia motisha ya kujiandaa kwanza. Tazama sijasema Mungu hukupa hazina. Nilisema Yeye hufunua hazina, yaani jibu. Watu wengi sana wameelewa vibaya ufunuo wa hazina kama wakati wa kunyakua hazina, na wamepata matokeo ya kutisha. Mungu daima atakuelekeza kwa mafunzo na maandalizi kabla ya kukutuma kumiliki hazina.

Najua mimi kama kijana, Mungu alinipa maono ambapo nilikuwa nimesimama huku nikiwa nimeshikilia Biblia mkononi mwangu. Nikiwa nimesimama pale, sikujiona nikihubiri kutoka kwa Biblia tu bali pia niliona chumba na watu niliokuwa nikiwahubiria. Sauti ilinena nami nilipoona maono hayo. "Ninakuita uhubiri Neno Langu." Nilisikia hivyo mara tatu kisha ono likatoweka. Nilikuwa na umri wa miaka 19. Nilikuwa nikifanya kazi katika duka la pizza la babangu wakati huo na kwa kweli sikujua maono hayo yalimaanisha nini kabisa. Nilijua kwamba niliitwa kuhubiri Neno la Mungu, lakini sikujua kwa jinsi gani au mahali hilo lingetukia.

Kwa kweli, huo ulikuwa wito wa maandalizi. Haikuwa muda mrefu

sana baada ya Mungu kunipa ufunuo huo aliponiambia niende kwenye shule ya Biblia na kisha kuingia katika chuo kikuu cha Kibiblia kiitwacho ORU. Huko nilikutana na mpenzi wa maisha yangu, Drenda. Tulipotoka ORU tulianza biashara ya kifedha, mpango ambao sikuuelewa wakati huo. Wito wa Mungu maishani mwangu ulikwenda wapi? Mungu alikuwa na mpango. Alitumia wakati huo kunizoeza katika masuala ya kifedha ya maisha, na kunizoeza katika sheria na kanuni za Ufalme Wake, ambazo zimekuwa msingi wa huduma yangu. Pia alitumia muda huo kunisaidia kukua katika ujasiri maana niliogopa sana kuzungumza na watu tangu utotoni.

Haikuwa hadi Septemba 1, 1995 ambapo Mungu alituongoza kuzindua kanisa letu katika orofa ya chini ya kituo cha redio cha Kikristo. Ibada yetu ya kwanza ilikuwa ya jioni, na niliposimama mbele ya watu, niliona picha kamili ya maono yale Mungu alikuwa amenipa miaka 21 awali.

Kwa hivyo elewa kwamba unapopata maono, mwelekeo, au wazo, kwa kawaida haimaanishi uanze wakati huo huo. Mungu atakuambia wakati wa kuanza jinsi ile ile alivyokupa mpango. Atanena nawe, nawe utajua.

Tulikuwa washirika wa kanisa dogo karibu na kwetu mwaka wa 1995; na katika ibada ya Jumapili jioni, Mungu alianza kuzungumza nami. Sikuweza kusikia alichokuwa akisema mchungaji maana Roho wa Mungu alikuwa juu yangu kwa nguvu sana. Nilijua wakati wa kutekeleza ulikuwa umefika! Itakuwa vivyo hivyo kwako.

Mimi na Drenda tumependezwa sana kuona yote ambayo Mungu amefanya, lakini shauku yetu ni yote anayoyafanya!!!!! Tumejitolea kuhubiri na kufundisha ujumbe huu wa Ufalme maisha yetu yote. Hakuna kinachotufurahisha zaidi kuliko kuona nyuso za watu ziking'aa wanapopata ufunuo tunapofundisha. Tunajua maana ya hilo; wanapata majibu.

Tunajua kwamba Ufalme ni jibu lako pia! Kwa hivyo kanuni ya tano ambayo Mungu alinifundisha ni ipi?

**Hatua #5: Unapojua wakati, mbinu, na mahali, usikawie! Pili, usishangazwe na mapambano.**

Wewe na Mungu mnaweza kutimiza kazi hiyo, bila shaka! Kumbuka tu kwamba ni mapenzi ya Mungu kwamba ufanikiwe.

> *Mpendwa, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya njema, kama vile roho yako ifanikiwavyo.*
>
> — 3 Yohana 2 (Tafsiri ya 'NASB')

Usiruhusu mtu yeyote akuambie kwamba si mapenzi ya Mungu kwako kuwa na afya njema na kufanikiwa maishani! Hiki ndicho Shetani alichoiba kutoka duniani ambacho Mungu amekurudishia katika Yesu Kristo. Dini imewafundisha watu uwongo kama huu kumhusu Mungu. Wakati mwingine watu wanahitaji kuondoa mafundisho ya hadithi za tamthiliya kabla ya kujifunza ukweli. Nilipokea barua pepe ifuatayo hivi majuzi, ambayo inadhihirisha hitaji la kufanya upya akili yako kwa kile anachosema Mungu.

*Mpendwa Gary,*

*Jina langu ni Annette. Nililelewa katika nyumba ya mchungaji Mbaptisti, niliokoka nikiwa mtoto, na nilimpenda Yesu sana. Mara tu nilipokuwa mtu mzima nilibatizwa katika Roho Mtakatifu na nikaanza kuelewa ibada ya kweli, uponyaji, ukombozi, karama za kiroho, na kweli nyinginezo kuhusu Ufalme wa Mungu. Nilijifunza kanuni za msingi za kupanda na kuvuna kupitia waalimu mbalimbali katika mwili wa Kristo. Lakini haikuwa hadi mume wangu, John, "alipojikwaa" kutokana na mafundisho yako ndipo nilianza kutambua kwamba nilikuwa na tatizo la kweli la kuamini kwamba Wakristo—hasa wachungaji au watu katika huduma—wanapaswa kutafuta jinsi ya kufanikiwa zaidi ya kutosheleza mahitaji yao ya kimsingi. Tuligundua kwamba hakuna hata mmoja wetu aliyeelewa kikweli jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi.*

*Tulifanya kazi ya huduma na tulikuwa waaminifu kutoa zaka. Pia tulikuwa watoaji wakarimu na hata tulifundishwa kanuni ya kupanda na kuvuna. Lakini tulihisi kwamba tuliishi maisha ya starehe kiasi na hilo ndilo tu tulilopaswa kutarajia. Hiyo ilikuwa hadi msimu wa vuli wa 2003 wakatu tulikuwa na moto mbaya kwenye kizimba chetu ambapo tulikuwa na makao makuu ya biashara yetu na huduma. Kisha matukio mengine kadhaa yalitokea ambayo yalibadilisha kila kitu. John alianza kuwa na matatizo ya mara kwa mara ya moyo, na hatimaye kuhitaji upasuaji wazi wa moyo. Hatukuwa na bima ya afya wakati huo, na tulianza kutozwa bili kubwa za hospitali. Kutoweza kwake kufanya kazi kulifanya mambo kuwa mabaya zaidi. Na kisha baadhi ya maamuzi mabaya kwa upande wetu yalisababisha masuala makubwa ya kifedha. Kufikia mwaka wa 2015, maisha yetu ya kawaida ya kifedha yalikuwa yamebadilika kutoka kuwa mazuri hadi yale ya kulemewa na madeni mengi, ikiwa ni pamoja*

*na ushuru wa siku za nyuma.*

*Siku zote tumekuwa wakarimu kwa sababu tunapenda kutoa na tunaamini kupanda na kuvuna. Tulimtafuta Bwana sana kuliko wakati mwingine wowote ili kupata majibu. Kisha John alijikwaa na mafundisho yako katika runinga. Mwanzoni alisema, "Huwezi kumnunua Mungu hivyo" kisha akazima runinga. Lakini baada ya siku chache, alipata kipindi chako tena, na wakati huu hakuweza kuacha kusikiliza. Aliagiza rasilimali zako zote za mafundisho uliyokuwa nayo wakati huo! Tulilishwa na nyenzo hizo kwa miaka miwili kabla ya kuweza kuacha imani ya kichaa kwamba ni makosa kutaka kuwa na utele na zaidi ya kutosha.*

*Siku moja, tulikuwa tukitazama, kwa mara ya kumi hivi, DVD fulani ambapo unafundisha kutoka Mathayo 17 kuhusu Yesu alipomwambia Petro avue samaki na kutumia sarafu kinywani mwake kulipa kodi, pamoja na mfano kutoka kwa 2 Wafalme 4 kuhusu mwanamke ambaye alitumia kile alichokuwa nacho nyumbani mwake.*

*Ghafla nikakumbuka kwamba miaka michache awali rafiki mmoja alikuwa ametupea sarafu ya dhahabu kama malipo ya kazi fulani tuliyomfanyia. Haikutosha kulipa deni letu, bali ni "kitu" tulichokuwa nacho nyumbani mwetu ambacho tungeweza kupanda! Tulipanda sarafu hiyo katika huduma yako na tukawa Washirika wa Mduara wako wa Ndani na tukangoja kuona kile ambacho Mungu angefanya baadaye.*

*Kwa muda wa miezi michache iliyofuata, tuliendelea kulishwa na mafundisho yako, na tulijitahidi kutozama tulipokuwa tukifanya malipo ya madeni. Kisha usiku mmoja, niliota ndoto ambayo Mungu alinionyesha kwamba kiasi kikubwa cha pesa kilikuwa kikija kwetu. Katika majuma yaliyofuata, tuliona baraka ndogo za kifedha zikiingia. Tuliendelea kuomba na kutoa zaidi kama Mungu alivyotuelekeza, na tulitangaza kweli za Mungu na kumsikiliza ili kuhakikisha kwamba tunatii kila kitu tulichoamini alikuwa akituambia tufanye.*

*Kisha hali ikabadilika, jambo ambalo tulidhani halingeweza kutokea. Tuliona utimizo wa ndoto hiyo ukitimia baada ya muda mfupi. Kiasi cha pesa tulichopokea kilikuwa juu sana na zaidi ya kile tulichohitaji ili kulipa madeni tuliyodaiwa. Sasa tumetoka kwa madeni. Tunatafuta mikakati ya*

> *jinsi ya kuwekeza kwa busara na kuishi maisha ya sehemu maradufu ili tuweze kutoa kwa ukarimu, kila wakati na katika kila hali.*
>
> —John na Annette

Tunapata barua pepe za aina hii kila wakati kutoka kwa watu wanaojifunza ukweli kuhusu Mungu na Ufalme Wake, ambao wanatambua kwamba wamedanganywa na dini.

Niligundua kwamba mara akili yangu ilipofanywa upya kuhusu wema wa Mungu na Neno Lake, basi niliweza kukua katika ufunuo niliohitaji kuwa huru. Kumbuka, usiwe na shaka na Mungu. Ikiwa kuna hali fulani maishani mwako ambayo inaweza kuonekana kuwa umeshindwa na Ufalme wa Mungu, fanya yale ambayo wanafunzi walifanya. Hawakumuuliza Yesu, "Yesu, kwa nini hukumtoa yule pepo?" La, waliuliza, "Kwa nini hatukuweza kumtoa yule pepo?" Walijua kwamba tatizo lilikuwa upande wao, na wakamwomba Yesu awasaidie kulielewa. Ikiwa huoni kile ambacho Biblia inasema ni chako katika maisha yako, mwombe Mungu akuonyeshe sababu! Atanena nawe na kukusaidia kujifunza jinsi Ufalme Wake wa ajabu unavyofanya kazi.

**ATANENA NAWE NA KUKUSAIDIA KUJIFUNZA JINSI UFALME WAKE WA AJABU UNAVYOFANYA KAZI.**

Hivi majuzi, mfanyabiashara katika kanisa langu alipata taarifa kutoka kwa benki yake kwamba pesa za ruzuku ya serikali alizoahidiwa zilikuwa zimekataliwa.

Alikuwa ametarajia pesa hizo na alikuwa na mipango kuzihusu. Bila msaada huo, angelazimika kuwaachisha kazi wafanyikazi wake. Alipouliza benki kwa nini fedha hizo zilikataliwa, hawakuweza kujibu kwa nini. Kwa kuwa alifikiri pesa hizo zilikuwa zikija, aliwekeza pesa alizokuwa nazo kwenye vifaa alivyohitaji. Lakini sasa kwa vile pesa hazikuja, alijikuta katika hali ya ukosefu wala hakujua afanye nini. Kitu pekee alichokuwa nacho ni kadi alizopewa na mtu fulani kama zawadi. Mara moja alizipeleka kanisani, kwa sababu alijua alipaswa kupanda kile alichokuwa nacho na kumwamini Mungu amsaidie katika kipindi hiki kigumu. Masaa machache baada ya kutoa kadi hizo kanisani kama mbegu, benki ilimpigia simu na kumwomba msamaha kwamba lazima kulikuwa na kosa fulani. Walimtumia pesa hizo.

## Una Sehemu ya Kutekeleza

Ninapomalizia, hebu nikupe maneno yangu ya mwisho kuhusu kunyakua pesa unazohitaji. Nimegundua kwamba watu wengi wa Mungu wana mioyo ya kutoa, mioyo inayowajali wengine, lakini hawana pesa. Ninaamini kwamba sababu kuu ya watu kushindwa kuona faida katika utoaji wao ni mtazamo mbaya wa kile kinachopaswa kutokea baada ya kutoa. Wakristo wengi wanaamini uwongo kwamba Mungu atawaletea pesa wanazoamini kupata. Lakini hilo haliwezekani maana Mungu hana pesa. Pesa zote ziko duniani na ni bidhaa tu ya biashara (kununua au kuuza kitu).

Kwa hivyo mara tunapotoa, ikiwa tunaelewa kipengele hiki cha mchakato, lazima tumsikilize Roho Mtakatifu kwa ajili ya mpango, mwelekeo, au wazo tutakaloliunda au kulitumia kunyakua mali sokoni. Hii haimaanishi kuwa lazima uwe na biashara, lakini Roho Mtakatifu atakuelekeza mahali fulani sokoni ambapo utaweka wavu wako. Wavu ni kitu chenye uwezo wa kunyakua au kupata pesa sokoni. Mungu ataelekeza hatua zako na mpango unaopaswa kufuatwa. Kwa watu wengi, ninaamini kuwa wavu bora zaidi, wa haraka na ulio na uwezo ni biashara. Ninaposema biashara, siondoi kufanya kazi katika shirika fulani, lakini wavu unahitaji kuwa mkubwa vya kutosha kuvua samaki unaohitaji. Inaweza kuwa biashara yako mwenyewe au ya mtu mwingine.

Lakini linapohusu suala la nyavu, kwa uzoefu wangu, watu wengi huvua nyangumi kwenye bafu. Hebu nielezee. Hebu tuseme mtu anafanya kazi katika duka la chakula na mapato yake ni $10 kwa saa. Lakini sasa anatamani kulipia nyumba yake binafsi dola 150,000 na anataka kutumia sheria ya Ufalme kuitimiza hilo. Sawa, vema hadi hapo.

Kisha, akasikia kuhusu kupanda na kuvuna, yaani sheria ya Ufalme, na akapanda na kuamini kuilipia nyumba hiyo. Tena, vizuri kufikia hapo. Lakini kwa sababu moja au nyingine, akafikiri kwamba pesa zitajitokeza tu. Anajua kwamba kazi yake haina uwezo wa kunyakua pesa za kutosha kulipia nyumba, kwa hiyo akamtumainia Bwana (na hivyo ni vyema). Lakini ninaposema “tuweke tumaini letu kwa Bwana,” unahitaji kuelewa ninachosema ni kwamba tunaweka tumaini letu kwa Bwana ili atupe hekima na mwelekeo wa kunyakua fedha hizo. Na hiyo inaweza kumaanisha mabadiliko makubwa yatahitajika.

Wajua, jambo ambalo watu hushindwa kutambua ni kwamba huenda Mungu akahitaji kuwaelekeza kwenye ziwa jipya ili kukamata nyangumi, si

beseni lao la kuogea walilozoea. Hakuna nyangumi kwenye beseni lako la kuoga! Kulipia nyumba $150,000 katika miaka michache ukiwa na mapato ya $10 kwa saa itakuwa vigumu. Lakini Mungu anajua walipo samaki na anaweza kukuelekeza kwenye sehemu na njia sahihi ya kupata samaki unaohitaji ili kufikia lengo lako. Unakumbuka hadithi ya Petro na samaki wengi waliovuliwa? Petro alikuwa amevua samaki usiku kucha na hakupata chochote, lakini Yesu alimwambia mahali pa kuvua; na baadaye, mashua ya Petro haikuweza kuchukua samaki wote. Tofauti? Neno la mwelekeo, "Shusheni nyavu zenu kwenye kilindi cha maji." Wajua, Petro alikuwa akivua samaki mahali pasipofaa, lakini Yesu alimwambia jambo la kufanya na mafanikio yake yakabadilika.

Mimi na Drenda tulipokuwa na madeni mengi, ilitubidi tujifunze kumsikia Mungu na kumfuata kwenye maziwa makubwa na makubwa zaidi ili kuvua samaki tuliohitaji. Mwongozo wa Mungu uliendelea kutupeleka kwenye maji yenye kina kirefu zaidi na zaidi. Kusema kweli, Mungu alitupeleka mbali sana hata hatungeweza kuona ardhi tena, jambo lililotutisha sana maana hatukuwa tumewahi kufika hapo awali, na tulitishwa sana hasa dhoruba zilipotokea.

Kwa kuwa watu wengi wanamngoja Mungu ili pesa zijitokeze, haingii akilini mwao kusikiliza kusikia kitu ambacho ni kigeni kwao kinachowaelekeza katika maeneo mapya na ya kutisha ambayo hawajawahi kufika hapo awali. Watu wengi hutazama tu yale wanayoyajua tayari. Lakini nyangumi hawako kwenye bafu yako. Unahitaji kwenda kwa maji ya kina.

Kwa hivyo kumbuka, hatupaswi kutofanya kazi mara tunapotoa matoleo. Tunapaswa kushikilia Neno la Mungu na kujua kwamba Mungu atatuongoza kwenye mavuno. Lakini ni lazima tusikilize mwelekeo huo, tuufuate, kisha tuwe na nyavu za kuwakamata nyangumi tunapofika huko.

Watu wengi huchukua hatua za kubadili ziwa lakini wanashindwa kubadili mbinu zinazotumika kupata mavuno yao. Ndoano ya samaki mdogo hawezi kumkamata nyangumi. (Sisemi kwamba tunapaswa kukamata nyangumi. Ninatumia huu kama mfano tu kutokana na ukubwa wao.)

Ukishafika mahali sahihi, mbinu zako lazima ziwe na uwezo wa kuhimili uzito mkubwa na shinikizo linalohitajika kunyakua mavuno makubwa. Yote haya yanachukua muda kuandaa. Mara nyingi, Mungu anajua kwamba hatuna uwezo wa kumkamata nyangumi tunayewinda mara tunapokutana naye moja kwa moja. Lakini Mungu atatuzoeza, na tunaweza kuwa na hakika kwamba tutavuta samaki hao ufukweni ikiwa hatutazimia.

Kwa hivyo katika kujikumbusha, tunahitaji kuacha kufikiria kuhusu

pesa za miujiza au kile ninachoita mawazo ya kisanduku cha barua (ingawa Mungu hufanya mambo ya kushangaza). Badala yake, tunahitaji kufanya kazi na Mungu, kujiandaa kwa ajili ya mavuno, na kutekeleza sehemu yetu ili kunyakua kila fursa ambayo Mungu anaweka mbele yetu.

Nguvu ya Kuwa na Riziki imewekwa mikononi mwako. La, sizungumzii jina la kitabu changu. Ninazungumza juu ya Roho Mtakatifu na Ufalme ambamo Mungu amekuweka. Kwa hivyo jitahidi sana, na uwalete wengi kwa Kristo kupitia kwa mafanikio yako na mfano wako.

Nimeona barua pepe hii ikiingia, na nikafikiri ni ukumbusho mzuri tunapotia tamati.

> *Katikati ya uchumi wa dunia kuporomoka, madeni mawili ya $4000 na $8,000 ya biashara yetu yalifutwa! Ila kuna zaidi!! Tulikuwa tukichunguza fedha za biashara yetu na tukagundua kwamba, kufikia leo, mapato yetu ya jumla ya biashara ya mwaka wa 2020 hadi sasa yamepita mapato yetu yote ya jumla ya 2019! Tumefanikiwa zaidi na zaidi ya yote tunayoweza kuomba au kufikiria (Waefeso 3:20) wakati uchumi wa dunia uliolaaniwa unashindwa! Tunafurahia sana kile Mungu anachofanya. Yeye ni mwaminifu SANA kutimiza Neno Lake!!*

> *Asante, asante, asante Gary na Drenda, familia yenu, wafanyakazi wenu, na washirika wenu kwa kuleta Neno la Mungu katika maisha yetu! Tuliishi kwa miaka 17 katika umaskini na ufukara—kama Gary na Drenda walivyoishi kwa miaka 9—hadi wachungaji wetu walipoanza kuonyesha mafundisho ya video ya mfululizo wa Fixing the Money Thing Jumatano jioni kanisani. Hiyo ni miaka 5.5 iliyopita, na hatujawahi kuwa kama tulivyokuwa awali!! Asante tena, na mbarikiwe!*

Rafiki, nisimulie hadithi zako kwenye anwani ya mtandao GaryKeesee.com. Wengine wanahitaji kusikia jinsi Ufalme unavyofanya kazi katika maisha yako.

# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA
## Nguvu ya Kuwa na Riziki

Je, unahangaika maishani...
au una uwezo wa kuota ndoto kubwa?

Wewe ni mtumwa wa madeni...
au unafuatilia kusudi ulilokusudiwa na Mungu?

Ni lipi kati ya haya linalosikika zaidi kama wewe?
Ni kitu gani kitakacholeta tofauti katika MAISHA YAKO?
*Riziki.*

Sote tunaweza kukubaliana kwamba kuwa na riziki ya kutosha kwa ajili ya mahitaji maishani ni muhimu.

Lakini je, kweli unaelewa *NGUVU* ya riziki?

Gary Keesee anataka kulirahisisha jambo hili.

Katika awamu hii ya nne ya mfululizo wa "Mapinduzi Yako ya Kifedha," Gary anafichua mojawapo ya vipengele muhimu zaidi vya mafanikio yake na mafanikio ya wengine, na siri nyingine MUHIMU ya Ufalme wa Mungu: *Nguvu ya Kuwa na Riziki!*

Jifunze:

- HATUA TANO ZA KIMSINGI unazoweza kuchukua ili kupokea riziki unayohitaji.
- Umuhimu wa imani na jinsi unavyoweza kujua wakati huna imani.
- Jinsi kuahirisha kunavyoweza kuwa jambo la hatari.
- Ikiwa unaweza kuamini kushinda bahati nasibu (ndio, hili limo humu).
- Na mengi zaidi!

Jiunge na Gary kwenye safari hii ya kufumbua macho, na ugundue jinsi ya kufanikisha Nguvu ya Riziki maishani mwako!



Gary Keesee ni mwandishi, mmnenaji, mjasiriamali, mtaalamu wa fedha, na mchungaji ambaye ana shauku ya kusaidia watu kuwa washindi maishani, hasa katika maeneo ya imani, familia, na fedha. Gary na mkewe, Drenda, wameanzisha biashara kadhaa zilizo na fanaka, na ndio waanzilishi wa huduma iitwayo Faith Life Now, ambayo ina vipindi viwili vya televisheni—*Fixing the Money Thing* na *Drenda*, kongamano kote ulimwenguni, na rasilimali za vitendo. Wao pia ni wachungaji wa Kanisa la Faith Life karibu na Columbus, Ohio.

P. O. Box 779, New ALBANY, OH 43054, USA